# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NNE

## Kikao cha Tano – Tarehe 13 Septemba, 2016

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:** Maswali.

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, (TAMISEMI). Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Justus Nditiye, Mbunge wa Muhambwe, sasa aulize swali lake.

Na. 56

### Shirika la *UNHCR* Kujenga Wodi Hospitali ya Wilaya ya Kibondo

**MHE. *ENG.* ATASHASTA J. NDITIYE** aliuliza:-

Je, Shirika la *UNHCR* lina mpango wowote kwa usimamizi wa Serikali wa kujenga angalau wodi tatu za kulaza wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kibondo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Justus Nditiye, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ipo katika mazungumzo na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Wakimbizi *(UNHCR)* kuomba msaada wa kujengewa wodi ya wanawake katika Hospitali ya Wilaya ya Kibondo ili kukidhi mahitaji yaliyopo. Maombi hayo yaliwasilishwa na Halmashauri kupitia barua ya tarehe 30 Machi, 2016 yenye Kumb. Na. HW/A/D.30/22/Vol.1/23 na mazungumzo yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo imetenga shilingi milioni 140 kwa ajili ya ujenzi wa wodi moja katika hospitali hiyo ya Wilaya ya Kibondo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Nditiye swali la nyongeza.

**MHE. *ENG.* ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Ninaamini Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba zahanati karibu nane zimekwishapata umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Kwanza na ya Pili, lakini hazijaunganishwa.

Je, ni lini Wizara ina mpango wa kuunganisha umeme kwenye Zahanati hizo nane?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa hospitali alizotaja za Kibondo na Kasulu zote zimeunganishwa na umeme lakini hazijawashwa. Utaratibu wa kuwasha hospitali zote za Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine ya jirani zinafanyika mwezi wa 11 na 12 mwaka huu wa 2016.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilago, swali la nyongeza.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii.

Kwa kuwa suala la wakimbizi ambalo linaathiri Wilaya ya Kibondo, vilevile limeathiri Wilaya ya Kakonko, Jimbo la Buyungu.

Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuwashauri watu wa *UNHCR* kutoa huduma za afya katika Kituo cha Afya Wilaya ya Kakonko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuzungumza wazi kwamba

tuwashukuru wenzetu wa *UNHCR* katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano mwezi uliopita nilikuwa katika Mkoa wa Katavi. Miongoni mwa kazi kubwa sana waliyoifanya kule licha ya kusaidia katika miundombinu, lakini nimeona wamesaidia *ambulance* katika maeneo yale.

Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba kwa suala analolizungumza Mheshimiwa Mbunge, nadhani hili ni wadau wetu wa karibu sana, ofisi yetu ya Mkoa kule itafanya utaratibu kuangalia ni jinsi gani tutafanya; na kwa Mkoa wa Kigoma kwenda kutoa juhudi hizo *especially* katika sehemu ya afya. Mwisho wa siku tunahitaji wananchi wetu katika eneo lile waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazo zuri sana, nadhani katika Serikali tunalichukua hili kwa ajili ya kuleta ule msisitizo tu wa makubaliano ya karibu kwamba lile linalowezekana basi liweze kufanyika, wananchi wa eneo lile waweze kupata huduma vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 57

**Manispaa ya Moshi Kutangazwa Kuwa Jiji**

**MHE. ANTONY C. KOMU (K.n.y. MHE. RAPHAEL J. MICHAEL)** aliuliza:-

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ilianza mchakato wa kuifanya Jiji tangu mwaka 2012 baada ya kupata baraka za Rais Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Kilimanjaro *(RCC)* na Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Moshi *(DCC)* na sasa mchakato huo umekamilika katika hatua zote za kikanuni.

Je, ni lini Serikali itatangaza Manispaa ya Moshi kuwa Jiji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri ya Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika vikao vyote vya kisheria vimekaa na kuridhia pendekezo la Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Jiji. Hapo awali, maombi hayo yaliwasilishwa Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya maamuzi. Hata hivyo, maombi hayo yaliyejeshwa ili

yafanyiwe marekebisho kutokana na upungufu uliobainika kulingana na vigezo na taratibu zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa timu ya uhakiki kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ipo katika uhakiki wa maombi ya maeneo mapya ya utawala yakiwemo maeneo kutoka Manispaa ya Moshi ili kuhakiki vigezo vilivyozingatiwa katika kuanzisha maeneo hayo. Baada ya kukamilika kwa zoezi hilo nchi nzima, Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa atashauriwa ipasavyo kuhusu maombi haya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raphael Michael, swali la nyongeza.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yake kwa sababu hayupo, yupo safari.

Pamoja na majibu ya Naibu Waziri; jambo hili limechukua muda mrefu na kama nchi ilivyokwishaamua kwamba inakwenda kwenye mpango wa viwanda na uchumi wa kati, jambo hili ni muhimu sana. Sasa nataka kujua:-

(i) Ni lini sasa huo mchakato utakamilika ili jambo hili liweze kuanza?

(ii) Napenda kujua vilevile kutoka kwenye Serikali, ni mambo gani hayo hasa ambayo yamepelekea huo mchakato kurejeshwa tena kwenye kufanyiwa marekebisho na vitu kama hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa, swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, limeulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Antony Komu. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama nilivyosema kwamba tukifanya rejea Bunge lililopita, nilisema kuna timu ya TAMISEMI itapita maeneo mbalimbali; na lengo kubwa ni kubaini kwamba yale maombi yaliyoletwa kutoka katika Ofisi za Mikoa baada ya vikao vya *RCC* kukaa, kwamba maombi yale sasa wataalam wakienda kufanya tathmini wataona jambo lipi limekamilika na jambo lipi halijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri naomba nikujulishe kwamba ofisi yetu imeshatuma timu katika maeneo hayo yote na kazi hiyo wameshamaliza. Hivi sasa wana-*compile* ripoti yao baadaye kuweza kutushauri vizuri jinsi gani ya kufanya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Komu vuta subira jambo hili litaenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili kwamba mambo gani mwanzo yalikuwa hayajakamilika; ni kwamba ukiangalia Mji wa Moshi, *square*

*kilometer* karibu 58 peke yake, yaani ni eneo dogo sana kuwa Jiji. Ndiyo maana walidhani kama ingewezekana ni kuongeza eneo lile la utawala na ndiyo maana nadhani wameona maeneo waliyokubaliana katika muhtasari wa mwisho, eneo limeongezeka mpaka maeneo ya Hai na maeneo mengine. Ina maana kwamba eneo limevuka kutoka zile *square kilometer* 58 imeenda mpaka karibu 142.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na mambo mengine hasa yanayohusu *master plan.* Kwa hiyo, vitu hivi vyote vilileta mrejesho, walipelekewa mrejesho watu wa Moshi kule kwenda kuvifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yangu ni kwamba marekebisho yale yameshafanyika, sasa wahakiki wetu walivyoenda kuangalia kule *site,* watajua ni jinsi gani vile vilivyoelekezwa vimeweza kufikiwa vizuri na baadaye Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atafanya maamuzi. Naomba tusiwe na hofu, kila kitu kitaenda kwa utaratibu ambao umepangwa katika ofisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Desderius Mipata, swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namanyere ni moja ya mamlaka iliyotembelewa na timu ya uhakiki kutoka Serikali za Mitaa na kwa taarifa tulizozipokea ni kwamba mamlaka hiyo ilikuwa imetimiza vigezo vyote na kwamba kulikuwa na dosari ndogo ndogo ambazo kwa kweli wataalam wetu wameshaleta ripoti na kukamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua ni lini hasa wananchi wa Namanyere wategemee kupata hicho walichokiomba kuwa Mamlaka ya Mji kamili wa Halmashauri ya Mji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka katika Bunge lilipita nilijibu swali la Mheshimiwa Mipata na kaka yangu Mheshimiwa Malocha pale, walipokuwa wanazungumza suala zima la Namanyere na sehemu ya Sumbawanga. Ndiyo maana kati ya tarehe 14 na 15, nilikuwa Rukwa na Katavi na niliweza kufika mpaka Namanyere. Hata hivyo, timu yetu ya wataalam ilifika Namanyere kufanya uhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali kwamba zoezi hili sasa litakuwa lipo katika *stage* ambayo ni muafaka sana, mambo yatakapokamilika.

Naomba Mheshimiwa Mbunge asiwe na hofu, ni kwamba yale maamuzi sahihi yatafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio yeye peke yake, hata akina Profesa Maji Marefu hapa, mpaka Mzee wangu hapa wa Mpwapwa, wote wana masuala hayo hayo. Kwa hiyo, tuondoe hofu, ofisi yetu inafanya kazi, tutapata mrejesho muda siyo mrefu sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Dodoma ni Makao Makuu ya nchi; na kwa kuwa Manispaa ya Dodoma imekamilisha vigezo vyote vya kupata hadhi ya kuwa Jiji; na kwa kuwa majengo ya Manispaa ya Dodoma yamejengwa kitaalam, yamefuata *master plan*, hakuna *squatters.* Ni lini Serikali sasa itatangaza Mji wa Dodoma kuwa Halmashauri ya Jiji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Lubeleje anafanya rejea ya siku alipokuwa akiniambia suala la Jiji la Dodoma; lakini nadhani ombi lake alivyokuwa anazungumza vile tukiwa barabarani, Mungu amelitilia tunu juu yake kiasi kwamba sasa hivi naona Serikali yote kiukubwa wake yote inahamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili nadhani halina mashaka, ni taratibu tu zitakamilika hapa na kwa sababu michakato mipana inakwenda na Serikali yote inahamia Dodoma, uwanja wa ndege unaimarishwa, basi nadhani vikao sahihi vitakaa na kufanya mapendekezo haya. Ofisi ya Rais - TAMISEMI haitasita kwa sababu nchi kwa ujumla wake sasa, Serikali yote inahamia Dodoma.

Kwa hiyo, ni mambo ya kimchakato tu, Mheshimiwa Lubeleje avute subira na tunavyoendelea kuliimarisha Jiji letu la Dodoma, nadhani itakuwa ni sehemu ya fahari ya Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka. Aah, Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nataka

kuongezea kwenye swali lililouliza kwamba je, ni lini Dodoma itatangazwa kuwa Jiji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tu Dodoma sasa ndiyo tunafanya jitihada za kuhamia kwa sababu tayari imeshaamuliwa kuwa ndiyo Makao Makuu ya nchi yetu, kwa kawaida na kwa utaratibu ni lazima iwe Mamlaka ya Jiji. Kwa hiyo, utaratibu huu utakwenda sambamba na hii jitihada inayofanyika, lakini pia Dodoma ina faida kubwa kwamba walipokuwa wanatenga na kuitengenezea ramani yake, walitenga mipaka mikubwa, ina *square kilometer* zaidi ya 250,000. Kwa hiyo, ni eneo kubwa sana na linafaa na lina sifa zote kuwa Jiji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Mbunge wa Muleba Kusini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Mendrad Kigola.

Na. 58

**Shule za Sekondari - Muleba**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA (K.n.y. MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA)** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Muleba in shule 39 za sekondari za kata na kati ya hizo, shule 31 hazina walimu wa vipindi muhimu na nyingine zina walimu wa ziada wasio na kazi; mfano shule 12 hazina walimu wa hesabu kabisa, shule tisa baiolojia, shule nane kemia, shule 18 walimu wa fizikia na shule 10 hazina kabisa walimu wa uraia.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na tatizo hilo na kuliondoa ili kuokoa kizazi cha vijana watakaoishi katika karne ya 21 bila kusoma masomo ya sayansi?

(b) Je, kuhusu walimu wa ziada takribani 213 wasiohitajika kwenye sekondari kwa sasa hivi, Serikali itaruhusu Halmashauri iwapange kufundisha kwenye shule za msingi ambapo kuna upungufu mkubwa kuliko kuingia gharama kuwahamisha na kuwarejesha tena wakihitajika kwa sababu shule za sekondari zinaendelea kupanuka?

(c) Je, Serikali itasaidiaje Halmashauri ya Muleba kutengeneza programu maalum ya mafunzo kwa walimu wa ziada kujifunza kufundisha masomo mengine ambayo walimu wake hawatoshi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Mbunge wa Muleba Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kuwapanga walimu wa sayansi moja kwa moja katika shule badala ya Halmashauri kama ilivyokuwa hapo awali ili kuleta uwiano sawa mashuleni. Vilevile Serikali imeandaa mkakati wa kuwaajiri wahitimu wa Shahada za Sayansi ambazo sio za Ualimu baada ya kuwapa mafunzo ya muda mfupi kuhusu mbinu za ufundishaji na maadili ya ualimu. Tayari kibali kimeombwa katika Ofisi ya Rais - Utumishi kwa ajili ya utekelezaji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya tathmini ya mahitaji ya Walimu wa masomo ya sanaa kwa kila Halmashauri ili kubaini maeneo yenye ziada na yenye upungufu ili kusawazisha ikama. Mpango wa Serikali uliopo ni kuwahamisha Walimu wa ziada wa masomo ya sanaa kwenda kufundisha katika shule za msingi ndani ya Halmashauri husika. Kabla ya kuanza utekelezaji wa mabadiliko haya, Serikali itatoa waraka maalum kwenda katika Halmashauri zote.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu wa mafunzo ya walimu, Halmashauri moja haiwezi kuwa na mfumo wa pekee wa wa kuandaa walimu kwa sababu ni vigumu kudhibiti ubora wa mafunzo hayo kwa walimu. Pamoja na nia nzuri, lakini ni vigumu kwa walimu hao wa ziada ambao ni wa masomo ya sanaa, mfano ni wa Kiswahili, Kiingereza au Uraia kupewa mafunzo maalum kufundisha masomo ya Hisabati, Kemia au Fizikia kwa sababu wengi hawana kabisa msingi wa uelewa wa masomo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kuongeza udahili wa walimu wa sayansi katika vituo vya ualimu kadiri iwezekanavyo ili kukidhi mahitaji. Mpango wa muda mfupi ni kuwatumia wahitimu wa shahada za masomo ya sayansi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi kama ilivyoelezwa katika sehemu (a) ya jibu langu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigola, swali la nyongeza.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu maswali vizuri, lakini tunajua kabisa kwamba kuna tatizo kubwa sana la walimu wa sayansi katika Wilaya zote. Sasa je, Serikali ina mkakati gani wa kuchagua chuo kimoja kuweza kusomesha

walimu wa sayansi tu? Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Mkwawa pale, tungeamua kitoe masomo ya sayansi ili tuweze kupata walimu wengi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa nini Serikali sasa isitoe mkopo kwa asilimia mia moja kwa wale wanafunzi ambao wanasomea masomo ya sayansi ili kuwavutia wanafunzi waweze kujiunga na ualimu wa sayansi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la mkakati wa kuwapata walimu wa sayansi, kama unavyofahamu kwamba tayari Serikali ilishachukua hatua na kama mnavyokumbuka kwamba tulikuwa na wanafunzi zaidi ya 7,800 ambao walikuwa katika Chuo cha *UDOM* ambao kwa sasa tumewatawanya katika vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao wana vigezo sasa hivi kwa kufundisha shule za sekondari ni zaidi ya walimu 6,305 wakishamaliza masomo yao wataweza kwenda kwenye hizo shule. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kuweka mikakati ya kufundisha walimu wa sayansi na wakati huo huo kuhakikisha kwamba maabara kwa ajili ya shule za sekondari ili kupata wanafunzi wengi zaidi katika maeneo ya sayansi yaweze pia kukamilika na kupewa vifaa vinavyostahili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imetangaza kwamba nchi yetu sasa masomo ya sayansi ni lazima kwa wanafunzi wetu; lakini hakuna maandalizi ambayo yamefanyika mpaka sasa, hatuna walimu hao kabisa. Nitolee mfano katika Jimbo langu la Babati Mjini, walimu wa *mathematics* katika shule kumi za sekondari, ni shule moja tu ndiyo ina mwalimu wa hesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifahamu, Serikali haioni kwamba inawachanganya wananchi wa Tanzania katika kutoa kauli zao wakati hawajajiandaa kukabiliana na tatizo hilo? Ni lini wanaajiri walimu hao wa sayansi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, swali la nyongeza huwa ni moja. Kwa hiyo, wewe umeuliza hapo mawili. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, jibu swali moja tafadhali.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba wanafunzi kusoma sayansi kama somo la lazima halijaanza, lakini Serikali iko katika maandalizi. Hatua muhimu ambayo imefanyika ni kuhakikisha kwamba kila shule inakuwa na maabara ambapo hizi maabara tunashukuru kwamba zimejengwa kwa ushirikiano na wananchi hatua inayofuata, sasa hivi Serikali ipo katika utaratibu wa kuhakikisha kwamba maabara zote za sayansi zilizojengwa kwenye shule za sekondari zinakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali wa kwamba masomo ya sayansi yatakuwa ni ya lazima, unaendana sambamba na Sera ya Elimu ya mwaka 2014 ambapo elimu inakuwa ya msingi kwamba wanafunzi wanasoma kuanzia msingi mpaka sekondari. Kwa hiyo, Serikali bado ipo katika maandalizi ya kuhakikisha kwamba inatengeneza mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mafunzo kwa Walimu ni kwamba sasa hivi kuna vyuo 10 ambavyo tumeviangalia na tunaviimarisha maabara zake ili ziweze kutoa mafunzo zaidi kwa masomo ya sayansi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Pauline Gekul.

Na. 59

**Maslahi kwa Watumishi wa Sekta ya Afya**

**MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MHE. ZUBEDA H. SAKURU)** aliuliza:-

Kuwepo na matukio ya vifo visivyokuwa vya lazima kunatokana na kutokuwepo kwa motisha kwa madaktari na wauguzi kwa kulipwa viwango duni vya mishahara na kutolipwa posho zao kwa wakati.

Je, Serikali inakabiliana vipi na changamoto ya maslahi kwa watumishi wa sekta hii muhimu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na madaktari, matabibu pamoja na wauguzi nchini ambapo Serikali imeendelea na jitihada zake za kuboresha mishahara ya

watumishi wake mwaka hadi mwaka ikiwemo ya wataalam wa sekta ya afya kwa kuzingatia uwezo wa Serikali wa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utafiti wa tathmini ya kazi na punde tathmini hiyo itakapokamilika, Serikali itapanga mishahara na motisha upya kwa watumishi wote wa umma wakiwemo wa sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kutokana na ukweli huu kati ya mwaka 2010/2011 hadi mwaka 2016/2017 vianzia mishahara kwa kada za wauguzi vimeongezwa kutoka shilingi 614,000 hadi kufikia shilingi 980,000 kwa mwezi kwa wahitimu wa shahada na shilingi 425,000 hadi shilingi 680,000 kwa wahitimu wa stashahada. Aidha, shilingi 260,000 hadi shilingi 432,000 zimekuwa zikilipwa kama kianzio cha mshahara kwa wahitimu wa astashahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vianzia mishahara kwa kada za madaktari na maafisa tabibu katika kipindi hicho vimeongezwa kutoka shilingi 886,800 hadi shilingi 1,480,000 kwa wahitimu wa shahada na shilingi 425,000 hadi shilingi 680,000 kwa wahitimu wa stashahada na mwisho shilingi 260,000 hadi shilingi 432,000 kwa wahitimu wa astashahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2016/2017, vianzia mshahara hivi ni vikubwa zaidi ikilinganishwa na vile vya watumishi wa Serikali Kuu na walimu kwa kuzingatia ngazi ya elimu zao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Serikali Kuu kwa watumishi wenye astashahada wameanzia na shilingi 309,000; kwa walimu wameanzia na shilingi 419,000, kwa wauguzi wameanzia na shilingi 432,000; na kwa matabibu na madaktari wameanzia na shilingi 432,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa stashahada, Serikali Kuu kianzia mshahara kimeanza na shilingi 525,000, kwa upande wa walimu wenye stashahada ni shilingi 530,000, wauguzi shilingi 680,000/= na tabibu na madaktari shilingi 680,000. Kwa upande wa shahada, Serikali Kuu wameanzia na shilingi 710,000, walimu shilingi 716,000, wauguzi shilingi 980,000 na kwa upande wa matabibu na madaktari wenye shahada shilingi 1,480,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa wataalam wa afya na watumishi wote kwa ujumla kufanya kazi kwa bidii na kwa kuzingatia viapo na maadili ya kazi zao. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi kwa kadri uwezo wake wa kulipa utakavyoimarika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kabla hujaondoka tusaidie, hii Serikali Kuu astashahada ni kiasi gani, ni shilingi 390,000 au ni shilingi 309?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni shilingi 390,000.

**NAIBU SPIKA:** Watu wa *Hansard* mlipate hilo sawasawa. Mheshimiwa Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa pamoja na mishahara ya watumishi hawa wa sekta ya afya, Serikali ilikuwa ikitoa motisha mbalimbali ikiwemo *on call allowance* kwa wauguzi wetu; lakini hadi hivi tunavyoongea Serikali haipeleki pesa hizi kwa wakati; na nitoe mfano kwa Hospitali yangu ya Mrara katika Jimbo la Babati Mjini, tangu mwezi wa pili wauguzi wale katika hospitali ile tangu mwezi wa pili hawajalipwa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifahamu, ni kwa nini Serikali haipeleki fedha hizi kwa wakati kama ilivyoahidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa katika bajeti iliyopita *OC* katika Halmashauri zetu na katika hospitali zetu zilipunguzwa kwa zaidi ya asilimia 60; nitoe mfano wa hospitali yangu ya Mrara, ilikuwa inapokea *OC* ya shilingi milioni 154 lakini ikapunguzwa hadi shilingi milioni 46 kwa mwaka na hizi fedha sasa zilipe likizo za watumishi, maji na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifahamu kauli ya Serikali, ni kwa nini fedha hizi zimepunguzwa ilhali mambo haya sasa yamekwama? Mfano sisi, zaidi ya shilingi milioni 10 hospitali inadaiwa, imeshindwa kulipa *BAWASA* bili ya maji. Serikali iko tayari kufikiria kuhusu uamuzi huu wa kupunguza *OC* katika hospitali zetu za Wilaya ili waweze kuziendesha hospitali hizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Eeh, unisamehe Mheshimiwa Pauline Gekul, ni Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini, ulitokea Viti Maalum, uniwie radhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala lake la kwanza kwamba ni kwa nini Serikali haipeleki kwa wakati posho mbalimbali hususan ya *on call*

*allowance,* nimejaribu kufanya ziara katika maeneo mbalimbali, ni kweli posho hii imekuwa ikichelewa, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba itaendelea kutolewa kwa wakati kwa kadri hali ya uchumi itakavyoendelea kuimarika kwa sababu fedha hizo tayari zilishapangwa katika bajeti, kwa hiyo, zitatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na *OC* kupunguzwa, haijapunguzwa kwenye *OC* za Hospitali ya Mrara peke yake, ukiangalia nchi nzima fedha za matumizi mengineyo zilipunguzwa na wote tunajua kabisa, tulikuwa na malengo ya aina gani kama nchi, asilimia zaidi ya 40 imepelekwa katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba watumishi waendelee kuvuta subira, tutakapoenda katika *mid year review,* siwezi kulisemea hili kwa Wizara ya Fedha, tunajua kabisa kila mwaka mwezi Januari au Februari huwa kuna *mid term year review.* Kwa hiyo, hilo niwaachie wao, naamini itakapofika wakati huo, wataona ni maeneo gani yanayoweza kufanyiwa maboresho ili kuweza kuendana na wakati. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu unakwenda sana, tunaendelea. Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 60

**Mlundikano wa Madeni ya Watumishi**

**MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Kumekuwa na mlundikano wa madeni ya watumishi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyalipa madeni hayo?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa hakuna madeni tena?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kupokea na kuhakiki madai ya watumishi wa umma yanayohusu mishahara na kuyalipa kwa kadri ya uwezo wake wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 Serikali ililipa madai ya malimbikizo ya mshahara ya shilingi 56,293,372,627.37 ambayo yalilipwa kwa watumishi 55,688 waliokuwa na madai yaliyotokana na kupandishwa vyeo, ajira mpya na sababu nyinginezo.

Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Serikali imeendelea kulipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2016 watumishi 31,032 walilipwa jumla ya shilingi 28,929,095,373.89.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 7,871 yenye jumla ya shilingi 13,754,462,429.29 tayari yamehakikiwa na yameshaingizwa kwenye mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara na yanasubiri kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya watumishi 8,776 yenye jumla ya shilingi 15,590,586,474.69 yanaendelea kuhakikiwa ili yaweze kuingizwa kwenye mfumo tayari kwa kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shughuli za kila siku madeni huzalishwa, lakini ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba madeni haya yanalipwa mara yanapojitokeza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, niulize maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa kila mwaka mwezi Julai kunakuwa na ongezeko la mshahara, kupanda vyeo ama madaraja kwa watumishi, lakini mpaka sasa Serikali haijafanya chochote.

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa watumishi katika kuhakikisha kwamba hakutakuwa na mlundikano tena wa madai kwa kupandisha mishahara ya watumishi?

Pili, je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha madai haya hayatakuwepo tena? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimhakikishie tu kwamba tunaendelea kulipa madeni haya kwa kadri yanavyojitokeza na kwa kweli ukiangalia tangu mwaka 2013 tulipoanza kutumia mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara, madai haya yamekuwa yakiendelea kupungua kwa nyakati mbalimbali.

Vilevile kwa upande wa madeni yanayotokana na kupandisha mishahara na kwa madeni yanayotokana na upandishwaji wa vyeo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tulishatoa maelekezo kwamba ni lazima madai haya yalipwe kupitia mfumo pindi watu hawa wanapopandishwa vyeo pamoja na madai haya yanapokuwa yamejitokeza ili kuhakikisha kwamba hatuleti milundikano ya madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunakikisha tunakuwa na mkakati endelevu, yapo madai mengine yanatokana na watumishi kuhama, tumeshaelekeza tuhakikishe kwamba mtumishi hahamishiwi kama hakuna fedha za uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai mengine ambayo yamekuwa yakijitokeza kwa wingi ni masuala au madai ya posho ya kukaimu. Tumeshaelekeza pia na yenyewe, pindi barua ya kukaimishwa na marekebisho ya mshahara yanapotoka, basi mtumishi aingiziwe marekebisho hayo mapema na marekebisho ya mshahara yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukishuhudia baadhi ya waajiri wamekuwa hawatengi fedha kwa ajili ya matibabu, likizo na posho zao nyingine, matokeo yake imekuwa inasababisha sasa pindi mtu anapotakiwa kwenda likizo, inaleta madeni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaagiza waajiri wote, wanapokuwa wanapanga bajeti zao za kila mwaka, wahakikishe stahili za msingi na za kisheria na za kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma zinatengwa ili kuhakikisha kwamba hawasababishi madeni, lakini vilevile kuhakikisha tunazingatia haki za msingi za watumishi hao. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 61

### Eneo la *Buhemba Holding Ground* (KABIMITA)

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Eneo la *Buhemba Holding Ground Farm* (KABIMITA) linalomilikiwa na vijiji vitatu vya Magunga, Milwa (Wilaya ya Butiama) na Mekomarino (Wilaya ya Bunda) kwa ajili ya kilimo na ufugaji ambalo lilitolewa na Serikali tangu miaka 1970 na 1980 kama kituo cha kukusanyia mifugo (ng'ombe) na kuwatibu kabla ya kupelekwa kwenye mnada wa ng'ombe Bukoba; na sasa ni miaka 33 eneo hili linatumiwa na wakazi wa vijiji hivyo kwa ajili ya makazi, kilimo na ufugaji.

Je, ni lini Serikali itatoa tamko rasmi kwamba eneo hilo ni mali ya vijiji hivyo kisheria ili kuondoa dhana ya kuwa eneo hili ni mali ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha *Buhemba Holding Ground* chenye ukubwa wa hekta 2,446 kilijengwa mwaka 1949 na Serikali ya kikoloni kwa ajili ya kukagua, kukarantini na kunenepesha ng'ombe, mbuzi na kondoo waliokuwa wanauzwa nchi za jirani. Baada ya uhuru kituo hiki kilikabidhiwa kwa Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya mifugo hadi mwaka 1975 kilipokabidhiwa kwa Kampuni ya Biashara ya Mifugo Tanzania (KABIMITA) ili kitumike kwa karantini na kunenepesha mifugo kwa ajili ya kuchinjwa katika viwanda vilivyokuwa vinamilikiwa na *Tanganyika Packers Limited* vya Arusha na Kawe, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 1980 hadi mwaka 1982, kampuni ya KABIMITA ilikitumia kituo husika kukarantini mitamba ya ng'ombe wa asili kwa ajili ya maandalizi ya kuisafirisha kwenda Uganda kupitia sehemu ya kupakilia mifugo ya Kituo cha *Bweri Holding Ground* cha Musoma Mjini. Mwaka 1984 Kampuni ya KABIMITA ilifutwa na kituo hicho kilihamishiwa kwenye Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1993, Wizara kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* ilianzisha mradi wa uendelezaji wa miundombinu ya masoko ya mifugo ya Tanzania *(Tanzania Livestock Marketing Project)*. Mradi huo uliendeleza kituo hicho kwa kuweka alama za kudumu kwenye mipaka, kujenga ofisi za nyumba na nyumba ya

Meneja wa Kituo, kukarabati nyumba za watumishi na kununua vitendea kazi kwa gharama ya shilingi milioni 104.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya karantini na *Holding Ground* nchini yanalindwa kwa mujibu wa Sheria Namba 17 ya Kuzuia Magonjwa ya Mifugo ya mwaka 2003 na Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006. Maeneo haya ni kwa ajili ya matumizi ya mifugo ya biashara ambayo ni lazima iwekwe chini ya karantini ili kufanya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo kabla ya kuchinja kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeruhusu wananchi kutumia eneo hilo kwa shughuli mbalimbali huku ikiendelea kuwa chini ya umiliki wa Wizara. Hata hivyo, Serikali inatoa rai kwa wananchi kutopanda mazao ya kudumu na kujenga makazi katika eneo hilo pamoja na vituo vingine vya karantini na *Holding Ground* nchini.

Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wabunge muwaelimishe wananchi juu ya umuhimu wa maeneo haya katika ukuaji wa tasnia ya nyama nchini ili mifugo na bidhaa zitokanazo na mifugo ziweze kukubalika katika masoko yenye ushindani kikanda na Kimataifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, je, ni lini Serikali yetu sikivu itafanya tathmini ya hali halisi ya maeneo haya ambayo ukienda kwenye maeneo hayo kuona hali halisi; na kwa bahati nzuri katika eneo hili kwenye Bunge lililopita niliuliza swali na Waziri wa Kilimo enzi hizo, Mheshimiwa Mwigulu na Naibu mwenyewe nashukuru sana kwa kufika kwenye maeneo yangu; hali halisi ya eneo hilo halipo, watu wameshajenga. Sasa je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya hali halisi kujua maeneo haya ambayo wanamiliki hewa kumbe wananchi wote walishakali na kujenga shule za msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutokana na Sheria Namba 17 na Namba 10 alizozitaja Mheshimiwa Naibu Waziri zimechelewa sana kwa wananchi wa Kijiji cha Mikomalilo, kwa sababu walishajenga na kulima mazao ya kudumu. Je, ushauri wake sasa haoni umechelewa sana ili kuwashauri watu walime mazao ambayo siyo ya kudumu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umuhimu na haja ya kufanya tathmini kuangalia hali halisi ya eneo la *Holding Ground* husika, Serikali inafahamu tosha kwamba ndiyo wananchi wamekuwa wakilitumia hilo eneo tokea miaka ya 1980; lakini kwa sasa hata pamoja na kwamba kuna maeneo ambayo yamevamiwa, hata yale ambayo yamebaki bado sisi tunaona kwamba ni muhimu kwa ajili ya matumizi ya Wizara na tusingependa kutumia kigezo cha kwamba kimevamiwa kuruhusu sasa; kwa sababu itamaanisha kwamba katika maeneo mengine wananchi vilevile wanaweza kuvamia.

Kwa hiyo, jitihada iliyopo sasa ni kuangalia namna gani tunaweza kunusuru maeneo yaliyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, tukiruhusu maeneo yote ya Serikali yachukuliwe na wananchi baadaye Serikali ikihitaji maeneo tunaanza tena ugomvi na mgogoro na wananchi kwa sababu Serikali mara kwa mara itahitaji maeneo kwa ajili ya maendeleo ya kiujumla kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu hili la swali la kwanza la nyongeza, vilevile linajibu swali la pili kwamba tamko hili la kusema wananchi wasijenge, halijachelewa. Hata mwaka 1980 waliporuhusiwa, makubaliano ilikuwa ni kwamba wasipande mazao ya muda mrefu na wala wasijenge.

Kwa hiyo, wananchi wamekuwa wakifahamu na ndiyo maana hata Mheshimiwa Mbunge leo analiuliza hili swali wakati anafahamu kwamba huo ndiyo utaratibu uliokuwa ukitumika tokea mwaka 1980.

Kwa hiyo, sisi kama Wizara hatujachelewa, kilichotokea ni kwamba wananchi hawajafuata makubaliano ambayo tuliwekeana tokea eneo hilo lianze kutumika na wananchi mwaka 1980.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, sasa aulize swali lake.

Na. 62

**Kiwanda Kwa Ajili ya Viungo vya Chakula**

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB** aliuliza:-

Baadhi ya wakulima wa Tarafa ya Amani na Muheza wanalima kwa wingi viungo mbalimbali kama pilipili manga, karafuu, hiliki na mdalasini lakini hakuna viwanda kwa ajili ya kusindika mazao hayo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia kupata kiwanda wakulima wa mazao hayo kwa ajili ya mazao yao?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuwatafutia wananchi hao wanunuzi wa uhakika wa mazao hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO)* Mkoa wa Tanga katika mpango kazi wake wa robo mwaka ya pili yaani Oktoba - Disemba, 2016, imeweka mkakati wa kufanya uchambuzi yakinifu *(needs assessment)* kwa wakulima wa viungo vya vyakula mkoani humo wakiwepo wa Tarafa za Amani na Muheza. Lengo la mkakati huo ni kubaini mahitaji mahususi ya wakulima hao yakiwemo ya kiteknolojia na masoko ili kuzipatia ufumbuzi wa kudumu changamoto wanazokabaliana nazo hivi sasa ya kiwanda cha kusindika mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetenga fedha za kuratibu utekelezaji wa mkakati wa kuendeleza mazao ya bustani yakiwemo mazao ya viungo wenye lengo la kuongeza uzalishaji na tija. Vilevile Serikali kupitia Wizara ya Viwanda imekuwa ikitoa teknolojia mbalimbali za usindikaji mazao zikiwemo za mazao ya viungo kwa wakulima wa Mkoa wa Tanga kupitia karakana ya uendelezaji teknolojia *(Technology Development Centre)* iliyopo Arusha ambapo teknolojia za usindikaji mazao yakiwemo ya viungo hutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viungo vinavyozalishwa nchini vina soko la kutosha ndani na nje ya nchi hususani katika nchi za Uturuki, India na Uarabuni. Changamoto ni namna ya kulifikia soko hilo katika viwango na ubora unaotakiwa. Katika Wilaya ya Muheza kuna Makampuni kadhaa yanayonunua viungo na kati ya hayo ni Jumuiya ya Wakulima wa Kilimo Hai Usambara Mashariki (JUWAKIHUMA), *Golden Food Product* na *TAZOP*.

Hivyo, Serikali inaandaa mkakati wa kutoa elimu juu ya mbinu bora za uzalishaji wa viungo ili kuinua ubora wa viungo pamoja na mavuno kwa eneo hili kukidhi mahitaji ya makampuni yanayonunua na kuuza viungo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la *SIDO* imekuwa ikiwashirikisha wakulima katika maonesho kwa nia ya kujifunza na kupata masoko. Mathalan kwa mwaka 2015/2016, wakulima wa viungo kutoka Tarafa za Amani na Muheza ni miongoni mwa washiriki wa maonesho ya *SIDO* Kanda ya Mashariki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Adadi Rajab, swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, ni kweli kabisa kwamba viungo vina soko kubwa ndani na nje ya nchi kwa sababu mimi mwenyewe naona jinsi hawa wanunuzi wa kutoka nje wanavyohangaika wakati wa msimu pale Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, ni lini Wizara itawapeleka wataalam hao kuhakikisha kwamba wanainua ubora wa wakulima hao waweze kujua namna ya kulima vizuri pamoja na kuhifadhi mazao hayo ambayo wanayazagaza nje nje tu?

La pili, kama ambavyo Wizara imesema kwamba imetenga fedha za kusaidia bustani pamoja na wakulima wa hivi viungo, mna uhakika gani kwamba wakulima wangu wa Amani na Muheza fedha hizo ambazo zimetengwa watazipata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni lini wataalam wa Wizara wataenda kushirikiana na wakulima katika Jimbo lake ili kuweza kuwa na kilimo cha tija, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa kutoa taaluma na uelewa kwa wakulima ni utaratibu ambao ni endelevu kupitia Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba kuna changamoto ndiyo zinawakabili, lakini katika bajeti yetu na ile ya TAMISEMI zimetengwa fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Maafisa Ugani wanafanya kazi na kuweza kuwafikia wakulima ili waweze kuzalisha kwa tija zaidi.

Vilevile labda nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu Pemba tuna kiwanda kizuri sana ambacho kinachakata viungo, tutashirikiana na Halmashauri ili kuona namna gani wakulima wanaweza vilevile wakaendelea kutembelea kiwanda hicho na kujifunza kinachofanyika ili pamoja na kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, tuangalie ni namna

gani tunaweza vile vile kuwa na kiwanda kinachoweza kuchakata viungo ili tufikie ufanisi kama walivyofikia wenzetu kutoka Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwamba tutafanya vipi kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa zinawafikia wakulima; nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inatembea katika ahadi zake. Kwa hiyo, yale yote ambayo tumepanga na kutenga kwa ajili ya wakulima wetu, tutahakikisha kwamba tunafuatilia ili ziweze kuwafikia bila kupotea.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando, sasa aulize swali lake.

Na. 63

**Kutochanganya Dini na Siasa**

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI** aliuliza:-

Kwa kuzingatia usalama na utulivu wa nchi yetu, viongozi wa Serikali wamekuwa wakitoa kauli zenye msisitizo kwa wananchi kuepuka kuhubiri siasa katika nyumba za ibada na kuchanganya dini na siasa katika mikutano.

Je, ni kifungu gani cha Katiba au Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambacho kinafafanua juu ya kauli hizo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaeleza katika utangulizi wake kuwa Tanzania inaongozwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia, ujamaa na isiyokuwa na dini.

Aidha, Ibara ya 3(1) ya Katiba hiyo hiyo inaeleza kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa isiyokuwa na dini na yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Ibara ya 19(1), (2) na (3) inaeleza kuwa kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ibara ya 3(2) inaeleza kuwa mambo yote yanayohusu uandikishaji na uendeshaji wa vyama vya siasa nchini yatasimamiwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba na sheria iliyotungwa na

Bunge kwa ajili hiyo. Hivyo basi, sheria ya vyama vya siasa Sura ya 258 inaeleza bayana katika kifungu cha 9(2) kuwa chama cha siasa, hakitastahili kusajiliwa endapo katiba yake au sera zake zina mwelekeo wa kuendeleza maslahi ya imani ya kidini au kundi la kidini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Othman Haji, swali la nyongeza.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo itatokea kiongozi wa Umma atazungumzia masuala ya kisiasa ndani ya nyumba ya ibada; je, ni kifungu gani cha katiba au sheria kinachoweza kumtia hatiani kiongozi huyu? *(Makofi)*

Swali la pili, iwapo katika matamshi yake aliyoyazungumza katika nyumba hiyo inakwaza jamii moja katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania.

Je, ni adhabu gani amestahiki Kiongozi kama huyu? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilishaeleza katika jibu langu la swali la msingi kwamba mtu yeyote ambaye atafanya kinyume na ambacho Katiba inaelekeza na vilevile sheria, atakuwa amefanya makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize tu hapa kwamba, Katiba ya nchi ndiyo inayozaa sheria. Kwa hiyo, siyo siyo tu mtu, hata chama cha siasa ambacho kinaendekeza masuala ya kidini nacho kinakuwa kimekosea, lakini siyo suala la mtu mmoja kuamua kuwa umekosea, kuna utaratibu wa kuweza kulifikisha hilo suala mbele ya Msajili wa Vyama vya Siasa na hatua za kisheria kuweza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo kwa viongozi wa Kiserikali, anaingia kwenye Kanisa au Msikitini, siyo Serikali iweze yenyewe kuwa kila sehemu, lakini ijengwe hoja na wananchi ambao wamefika pale na huko ndiko kulinda utawala wa sheria katika nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 64

**Kutungwa kwa Sheria ya Kutambua Haki ya Msaada wa Kisheria**

**MHE. FATMA HASSAN TOUFIQ** aliuliza:-

Sheria ya Kutambua Haki ya Msaada wa Kisheria *(Legal Aid)* ambayo pia inawatambua wasaidizi wa kisheria *(paralegals)* mchakato wake umeanza tangu mwaka 2010 kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo taasisi zisizo za Kiserikali, lakini sheria hii imekuwa ni ya muda mrefu na sasa ni zaidi ya miaka sita bado haijatajwa wala kuletwa Bungeni.

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuhakikisha sheria hii inatungwa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha hatua zote za awali za kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria katika Bunge lako Tukufu. Muswada huo unalenga kuweka utaratibu wa kisheria wa kuratibu huduma ya msaada wa kisheria nchini na kuwatambua Wasaidizi wa Kisheria waliokidhi vigezo mahususi vya ujuzi katika utoaji huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali baada ya kutungwa kwa sheria hii ni kuhakikisha huduma ya msaada wa kisheria inapatikana nchi nzima hususani kwa wananchi walio vijijini na ambao hawana uwezo wa kumudu gharama za Mawakili ambao wengi wao wanaishi na kufanya shughuli za mijini tu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA HASSAN TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imeshakamilisha hatua za kuwasilisha muswada huu, je, ni lini muswada huu utawasilishwa Bungeni?

Swali la pili, je, Serikali ina mpango wowote wa kuandaa mtaala wa Wasaidizi wa Kisheria ili wote waweze kupata mafunzo kulingana na mtaala huo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Fatma Toufiq kwa maswali yanayogusa wananchi wa kawaida na hili suala kwa kweli hata sisi kama Wizara tunaona ni muhimu na ndiyo maana tumelifuatilia kwa karibu na Serikali imeridhia tuweze kuja na muswada huo ambao utajadiliwa na Bunge.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya taratibu kukamilika, muswada huu hautakuja moja kwa moja Bungeni hapa lakini utapitia katika Kamati, pia tutakuwa na mjadala wa muda mrefu kabla ya kuja na *text* ambayo Waheshimiwa Wabunge mtakuja kuijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maandalizi ya kutosha tumeyafanya, kwa mfano, sasa hivi tuna mitaala kabisa iliyowekwa kwa ajili ya kuwafundisha hawa Wasaidizi wa Sheria. Ni kazi kubwa imefanywa na Chama cha Wanasheria Tanganyika na ninaomba nimhakikishie tu kwamba tumejiandaa vizuri sana kubeba hili jukumu.

Tunasema hivyo kwa sababu Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaongelea kuhusu usawa mbele ya sheria. Tunaamini Muswada huu unatupeleka Watanzania karibu zaidi katika kukidhi mahitaji ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ili uwepo usawa wa kutosha kabisa mbele ya sheria.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Almasi Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 65

**Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria Hadi Tabora**

**MHE. ALMASI A. MAIGE** aliuliza:-

Sehemu kubwa ya Jimbo la Tabora Kaskazini, Uyui halina maji chini ya ardhi na hivyo wananchi hawawezi kupata maji kwa kuchimba visima, hivyo Serikali ikabuni mradi wa kuleta maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria kupitia Shinyanga, Kahama, Nzega mpaka Isikizya na maeneo mengine ya Mkoa wa Tabora.

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi huo ili wananchi wa Jimbo la Tabora Kaskazini katika vijiji vya Isikizya, Upuge, Majengo na Kanyenye wapate huduma ya maji?

(b) Kwa kuwa bomba hilo la maji litatoa maji umbali wa kilometa 25 kushoto na kulia na kuwafikia wananchi wachache; je, Serikali haioni kuna sababu ya kuanzisha mradi wa kuchimba mabwawa na kukinga maji ya mvua kama chanzo kingine cha maji kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka katika Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Sikonge pamoja na vijiji 89 vilivyopo ndani ya kilometa 12 kwa kila upande kutoka bomba kuu. Kwa sasa taratibu za kupata wakandarasi wa ujenzi wa mradi huo zinaendelea ambapo ujenzi wa mradi unategemewa kuanza mwezi Disemba, mwaka huu wa 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, bomba kuu la kutoa maji Ziwa Victoria litahudumia vijiji vilivyopo ndani ya kilometa 12 kila upande. Aidha, Serikali itaendelea kubuni vyanzo vingine vya maji ikiwemo ujenzi wa mabwawa ya uvunaji maji ya mvua na uchimbaji wa visima virefu ambapo katika mwaka wa fedha 2016/2017 imetenga kiasi cha shilingi milioni 754.4 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika vijiji vya Halmashauri ya Uyui.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa vile Serikali imebuni mradi huo ambao utatusaidia sana sisi Wana-Uyui hasa Tabora Kaskazini, je, Serikali sasa iko tayari kuviorodhesha vijiji ambavyo vitakuwa katika mradi huo ili vijiji ambavyo havitakuwa ndani ya mradi tuvishughulikie kuvipatia maji?

Swali la pili kuhusu mradi wa Malambo ya maji, je, Serikali sasa iko tayari kutoa ahadi kwamba iko tayari kuanza utafiti wa wapi malambo hayo yatachimbwa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na swali la pili kuhusu mpango wa Serikali kujenga mabwawa, kwanza

naomba nitoe taarifa kwamba kulingana na *survey* ambayo tumeifanya, tuna mabwawa 3,000 ambayo yameshajengwa hapa nchini kwetu. Katika hayo, asilimia 50 yanafanya kazi na asilimia 50 hayafanyi kazi.

Kwa hiyo, mpango tulionao ni kuhakikisha kwamba haya asilimia 50 ambayo hayafanyi kazi tunayafanyia ukarabati. Pamoja na hiyo, Bunge la Bajeti lililopita tulielekeza kila Halmashauri wahakikishe kila mwaka wanasanifu bwawa moja na wanaleta ili tuweze kutenga fedha kuhakikisha kwamba kila Halmashauri kila mwaka inajenga bwawa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuhusu ni vijiji gani ambavyo vimeainishwa kwenye huu Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria kupeleka Tabora? Maeneo yatakayopitiwa na mradi huu ni pamoja na Kata ya Upuge; ambayo ni Kijiji cha Upugwe, Muhogwe, Lungunya na Kasenga vitapata maji.

Kata ya Magiri ambayo ni kijiji cha Magiri, Imalampaka, Kalemela vitapata maji. Kata ya Isikizya; ambapo kijiji cha Ilalwasimba, Isikizya, Igoko, Ibushi vitapata maji. Kata ya Ibelamailundi; kijiji cha Ibelamailundi, Mtakuja, Itobela, Isenegeja vitapata maji na pia Kata ya Ilolangulu; ambapo Kijiji cha Kasisi 'A,' Ngokolo na Isenga vinatarajiwa kupata maji kupitia katika mradi huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Susan Peter Maselle Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 66

**Askari Wanaowabambikizia Watu Kesi**

**MHE. SUSANNE P. MASELLE** aliuliza:-

(a) Je, Serikali imechukua juhudi gani za makusudi kudhibiti vitendo vya kubambikizia watu kesi vinavyofanywa na baadhi ya askari wasiokuwa na maadili?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuanzisha kitengo cha siri ndani ya Jeshi la Polisi kitakachoshughulikia adha hii?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susanne Maselle, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni, miongozo pamoja na taratibu na wale wanaobainika kukiuka maadili ya Jeshi, huchukuliwa hatua kwa kuwashitaki kijeshi kwa mujibu wa *PGO* 103 na 104 kwa kuwapa adhabu mbalimbali ikiwepo kuwafukuza kazi anaobainika kukiuka maadili ya Jeshi ikiwemo kubambikia watu kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imefanya jitihada za kuanzisha Kitengo cha Malalamiko katika ngazi ya Makao Makuu, Mikoa na hata Wizara ili kutoa mwanya kwa mtu yeyote anayeona kuwa ameonewa, kuwasilisha malalamiko yake na malalamiko hayo kushughulikiwa. Hata hivyo, raia wanayo haki ya kulalamika katika vyombo vingine vya kisheria wanapoona hawatendewi haki kwa mujibu wa sheria za nchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limeweka wazi utaratibu wa namna ya kuwashughulikia askari wasio waaminifu, hivyo halitakuwa tayari kuanzisha kitengo cha siri kwa kazi hiyo kwani utaratibu uliopo unashuhudia na umekuwa na mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, siku za usoni kama hivyo ilivyo kwa mikoa michache hapa nchini ambapo kazi ya polisi itabaki kuwa ni ya kupeleleza kesi na mwenye mamlaka ya kupeleka kesi mahakamani ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susanne Maselle, swali la nyongeza.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika,Serikali inatoa kauli gani kwa Jeshi la Polisi kupitia askari wasio waadilifu wanaokamata watu hasa viongozi na wafuasi wa UKAWA na kuwaweka mahabusu kwa zaidi ya saa 24 bila kuwapeleka mahakamani wakijua kwamba wanavunja sheria kwa kuwabambikizia kesi za uchochezi na *CyberCrime?* Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linapokamata watu huwa haliangalii itikadi zao na linapowafikisha watu mahakamani haliwaulizi kadi ya chama alichonacho, bali Jeshi la Polisi hukamata watu kufuatana na kosa alilofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa Watanzania wengine, akishakamatwa, kuna hatua ambazo zinafanyika na baada ya hapo anafikishwa mahakamani. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea!

Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 67

**Gereza la Ilagala Kuhodhi Eneo Kubwa la Shamba**

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA** aliuliza:-

Gereza la Ilagala limehodhi eneo kubwa la shamba na kufanya wananchi wa Kata ya Ilagala kukosa maeneo ya kulima.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa sehemu ya eneo kwa ajili ya wananchi wa Ilagala ili na wao waweze kupata maeneo ya kulima?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Ilagala ni gereza la kilimo na mifugo ambapo linamiliki jumla ya ekari 10,760 na kati ya ekari hizo, ekari 4,500 ziko katika milima na mabonde ambapo zimehifadhiwa kwani ni vyanzo vya mito katika eneo hilo. Ekari 3,000 zimetengwa na zinatumika kwa ajili ya ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo; na ekari 5,000 kwa ajili ya makazi na ekari 2,760 ni kwa ajili ya kilimo cha mazao ya mahindi; mahindi ya mbegu, michikichi, mihogo, mbaazi, mboga pamoja na matunda. Hata hivyo, pamoja na shughuli tajwa hapo juu, eneo hilo bado halitoshelezi kwa ajili ya mahitaji yaliyokusudiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasna Mwilima swali la nyongeza.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nitake tu kumhakikishia kuwa eneo hilo la ekari 10,760 na hizo ekari 5,760 ambazo yeye amezitolea majibu kwamba zinatumika kwa ajili ya mifugo na kilimo, nimhakikishie tu kwamba eneo kubwa halijaendelezwa kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna zadi ya ekari 4,500 hazijaendelezwa kwenye kitu chochote. Gereza hawajalima wala hawana mifugo. Wananchi wa vijiji vitatu, kijiji cha Kabeba, Ilagala na Sambala hawana maeneo ya kulima na

historia inaonesha walichukua zaidi ya ekari 4,000 bila makubaliano na vijiji hivi vitatu.

Swali langu je, ni kwanini Mheshimiwa Waziri asielekeze gereza litoe angalau ekari 1,500 ili na hawa wananchi wa Jijiji vitatu wapate maeneo ya kulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kumekuwa na tabia ya baadhi ya Maafisa Magereza kuwakamata wananchi wa vijiji hivi vitatu kuwapiga, kuwanyang'anya zana zao za kilimo, lakini pia kuwafungulia kesi na kuwapeleka mahakamani. Je, Mheshimiwa Waziri, kama Serikali anatoa tamko gani kwa wananchi wa vijiji hivyo vitatu ambao wamekuwa *harassed* na Maafisa wa Gereza la Ilagala? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Hasna Mwilima kwa jinsi anavyofuatilia mambo ambayo wananchi wake wamemtuma na kwa kweli yeye ni Mbunge makini, hata juzi nilipita kule wakasema hata uchaguzi ungefanyika leo, angeshinda kwa kiwango kikubwa kuliko kilichopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwenye suala hili alilolisemea, ni kweli kuna ekari ambazo hazijaendelezwa, lakini kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, zile zilizoachwa ni zile ambazo zimewekwa kwa sababu ziko kwenye chanzo cha maji ambayo yanatumika siyo tu kwa gereza, yanatumika hata kwa wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wa malengo mapana ya taasisi zetu hizi za magereza ni hasara kuwa na wafungwa wanaolishwa kwa kodi za walipakodi halafu wakawa hawana kazi ya kufanya. Kwa hiyo, hicho tunachosema hata eneo lile lililopo halijatosheleza tunamaanisha malengo marefu ya kuweza kuwatumia wafungwa wanaoweza kufanya kazi ikiwa ni sehemu ya kuwarekebisha ili magereza yetu yaweze kujiendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu tamko la Serikali kwa wale wananchi ambao wananyang'anywa vifaa; moja niseme Serikali ya Wilaya ambako ndiko na Jimbo lilipo ni vizuri wakapanga matumizi bora ya ardhi na wanaweza hata wakawasiliana na Wizara ya Ardhi ili kuwatafutia wananchi maeneo mbadala ya kufanya kazi hizo ili wasiingie bila ruhusa katika maeneo ya Magereza na hivyo kusababisha mgongano huu ambao unasababisha wao kukamatwa. Lakini maeneo yote ambayo yana Magereza, tunaendelea kuhimiza mahusiano bora kati ya Taasisi hizo za Serikali pamoja na wananchi wanaozunguka maeneo husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 68

**Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** aliuliza:-

Baada ya ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya *FDC* – Njombe na kile cha Ulebwe kilichopo Wanging'ombe.

(a) Je, ni fani zipi zitaanza kutolewa katika vyuo hivyo?

(b) Je, ni wananchi wangapi wanatarajia kufaidika na vyuo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDC)* Njombe na kile cha Ulebwe kilichopo Wanging'ombe, Serikali itaendelea kuimarisha na kutoa mafunzo yale yale yaliyokuwa yanatolewa hapo awali, yaani mafunzo ya ufundi stadi katika fani za ufundi magari, ufundi chuma, useremala, uashi, umeme wa majumbani, ushonaji, kilimo na mifugo katika Chuo cha Njombe na fani za useremala, ushonaji, uashi, umeme wa majumbani, kilimo na mifugo katika Chuo cha Ulebwe.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na uwezo na vyuo hivyo, Chuo cha Mendeleo ya Wananchi Njombe kina uwezo wa kunufaisha wananchi 180 wa kukaa bweni na wananchi 70 wa kutwa, wakati Chuo cha Wananchi Ulebwe kina uwezo wa kunufaisha wananchi 80 wa kukaa bweni na 40 wa kutwa na hivyo kufanya jumla ya wananchi wanufaika 370 kwa mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward Mwalongo, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ulebwe ni chuo ambacho kina eneo linalozidi hekta 94 na kwa sasa hivi ninavyoongea, kina wanafunzi 64 tu.

Je, Serikali haioni kwamba sasa kutokana na mazingira mazuri ya Ulebwe kuna ulazima wa kubadilisha mifumo katika chuo kile na kuimarisha fani za kilimo na mifugo ili kusudi vijana wa Njombe waweze kunufaika na chuo kile? *(Makofi)*

Swali la pili, vijana wengi wamekuwa hawasomi hivi vyuo kwa sababu ya mfumo wanautumia kufundishia ambao ni wa *VETA* ambao sasa unatumia zaidi lugha ya Kiingereza katika mitaala pamoja na mafunzo yote na vijana wengi hawana uwezo wa lugha hiyo ya Kiingereza; je, Serikali iko tayari kuandaa mitaala ya Kiswahili ili iweze kuwasaidia vijana wadogo wanaomaliza elimu ya msingi na sekondari waweze kunufaika na haya mafunzo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kubadilisha mafunzo katika chuo hicho, napenda tu kumfahamisha Mheshimiwa Mwalongo kwamba kwa mujibu wa Katiba yetu kifungu cha 9(i) kinazungumzia kwamba utajiri wa nchi na rasilimali utaelekezwa zaidi katika kuhakikisha kwamba unatoa umaskini, maradhi na ujinga katika maeneo yetu yote. Vilevile inaendelea kwa kusema kwamba haki ya kupata mafunzo au elimu ni ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo hivi vya *FDC* vilianzishwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba wananchi wote hata wale ambao hawajafika kidato cha nne au darasa la saba wanapata mafunzo na kuweza kuwasaidia kukimu katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni mtazamo wangu kuona kwamba vyuo hivyo viimarishwe ili kuweza kutoa mafunzo kwa wananchi wengi zaidi ambao bado tunao katika maeneo yote. Sio wote kwamba wamefika darasa la saba au kidato cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile suala la kufanya mafunzo haya lazima yafanane na *VETA,* Wizara inaona kwamba iko haja ya kuona kwamba mafunzo yanayotolewa katika vyuo hivi vya *FDC* yanakidhi uwezo wa wananchi hao kuweza kuyatumia kikamilifu kwenye kazi zao na hivyo siyo lazima yafundishwe kama ilivyo Vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo, naona kwamba kwa siku za nyuma kulitokea na mkanganyiko kidogo wa kuona kwamba Vyuo vya *VETA* ni bora kuliko *FDCs,* lakini tungependa kuona kwamba *FDCs* zifanye kazi kwa malengo yake na *VETA* zifanye kazi kwa malengo yake, lakini vyuo vyote viimarishwe na kuweza kutoa mafunzo stahiki kwa walengwa wanaohusika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 69

**Kufungua Ubalozi Sudan Kusini**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Sudan Kusini imekubaliwa kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Je, ni lini Serikali itafungua Ubalozi katika nchi hiyo ili kutengeneza mazingira ya kunufaika na fursa zilizoko katika nchi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa la Sudan Kusini lilianzishwa mwezi Julai, 2011 baada ya kura za maoni za wananchi wa nchi hiyo kuamua kujitenga kutoka nchi ya Sudan na kuunda Taifa jipya ya Sudan Kusini. Aidha, mwezi Aprili, 2016 nchi ya Sudan Kusini ilijiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa sasa Tanzania haina Ofisi za Ubalozi nchini Sudan Kusini. Katika kipindi hiki ambacho Serikali haijafungua Ubalozi nchini Sudan Kusini, shughuli za Kibalozi kwa nchi hiyo zinafanywa na Ubalozi wetu, Nairobi nchini Kenya.

Malengo ya Wizara kwa mwaka 2016/2017 ni pamoja na kuongeza uwakilishi wetu nje ya nchi kwa kufungua Balozi mpya na Ofisi za Kikonseli hususan katika nchi ambazo Taifa linanufaika zaidi na fursa za kiuchumi kama vile soko la bidhaa zetu, biashara, uwekezaji, ajira pamoja na utalii.

Aidha, naomba ieleweke kuwa licha ya kuwepo kwa fursa hizo, maamuzi ya kufungua Ofisi za Ubalozi nchini Sudan Kusini pamoja na uendeshaji wa shughuli za Ofisi za Ubalozi zitakazofunguliwa zitategemea na Serikali itakapokuwa tayari Kibajeti.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu imeeleza kwamba kufunguliwa kwa Ubalozi kutategemea masuala ya kibajeti; je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kufungua ile tunaita *Honorary Consul* kwa sababu ile haina gharama zozote ambazo Serikali itaingia zaidi ya kupata tu mtu ambaye ni mwaminifu na mwadilifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kufungua *Honorary Consuel* ambapo siyo suala lenye gharama kibajeti kama ambavyo Serikali imejibu katika swali la msingi, ni jambo la msingi kwa sababu litawezesha kufungua fursa zaidi za kiuwekezaji siyo tu katika Sudan ya Kusini, lakini pia katika maeneo mengine ambako Serikali imeshindwa kufungua Balozi kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kufungua fursa hizi za uwakilishi wa heshima, tunapanua wigo wa kuongeza uwekezaji na biashara na hivyo kuongeza mapato ya Serikali ambayo mwisho wa siku wananchi wa Mafinga na Tanzania kwa ujumla watanufaika katika kuboresha huduma zao za kijamii. *(Makofi)*

Je, Serikali iko tayari pia sasa kufungua Uwakilishi wa Heshima katika Mji wa Lubumbashi ambako kuna fursa kubwa za kibiashara baina yetu sisi Tanzania na nchi ya Demokrasia ya Kongo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba kufungua Uwakilishi wa Heshima ni njia mojawapo ya kuwa na uwakilishi wa nchi yetu katika nchi nyingine, lakini vilevile kuna utaratibu wa Kikonseli lakini na ule utaratibu wa kawaida wa kufungua Ubalozi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo ni kati ya njia ambazo tungeweza kutumia nchini Sudan Kusini, lakini kwa sasa Wizara inafikiria zaidi kujipanga kufungua

Ubalozi kamili badala ya kufungua *Consul* au kutafuta Uwakilishi wa Heshima. Hii ni kwa sababu nchi ya Sudan Kusini ni moja kati ya wanachama wa Jumuya yetu ya Afrika Mashariki, kwa hiyo, ningependa kuwa na Ubalozi kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati bado tunaelekea kule, tunajipanga, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kitendo cha nchi ya Sudan Kusini kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki inatoa fursa nyingi sana na inarahisisha wananchi kuweza kunufaika na fursa zilizoko kule hata bila kuwepo na Ubalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaruhusu pamoja na mambo mengine urahisi wa kusafirisha bidhaa, lakini vilevile huduma na kazi kwenye hizi ambazo ni wanachama.

Kwa hiyo, tayari kuna mazingira mazuri ambayo yanarahisisha wananchi kuweza kunufaika na hizo fursa hata bila kuwa na uwakilishi wa kiheshima bila kuwa na *Consul* au kuwa na Ubalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema Wizara inajipanga, tunatambua umuhimu wa Sudan Kusini kama wanachama wa Afrika ya Mashariki, tunatambua fursa lakini huko ndiyo tunaelekea, lakini tunajipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Mbunge amezungumzia kuhusu kufungua Uwakilishi wa Kiheshima Lubumbashi. Napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kweli kabisa tunatambua fursa zilizopo Lubumbashi, tunafahamu fursa zilizopo katika ukanda huo wa *DRC,* lakini kwa sasa Serikali na Wizara imejielekeza zaidi katika kuimarisha shughuli za Kibalozi kwa sababu tunafikiri bado inakidhi matakwa hayo ya fursa zilizopo, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimishiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 70

**Ujenzi/Ukarabati wa Ofisi za Ubalozi**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Ofisi nyingi za Balozi zetu katika nchi mbalimbali zimekodishwa. Aidha, ofisi nyingine ujenzi haujakamilika au hazijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu sasa na ofisi nyingine zina madeni makubwa.

(a) Je, ni lini ujenzi wa baadhi ya ofisi za Ubalozi zitakamilika ikiwemo ya Msumbiji?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati ofisi chache za Ubalozi zilizopo pamoja na kununua samani mpya?

(c) Je, kwa nini Serikali isilipe madeni ya Balozi zetu kwa wakati ili kuepusha aibu kwa Taifa?

**NAIBU WAZIRI KILIMO, MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa ofisi na makazi ya Balozi zetu umekuwa ukitekelezwa kwa awamu kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha za bajeti ya maendeleo. Mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilipanga kutekeleza miradi ya ujenzi katika Balozi zake ikiwemo Maputo, Nairobi na Stockholm na uboreshaji wa mifumo ya mawasiliano kati ya Balozi na Makao Makuu wa Wizara. Mradi wa Maputo umepangiwa shilingi 1,316,435,000. Tunategemea utekelezaji wa mradi huu ufanyike pale Wizara itakapopokea fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa fedha za bajeti ya maendeleo hazikidhi mahitaji, Wizara inaendelea kushirikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama vile Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* na Taasisi ya Miradi ya Maendeleo ya Miundombinu katika ujenzi wa majengo ya ofisi na vitega uchumi katika Balozi zetu. Wizara inaamini uamuzi wa kuishirikisha mifuko hiyo itaongeza kasi ya ujenzi wa majengo ya ofisi katika Balozi zetu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Wizara uliopo hizi sasa katika kukarabati majengo ya ofisi yaliyopo kwenye Balozi zetu ni kuendelea kuiomba Serikali kutenga fedha za bajeti ya maendeleo; pili, kuelekeza Balozi zetu kutumia utaratibu wa karadha *(mortgage finance)* ili kuwezesha Balozi kupata fedha za ukarabati, kununua na kujenga majengo ya ofisi na vitega uchumi; na tatu, kuishirikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iliyopo nchini kutekeleza miradi ya Wizara Balozini kwa Wizara kuingia makubaliano na vyombo hivyo. Aidha, Wizara itaendelea na utaratibu wa kununua kwa awamu samani mpya za ofisi kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika nyakati tofauti imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya Balozi zake nje. Serikali ilitoa kiasi cha shilingi 7,315,720,301.84 kulipa madeni ya Wizara yaliyohakikiwa na Wakaguzi wa Hesabu. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 deni lililobaki ni shilingi 15,540,603,526. Madeni haya yameanza kukaguliwa na Hazina, hivyo ni matarajio yetu kuwa baada ya kukamilika kwa ukaguzi huo, Hazina itatoa fedha za kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Hazina imetoa mwongozo unaoelekeza kuandaa mpango wa bajeti ambao unaelekeza madeni yote ya Wizara, Wakala na Taasisi za Serikali kulipwa moja kwa moja na Hazina.

**NABU SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka swali la nyongeza

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

La kwanza, kumekuwa na utaratibu wa Watanzania wanaofariki nje ya nchi, ndugu zao wanaokuwepo hapa nchini hupata taabu, adha na kucheleweshwa kuletewa maiti. Inafikia familia za kimaskini zinauza hata vitu vyake ili kuweza kuleta ile maiti nchini. Je, ofisi za Ubalozi zimejipanga vipi kuhakikisha Watanzania wenye hali duni maiti zao zinapopatikana kule ziletwe nchini haraka? *(Makofi)*

Swali la pili, kuna baadhi ya Balozi zina utaratibu wa kupanga siku maalum za kuwahudumia Watanzania, hususan tabia hiyo ilikuwepo katika Ubalozi wetu wa Afrika Kusini. Tabia ile ilileta matatizo na usumbufu kwa Watanzania ambao wanataka huduma katika ofisi za Ubalozi.

Je, sasa hivi wamejipanga vipi kuhakikisha Watanzania wanaotaka huduma kwenye Balozi zao nje ya nchi yetu wanapata huduma haraka? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**NAIBU WAZIRI KILIMO, MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba kwa nyakati tofauti kumeripotiwa baadhi ya Watanzania ambao wamefiwa na ndugu zao kupata taabu katika kusafirisha miili, lakini katika hali ya jumla Balozi zimekuwa zikisaidia sana pale wanapopata taarifa sahihi kwa wakati.

Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge kwamba mara nyingine ucheleweshaji unatokea kutokana na Balozi zetu kuweza kupata taarifa kwa wakati, lakini katika hali ya jumla, kati ya masuala ambayo Balozi wetu zinatakiwa zishughulikie ni kuhusu maslahi ya Watanzania wanaoishi huko ikiwa ni pamoja na pale wanapopata taabu, wanapopatwa na matatizo ikiwa ni pamoja na kifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna changamoto ambazo zimetokea, kila wakati Wizara imekuwa ikichukua changamoto hizo na kuzifanyia. Kwa hiyo, tunaamini huko mbele tunakoelekea, changomoto hizi zitaendelea kupungua na hasa sasa katika Serikali ya Awamu ya Tano ambayo imejikita katika kuleta ufanisi na nidhamu katika utumishi wa umma. Kwa hiyo, tunaamini upungufu na changamoto ambazo zimekuwa zikitokea nyuma, zitapungua kama siyo kuondoka moja kwa moja.

Ni rai ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu Balozi zetu kupanga siku maalum kwa ajili ya kuwatumikia na kutoa huduma kwa Watanzania, pendekezo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri, Wizara italiangalia, lakini ifahamike kwamba hakujaripotiwa kwa kiwango kikubwa kuhusu Watanzania kushindwa kupata huduma za kibalozi, lakini kama nilivyosema tutalipeleka na kuliangalia na iwe ni moja kati ya njia za kususluhisha changamoto ambazo zinatokea.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nilete kwenu wageni waliotufikia asubuhi hii.

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge na wa kwanza ni mgeni mmoja wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, ambaye ni mpiga kura wake kutoka Busanda Mkoani Geita, huyu ni Ndugu Julius Zabron. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 29 wa Mheshimiwa John Kadutu ambao ni wanakwaya wa Nyakato Moravian kutoka Jijini Mwanza wakiongozwa na Mwenyekiti wa kwaya hiyo, Ndugu Benson Mwaipaja. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambao ni Waandishi wa Habari kutoka Redio Kwizera ilipo Ngara Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni mmoja wa Mheshimiwa Angelina Malembeka, ambaye ni Diwani wa Kata ya Pugu Stesheni, Jimbo la Ukonga Dar es Salaam; na huyu ni Mheshimiwa Yohana Ng'ong'a. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 18 wa Mheshimiwa Mendrad Kigola, ambao ni Madiwani 21 na viongozi watano wa CCM kutoka Mufindi, Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Pia tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Oscar Mukasa, ambao ni wawekezaji kutoka Kampuni ya *Profile Africa Limited*. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Devotha Minja, ambao ni wapiga kura wake kutoka Msowelo Kilosa, Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni mmoja wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, ambaye ni kaka yake kutoka Karagwe Mkoani Kagera, anayeitwa Medard Birusya. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na hao ni wanafunzi 60 na walimu nane kutoka Shule ya Msingi Maria De Matius iliyopo Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi watatu kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, *campus* ya Mbeya. Karibuni sana wageni wetu mliotutembelea leo Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine linalotoka kwa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji; anawatangazia kikao cha Kamati ambacho kitafanyika leo tarehe 13 Septemba, 2016 saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa 'C'. Wajumbe wa Kamati hii mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine limenifikia sasa hivi ni la kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ambalo linasema tayari wamekamilisha kazi ya utengenezaji wa vitambulisho vya Taifa na wapo hapa Bungeni kwa ajili ya zoezi la ugawaji wa vitambulisho hivyo. Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote ambao mliweza kujisajili na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, mnaombwa mfike kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa katika chumba kilichokuwa kinatumika kama zahanati ili mpatiwe vitambulisho vyenu.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge ambao hamkuwahi kujisajili, mnaombwa mfike katika ukumbi huo kwa ajili ya usajili ili pia muweze kupatiwa vitambulisho.

Waheshimiwa Wabunge, jambo moja kwa ajili ya kukumbushana kuhusu maswali; maswali tunayoyauliza yanapelekea majibu kuwa marefu sana na hivyo kutukosesha sisi wenyewe nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa sababu hiyo, kwa sababu kanuni zinataka Waziri aliyeulizwa swali ajibu kwa kikamilifu, inaleta taabu sana kwa mtu anayekuwa amekaa hapa kuendesha

kikao kwa sababu inabidi amruhusu mtu yule tu mwenye maswali yake ndiyo muda wetu unakuwa umeenda sawa sawa na kanuni.

Kwa sababu hiyo, ni rai yangu kwenu kwamba maswali tunayoyauliza kwa sababu fursa zipo za kuuliza nyakati nyingi, tuulize maswali mafupi na naiomba Serikali ilete majibu mafupi ili Wabunge wengi wapate fursa ya kuuliza katika maeneo hayo ambayo yanazungumziwa humu Bungeni. Tusipofanya hivyo, maana yake kila Mbunge na swali lake atajibiwa yeye peke yake bila Mbunge mwingine mwenye tatizo kama hilo pia kuweza kusikilizwa na Waziri na kupatiwa jibu.

Kwa hiyo, nawakumbusha tu kwa sababu mnaendelea kupeleka maswali kwa vikao vijavyo vya Bunge, tafadhali pelekeni maswali mafupi na nazitaka Wizara kuleta majibu mafupi ili tuweze kwenda vizuri na muda wetu ambao kikanuni hatujaubadilisha.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea. Katibu.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mwongozo wa Spika.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:** Kauli za Mawaziri.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) nikifuatilia kipengele cha Kanuni ya 46, sitasoma kwa ajili ya kutunza muda. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alipokuwa akijibu swali namba 66 la Mheshimiwa Susanne Maselle, binafsi naona hakujibu sawa sawa. Nafikiri ni vyema suala hilo likaulizwa tena na likapangiwa muda liweze kujibiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongea leo, kuna vijana zaidi ya 20 wamekaa ndani ya Jeshi la Polisi kwa maana ya Vituo vya Polisi zaidi ya siku 30 bila kupelekwa mahakamni kwa kisingizio au kwa makosa ya kwamba walifanya uchochezi wa kimtandao. Nadhani Mheshimiwa Waziri labda hajafanya tafiti au hajapewa jibu sahihi kwa ajili ya swali la Mheshimiwa Susanne Maselle. Naomba apangiwe muda ndipo lije lijibiwe sawa sawa na uhitaji wa Mheshimiwa Susanne Maselle, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na Kanuni ya 46 kuhusu maswali kujibiwa kikamilifu.

Kwa kuwa Mheshimiwa Susanne Maselle aliuliza swali la nyongeza na akajibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, inanipasa nikaangalie liliulizwaje hilo swali na majibu yaliyotolewa ili niweze kutoa Mwongozo ambao uko sawa sawa kwa sababu kwa sasa hivi sitaweza kujua swali mahususi liliulizwaje na majibu yametoka vipi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mwongozo wangu ni huo kwamba nitautoa baadaye nikishafuatilia Taarifa Rasmi za Bunge na namna swali lilivyoulizwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaah!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri naomba ukae tafadhali. *(Makofi)*

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Kuahirisha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe hoja kwa Kanuni ya 47, ambayo inasema baada ya muda wa maswali kwisha Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli zote za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi na la dharura kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku tatu zilizopita kumetokea mtetemeko wa ardhi Mkoa wa Kagera, Bukoba na maeneo mengine mpaka Mwanza. Hivi tunavyozungumza, hali ni mbaya sana na watu wanalala nje, maisha yamekuwa mabaya na kuna uwezekano mkubwa sana wa kutokea milipuko ya magonjwa kwa sababu watu wanaumwa na mbu, shule ya Ihungo vijana wako nje, hawana pa kulala wala pa kusomea lakini shule haijafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu alienda Bukoba, lakini tumefuatilia kwenye vyombo vya habari na watu wetu walioko kule, hakuna kitu ambacho Serikali imeahidi au imetoa kwa uharaka kwa ajili ya tukio hilo kwa maana ya kwamba wananchi wale wapate sehemu ya kulala, chakula cha uhakika na maji; mpaka tunaona wenzetu kutoka Kenya kwa maana ya Serikali ya Kenya imetoa mabati, maturubai na blanketi lakini Serikali yetu haijajadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa natoa hoja kwamba kwa kuwa Bunge ndiyo chombo cha wananchi na ndilo lenye mamlaka ya kuiagiza Serikali kwa niaba ya wananchi ishughulikie hilo suala kwa udharura, natoa hoja kwamba Bunge liahirishwe tujadili hilo jambo hapa na Waheshimiwa Wabunge watoe kauli kuiagiza Serikali ili matatizo yale yashughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hoja imeungwa mkono! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Tamu hiyo… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Heche ametoa hoja kwamba Bunge liahirishwe ili tuweze kujadili jambo la dharura ambalo limetokea hivi karibuni kwa wenzetu ambao wameathirika sana kwa kweli; na wote ambao hata kama hatuko Bukoba, lakini tumepata taarifa mbalimbali za wenzetu waliopoteza maisha, walioumia na wengine ambao hawana makazi kwa sasa; na pengine hawana hata yale mahitaji ya kawaida ambayo mwanadamu yeyote anapaswa kuwa nayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa hiyo hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 47, lakini sasa katika hii karatasi yetu inayoonesha orodha ya mambo yanayopaswa kufanywa leo na ambayo iko mbele yenu, mtaona kwamba kuna hoja ambayo inafuata ni Kauli za Mawaziri.

Waheshimiwa Wabunge, nawashauri kwamba kwa sababu mjadala tutakaoanza kuujadili ni lazima tuwe na taarifa ambazo ziko kamili; tuanze kwa kusikiliza Kauli za Mawaziri halafu tuone kama tuna sababu ya kufanya hivyo, tutaweza kuendelea baada ya hapo. Katibu!*(Makofi)*

**NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:**

## KAULI ZA MAWAZIRI

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa niaba ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuwasilisha taarifa ya awali kuhusu maafa yaliyosababishwa na tetemeko la ardhi lililotokea Mkoani Kagera siku ya Jumamosi, tarehe 10 Septemba, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 10 Septemba, 2016 majira ya saa 9.00 alasiri Mkoani Kagera, Mkoa wa Kagera ulipatwa na tetemeko la ardhi linalokadiriwa kuwa na ukubwa wa kiwango cha 5.7 katika vipimo vya *richter*. Tetemeko hilo limesababisha maafa makubwa kwa baadhi ya wakazi wa Mkoa wa Kagera na kwenye taasisi mbalimbali zilizoko mkoani humo. Mpaka asubuhi hii idadi ya vifo vilivyoripotiwa kusababishwa na tetemeko hilo katika Mkoa wa Kagera ni 17; majeruhi waliolazwa katika hospitali mbalimbali zilizoko katika Mkoa wa Kagera ni 169, majeruhi waliotibiwa na kuruhusiwa ni 83 na majeruhi kwa jumla, wote ni 252. Aidha, nyumba za makazi zilizoanguka ni 840 na nyumba za makazi zenye nyufa ni 1,264. Vilevile majengo ya taasisi yaliyoripotiwa kuanguka ama kupata nyufa ni 44.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatao ni ufafanuzi na mchanganuo wa takwimu unaoonesha maafa yaliyosababishwa na tetemeko la ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Mkoani Kagera:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Bukoba, vifo vilivyoripotiwa ni 15, majeruhi waliopo hospitali ni 142, majeruhi waliotibiwa na kuruhusiwa ni 61, nyumba zilizoanguka ni 753 na nyumba zilizopata nyufa ni 1,037.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari ya Ihungo; ukumbi wa shule hiyo umeanguka, bweni moja limeharibika kabisa, limeanguka, mabweni yaliyoharibiwa na hayafai kukaa ni sita, madarasa yaliyobomoka na hayafai kutumika ni 16, vyoo vilivyoharibika, matundu 25, mabafu ya kuogea yaliyoharibiwa ni mawili, Kanisa lililobomoka ni moja, Msikiti umebomoka mmoja; mtego wa radi umeanguka mmoja, maabara zilizopata nyufa ni tatu, nyumba za Walimu tatu zimeanguka na 17 zimepata nyufa, jumla ni 20.

Katika Sekondari ya Kashenge darasa moja limepata nyufa, lakini Shule ya Sekondari ya Buhembe nyumba za walimu zilizopata nyufa ni moja; vyoo vya wanafunzi vilivyopata nyufa ni kimoja; lakini pia, Jeshi la Polisi *(Police Marine)* kuta zake zimeanguka; *NSSF* jengo limepata nyufa; lakini Chuo cha Afya Kagemu mabweni yaliyoanguka kuta ni matano, jengo la utawala na lenyewe limepata nyufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi, vifo vilivyoripotiwa ni mtu mmoja amefariki, majeruhi walioko hospitali ni 14, majeruhi waliotibiwa na kuruhusiwa ni 18 na nyumba zilizobomoka ni 44.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, nyumba zilizobomoka kuta na kuanguka ikiwa ni pamoja na zahanati mbili, moja inatumika na nyingine inajengwa ni 84 na nyumba zilizopata nyufa ni 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Bukoba, vifo vilivyoripotiwa ni mtu mmoja amefariki; majeruhi waliopo hospitali ni wawili; nyumba zilizobomoka ni 36 na nyumba zilizopata nyufa ni 215.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekondari ya Nyakato, mabweni sita yameharibika hayawezi kukaliwa na nane yamepata nyufa, jumla 14. Madarasa matano yameharibika na 15 yamepata nyufa, jumla 20. Maabara moja imepata nyufa, vyoo vyenye nyufa ni vinne na bwalo la shule hiyo limepata nyufa. Nyumba za walimu nane zimeharibika, haziwezi kukaliwa na nyumba 17 zimepata nyufa; jumla 25. Jengo la Utawala na lenyewe limepata nyufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, majeruhi walioko hospitali ni watano na Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa majeruhi walioko hospitali ni sita; majeruhi waliotibiwa na kuruhusiwa ni wanne na nyumba zilizobomoka ni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali mpaka sasa hivi ni:-

(i) Kuokoa watu na kuwapeleka hospitali kwa ajili ya matibabu.

(ii) Kuwapatia makazi ya muda baadhi ya wananchi ambao nyumba zao zimeathirika kwa majirani.

(iii) Kuwahamasisha wananchi waweze kusaidiana.

(iv) Serikali kuendelea kutibu wagonjwa bure na wenye Bima za Afya kutumia Bima zao.

(v) Tumeongeza nguvu ya Madaktari Bingwa 15 kutoka Mkoa wa Mwanza ili waweze kutoa huduma haraka kwa wahanga.

(vi) Serikali imeelekeza wanajiolojia watoe hofu wananchi na watoe maelezo ya kisayansi kuhusu hali hiyo.

(vii) Tumewaagiza Wakurugenzi wa Manispaa ya Bukoba na Wakurugenzi wa Halmashauri ya Bukoba, wafunge Shule za Ihungo Sekondari na Nyakato Sekondari kwa kuwa zina hali mbaya; hakuna vyoo, mabweni yameharibika sana, mifumo ya maji imeharibika na Shule ya Ihungo imefungwa jana jioni. *(Makofi)*

(viii) Serikali inaendelea kuhakikisha hatua za dharura zinachukuliwa kwa kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha kuwa hatua za muda mfupi na za muda mrefu zinatambuliwa na kutekelezwa ili kuwasaidia wahanga. Serikali inaendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu na kuchukua tathmini mara kwa mara ili kutambua athari zilizosababishwa na tetemeko la ardhi na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawaomba wadau wote wa ndani na nje wanaotaka kuchangia, wawasiliane na Ofisi ya Waziri Mkuu na Kamati ya Maafa ya Mkoa tu. Aidha, Serikali inatoa onyo kali kwa yeyote mwenye nia ya kutumia maafa haya kama sehemu ya kujinufaisha, Serikali itashirikiana na wadau wote wenye nia njema ya kusaidia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za jambo hili zitaendelea kutolewa kadiri zitakavyopatikana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali. Mtakumbuka kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 11 Septemba alifika Kagera na kuona tukio lililotokea na tumeendelea kuchukua hatua ambazo kuanzia leo mchana mtaanza kuziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayehusika na masuala ya maafa yuko kule Kagera akishirikiana kwa karibu sana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na tunaendelea kupata taarifa kila mara juu ya hatua ambazo zinaendelea kuchukuliwa. Leo asubuhi nimepata taarifa kutoka kwa Mkuu wa Mkoa ya hatua mbalimbali zinazochukuliwa. Nitoe wito na kuwaomba wananchi wenye nia njema, kama nilivyosema, wa ndani na nje kushiriki katika kusaidiana katika majanga. Pia nitoe wito kwa wananchi wa Kagera na maeneo yote yaliyoathirika na tetemeko kuwa watulivu na kuonesha ushirikiano na Serikali katika kuhakikisha kwamba changamoto zilizopo zinatatuliwa kwa kasi ili kuepusha au kupunguza ukubwa wa madhara yanayotokana na tetemeko hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na pia, nawashukuru kwa kunisikiliza. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Kutengua Kanuni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antony Komu, naomba ukae tafadhali na uzime *microphone.*

Waheshimiwa Wabunge, tumeisikia Kauli ya Waziri Mkuu ambayo imetolewa na Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhusu jambo ambalo limetupata katika nchi, jambo ambalo ni zito, watu wamepoteza maisha na viongozi wameenda huko; na hapa tumepata hatua ambazo Serikali imechukua.

Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 48(4), maana yake ni kwamba hili jambo limefuata utekelezaji ule unaotarajiwa na sheria, kwa sababu katika hali ya kawaida, Ofisi ya Waziri Mkuu, eneo la maafa liko ofisi hiyo na kwa kuwa tumeletewa hii taarifa inayoonesha kwamba Serikali imechukua hatua kadhaa katika kushughulika na hili jambo, Waheshimiwa Wabunge nadhani tuwape muda wa jambo hili, litaenda mpaka lini? Nadhani kwa sababu bado tuko Dodoma, leo ni Jumanne, nadhani Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye amekwenda huko, atakaporudi na pia Waziri Mkuu atakaporudi, tutawataka watupe taarifa kwamba wamefikia wapi mpaka hapo ambapo watakuwa wamerudi, kwa sababu, wako huko Bukoba wakifuatilia jambo hilo. Kwa sababu hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 48(4) naamua kwamba huu mjadala hatutaweza kuwa nao kwa sababu tumeshapata taarifa. *(Makofi)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Hoja ya Kuahirisha Mjadala. *(Makofi)*

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Kutengua Kanuni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Nimesimama kwa Kanuni ya 69(1); "Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye anaweza kutoa hoja kwamba mjadala huo sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia, atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala huo uahirishwe."

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Kauli ambayo Serikali imetoa Bungeni, lakini jambo hili ni zito, ni tukio la kwanza kubwa ambalo linatokana na tetemeko la ardhi katika nchi yetu. Matukio kama haya tumezoea kuyasikia kwa wenzetu na kuyaona katika Mataifa mbalimbali, lakini safari hii limetokea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wananchi wote wa Mkoa wa Kagera na Watanzania wote kwa ujumla kutoa rambirambi kwa wote

waliokumbwa na maafa katika tukio hili, lakini naomba kwa heshima na taadhima kubwa, Bunge lako Tukufu angalau kwa nusu saa tujadili mjadala huu ili angalau na sisi kama Bunge tuonekane tumeungana na Watanzania katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja ya kuahirisha mjadala kwa nusu saa. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji naomba mkae nitoe maelezo kwanza ili mjue mnahojiwa jambo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Halima Mdee, uwe na heshima kidogo tu. Usinyooshe vidole kwa mtu anayeongoza kikao. Uwe na heshima kidogo, naomba ukae, nimesimama. Naomba ukae, nimesimama na usinyooshe kidole, uwe na heshima kidogo. Waheshimiwa Wabunge, nimesema hivi, hoja imetolewa nataka niwape melezo kabla hatujakubaliana ni kitu gani ninachowahoji.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane.

Mheshimiwa Rashid Shangazi ametoa hoja ya kuahirisha mjadala akiomba kwamba tujadili jambo hili ambalo limetupata kwa dakika 30 na ametoa maelezo hapo kwamba kwanza anataka kuonesha namna ambavyo Bunge linaungana na watu wa Bukoba kwa kujadili kwa hiyo nusu saa; na jambo hili ambalo limelipata Taifa kwa ujumla. Mheshimiwa Shangazi ameongea mambo mawili, ndiyo maana nimelazimika kusimama ili nitoe ufafanuzi. Ameongea mambo mawili; moja, ameongea kuhusu mchango wa Bunge, kwa maana ya Wabunge, lakini jambo la pili, alilolizungumza ni kuhusu kujadili ile kana kwamba tunataka sasa kujadili hoja ambayo imetolewa na Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu hizi, mjadala nitauruhusu, lakini kwa hoja moja aliyotoa Mheshimiwa Shangazi ya michango. Sitaweza kuruhusu mjadala wa kuhusu hoja ya Waziri kwa sababu Kanuni zetu haziruhusu na kwa sababu hoja hiyo nimewasomea Kanuni ya 48 inayoonesha

kwamba kama jambo hili linafuata utekelezaji wa kawaida wa sheria namna zilivyo, ndivyo itakavyokuwa. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ndiyo maana niliwaambia mtulie nieleze vizuri ili mjue nawahoji kwenye jambo gani. Kwa hiyo, nitawahoji kwenye jambo moja na siyo la kujadili Kauli ya Waziri kwa sababu Kanuni zetu haziruhusu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Kutengua Kanuni!

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nitawahoji kuhusu hoja ambayo kikanuni inaruhusiwa.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa nusu saa na mimi naitoa hiyo nusu saa. Wanaotaka kuchangia hoja wasimame ili niwaone.

**MBUNGE FULANI:** Hoja gani?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja gani?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkipiga kelele tutakuwa hatuelewani. Nimeshawaeleza ni hoja moja tu itajadiliwa. Kwa hiyo, nachukua watu sita ambao watapewa dakika tano tano kila mmoja. Tutaanza na Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Ryoba…

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Aeshi.

**MBUNGE FULANI:** *Gender.*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vulu.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Na sisi Mheshimiwa, Aeshi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Aeshi.

**NAIBU SPIKA:** Hawa ni watano na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Waziri wa ....

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Naibu Spika haiwezekani!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ngoja niwasomee majina ya watakaochangia.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae. Mheshimiwa Masoud anawakilisha *CUF*, Mheshimiwa Ryoba anawakilisha CHADEMA, Mheshimiwa Shangazi ni wa CCM, Mheshimiwa Zaynabu Vulu ni wa CCM, Mheshimiwa Tibaijuka ni wa CCM na Waziri wa Kilimo. Tutaanza na Mheshimiwa Shangazi. *(Makofi)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, naomba uendelee.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kama nilivyotangulia kusema hapo awali…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** CCM wengi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge tuwe tunafanya hesabu sawasawa. Wabunge wa CCM wakiwa saba Wabunge wa Upinzani wanakuwa watatu. Wabunge wa CCM wapo sita Wabunge wa Upinzani wanakuwa wawili. Mheshimiwa Shangazi, naomba uendelee. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba niendelee…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** *(Hakutumia kipaza sauti).*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko tafadhali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** *(Hakutumia kipaza sauti)*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko tumeshasikilizana, majina niliyotaja Wabunge wawili ni wa Upinzani.

**MBUNGE FULANI:** Watoke!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, naomba uendelee.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kutoa pole kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera na Watanzania kwa ujumla kwa tetemeko hili ambalo limeikumba Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Pia nipongeze kwa hizi jitihada za Serikali za haraka, tumeona siku ya Jumapili Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda eneo la tukio lakini sambamba na hilo, Mheshimiwa Rais alipaswa kuwa safarini Zambia kwenye shughuli za kumuapisha Mheshimiwa Rais wa Zambia lakini aliahirisha. Kwa hiyo, hiyo ni kuonesha kwamba Serikali imelichukulia jambo hili kwa nafasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hilo, kama ambavyo tumekuwa na utamaduni mbalimbali, katika Bunge letu Tukufu nadhani katika Bunge la Kumi yalipotokea maafa ya *MV Spice Island* kule Zanzibar, Bunge lilijadili na pia Wabunge tuliazimia kutoa rambirambi.

Naomba na mimi kwa nafasi hii niwashauri na nikushauri kama Kiti chako kitapendezewa basi sisi kama Wabunge na sisi tuchangie japo posho yetu ya kikao hiki cha leo ili angalau iwe sehemu ya kuwashika mkono wenzetu hawa wa Mkoa wa Kagera hasa wa Manispaa ya Bukoba kama sehemu ya rambirambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lazima tushukuru utukufu wa Mwenyezi Mungu katika jambo hili kwamba tunashukuru Mwenyezi Mungu kwamba limetokea mchana ndiyo maana hata maafa haya hayakuwa makubwa sana. Kama jambo hili lingetokea usiku watu wakiwa ndani huenda lingesababisha maafa makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuishauri Serikali tuhakikishe hii timu ya maafa ambayo ipo chini ya Waziri Mkuu iweze kusogea kwenye kanda mbalimbali. Tutakapokuwa na timu ya maafa ambayo ina-*operate* kutokea Dar es Salaam ndiyo maana wanachelewa kufika maeneo husika. Kwa hiyo, kwa funzo hili ambalo tumelipata basi Serikali ilichukue hili kwamba kuwe na timu za maafa za kikanda ili matatizo yanapotokea katika maeneo mbalimbali wananchi wetu waweze kupata msaada kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Na mimi niungane na Mheshimiwa Shangazi kuwapa pole wahanga wote kule Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa masikitiko makubwa mpaka sasa jitihada za Serikali hazioneshi kama zinatosheleza, inaonekana Serikali bado haijajipanga zaidi. Serikali inasema wadau wa nje na wa ndani waendelee kuchangia, ni jambo jema, lakini Serikali haijatuambia changamoto ambazo zinawakabili wahanga na majeruhi. Wangetuambia changamoto ambazo zimewakabili zaidi wenzetu ili na sisi Wabunge tukajua ni mambo gani ya msingi ambayo yapo. Serikali imesema tu wamefanya moja, mbili, tatu na Waziri Mkuu kaenda lakini ituambie kuna changamoto gani? Amesema Mheshimiwa pale kwamba watu wanaendelea kuteseka, wanaumwa na mbu, maradhi ya kuambukiza yanaweza yakatokea, vyakula ni shida na waliopo *site* wanasema mambo mengi na taarifa tunazo. Sasa Serikali ituambie ni mkakati gani wa ziada na wa haraka inao ili kuwasaidia watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo hiki ambacho kimetajwa cha *richter scale* kwa wataalam kwa Tanzania ni kikubwa. Inaelekea kuna majeruhi, vifo vilivyotokea, mali za wananchi zimeharibika na kadri ya siku zinavyokwenda bado tunaona jitihada za Serikali ambazo imekusudia kuchukua kwa wakati huu hazitoshelezi labda pangeandaliwa mpango madhubuti. Hivi kwa nini Serikali isiwe na mpango wa dharura kwamba inaandaa mazingira kwa wale wote waliopata madhara haya kukawa na fungu fulani la fedha ambazo watapatiwa kwa haraka ili kujenga imani kwa wananchi wa Kagera? Nyumba ambazo tayari zimeanguka basi Serikali itoe kauli ya haraka ili kujenga moyo watu wetu. Serikali inasema kwamba tumejiandaa, tumefanya hili na hili lakini bado wananchi wa Kagera wanaendelea kulalamika. Mimi nasema mambo haya siyo ya kupuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kwamba tujadili kwa muda wa nusu saa bado hatuwatendei haki wananchi, hili jambo ni kubwa. Tuendelee kujadili hata kama leo siku nzima itaondoka tutaongeza siku hata kama ni Jumamosi, tatizo ni nini? Kwa sababu Serikali inangoza wananchi ambao wamepata maafa makubwa lazima wananchi wapewe haki yao na wawakilishi wao ni Wabunge na ndiyo sisi, tuache tujadili kwa ufasaha, kwa kina tuangalie tunafanyaje ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kutoa pole kwa waathirika na naunga mkono suala la rambirambi kutolewa na Waheshimiwa

Wabunge maana na sisi tumeguswa, ni sehemu ya jamii hii lakini asilimia 95 Serikali inawajibika kwa watu wake. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nafasi yangu nimuachie John Heche aongee. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ndiyo nilikuwa wa kwanza na ulipaswa kuonesha tu heshima…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche usinifundishe kazi.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Nisikilize.

**NAIBU SPIKA:** Usinifundishe kazi nimeita watu waliosimama, nilioona mimi wanafaa, umepewa nafasi changia hoja.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Ungenisikiliza nijenge hoja zangu lakini usiniingilie, usiwe na *emotions* Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Usiijenge dhidi yangu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Basi.

**NAIBU SPIKA:** Mimi ndiyo naamua nani aongee.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Basi.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni hizi ndiyo zinazoniruhusu …

**MBUNGE FULANI:** Unajua kazi gani wewe?

**NAIBU SPIKA:** Mimi ndiyo naamua nani aongee na sasa umepewa nafasi ongea hoja, usimjadili Naibu Spika.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo halipaswi kutugawa, hili jambo linapasa kutuunganisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa kabisa, naomba nitoe pole za dhati kwa wananchi wote na mimi nilifikiri kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Masoud, Bunge hili ndiyo chombo cha wananchi na sisi tulipaswa kuonesha heshima zote kwa wananchi, tutoe siku nzima ya leo tujadili na tuielekeze Serikali ni nini cha kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemuona Waziri Mkuu ameenda kule, lakini hatujaona kitu chochote alichoenda nacho. Tulitegemea Waziri Mkuu aende na mahema na chakula tuone wananchi wanapewa msaada wa haraka. Kwa sababu ni janga sisi wengine tuliliona tangu jana, Wabunge wa UKAWA tulikuwa tumeshachangia laki moja moja na tunakubaliana pia kuongeza posho ya leo na ndiyo maana hata Mwenyekiti wetu yupo kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachosema ni kuwa kwenye karatasi hii ya Serikali kwa kweli hakuna *commitment* yoyote ya maana humu ya kwenda kuwaambia wananchi kwamba ni nini Serikali yao inaenda kufanya kule kwa ajili ya maisha yao. Kama hatuwezi kuisema hiyo *commitment* hapa Bungeni, tunaongea kwa kufumbafumba baadaye tukazungumze na vyombo vya habari mimi naona siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema ni kwamba Serikali itoe *commitment* ya haraka kuhusu chakula, makazi na kuhusu wale wananchi ambao unajua mtu amejikusanya kwa miaka 20 amejenga nyumba ndani ya usiku mmoja imebomoka, atahitaji miaka mingine 20 kuanza kujenga nyumba, Serikali inasema nini kuhusu kusaidia hawa watu waweze kujenga nyumba waweze kuishi na watoto wao? Hayo ndiyo mambo ambayo tunazaungumzia. Ndiyo maana wenzetu Wakenya wametoa mabati, mablanketi na magodoro. Serikali yetu inasema wananchi wajihamasishe wachangie, watu wa jirani wametoa lakini Serikali yetu haitaki kutoa *commitment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kujali itikadi, Bunge hili litakuwa halijawatendea haki wananchi kwa kushindwa kuiongoza Serikali itoe *commitment* ya wazi kusaidia maisha yao, tutakuwa hatujatenda haki yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Wabunge tunapojadili jambo hili wala hakuna mtu anayehitaji kushinda hapa, tuielekeze Serikali ni nini sisi kama Wabunge tunataka kifanyike kule kwa ajili ya ku-*rescue* maisha ya watu, kwa ajili ya ujenzi, chakula, maji, sehemu za kulala na afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba niunge mkono kwamba tutatoa mchango na sisi wengine tulishaguswa tumetoa, lakini Serikali itoe *commitment* hapa, ndiyo kilio chetu Wabunge wote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nami niungane na mtoa hoja Mheshimiwa Shangazi ya kuchangia posho yetu ya leo kwa ajili ya wahanga. Pia niseme kwamba tukio hili ni kubwa sana, tukio hili limegusa hisia, maisha na hali za wenzetu wa Mkoa wa Kagera na mikoa jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali lakini nitoe ushauri wangu. Serikali ijipange vizuri, suala hili ni zito, tunahitaji kuwa na mikakati thabiti ya hapo baadaye. Misaada, elimu ya maafa na elimu kwa ajili ya uokoaji iendelee kutolewa katika maeneo mbalimbali. Tumeshuhudia watu wanavyobebwa na tumeshuhudia watu wanavyohangaika.

Kwa hiyo, niiombe Serikali iendelee na juhudi zake ambapo tumemuona Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Maafa), lakini bado tunahitaji michango ya kutosha kama alivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwasihi baadhi ya watu tusichukue eneo hili kama eneo la kataka kupata maili katika siasa. Aliyeguswa ni binadamu, Waswahili tuna misemo yetu, wewe kama unatoa mkono wa kushoto basi mkono wa kulia usijue. Kama nia yako ilikuwa kusaidia endelea kusaidia, kama unaona mwenzio hasaidii wewe saidia ili watu waweze kupata misaada. Hapa tunajenga nyumba moja kwa nini tugombee fito? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iteuliwe Kamati ya dharura kutoka ndani ya Bunge hili ili waende kuwatembelea wahanga na kuwapa pole, kuwaona wafiwa na kuangalia wanawake na watoto walioathirika. Ikiwezekana hata wiki moja tukakae, tukajenge shule iliyobomoka na mabweni kwa ajili ya manufaa ya wenzetu. Hata hivyo, tahadhari ziwepo siku zinazokuja maafa kama haya hata kama hatukupata taarifa lakini wahusika katika maeneo husika wawe wanajua, tufundishwe jinsi ya kuokoa. Naipongeza Wizara ya Ndani sasa hivi watoto wetu wanajua kuvuka barabara. Basi tufundishwe hata kuokoa mtu anayepata ajali iwe ya tetemeko la ardhi, iwe ya kwenye maji au hata mtu anapogongwa na gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa sana Wajumbe wa nyumba hii (Bunge), kwanza, naomba niwape salamu kutoka Kagera. Nimefika hapa leo saa 12.00 asubuhi, nilitoka Bukoba jana saa 3.00 usiku na nilimuacha Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wetu ameshafika, kwa hiyo, naipongeza Serikali ipo kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Bukoba ni tete na mimi hapa nasimama kwa nyadhifa nyingi mojawapo kama mtaalam wa maafa ya namna hii. Niseme kweli nilikuwa Dar es Salaam lakini waliposema kwamba Kagera wamekumbwa na tetemeko ilibidi niende kuangalia hali hasa ikoje?

Nataka niseme kwamba kama Taifa tumshukuru Mungu wazungu wanasema; *it could have been worse*, ingeweza kuwa mbaya zaidi lakini bado mkono wa Mungu nauona pale umezuia tetemeko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana wananchi katika hali ya tetemeko na nashukuru sana upande wote wa nyumba hii, wenzetu kwa upande wa upinzani na sisi wa CCM naona hapa wote tuna kauli moja, hapa hakuna siasa. Jana Rwamishenye mimi na Mheshimiwa Mbowe tumeshiriki mazishi ya mhanga mmoja, kwa hiyo, tulikuwa wote. Nadhani watu watatushangaa wakisikia tunavutana, sioni kama hapa tunavutana lolote, hapa tunazungumza, nashukuru sana umeruhusu na Mheshimiwa Shangazi ameleta hoja nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maafa watu wanataka faraja. Mimi nimefika Shule ya Wasichana ya Rugambwa, Serikali bado inaendelea na tathmini, pale nyumba tatu za walimu zimeanguka, nimekwenda kwenye bweni nililolala mimi lina nyufa na kadhalika. Bukoba Manispaa kati ya nyumba kumi, nyumba saba zina nyufa. Nje unaona ipo salama lakini ndani nyingine zitakuwa *condemned buildings* yaani hazitafaa kwa makazi ya binadamu. Kwa hiyo, hali ni tete na nafikiria hoja hii tuliyonayo mbele yetu ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifika katika Shule ya Ihungo kutoa mkono wa faraja nilimkuta Mwalimu Mkuu, Afisa Elimu wa Mkoa na wale vijana sikuwa na la kufanya, nilikuwa na shilingi 250,000 mfukoni nikaziweka mezani kwa sababu unawaachaje? Nikasema angalau watoto basi watafutiwe soda kwa sababu watoto wanalala nje, hali ni tete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiria kama Taifa sasa tuwe wamoja, tutafute misaada ya kimataifa ili iweze kutusaidia, inaitwa *international alert,* Umoja wa Mataifa wana utaratibu na nadhani Serikali inaendelea kushughulikia hilo. Waziri wetu mhusika Mheshimiwa Jenista Mhagama na timu yake wapo *on the ground*. Kitu muhimu ni kuhakikisha kwamba tathmini zinafanyika kitaalam siyo za macho, maana unaweza kuona nyumba iko salama lakini siyo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnapenda sana kusema mgongano wa maslahi, mimi mwenyewe nyumba yangu ya Bukoba kwa Tibaijuka mwenyewe nina *damage* kubwa sana na maafa haya yaliyo mengi hayana bima. Kwa hiyo, hapa itabidi Serikali ijaribu kusaidia, kuna sehemu misaada ya moja kwa

moja itakwenda, lakini kuna mbinu pia za kisera. Kwa mfano, kuweka Mfuko Maalum, wahanga wengine wana uwezo na mimi nikiwa mmoja wao wa kujitegemea, lakini angalau uwe na mkopo wa riba nafuu ili uweze kutengeneza nyumba yako, ndivyo inavyokwenda. Kwa hiyo, kuna mahali pengine ambapo utaweza kupeleka misaada ya moja kwa moja kuna mahali pengine hautaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali inafanya kazi hasa Waziri Mkuu kufika pale imeleta faraja kwa wana Kagera wote kujua kwamba sisi ni watu wa mbali hatupo peke yetu. Wanasema ng'ombe wa maskini hazai. Mheshimiwa hapa Waziri wa Fedha ametutangaza kama mkoa maskini Tanzania sasa kama haikutosha na tetemeko limekuja kumalizia yote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi hapa nasimama kwa niaba ya wana Kagera na nimekuja kama *eye witness,* nimejaribu kuwahi na Mheshimiwa Kigola ameuliza swali langu nashukuru, nilijua nitawahi lakini hasa nilikuwa nawahi kuwapa taarifa kama *eye witness* hali ni tete lakini faraja ni muhimu.

Kwa hiyo, Wabunge mkisikika na ninyi mnaweka faraja kidogo italeta heri kubwa sana. Mimi nafikiria mapendekezo ambayo yapo ambayo wanasema ni…

**MBUNGE FULANI:** Shilingi 500,000.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Utaratibu wetu ni posho ya siku moja, kwa kweli mimi nitafarijika lakini wanaoweza kujiongeza watajiongeza. Mimi jana nimetembelea Shule ya Mgeza Mseto, ni shule ya walemavu, watoto wote vilema na maalbino wa Kanda ya Ziwa wapo kwenye hiyo shule moja. Nilipofika pale nilikosa la kufanya nikatoa shilingi 250,000 kwa ajili ya kuwafariji watoto. Kwa hiyo, faraja ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, tutoe faraja tusiweke siasa, katika hili wote tupo pamoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba atakuwa msemaji wa mwisho.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme nasimama kama Mbunge, lakini pia niseme baadhi tu ya mambo ambayo kwa sasa ukiachilia mbali taarifa iliyotolewa kwenye Kauli ya Serikali yanaendelea kufanyika kwenye maeneo mbalimbali Mkoani Kagera na mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli *epicenter* ya tetemeko hili ilikuwa maeneo yale ya Mkoa wa Kagera lakini madhara yake hayakukomea katika Mkoa wa Kagera peke yake yamefika pia katika Mikoa ya jirani ya Mwanza, Geita na Shinyanga. Baadhi ya maeneo ya Shinyanga pia wamesikia hii mitetemeko na kwa hiyo eneo la maafa siyo dogo na haliko *limited* katika Mkoa mmoja wa Kagera isipokuwa na mikoa ya jirani pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali baada ya taarifa za tetemeko hili ilichukua hatua za dharura za awali kama sheria inavyotaka. Kamati za Maafa za maeneo yote husika zilitakiwa kuingia kazini na kuanza kuchukua hatua za kuokoa maisha.

Kwa hiyo, madhara yangekuwa makubwa kama hatua hizo za Serikali zisingechukuliwa mara moja ambazo kwa kiasi kikubwa zimeokoa maisha ya watu wengi. Zipo timu za madaktari wametolewa Dar es Salaam na Mwanza kama taarifa ilivyosema lakini kipo kikosi kingine sasa hivi kinajipanga kwenda huko kuhudumia watu wenye majeraha makubwa ambao inawezekana wasiweze kutibiwa katika hospitali na *facilities* zilizopo Mkoani Kagera. Serikali pia imeendelea kupeleka chakula kupitia Kamati za Maafa za Wilaya na Mikoa mbalimbali, dawa, wataalam kama nilivyosema, mablanketi, mahema yanaendelea kukusanywa na mengine yamekwishaanza kufika huko na haya yote hayasemi kwamba ndiyo mwisho wa jitihada za Serikali kukabiliana na hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri mwenye dhamana na mambo ya maafa yuko huko na vyombo vyetu vyote vya Serikali vimewekwa katika hali ya tahadhari na vinasaidiana kufanya tathmini. Kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, tathmini inapaswa kuwa ya kina na ya kitaalam kwa sababu tumekwishaona pia wakati wa janga la milipuko ya mabomu Dar es Salaam kule Temeke, tathmini ilifanyika vizuri na ikabaini kwamba katika jambo la namna hii wako watu wanataka ku-*take advantage* na kupata manufaa wasiyostahili, kwa hiyo tathmini itafanyika ya kina na ya kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tathmini hii, Serikali itafanya *commitment* ya namna gani imsaidie mmoja baada ya mwingine wahanga wote watakaokuwa wamebainika kwamba wanastahili kupata hudumu. Zipo taratibu za kisera kama ilivyosemwa, kuweka mapunguzo, kuweka viwango na kadhalika ili mwananchi apate nafuu ya kujirudisha tena katika hali yake ya kawaida baada ya madhara haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee kwenye hoja iliyo mezani kwamba mchango wetu uwe namna gani, mimi nipende pia kuunga mkono wazo la kwamba Waheshimiwa Wabunge wote tutoe posho yetu ya siku moja kwa ajili ya kuwasaidia wenzetu walioathirika. Lakini pia katika mazingira haya ya

namna hii, Mbunge ambaye ataona hata kutoa posho ya siku tano au kumi inampendeza basi afanye hivyo na wala isionekane kama ni kujitolea kulikopitiliza, hili ni jambo la kawaida tu. Mimi mwenyewe jimboni kwangu wako watu wameathirika sana, nyumba zao zimebomoka pia na tunaendelea kufanya tathmini ya kujua ni kwa kiasi gani wanahitaji msaada. Kwa hiyo, ndugu zangu misaada hiyo pia muilengeshe katika Jimbo la Buchosa ambalo pia limepata madhara haya ya tetemeko la ardhi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe pamoja na Bunge lako Tukufu, lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo tumeonesha kuguswa na suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hata wenzetu wa Kenya kama alivyosema Mheshimiwa Heche hawakuangalia mipaka yetu ya kijiografia, lakini waliangalia undugu. Hicho ndicho kitu ambacho hata mimi kimenisukuma kulishawishi Bunge lako hili kwamba angalau sasa na sisi tutoe rambirambi kupitia posho yetu hii ya leo na nashukuru kwamba Waheshimiwa Wabunge wameafiki suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nishukuru kwa maneno mazuri sana aliyosema Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kwa namna ambavyo yeye ameshuhudia kwa macho na namna ambavyo ameipa Serikali somo kwamba jambo hili linahitaji siyo *crash program,* lakini liangaliwe kwa mapana zaidi ili kila ambaye ameguswa kwa namna moja ama nyingine aweze kupata stahiki.

Mheshimiwa Naibu spika, lakini faraja ambayo tunaitoa itatujengea heshima Bunge kama mhimili kwa sababu tuna mazoea ya kufanya hivyo. Nimeambiwa hapa pia kwenye Tsunami iliyotokea Japan pia Bunge liliweza kusaidia. Kwa hiyo, ni jambo jema sana na ni jambo linalothibitisha utu wetu mbele ya macho ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashukuru sana na naomba nifunge hoja yangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, naomba utoe hoja uungwe mkono ili niweze kulihoji Bunge.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Nadhani katika michango yetu hoja iliyojadiliwa kwa kirefu ni hiyo ya kutoa mchango wa posho ya siku ya tarehe 13 Septemba, 2016.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, posho ya leo ya Waheshimiwa Wabunge itachangia maafa ya ndugu zetu Bukoba.

*(Bunge liliridhia kutoa posho ya tarehe 13 Septemba, 2016 kwa ajili ya Waathirika wa Tetemeko la Ardhi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa niaba ya Serikali, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kauli mbalimbali zilizosemwa hapa, lakini pia kwa faraja hiyo ambayo imetolewa hivi sasa na kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wote. Nawashukuru sana kwa niaba ya Serikali.

Kama alivyosema mtoa kauli, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI jambo hili ni letu sote na huu ni utamaduni wa Kitanzania, hii si mara ya kwanza, tumekuwa tukishuhudia Bunge hili likifanya mambo haya kila mara mambo makubwa yalipotokea. Kwa hiyo, nimesimama hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwashukuru sana wote na kwa kuwa maelekezo ni kwamba michango hii itatolewa kwenye Ofisi ya Maafa ya Mkoa au Ofisi ya Waziri Mkuu, tunataka kuwahakikishia kama Serikali michango hii itawafikia walengwa na itatumika kwa kadri nia zenu na faraja zenu mmeazimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba jambo hili mnavyoliona kubwa na Serikali inalichukulia kwa ukubwa huohuo ndiyo maana Mheshimiwa Rais ameahirisha ziara siyo kwamba ameahirisha ziara apumzike tu, hivi sasa anasimamia jambo hili. Mheshimiwa Waziri Mkuu hakuja leo ndiyo maana mnaniona mimi namsimamia hapa, baada ya kutoka Bukoba kwenda kujionea yale mambo leo ana-*organise* mambo makubwa kule Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kuzungumza na hao wadau wengine, Mheshimiwa Profesa Tibaijuka amesema, yapo mambo tunahitaji vilevile wenzetu hata wa nje waweze kutusaidia, upo utaalam hapa na hata wenzetu wa nje hawawezi tu kwenda Bukoba mmoja mmoja, huwa wanakuwa *organized*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Waziri Mkuu anafanya jambo hilo pamoja na kuainisha mambo kadhaa ambayo mmeyasema. Uzito huu ndiyo umemfanya Mheshimiwa Waziri Mkuu asije hapa Bungeni leo abaki Dar es Salaam kule kisimamia mambo haya, ni jambo kubwa. Uzito huu ndiyo umemfanya Mheshimiwa Rais asiende Zambia kule asimamie jambo hili liende vizuri, ni jambo kubwa. Ukiangalia tu haya mawili unaweza kukuta kwamba jambo hili kama Serikali tumelichukulia kwa umuhimu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hatuwezi kuanza kujenga nyumba za waathirika, tunahitaji utaalam tuthibitishiwe kwamba hata eneo walilopo pale linafaa kujengwa tena? Inawezekana ukaamua kujenga leo, kesho tetemeko lingine. Kwa hiyo, kuna mambo mengi sana yanafanyika chini kwa chini. Mheshimiwa Simbachawene asingeweza kuleta mkeka wa mambo yote ambayo Serikali inafikiria kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania waamini tu kwamba Serikali iko *serious,* ina uchungu mkubwa sana kwa namna ambavyo imekuwa inawajali watu wake na jambo hili litakwenda vizuri, tuendelee kushirikiana, tuwaombee majeruhi wapone haraka na wale waliotangulia mbele za haki tuwaombee kwa Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya michango yenu mizuri sana, naomba sasa tupate nafasi ya kuwaheshimu marehemu waliotangulia mbele ya haki, tusimame kwa dakika moja.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kuwakumbuka waliopoteza maisha kutokana na tetemeko la ardhi Kanda ya Ziwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza, nianze kwa kuwashukuru kwa michango mizuri mliyoitoa lakini nianze kwa mchango wa fedha ambao Waheshimiwa Wabunge mmekubali kukatwa posho ya siku ya leo ili tuweze kuwasaidia wenzetu walioathirika na hili tetemeko.

Pia nishukuru kwa michango mbalimbali iliyotolewa hapa na nichukue sasa fursa hii kwa kutumia hiyo michango iliyotolewa kuiagiza Serikali kwamba imalize hiyo tathmini mapema kwa sababu hata hao watu ambao tunataka kuwaweka pamoja ili watusaidie katika mambo mbalimbali hatutaweza kupata misaada iliyo kamilifu kama hatuna hata sisi wenyewe uhakika tumeathirika kiasi gani. Kwa mfano, ili umuombe mtu chakula lazima ujue unahitaji chakula gani na ndiyo maana Mheshimiwa Heche hapo alisimama akaeleza jambo la makazi, ma-*tent* mangapi yamepelekwa.

Mimi nataraji kwamba Waziri Mkuu atakaporudi na Mheshimiwa Jenista, Waziri ambaye yuko chini ya Wizara hiyo na tumeambiwa kwamba yuko huko Bukoba atatuletea sasa hiyo taarifa ya chakula mmepeleka kiasi gani ili tujue ndugu zetu kule si kwamba wako katika njaa, watakuwa katika taabu sawa lakini wasiwe na njaa, mtatueleza habari ya matibabu, hapa mmetaja madaktari lakini hiyo peke yake haitoshi, tupate taarifa za wale walioathirika, wametibiwa ama bado wanaendelea kusubiri dawa, vitu kama hivyo mkitupa taarifa itatusaidia.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Zaynabu Vulu alipendekeza kwamba iundwe Kamati, lakini Bunge hili linayo Kamati ya Kudumu ambayo inaweza kushughulikia jambo hilo, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, nadhani tuiachie hiyo Kamati ione namna bora ya kulifanya hili jambo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba tuendelee, Katibu.

**NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016 *(The Government Chemist Laboratory Authority Bill 2016)***

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016 *(The Chemist Professionals Bill, 2016)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina hapa ya wachangiaji wa siku ya leo, lakini sasa kwa sababu ya muda tuliobaki nao, naomba kwa wale watakaoweza watuachie dakika tano, tano ili kila mtu achangie dakika kumi ili tupate fursa kwa ajili ya Wabunge wote ambao ninayo orodha yao hapa. Tutaanza na Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe na Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab ajiandae.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Wizara ya Afya kwa kuleta muswada huu. Muswada huu ni muhimu sana kwa sababu wote tunajua umuhimu wa kemia katika maendeleo lakini vilevile teknolojia imepanuka sana kwa hiyo kuna

changamoto nyingi zinazotokana na upanuzi huo *therefore* huu muswada umekuja kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa muswada huu ni mkubwa, hii Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa ipo siku nyingi, lakini hawakuwa na sheria yao wenyewe, walikuwa wanatumia sheria za hapa na pale kukiwa na tatizo la mambo ya mazingira basi wanatumia Sheria ya Mazingira lakini kwa kutunga sheria hii sasa tutakuwa tumemuwezesha huyu Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa na sheria yake moja ambayo itaweza kuongeza ufanisi *(principal legislation)*. Sheria hii ikishatungwa itaifanya maabara hii kuwa ya mwisho na ya rufaa. Hii itampa nafasi mtu ambaye hajaridhika na matokeo ambayo yametoka labda kwenye hizi maabara ndogo ndogo aweze kupata mahali ambapo anaweza akakata rufaa na akaweza kusikilizwa, kwenye maabara kama za *TBS, TFDA* basi kama mtu atakuwa hajaridhika huko anaweza kukata rufaa kwenye hiyo maabara. Hivyo basi, kifungu cha nne (4) kwenye Muswada huu kieleze wazi majukumu ya Mkemia Mkuu wa Serikali kusudi sasa kusiendelee kuwa na migongano ambayo ilikuwepo kati ya majukumu ya hii maabara pamoja na maabara zile ndogo ndogo zinazoshughulika na hayo mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kifungu cha 10 kinazungumzia uteuzi wa Mkemia Mkuu na kinamtaka huyu atakayeteuliwa awe na shahada ya uzamili ya kemia au taaluma nyingine zinazofanana na hizo. Hata hivyo, tukumbuke sasa hivi vipo vyuo vingi, wengine *degree* tunapata tu kwenye *internet,* wengine tunapewa tu, ili kuondoa matatizo ambayo yanaweza kujitokeza tukakuta ameteuliwa mtu ambaye hana sifa zinazotakiwa hicho kipengele kiseme kwamba hiyo shahada ya uzamili iwe imetoka kwenye chuo kinachotambuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kifungu cha 16(4) kinachozungumzia usimamizi wa sampuli zinazopelekwa kwenye maabara kwa ajili ya uchunguzi, kinataka maabara isiwajibike kwa mabadiliko au muonekano wa sampuli utakaojitokeza wakati wa uchunguzi au hata baada ya uchunguzi.

Ndugu zangu, mkumbuke kwamba hii maabara itakuwa inapima kemikali, sumu, vinasaba, dawa za kulevya na sampuli za kesi za jinai, kwa hiyo, lazima tuwe waangalifu. Ikitokea mtendaji ambaye syo mwaminifu hiki kifungu cha 16(4) kinaweza kikatumika vibaya, ukakuta mtu unapeleka sampuli ukihisi kwamba ni sumu iende kupimwa ikapimwa lakini ukaambiwa kwamba hii haikuwa sumu ilikuwa ni chumvi au ukapeleka bhangi unakwenda kuangalia unakuta imeshakuwa mchicha. Kwa hiyo, napendekeza kwamba hicho kifungu kielezwe vizuri kusudi hao watu ambao siyo waaminifu wasiweze kukitumia vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi wanaume wengi wanawapa wanawake mimba, lakini wanawakana watoto. Wengine wanawapa mimba wanafunzi, wanawatelekeza, watoto wa watu wanaishia kufukuzwa shule na kwa sababu hawawezi kupata kazi kwa hiyo watakuwa hawana kipato, wataendelea kuwa maskini na watoto wao wataendelea kuwa maskini. Pia wote tunaona ukatili kwa watoto unaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna takwimu zimetolewa juzi juzi na Dawati la Jinsia na Watoto katika Jeshi la Polisi ambapo wamebaini kwamba kwa mwaka huu tu tangu mwezi Januari mpaka Julai, watoto 2,571 wamebakwa. Je, wamebakwa na nani? Unaweza ukakuta hata mtu mwingine unaishi naye humo ndani ndiye mbakaji, lakini hujui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwabaini wanaume wanaowakana watoto, wanawapa mimba wanawake lakini wanaogopa majukumu wanawakana watoto, kuwabaini wanaowapa wanafunzi mimba na kuwabaini hao wanaobaka watoto na kuwalawiti, Maabara hii ya Mkemia Mkuu wa Serikali inaweza ikatumika au itatumika kupima *DNA* ambayo itakuwa ni kipimo sahihi kuonesha ni nani amefanya tukio hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili watendaji wasije wakashawishiwa kwa rushwa kubwa au ndogo, napendekeza adhabu iongezeke ambayo iko kwenye kifungu cha 53. Adhabu kwenye kifungu hiki iongezeke ili isomeke kwamba *fine* isiwe chini ya shilingi milioni tano na kifungo kisiwe chini ya miezi kumi na mbili kusudi mtu aweze kupewa adhabu kubwa kufuatana na kosa atakalokuwa amelifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipendekeze kwamba sheria hizi zikishapita basi kanuni zitungwe haraka sana kusudi hizi sheria ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijajitendea haki na nitakuwa sijawatendea haki wana Kagera, mimi kama Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kagera ambaye ni mwakilishi bila ya kulizungumzia hili ambalo limetokea Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuwapa pole wenzangu wote ambao wako kule walioathirika kwa matatizo makubwa waliyoyapata ambayo yametokana na tetemeko la ardhi. Najua imetokea Kanda ya Ziwa lakini Mkoa wa Kagera umeathirika vibaya sana na hasa hasa Bukoba Mjini. Leo hii tumeambiwa watu 17 wameshafariki, tumesikia katika taarifa mbalimbali na kwamba watu zaidi ya 252 wamejeruhiwa, nyumba zaidi ya 840 zimeanguka, nyumba zaidi 1,264 zimepata nyufa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie ukifika pale Bukoba Mjini utakuta karibu nyumba zote zina nyufa, Bukoba Vijijini nyumba nyingi zina nyufa, Misenyi, Muleba na kadhalika lakini vifaa vya ndani vimeharibika kwa kweli ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana na kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuona umuhimu wa tatizo hili na akaamua kuahirisha ziara yake ili aweze kulishughulikia akiwa hapa hapa. Namshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa kwa upendo wake, kwa kuwajali watu na uharaka alioutumia kufika Bukoba kwenye *site* akaweza kuwafariji watu lakini akashiriki vilevile kwenye hatua za awali za mazishi. Niwapongeze viongozi wa Mkoa ambao wako kule kule, kuna Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi, Mstahiki Meya wa Manispaa, Madiwani, Kamati za Maafa wote hawalali sasa hivi kila mtu anahangaika afanye nini. Nimshukuru Waziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye yuko huko kwa sasa wanapanga mipango na kuangalia wanasaidiaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru na Wabunge wa CCM na Wabunge wa Upinzani ambao wamekwenda kule…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba Serikali iongeze nguvu ya kuweza kupeleka vitu haraka kwa sababu watu wanalala nje na mvua zimeanza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mushashu.

Waheshimiwa Wabunge, tuzingatie matakwa ya Kanuni ya154 ili Wabunge wengine mnaonyanyuka kachangia tusiendeleze hili jambo kwa sababu Kanuni hiyo inataka Spika akishatoa pole basi anakuwa ameshatoa kwa niaba ya Bunge zima, wengine wote tunatakiwa kuendelea na mjadala.

Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia muswada huu. Kwanza niseme tu mimi niko kwenye Kamati na nishukuru Waziri wakati wa majadiliano kwenye Kamati yetu vipengele vingi wakati tunajaribu kushauri walivipokea kwa mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile niko kwenye Kamati basi nitatoa ushauri kwa ujumla kwa sababu mengi tumeshayajadili tukiwa kwenye Kamati. Kifungu cha kwanza ambacho napenda kushauri ni kifungu cha 7(2) juu ya Mwenyekiti wa Bodi. Nashauri uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi utokane na Mtanzania. Kifungu hicho kisomeke; "Bodi itakuwa na Mwenyekiti Mtanzania atakayeteuliwa na Rais mwenye uzoefu usiopungua miaka kumi ya utawala na mtaalam mbobezi katika masuala ya sayansi." Msisitizo hapa awe Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha pili ambacho napenda kushauri ni kutoka kifungu hicho hicho cha 7 ambacho kinazungumzia juu ya Wajumbe wa Bodi. Pia napenda kushauri au kusisitiza kwamba katika kifungu hicho cha 7 kuongezwe herufi (j) kwa ajili ya wawakilishi wanaotokana na taasisi za maabara lakini (h) iwe ni wawakilishi wanaotoka kwenye vyuo binafsi vya elimu ya juu. Nasema hivi kwa sababu mara nyingi watu binafsi tumekuwa tukiwaweka pembeni katika baadhi ya masuala lakini kwenye masuala mengine tunasisitiza kwamba watu binafsi au mashirika binafsi yashirikishwe. Hivyo basi, kwa kuweka kipengele hiki tutakuwa tumepata uwakilishi kutoka sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri vilevile kwenye kifungu cha 10(1) juu ya uteuzi wa Mkemia Mkuu. Kifungu hiki kinasema kwamba Mkemia Mkuu atokane na watumishi wa umma. Mimi nashauri kuwa Mkemia Mkuu atoke miongoni mwa Watanzania siyo tu atoke kwenye utumishi wa umma ili tusionyeshe ubaguzi kwa sababu kwenye sekta binafsi unaweza ukawa na mtu mzuri ambaye ana vigezo vya kuweza kufanya kazi hiyo lakini tu kwa sababu yeye yuko nje ya utumishi wa umma basi tukaamua kumuacha hata kama ana vigezo. Kwa hiyo, nashauri hilo suala tuliangalie kusudi tuweke uwiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ambalo napenda kushauri ni kile kifungu cha 45 kinachozungumzia nia njema. Naomba hilo neno "nia njema" lisiwepo kwa sababu watu wengine wanaweza wakatumia kipengele hicho cha nia njema kwa ajili ya kufanya mambo ambayo siyo sahihi au maovu. Kwa hiyo, nashauri eneo hilo au kipengele hicho kitolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niishie hapo kwa sababu mambo mengi yameshasemwa na wengi wameshachangia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucia Mlowe kwa kututunzia muda. Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga ajiandae.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kupata nafasi hii kuweza kuchangia Miswada hii miwili ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada hii muhimu kwa sababu ni Miswada ya kitaalam na watendaji wake wengi ni wataalam wa fani mbalimbali. Mkemia Mkuu wa Serikali amekuwa akifanya kazi nyingi sana za kitaalam. Nimebahatika kufanya kazi na Mkemia Mkuu wa Serikali kwa miaka mingi, kwa kweli wanafanya kazi nyingi sana za upelelezi na Idara ya Upelelezi inamtegemea sana Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutoa taarifa mbalimbali za kitaalam za matukio mbalimbali ya makosa ya jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Upelelezi kwa muda mrefu imekuwa ikishirikiana na Mkemia Mkuu na inaendelea kushirikiana nayo kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali ili kukamilisha upelelezi wa makosa mbalimbali ya kemikali. Idara ya Upelelezi inayo *Forensic Unit* ambayo ina-*cover* mambo ya kitaalam kwa mfano utaalam wa maandishi, *ballistic*, *finger prints, cyber crime* na utaalam mbalimbali lakini hivi karibuni idara hiyo pia imeanzisha utaalam mwingine zaidi wa mambo ya kemikali, *toxicology* na mambo mengine mengi ya *bombing* na *drugs.* Ili kupunguza *workload* ya Mkemia Mkuu wa Serikali anapaswa kusaidia kwa kiwango kikubwa kabisa maabara nyingine ambazo zitakuwa zinafanya kazi za kimaabara hapa nchini ikiwepo na maabara iliyo chini ya Idara ya Upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata mafunzo kwa matukio makubwa ambayo yamewahi kutokea hapo nyuma na hata ukichukulia tukio hili la sasa hivi lilitokea huko Kagera la tetemeko la ardhi. Mwaka 1998 Ubalozi wa Marekani ulilipuliwa hapa nchini na ulipolipuliwa Watanzania walikufa pale na viungo vyao vilitawanyika kwa sababu lile bomu liliwatawanya kwa hiyo utaalam wa *DNA* ulihitajika lakini tulikuwa hatuna huo utaalam. Tulikuwa hatuna utaalam wa *bombing* kujua kwamba bomu ambalo lilipiga Ubalozi wa Marekani lilikuwa kubwa kiasi gani, lilikuwa na uzito kiasi gani hivyo hivyo tukio hili la tetemeko la ardhi ambalo limetokea huko Kagera hatujui ukubwa wake ni kiasi gani. Labda kwa mfano tetemeko hili la ardhi lingekuwa limetawanyisha viungo ingebidi sasa hivi navyozungumza wataalam wa *DNA* wanatakiwa wawe kule Bukoba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata lile tukio kwa mfano la 1998 ilikuwa ni fundisho kubwa sana kwa Idara ya Upelelezi hapa nchini ambapo tulikuwa ni weupe kabisa kwenye mambo ya kitaalam ya *DNA* na hata ilikuwa ni fundisho kwa Mkemia Mkuu wa Serikali.

Nashukuru sana baada ya pale Idara ya Upelelezi ya *FBI* ilitushauri na ikasisitiza kwamba *Forensic Units* za Polisi ambazo ziko duniani ni lazima ziwe

zina-*cover* maeneo yote haya ambayo ni muhimu ya *toxicology, DNA* na kadhalika ndiyo inakuwa imekamilika kwa sababu itasaidia wataalam kwenda kwenye matukio haraka na wataweza kusaidia kurahisisha kazi za Mkemia Mkuu. Namna ya kuchukua vielelezo pale, namna ya kuchukua sampuli mbalimbali yote hiyo ni utaalam ambao unatakiwa na ni utaalam ambao unatakiwa usaidiwe sana na Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sheria hii imekuja wakati muafaka na nashauri kabisa Waziri atakapokuja ku-*wind up* aonyeshe nia kweli kwamba Mkemia Mkuu wa Serikali yuko tayari kusaidia maabara nyingine ambazo ni muhimu kabisa ili kuweza kurahisishia kazi. Sasa hivi kuna kesi nyingi sana za mauaji, za *drugs,* kama Kamati tumetembelea kwenye magereza mbalimbali na kule ambapo zimekwama unakuta labda wanasubiri taarifa ya Mkemia kuhusu mauaji au *drugs* hizo. Kwa hiyo, sheria hii inatakiwa itoe nguvu kwa maabara hizi nyingine ili ziweze kusaidia kazi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia kwenye vifungu mbalimbali ambavyo viko katika Sheria hii ya Mkemia Mkuu wa Serikali na nimeona kwamba mambo mengi yameguswa lakini kuna mambo mengine ambayo yanatakiwa kuguswa kwa mfano hilo la kuhakikisha kwamba Mkemia Mkuu ana-*support* maabara nyingine, ni muhimu liwe wazi na liwe na kifungu chake maalum cha kuhakikisha kwamba Mkemia Mkuu anasaidia maabara nyingine hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napata pia wasiwasi kwenye kifungu cha 4 ambacho kinatoa *supremacy* na *referral*. Sijapata lugha sahihi ya kuweka katika kifungu hiki, lakini labda Mheshimiwa Waziri angetusaidia, Mkemia Mkuu yeye ni *operational, regulator* sasa itakuwaje tena awe *supremacy* na *at the same time* yeye ndiyo apelekewe rufaa? Ningeshauri labda kifungu hiki kingehamishwa aidha kipelekwe kwenye Bodi ile iweze ku-*oversee* maabara zote nchini ikiwepo na hii ya Mkemia Mkuu kama kuna tatizo lolote ambalo linatokea. Kwa hiyo, natashukuru kama suala hilo lingeangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 5 pia nina wasiwasi nacho ambacho kinakwenda sambamba na kifungu cha 4 pale kinaposema kwamba *results shall be final and conclusive.* Hii *final* na *conclusive* inanipa wasiwasi kidogo kwa sababu ripoti ambazo zinatolewa na Mkemia Mkuu ni za utaalam chini ya Sheria ya Ushahidi pia ambapo ripoti hiyo inaweza kutolewa na utaalam mwingine.

Kwa hiyo, ni lazima kuangalia badala ya kuweka *final and conclusive* inaweza ikasema labda taarifa ambazo zinatolewa ni *unreliable.* Kwa hiyo, labda Waziri angekiangalia kifungu hicho na kukirekebisha ili ku-*come up* na *good provision.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Rajab. Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Tisekwa Bunga.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel ajiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Kwanza, nimpongeze Waziri na Naibu wake na kwa msaada wa Mwanasheria Mkuu kuweza kuuleta muswada huu tuweze kuujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo lingekuwa ni maoni katika hii miswada ambayo tunapatiwa ni suala zima la tafsiri kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili, wakati mwingine kunatufanya Wabunge kidogo tuweze kuelewa tofauti. Kwa mfano, unakuta Kiingereza kinasema kwamba Mkemia Mkuu anateuliwa na Rais lakini ukienda kwenye Kiswahili imetafsiriwa kwamba Mkemia Mkuu atateuliwa na Waziri. Sasa inakuwa inatupotosha kwenye upande wa Kiswahili na sisi wengine siyo wengi tunaojua lugha hii ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala zima la huu muswada, muswada uko vizuri, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuweza kupokea maoni ya Kamati lakini na sisi Wabunge tuna maoni kidogo ambayo tungeomba yaingie na tutaweza kuleta Jedwali la Mabadiliko.

Sehemu ya kwanza ni kifungu cha 5(2)(a) katika dawa zilizotajwa pale upande wa kemikali zimetajwa tu za viwandani lakini kiujumla kwenye huu muswada tuna kemikali za viwandani na za majumbani. Sasa labda Waziri atatuambia ilikuwa ni kosa la kusahaulika au kiutaalamu kwenye kifungu hiki cha 5(2)(a) kwamba kemikali za majumbani hazitakiwi kutajwa. Hiyo tutaileta kwenye *schedule of amendment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ni kwenye sifa za Mkemia Mkuu. Kifungu 10(1) kinasema kwamba Mkemia Mkuu atateuliwa na Mheshimiwa Rais. Sasa kwenye sifa pale kuna uzoefu na masuala ya elimu, lakini kuna kitu kimoja ambacho kimesahaulika. Leo hapa tuna miswada miwili, wa Maabara na Wataalam *(Chemist Professional Act)*. Sifa mojawapo ya Mkemia Mkuu ambaye atateuliwa na Rais awe ni yule ambaye amesajiliwa katika Baraza letu la Wataalam wa Mambo ya Kemia, hilo nalo ni muhimu sana. Kuna watu ndiyo wamesoma, wana elimu nzuri lakini unakuta kwamba hayuko *professional,* mtu ana miaka 20 na elimu yake. Hata wenye fani zingine za uhasibu kama sisi kama hujasajiliwa na Bodi ya Uhasibu wewe siyo mhasibu, ni karani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi kimesema sifa awe ni mtu ambaye amefanya kazi kwenye taasisi za Serikali. Kwa mujibu wa michango ambayo imetolewa na Wabunge hapa tunahitaji tupate Mwenyekiti wa Bodi ambaye hatakuwa tu na uzoefu wa mambo ya utumishi lakini pia awe na utaalam wa mambo ya kemia ili awe ni mtu ambaye anasimamia vizuri hiki chombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 7(2) katika ile Bodi nzima kuna mwakilishi anayetoka Wizara ya Afya. Ukiangalia katika ile Bodi nzima ina wataalam wa fani mbalimbali, kuna mtu anayetoa Hazina, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kwenye vyuo lakini tungeomba kwa sababu hii taasisi ni nyeti na ni mambo ya kitaalam sana hayahitaji ubabaishaji basi mwakilishi anayetoka Wizara ya Afya awe angalau na uzoefu hata wa miaka mitatu na elimu yake iwe ya mambo ya kemia ili aungane na yule mwingne ambaye anatoka kwenye upande wa vyuo ambaye amesomea mambo ya kemia, *pathology* na baiolojia na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye huu muswada, kifungu cha 13(1) tumeona kwamba katika teuzi za watu wa maabara Waziri anashauriwa na Mkemia Mkuu lakini ukienda kifungu cha 14 kwenye uteuzi wa wakaguzi Waziri anashauriwa na Bodi. Sasa ukienda kwenye *hierarchy* maana yake kifungu cha 13 pale Bodi inakuwa imerukwa, Waziri anashauriana moja kwa moja na Mkemia Mkuu kwa hiyo Bodi itakuwa haijui Mkemia Mkuu na Waziri wameshauriana nini. Kwa hiyo, tunahitaji kifungu cha 13(1) Waziri ashauriwe na Bodi. Kwa hiyo, hii nayo tutaileta kwenye *schedule of amendment. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 15 cha wajibu wa hawa wakaguzi kwenye kuteketeza zile sampuli, pale inaonesha kwamba huyu mkaguzi aidha yeye au kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zinaweza kuteketeza hizi sampuli ambazo zimetumika kwa mujibu wa hii sheria, lakini sasa ukiangalia hapa tunakuwa hatuna ule udhibiti *(internal control)*. Kwa hiyo, tungeomba kwamba ashirikiane na isiwe ni mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ni cha 39 cha mambo ya mahesabu. Tunahitaji tuangalie kwamba baada ya mwaka wa fedha kuwe na miezi mitatu ya kuandaa ripoti halafu tena miezi mitatu inaongezeka kwa ajili ya ukaguzi, halafu ndiyo inaenda kwa Waziri na kwenye Bunge. Hapa kwenye hii *Bill* yetu tumeweka miezi mitatu ambapo mahesabu yanakuwa hayajafungwa. Kwa hiyo, lazima iwe miezi sita kwa Waziri kupewa na miezi mitatu wawe wamekamilisha kufunga mahesabu kama ilivyo kwenye Sheria ya Fedha. Pia *director's report* ni muhimu sana iwepo kwenye hii taarifa ili sasa aoneshe mwenendo mzima wa hii taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa *professionals* na yenyewe inaendana na hii kwenye mahesabu hapa vipindi viko tofauti. Tutavileta kwenye *schedule of amendment* ili Bunge liweze kutuunga mkono ili tuendane na sheria zingine za mambo ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa yoye hayo, naomba kushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwa sababu nime-*move schedule of amendment* naomba nijikite zaidi katika utekelezaji wa sheria yenyewe ambayo tunaenda kuiunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuunda hii sheria na tukaipata ni hatua moja, lakini vilevile tunaweza tukaenda kwenye hatua nyingine ya kuhakikisha tuna *infrastructure* ambazo zitawasaidia wataalam kutekeleza sheria yenyewe. Ukiangalia kwenye maabara yetu ya Mkemia Mkuu tunazungumzia kuweka vifaa vya kisasa na *infrastructure,* lakini ukienda Mbeya utawakuta wako kwenye chumba ndani ya *Regional Hospital,* Arusha kuna umaliziaji wa jengo, kweli kuna jengo zuri lakini inahitajika limaliziwe, lakini pia inatakiwa tuzigeuze zile *center* zetu ambazo ziko huko mikoani badala ya kuwa ni sehemu ya kukusanya tu *sample* iwe pia ni sehemu ambayo wanaweza wakafanya kazi yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza yote hayo unaweza ukaweka *infrastructure,* ukienda Muhimbili Mloganzila utaona wametenga eneo zuri kwa ajili ya *pharmaceutical industry* ambapo tukizingatia hilo tutapata sehemu

ambapo tutajenga kiwanda cha dawa na kitatusaidia kufundisha wataalam wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukishaweka hizo *structure* zote kuna suala linalokuja kwamba, je, kweli tuna *brain ambazo* zinaweza kufikiri katika hiyo *level* ambapo tunazungumzia masuala ya *DNA*? Kwa hiyo, ni lazima kama Taifa tufikirie tunatengenezaje kizazi ambacho kina uwezo wa kufikiri kama waliogundua *DNA*. Pia tuwe na uwezo wa kufikiria kama wale waliogundua vifaa ambavyo tunavitumia. Kwa sababu hata mfagizi wa maabara akikaa kwa muda mrefu na wataalam suala la kupima anaweza akajifunza na akapima na akatoa majibu sahihi, lakini la msingi, je, tuna *brain* kubwa za kuweza kufikiri katika hali ya utupu yaani kufika mahali pa kuona hayo mambo makubwa sasa *(intelligent quotient)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu kwenye maabara kama hizi kama Marekani sasa hivi wanasema kwa miaka 10 ijayo wanatengeneza namna fulani ambapo baba na mama wanaweza wakakutana wakatumia *genetic engineering technology* waka-*boost intelligence quotient* ya watoto na sisi Wabunge utakuta tunaenda huko Marekani ili tuzae watoto wenye uwezo mkubwa wa kufikiri.

Vilevile wanasema wanafanya *research* kwa kutumia hii hii *genetic engineering* kuhakikisha kwamba wana uwezo wa kuwa na *technology* ya ku-*boost adult intelligent quotient* ambayo hiyo ikitokea nitashauri Wabunge twende na sisi ili itu-*boost* tufike mahali kwenye mambo ya Kitaifa tuwe kitu kimoja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu na mimi baadaye nita-*move schedule of amendment,* leo sisi UKIMWI tunaona ni janga na kweli ni janga lakini *is a business opportunity*. Tungekuwa na *brain* kubwa tunaweza tukakaa chini tukajifungia kwenye maabara kama hizi wakati Marekani wanatafuta dawa na sisi tunatafuta dawa. Tukipata sisi na tukaweza kupata hakimiliki ya hiyo *technology* na kutumia Usalama wa Taifa na jeshi letu kuficha hiyo siri tunaweza na sisi tukauza hiyo *technology* na ikawa ni moja ya chanzo cha mapato katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Wazungu wameendelea na wamefika walipo siyo kwa sababu wana rasilimali nyingi, ni kwa sababu wana siri za kimaumbile ambazo ndizo wanazitumia kutuburuza kama wanavyotaka. Leo tunaongea hapa Bungeni wanaweza wakawa na uwezo wa kujua tunachokifanya, lakini vyote vinapatikana kwenye maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema tunakwenda kutunga sheria hapa na nime-*move schedule of amemdment* baadaye nitakuja kwenye hilo

lakini nachokisema ni kwamba kuwa na sheria, maabara nzuri na kila kitu ni jambo moja, lakini la msingi zaidi *do you have brains?* Naambiwa hapa nenda kwenye muswada, nikienda kwenye muswada kidogo, nisingependa sana niende kwenye muswada kwa sababu nita-*move schedules of amendment,* hii Ofisi ya Mkemia Mkuu iweze kupata *funding* kama linavyopata Bunge ambazo haziingiliwi. Ofisi hii iwe na *power* kubwa ya kufanya *research, research* kubwa kama hizi zinatakiwa watu waliotulia akili lakini tutayarishe watoto wetu toka wakiwa tumboni *(nutrition).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Musukuma alivyosema hapa kuhusu suala la mahindi na kilimo nilimuelewa sana na alivyokuwa anasema tulime bangi nilimuelewa sana, kwa sababu leo kama watu wetu wanalima mazao mengi ya chakula wanakosa soko na wanazuiliwa kuuza nje maana yake wakulima wetu watakata tamaa ya kulima na kiwango cha lishe kitashuka kwenye Taifa letu. *Impact* yake kubwa ni kwamba lishe ya watoto wetu itashuka na udumavu utaongezeka. Udumavu ukiongezeka tunapozungumzia kwenda kuwa na kizazi chenye uwezo wa kufikiri katika *level ya higher mind* hatuwezi kukipata kwa sababu udumavu umezidi katika nchi yetu. Ndiyo maana nasema kwamba pamoja na hayo yote ambayo tunayafanya hapa na tuta-*move schedules of amendments, let us think of making a generation* yenye *brain* kubwa inayoweza kufikiri kwa kiwango kikubwa. Kwa sababu kuwa daktari ni kitu kimoja lakini kuwa na uwezo wa kufikiri katika hali ya utupu ni kitu kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wana uwezo wa kutoka kwenye huu ubongo wa kawaida wanaenda kwenye siri za kimaumbile wanarudi wanaleta vitu vilivyo kwenye siri ya kimaumbile kwenye ubongo wa kawaida wanaviandika vinakuwa teknolojia wanatuuzia. Wakati mwingine wanaleta *solutions* za tiba kwa sababu wametayarishwa toka wakiwa wadogo tumboni kwa mama zao kwa lishe kubwa na vitu vingine na tunatapata *generation* inayoweza kufanya vizuri. La sivyo, tutaunda maabara mwisho wa siku tutakuwa na watu ambao kazi yao ni kukusanya *sample,* kupima, wazungu wanakuja wanachukua *sample* zetu wanatazama kwa kutumia *high mind* wanagundua vitu, wanatugeuza soko la teknolojia, soko la vifaa tiba, soko la kila kitu kwa sababu uwezo wa kufikiri katika hali ya juu hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nizungumzie kwa namna hiyo na naamini Profesa ananielewa vizuri ninapozungumzia kufikiri katika hali ya juu. Naomba niseme suala hilo ni la msingi sana, Waziri nakujua ni msikivu naomba iandike na tufikirie tutaunganishaje Wizara zote. Ulaya wamefika hapa walipo kwa sababu wanasema kuna mtu mmoja anaitwa Pilato alikuwa anatembea kwa kuangalia jua lakini alichokifanya baadaye akaanzisha Chuo Kikuu cha Hesabu na hesabu ina tabia ya kujaza misuli ya ubongo kama unavyobeba chuma na ndiyo hapo akagundua teknolojia, watu wakasoma pale wakaacha falsafa wakaanza

kugundua na ndipo Ulaya ikaenda juu. Leo Tanzania unaambiwa hesabu huwa ni somo la kawaida ambalo watoto wanafeli. Ukishasema hesabu na sayansi ni kawaida watoto kufeli Taifa hilo limekufa kiroho na kiakili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatakiwa turudi huko tufikiri tunapataje hawa watoto. Wakati mwingine tunampa Mheshimiwa Ndalichako watoto ambao wamedumaa hata wawachape kwa umeme hawataelewa. Kuanzia leo turudi kwenye kufikiria tunawatengenezaje watoto ili baadaye tupate Bunge ambalo halibishani, linatumia muda mwingi kufikiri mambo ya kitaifa na kawaida ya akili kubwa inapofika mambo ya msingi ukweli ni mmoja wanakwenda wakitofautiana mwisho wa siku wanakutana pale juu wanakubaliana, ndiyo sifa za akili kubwa. Hizo ndizo akili tunazozitaka na tuzitayarishe leo ili miaka 20 ijayo tuwe na Taifa na Bunge zuri ambalo linazungumza masuala mazito ya kitaifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mollel utatutafutia wafadhili wa kutupeleka huko maana wote tunataka watoto wetu wakizaliwa wawe na akili hiyo kubwa na nzito namna hiyo. Wewe umesema unataka kwenda huko na nimeona watu wakikushangilia inaonekana humu wako wengi, kwa hiyo, nadhani utaambatana na kundi kubwa. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mke wangu bado mdogo tutaenda. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Sawa. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika muswada ulioletwa hapa Bungeni. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote walioshiriki katika uandaaji wa muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati najaribu kupitia taarifa ya Kamati ya sekta husika, kimsingi wameridhia pamoja na mapendekezo machache sana ukizingatia kwamba Muswada huu umefanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa ndiyo maana naendelea kuwapongeza, hongereni sana kwa Muswada mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika maeneo machache kama ifuatavyo na la kwanza, ni ukweli usiopingika kuhusu umuhimu wa maabara ya Mkemia Mkuu lakini kwa kipindi kirefu sana kulikuwa na ufinyu mkubwa sana wa kibajeti kiasi kwamba zile kazi ambazo walitakiwa kuzifanya kwa ufanisi hawakuweza kuzifanya. Kwa kuletwa kwa Muswada huu na kuwa

na *subvote* yake ambayo itasomwa kupitia Wizara husika, naamini Idara hii itatengewa pesa za kibajeti za kutosha. Tafsiri ya bajeti ni kwamba unaipa uwezo mkubwa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuweza kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Ofisi hii ilikuwa na ufinyu mkubwa sana wa bajeti. Taarifa zinaonesha kwamba kuna kipindi walikuwa na uwezo wa kuwa na mapato ya shilingi bilioni mbili. Naomba niipongeze Wizara kwa kushirikiana na Mkemia Mkuu wa Serikali wamepandisha kiwango cha mapato kutoka shilingi bilioni mbili mpaka kufika shilingi bilioni 10. Ukitaja shilingi bilioni 10 inaweza ikaonekana kama ni pesa nyingi lakini ukilinganisha na majukumu yake na hasa kutokana na kuongezeka kwa kesi za kijinai ambazo zinahitaji uchunguzi ufanyike ili kesi ambazo zimerundikana ziweze kupatiwa ushahidi kiasi hiki cha pesa hakitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote ni mashuhuda kwamba wakati polisi wamekuwa wakikamata hayo yanayoitwa madawa ya kulevya lazima taarifa kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ipatikane ambayo inathibitisha kwamba haya kweli ni dawa za kulevya au sivyo. Nitaomba niunganishe na wachangiaji wengine ambao wanasema kwamba ni vizuri kazi hii ikaachiwa polisi, mimi nasema hapana. Nasema hapana kwa sababu gani?

Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa mashuhuda tukipata taarifa kwamba kuna watu ambao wanabambikiziwa kesi kutokana na baadhi ya polisi kutokuwa waaminifu sasa kama tutampa na kazi yeye ndiyo a-*prove* kwamba sampuli hii ni madawa ya kulevya au la maana yake tunataka akamate yeye mwenyewe, afanye uchunguzi yeye mwenyewe, akatoe ushahidi yeye mwenyewe jambo hili halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi itasaidia kwamba hata pale ambapo mahakamani unapelekwa ushahidi kutoka kwenye chombo ambacho ni *independent* ushahidi ule utaaminika na kila mtu atajua kwamba ametendewa haki. Sikubaliani hata kidogo pamoja na polisi kuwa na kitengo chao cha *forensic,* lakini wafanye kazi zile ambazo zitawasaidia katika kufanya uchunguzi wao ili kubaini matukio lakini siyo kupata uhakika kwamba ushahidi unaopelekwa mahakamani wao wawe ndiyo wameutengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni mashuhuda kuna kipindi tuliambiwa zimekamatwa dawa za kulevya mara unaambiwa kwamba ilikuwa ni unga wa muhogo, sijui unga wa mahidi. Sasa tukienda kwa utaratibu huu sidhani kwamba tutakuwa tunatenda haki. Kwa kukitengea kitengo hiki bajeti ya kutosha tuna imani kabisa Ofisi za Kikanda zitaimarishwa na uchunguzi ambao unafanyika majibu yake yatapatikana kwa kipindi muafaka na hivyo huu mlundikano wa sampuli nyingi ambazo lazima zipelekwe Dar es Salaam itakuwa imepungua kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba muswada huu umetendewa haki na Kamati ya Kisekta niishie kwa kutoa huo mchango mdogo na kuunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kandege. Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi nitachangia kwa kutaka baadaye nije nipate ufafanuzi zaidi hasa kuhusiana na *Chemist Professionals Act*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia majukumu ya Baraza pamoja na mambo mengine ni kupitisha vile vyuo ambavyo vitafundisha hawa ma-*professionals*. Siku za nyuma tumeona matatizo ya vyuo hivi binafsi ambavyo vimekuwa havifuati maadili na kwa ajili hiyo vimekuwa vinatoa mafunzo na vyeti ambapo watumishi wake wakienda kwenye kazi wanakuwa *substandard* katika utumishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika majukumu ya Baraza litusaidie kuangalia vile vyuo vyenye *intergrity* ambavyo vinaweza kuruhusiwa kutoa hao wataalamu. Nasema hivi kwa sababu vyuo vingine vya binafsi vinapenda vifaulishe na kutoa watu ambao kwa kweli wakienda sehemu za kazi hawafanyi sawasawa na vyeti vile. Nia yao ni kutoa vyeti hivyo ili waweze kuendelea kuonekana wanafanya kazi. Nimeshuhudia sehemu mbalimbali ambapo wataalamu wamekuwa wakitoa majibu ya utafiti waliofanya na kuonesha ni vitu viwili tofauti sana wakati wako *qualified.*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nataka nizungumzie matumizi ya hivi vyeti ambavyo hao wataalamu watapewa wakishaandikishwa na Baraza hili. Wataalam hao kwa vile hawako wengi utakuta mtaalam mmoja amejiandikisha katika sehemu tatu au nne za kufanyia kazi na cheti chake kinatumika katika sehemu hizi mbalimbali. Utakuta maabara hasa za hospitali binafsi zinatumia vyeti vya wafanyakazi ambao hawafanyi kazi pale, wamelipwa ili wakija wakaguzi wanaona vile vyeti viko pale na wanaona kweli hii maabara iandikishwe maana ina wataalam na kumbe vile vyeti vilivyotumika wale wataalamu hawafanyi kazi katika maabara zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda Baraza na Kamati zitakazoundwa zitusaidie kusimamia kanuni za maadili na mwenendo wa wataalamu wawe na uhakiki wa kuonesha kwamba kweli mtaalam ambaye ameandikishwa katika maabara ile ndiyo yuko pale na anafanya kazi pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ninaloliona katika maabara zetu siyo nyingi, lakini *relatively* za hali ya juu maana nimepita maabara nyingi kwa sababu zangu mwenyewe, unakuta mkemia yule anayefanya kazi pale anaweza kutumia *reagents* ambazo zimepitwa na wakati. Mara nyingi hizi *reagents* zinatumika kwa vile mwenye maabara hataki kupata hasara. Hawezi kusema hapana hizi tusizitumie kwa vile zime-*expire* matokeo yake zinatoa majibu ya *analysis* ambayo siyo sahihi. Sasa tujue hizi Kamati zitakuwa na jukumu la ku-*inspect* kila wakati kuona *reagents* zinazotumika kufanya *analysis* katika sampuli mbalimbali zinakuwa hazijapitwa na wakati ili tusitoe majibu ambayo sio sahihi kutokana na *reagent* ambazo zime-*expire*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu kwa vile mara nyingi ina tatizo la ukatikaji wa umeme na *reagents* nyingine zinatakiwa zikae katika *temperature* fulani na majenereta ya sehemu zile za kazi hayafanyi kazi zile *reagent* huwa zinabadilika matokeo yake hata yule *analyst* akifanya kazi atapata majibu ambayo sio sahihi.

Naomba Kamati hizi zitakazoundwa pamoja na Baraza lenyewe liwe na majukumu ya ziada ya kufanya *inspection* ambayo ni *ad-hock* maana tumeshaona wakitoa ratiba kwamba leo wanapita kunawekwa mambo ya ajabu ajabu, wanaletwa wataalam ambao hawapo katika maabara ile na kuoneshwa kwamba yuko pale, siku hiyo zitakuwa *displayed reagent* ambazo ni nzima na wakati mwingine maabara nyingine wanakodisha vyombo kutoka makampuni mengine *inspection* ikishapita vile vifaa vya maabara vinarudishwa kwa wenyewe.

Kwa hiyo, ningeshauri Muswada huu pia uzingatie haya ninayozungumza hapa ili utafiti utakaokuwa unafanyika katika maabara zetu na hata tukiwa na wataalam ambao ni wasomi zifanywe kwa uhakika na yapatikane majibu ambayo ni ya kisayansi na sio ya kulipua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kaboyoka. Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwenye hii miswada miwili halafu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto atafuata.

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi niliyopata. Kwanza, napenda kuanza kwa kueleza masikitiko yangu kwamba hizi *document* tunazopitia za miswada mbalimbali hakuna hata moja ambayo mimi nimeweza kui-*access*. Nashindwa kuelewa ni kwa nini. Najua Mbunge asiyeona niko peke yangu lakini sitaki kufikiri kwamba Bunge

halinithamini, lakini najua kwamba kukiwa na ile *will, accessibility* ya hizi *document* naweza kuipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuitambua Wizara ya Elimu ambayo inanijali sana kwa sababu wao wanahakikisha kwamba nimepata *document* zao *at least two days in advance,* nimezisoma lakini hakuna Wizara nyingine yoyote ambayo inanikumbuka, kwa hiyo nasikitika kwa hilo. Hata *Order Paper,* tangu tumeanza Bunge hili bado sijaweza kupata *Order Paper* yoyote katika *braille*. Kwa hiyo, naomba nisionekana niko peke yangu, nafikiri nina haki sawa na Wabunge wenzangu, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichangia hoja iliyo mbele yetu napenda kuchangia kwa kifupi tu kuhusu Mkemia Mkuu wa Serikali na Bodi yake. Wabunge wengine hapa walichangia tangu juzi wakisema kwamba hii Bodi haina wanawake, mimi naenda mbele zaidi nikisema hii Bodi pia inatakiwa iwe na mtu mwenye ulemavu kwa sababu kuna masuala mbalimbali ambayo Bodi ikiwa na mwakilishi ambaye anaelewa masuala ya watu wenye ulemavu atakuwa katika *position* ya kuishauri ipasavyo. Kwa mfano, kuna watu wenye ulemavu mbalimbali hasa ulemavu wa akili ambao wanabakwa na wengi wanabakwa na *family members* iwapo katika *composition* ya hiyo Bodi atakuwepo mtu mwenye ulemavu atakuwa katika *position* ya kutetea masuala kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunavyojua ulemavu pia unatokana na *genetics,* kwa hiyo, wale akina mama wanaokuwa wajawazito ambao kwa njia moja au nyingine watoto wao watazaliwa na ulemavu, akiwepo mtu katika hii Bodi ataweza kutoa ushauri na kuandaa hawa akina mama kisaiokolojia ili watakapojifungua wakiwa na watoto wenye ulemavu watakuwa wameshaelewa na itapunguza matatizo ya akina mama au akina baba kuwatelekeza watoto wao kwa ajili ya ulemavu au kuwa-*abandoned.*

Kwa hiyo, nashauri Waziri anayehusika na huu muswada amuingize katika hii Bodi mtu mwenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha, nitaeleza baadaye yale mambo yote uliyoyatoa ambayo yanahitaji kujibiwa na Ofisi ya Spika.

Kwa sasa nimkaribishe Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya kuhitimisha hoja.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kutumia fursa hii kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali zaidi wakichangia kwenye Muswada wa Kuunda Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, lakini pia Muswada wa Kutunga Sheria ya Kusimamia Wataalamu wa Kemia ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita zaidi kutoa ufafanuzi kwenye hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwenye muswada huu wa pili unaowahusu wataalamu wa kemia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza, naomba uniruhusu nitoe pole na salamu za rambirambi kwa wahanga wa tetemeko la ardhi lililotokea kule Bukoba na mikoa ya jirani ya Kanda ya Ziwa. Pia niwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia kwenye miswada hii, michango yao tumeichukua kwa umakini na tumeifanyia kazi na mengi ya maoni ya Wabunge kwa kweli yalilenga kuboresha sheria hizi. Kwa kiasi kikubwa maoni yao tumeyazingatia na mengi tumeyachukua. Kuna machache hatukuyachukua na tuna sababu za msingi za kufanya hivyo na nitatumia fursa hii kufafanua kwenye baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kabla ya yote, nitoe neno la utangulizi kama ambavyo wasemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani walivyotoa utangulizi kwenye hoja zao mbalimbali. Kwa mfano, Mheshimiwa Esther Matiko aliyesema kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani alizungumzia kwenye ukurasa wake wa pili kwamba Operesheni UKUTA ingeweza kurejesha utawala wa sheria unaojali demokrasia na haki za binadamu. *(Makofi)* **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusoma hii taarifa yake kwa umakini sana pamoja na ile ya mwenzake nikabaini kwamba pengine wasemaji hawa hawajui tafsiri halisi ya demokrasia, uhuru na haki za binadamu kama ambavyo zinasemwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Naomba kusema tu kwamba uhuru wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko utaanzia kwake pale alipo, lakini utaishia pale ambapo uhuru wa mwenzake unaanza. Vilevile haki za Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko zitaanzia pale kwake anavyozitambua yeye lakini zitaishia pale ambapo haki za mwenzake zinaanza. Sasa tukienda kwa msingi huo maana yake tutaheshimiana kwenye nchi na kwenye jamii. *(Makofi)* **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba yetu inatoa uhuru lakini pia inaweka mipaka kwamba mimi nina haki ya kufanya shughuli zangu mbalimbali za kisiasa, za kijamii lakini haki hizi zinalindwa na Katiba kama ambavyo tumesema awali lakini pia haki hizi zinawekewa mipaka kwamba pale ambapo haki zangu zinaishia basi haki za wengine nao kufanya siasa, kufanya shughuli mbalimbali za kijamii zinaanza. Kwa maana hiyo uhuru, haki pamoja na mipaka hii ambayo inawekwa na Katiba kwa kweli inalenga kutufanya tuishi kwa kupendana, kwa kushirikiana na bila kugombana. Kwa mfano, kama wewe unaona una haki ya kufanya maandamano usisahau kwamba na wenzako wana haki siku hiyo ya kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo. **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**TAARIFA**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo haki ya mtu mmoja…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo, Mheshimiwa Waitara, Taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa Kanuni ile ile iliyotumika kuzuia maneno hayo kwenye hotuba zetu mbalimbali inamhusu na yeye na wewe Mheshimiwa Naibu Spika bahati nzuri ulikuwa kwenye Kiti ukatoa *ruling* kwamba mambo hayo yasiingizwe kwenye *Hansard.*

Kwa hiyo, tunaomba hayo yote anayoyazungumza yafutwe aende kwenye hoja ambapo ni kujibu hoja mbalimbali kuhusu Miswada miwili aliyowasilisha Bungeni hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Kanuni ya 86 inatoa masharti kuhusu muswada unapokuwa unasomwa Mara ya Pili, nimekumbushwa hapo kwamba mambo yanayojibiwa ni yale ambayo tuliyakataa kwa mujibu wa Kanuni ya 86 kwa maana hiyo hayapo kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kwa hiyo, yanapojibiwa kule kwenye *Hansard* hayatakutwa sasa mtu hataweza kujua yanajibiwa kutoka wapi. Kwa hiyo, nakusihi kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ujielekeze kwenye hoja zile zilizotolewa katika muswada. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kama yameondolewa kwenye

*Hansard* na mimi nafuata maelekezo yako sitajibu hoja hizo. Nilidhani kwamba kwa kuwa yameandikwa basi bado yamo kwenye *Hansard,* kwa kuwa yamefutwa basi tunaendelea na hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Wanataaluma ya Kemia ambao umechangiwa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, pia kuna maoni ya Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Godwin Mollel na Mheshimiwa Nagenjwa Livingstone Kaboyoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kujibu hoja mahsusi za Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambaye kwenye kifungu cha 4(3)(c) alipendekeza kifutwe ili kuzuia Baraza kutokujiingiza kwenye biashara na badala yake Baraza libaki kwenye kusimamia shughuli na maslahi ya wanataaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yetu ya ufafanuzi kwenye kifungu hiki ni kwamba hiki kifungu kinalenga kuliruhusu Baraza kukopa ama kukopeshwa ili liweze kujiendesha. Hivyo ni vema kifungu hiki kikabaki kama kilivyo na sababu ni rahisi tu kwamba tunapotunga Baraza maana yake mabaraza haya yanakuwa ni *corporate entity* ambayo inaweza ikashtaki na inaweza pia ikashtakiwa. Kwa maana hiyo, kinakuwa ni chombo kamili kabisa ambacho kinaweza kufanya shughuli mbalimbali za kibiashara na hata kumiliki mali. Kwa msingi huo, Baraza hili litafanya kazi yake kama vile taasisi nyingine ambazo ni *corporate entities* zinavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na Mheshimiwa Lucy Owenya walipendekeza kifungu cha 4(4) kifutwe kwa kuwa kinawanyima wanataaluma uhuru wa kufanya kazi zao kwa ufanisi. Maelezo yetu ni kwamba muswada huu ni wa Serikali ambapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mshauri mkuu wa shughuli mbalimbali za Serikali kwenye masuala yote yanayohusu sheria. Hivyo ni busara Mwanasheria Mkuu wa Serikali akahusika katika utekelezaji wa sheria yenyewe na kwa maana hiyo kifungu hiki hatutakifuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani alipendekeza kwenye kifungu cha 4(7)(e) kiboreshwe kwa kuongeza neno "*lecturer*" baada ya neno "*senior.*" Serikali imepokea ushauri huo na itazingatiwa kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo na

Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, walipendekeza kwa pamoja kifungu cha 4(7)(h) kifutwe wakidai kwamba hakijaeleza huyo mwakilishi kutoka Idara Kuu ya Utumishi wa Umma anayependekezwa kuwa Mjumbe wa Baraza ni nani, atakuwa na sifa gani na kwa nini anapendekezwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wanataaluma ya Kemia?

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yetu ya ufafanuzi ni kwamba Serikali imepokea ushauri huo na tumeuzingatia na sasa tunarekebisha kifungu cha 4(7)(h) kwa kufuta kifungu hicho na kumbadilisha mwakilishi kutoka Menejimenti ya Utumishi wa Umma na badala yake kumweka mjumbe mwenye taaluma ya kemia kutoka maabara binafsi. Hivyo, kipengele cha (h) sasa kitakuwa kinasomeka; *"a chemist representing private laboratories."* Tunawashukuru Wajumbe wa Kamati pamoja na Wabunge hawa niliowataja kwa mapendekezo yao ambayo yametupa na sisi ufunuo kidogo tukaona kweli kuna haja ya kushirikisha sekta binafsi kwenye Baraza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na maoni kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mheshimiwa Kangi Alphaxard Ndege Lugola, Mheshimiwa Lucy Owenya pamoja na Mheshimiwa Mwita Waitara kwamba kwenye kifungu cha 4(7)(a) hadi (i) wanataaluma wachaguane wenyewe badala ya sheria kumpa mamlaka Mheshimiwa Waziri kuteuwa Wajumbe wa Baraza hali ambayo walidhani italifanya Baraza kukosa uhuru wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yetu ni kwamba Baraza la Wanataaluma ya Kemia linaloundwa chini ya Muswada wa Sheria hii ni utekelezaji wa Sera ya Afya ya mwaka 2007 ambayo imetamka kuwa Mabaraza ya Taaluma yataendelea kuundwa ili kuratibu wanataaluma mbalimbali wa sekta ya afya. Hivyo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya afya ambaye ndiye msimamizi wa Sera ya Afya ana wajibu wa moja kwa moja wa kuunda na kusimamia Mabaraza yote yanayoanzishwa chini ya Sera ya Afya. Aidha, wanataaluma wako huru kuanzisha na kusajili umoja wao chini ya sheria nyingine mfano kupitia *The Societies Act,* Sura ya 337 na kujisimamia wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa labda nieleze tu, nilipokuwa nikisikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali niligundua kwamba pengine tafsiri ya neno "*professionals*" halifahamiki vizuri. Kiuhalisia ni kwamba duniani ili mtu uitwe mwanataaluma ama *professional* ni lazima uwe na vitu, kwa uchache ni vitatu vifuatavyo; cha kwanza uwe umesomea taaluma yenyewe, lakini cha pili ukubalike na wanataaluma husika kama na wewe ni mwanataaluma mwenzao na cha tatu usajiliwe na mamlaka ya Kiserikali inayoratibu shughuli za utekelezaji wa taaluma ambayo umesomea.

Sasa ukiwa na vitu hivi vitatu tunaweza tukasema wewe ni *professional.* Kwa maana hiyo, hapa tunazungumzia ya kwamba tunaunda Baraza hili la Wanataaluma ya Kemia ili kupata ile sifa kwamba wanataaluma wa kemia sasa wasajiliwe, watambulike na wawe *regulated* na chombo cha Kiserikali ambacho kitasimamia maadili na vitu vingine vinavyohusu taaluma ya kemia nchini. Wao wenyewe wanataaluma wa kemia wanapaswa, baada ya kuwepo kwa sheria hii sasa na kutambulika rasmi, waunde taasisi yao ya hiari ambapo mtu akitaka kuwa miongoni mwa mwao aweze kujiunga, atambulike na hapo sasa atakamilika kuwa *professional* wa masuala ya kemia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maombi kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambapo wanapendekeza kifungu cha 9(1) kitoe uhuru kwa Mheshimiwa Waziri kuteua Msajili wa Baraza kutoka ama ndani ya utumishi wa umma au sekta binafsi. Tumeyatafakari maoni haya na maelezo yetu ni kwamba Baraza hili limeanzishwa kwa mujibu wa Sera ya Afya na hivyo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya afya ambaye pia ndiye msimamizi mkuu wa sera hii ni vema akateua Mtendaji Mkuu wa Baraza.

Aidha, kwa kuwa Baraza hili ni chombo cha Serikali ni vema Msajili wa Baraza akatoka miongoni mwa watumishi wa umma. Hii ni katika msingi tu kwamba kwenye utumishi wa umma kuna utamaduni wake ambapo tunaamini kwamba Baraza hili likipata mtu ambaye anatokana na utumishi wa umma ataendeleza utamaduni ule ambao upo ndani ya utumishi wa umma na pengine kutoka kwenye sekta binafsi kunaweza kukaathiri utekelezaji wa majukumu ambayo yanaendana na tamaduni za ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maoni kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani ambapo wanapendekeza kifungu cha 14(1) kiboreshwe kwa kuongeza maneno; "katika chuo au taasisi inayotambulika," baada ya maneno "kipindi cha mwaka mmoja."

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepokea ushauri huo na tumesema tutauzingatia ushauri huu wakati wa kuandaa kanuni chini ya kifungu hicho cha 14(2). Tumeona hakuna haja ya kuweka kwenye sheria, tutaenda kuweka kwenye kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe kwenye kifungu cha 14 alipendekeza kwamba Serikali inapaswa kuweka fungu la fedha kwa ajili ya kuwalipa wakemia wanapokuwa katika mafunzo kwa vitendo. Ushauri huu pia tumeupokea lakini tunaona ni jambo la kiutekelezaji, litafanyiwa kazi utekelezaji wa sheria utakapoanza. Hii inatokana na msingi kwamba wanataaluma wengine ambao wanasajiliwa chini ya Mabaraza ambayo yako chini ya Wizara ya Afya kama vile wanataaluma ya udaktari wa meno na udaktari wa tiba na wauguzi, wanapokuwa kwenye mafunzo kwa vitendo

*(internship)* huwa wanalipwa 80% ya mshahara ambao angepaswa kulipwa mhitimu ambaye ameajiriwa rasmi kwenye cheo husika. Kwa maana hiyo, haitakuwa tofauti pia kwa wanataaluma hii ya kemia ambao wako chini ya Wizara ileile moja ya Afya. Tumesema katika utekelezaji Serikali itaweka utaratibu wa kulishughulikia jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maoni mengine kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani ambao wanapendekeza kwenye kifungu cha 13 na cha 14, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ishirikishwe katika sheria hii kwa kuwa vifungu hivyo vina majukumu ambayo yanagusa Wizara hiyo moja kwa moja. Serikali imepokea ushauri huo lakini marekebisho hayo yamezingatiwa katika Jedwali la Marekebisho ya Sheria ambapo kifungu cha 6(h) kimerekebishwa. Tumepokea ushauri huo na tutaleta kwenye Jedwali la Marekebisho hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maombi mengine kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwenye kifungu cha 18 wanapendekeza viongezwe vifungu viwili vidogo kama ifuatavyo; kifungu cha 18(4) ambacho kinasoma; *"any person aggrieved by the decision of the Council made under subsection (1) may appeal to the Minister ninety days from the date of the decision of the Council."*

Vilevile wanapendekeza kwenye kifungu cha 18(5) ambapo wanataka isomeke kwamba, *"any person dissatisfied by the decision of the Minister may appeal to the High Court within ninety days from the date of the decision of the Minister."* Maelezo yetu ni kwamba tunapokea ushauri huo lakini hata hivyo maoni hayo tayari yamezingatiwa katika kifungu cha 34 cha muswada huu. Aidha, haki ya kukata rufaa Mahakama Kuu ni haki ya msingi ya Kikatiba ambapo mtu ambaye hajaridhika na maamuzi yoyote ya chombo cha chini ya Mahakama Kuu ana haki ya kukata rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tu Waheshimiwa Wabunge utaratibu huu naweza nikasema ni *generic* kwenye sheria zote ambazo ziko chini ya Wizara ya Afya ambazo zinaanzisha Mabaraza mbalimbali ya taaluma. Kama umesajiliwa chini ya Baraza la Madaktari wa Tiba na Madaktari wa Meno Tanzania *(The Medical Council of Tanzania)* ukawa daktari kama mimi hivi ambavyo nimesajiliwa, ukishtakiwa kwenye Baraza kwa makosa ya kitaaluma, ukahukumiwa na haukuridhika maana yake unaweza ukakata rufaa kwenda kwa Waziri mwenye dhamana na mambo ya afya.

Pia ukikata rufaa ukampa maelezo yako akakusikiliza na bado uamuzi ukabaki ule ule ama akatoa uamuzi mwingine ambao pia haujaridhika nao, unapata haki ya kuendelea mbele kwenye Mahakama Kuu kukata rufaa kwa ajili ya uamuzi wa kisheria ambao utatolewa na mahakama huko mbele.

Kwa hiyo, hakuna haki ambayo inaweza ikazibwa kwa kuweka tu sheria kwamba wakate rufaa kwa Waziri. Hii ni fursa kwamba pengine Waziri anaweza akaamua kwa kuzingatia mambo mengi zaidi mbali na kuzingatia sheria na kanuni anaweza akazingatia pia hali ya usalama na mambo ya siasa na vitu vingine kama hivyo. Kwa hiyo, hii ni fursa ya muhimu sana ambayo wananchi wanaipata kupitia kwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maombi mengine kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pamoja na maoni kutoka kwa Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ambao kwa pamoja wanapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 4(7)(h), kifungu cha 8(4), kifungu cha 9(1), kifungu cha 11(1)(b), kifungu cha 13(2)(a),(i)(ii) na (iii), kifungu cha 16(1), kifungu cha 18, kifungu cha 28(2) na kifungu cha 33(2).

Maelezo yetu ni kwamba Serikali imepokea mapendekezo hayo, tumeyafanyia kazi na tumeyaingiza kwenye Jedwali la Marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maoni vilevile kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani yanayohusu kifungu cha 21(1)(a), (c)na (f) ambapo wanapendekeza viondolewe ili kulifanya Baraza kuwa huru wakati wa utekelezaji wa majukumu yake bila kuingiliwa na Serikali. Lengo la Baraza kutengewa fedha na Serikali ni kuliwezesha kuanza kufanya kazi katika hatua za awali ili Serikali itakapojitoa liweze kusimama na kujiendesha lenyewe. Hivyo, ni vyema vifungu hivi vyote vikabaki kama vilivyo kwa sababu ni fursa ya kuliwezesha Baraza lianze kusimama kwa miguu yake wakati tu linapoanzishwa lakini kama nilivyosema pale mwanzo, Baraza litakuwa lina sura ya *individuality* na kwa maana hiyo linaweza likafanya biashara, linaweza likaweka vitega uchumi, linaweza likaweka tozo ambazo zitalisaidia kukusanya pesa za kujiendesha na hivyo halitakuwa limeingiliwa na mamlaka yoyote ile.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri unahitaji muda zaidi ili niongeze nusu saa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Hapana, nahitaji kama dakika tano tu.

**NAIBU SPIKA:** Basi acha niwahoji Wabunge kwa sababu dakika zitazidi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) inanitaka nikitaka kuongeza nusu saa niwahoji Wabunge na ndicho ninachotaka kufanya sasa. Hoja ni kuongeza nusu saa ili Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kumaliza kuhitimisha hoja yake.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliridhia kuongeza muda wa nusu saa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imekubaliwa, Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilikuwa nazungumzia maoni kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na maoni hayo yalikuwa yanahusu kifungu cha 21(1)(a),(c) na (f), viondolewe ili kulifanya Baraza kuwa huru wakati wa utekelezaji wa majukumu yake. Lengo la Baraza kutengewa fedha nimekwishakueleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maelezo kuhusu mchango wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ambaye anapendekeza vifungu vya 22 na 23 kwamba muda wa miezi mitatu ni mfupi kwa mamlaka kuweza kuwasilisha taarifa ya fedha iliyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Tumepokea ushauri huo na ushauri huo tutauzingatia kwenye Jedwali la Marekebisho ambalo litawasilishwa baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maombi mengine kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hususan kwenye kifungu cha 28(2) neno "hatachukuliwa" liangaliwe na kufanyiwa marekebisho kwani inaonekana kuharibu maana ya kifungu ukilinganisha na jinsi kinavyosomeka kwenye muswada wa Kiingereza. Tumepokea ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maoni mengine kutoka kwa Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo ambaye anapendekeza kifungu cha 30(2) kwamba iwapo kutatokea shauri la mwanataaluma lipelekwe kwenye Kamati ya Nidhamu kwanza kabla ya kufika kwenye Baraza. Kifungu cha 4(8) na kifungu cha 8(2) na (3) vimeweka namna Baraza na Kamati zake zitakavyojiwekea utaratibu wa kuendesha shughuli zake.

Aidha, Mheshimiwa Waziri amepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni za uendeshaji wa Baraza husika. Hivyo, hatuoni haja ya huu utaratibu anaoupendekeza Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo kuingizwa kwenye sheria hii. Tayari vifungu vingine vinatoa fursa ya namna ambavyo Mheshimiwa Waziri atatunga kanuni ambazo zitaelekeza utaratibu mzima wa kushughulika na masuala yanayohusu nidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho alikuwa ni Mheshimiwa Joseph George Kakunda ambaye alipendekeza kwamba muswada uainishe mawasiliano ya kisekta katika kuajiri na kusimamia wanataaluma. Serikali imepokea ushauri huo. Hata hivyo, katika utendaji wake wa kazi Serikali ina ngazi mbalimbali katika kufikia maamuzi, kwa mfano, Kamati ya Makatibu Wakuu, Baraza la Mawaziri ambapo masuala ya kisera na kisekta hujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hapa amechangia Mheshimiwa Godwin Oloyce Mollel kwamba Taifa liandae *brains*. Alisema tunatunga sheria na tutaweka utaratibu lakini pengine hatuna *brains* za kutosha kuweza kufikiri kwa kiwango cha watu waliofikiri na kutengeneza *DNA*. Ni maoni yangu kwamba pengine mashaka ya Mheshimiwa Mbunge yako *misplaced* kwa sababu kwa hivi tulivyo tu bila *intervation* yoyote tayari Tanzania imekwishafanikiwa kutoa wataalam wa *level* za Kimataifa. Nina furaha kusema baadhi ya wataalam hao ambao wana viwango vya *brains* za Kimataifa wamo ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna watu wengi ambao wamebobea na wameleta sifa kubwa katika nchi yetu na wametoa mchango mkubwa kwenye maendeleo ya sayansi duniani. Nitakutaja wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika ni msomi wa Kimataifa, nitamtaja Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo ni msomi wa Kimataifa, nitamtaja Profesa na mwalimu wa wachumi wengi waliomo humu ndani Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango ni msomi wa kiwango cha Kimataifa, nitamtaja Mheshimiwa Profesa Maghembe ni msomi wa kiwango cha Kimataifa, nitamtaja Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe ni msomi wa Kimataifa na wote hawa wametoa michango mikubwa ambayo inaashiria kwamba usomi wao siyo wa kubabaisha ni wa viwango vya kimataifa, lakini pia *brain* walizonazo ni za viwango vya kimataifa.

Kwa hiyo, hakuna shaka lolote lile kwamba tunatengeneza Taifa la watu ambao hawana *brain* za kutosha labda pengine kwa sababu za udumavu na vitu vingine kama hivyo, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye kizazi chetu sisi, acha kizazi cha akina Profesa Muhongo na *generation* ya watoto wetu sisi, wajukuu wa akina Profesa Muhongo, Tanzania itapaa katika hali ambayo ni ya ajabu sana. Kwa sababu nikiviangalia vipaji vya watoto wangu akina Sheila na *HK Junior* ninaona watakwenda mbali zaidi ya pale nilipofikia mimi. Kwa hivyo, nina uhakika nchi hii imejipanga vizuri, *brain* za watoto wa kizazi hiki kilichopo sasa na kinachokuja zitakuwa ni moto wa kuotea mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kazi yetu hapa Bungeni tujadiliane kama hivi ambavyo tumefanya kwenye sheria hii ambapo mmetoa maoni mazuri na sisi tumeya-*consider* kwa sababu mmetumia *brain* nina uhakika na ndiyo maana na sisi tumeweza kutumia *brain* vilevile kuyatafakari na kuona haya ni maoni mazuri hata kama yametolewa na wenzetu wa upinzani, tumeya-*consider* tumeyaweka kwenye sheria. Kwa hiyo, kazi yetu ya kwanza ni hiyo, kudumisha amani, upendo, mshikamano, kufanya kazi kwa weledi na kwa mijadala ambayo ina afya siyo kuzomeanazomeana lakini pia kujenga jamii ya watu wanaopenda kufanya kazi. Ndiyo ambacho Serikali ya Awamu ya Tano

imejikita kukitekeleza, kutaka Watanzania waheshimu kazi, wafanye kazi, wawe na nidhamu ya kazi ili tukue kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tatizo halipo kwa sisi wataalam lipo kwa sababu hatuna fedha za kutosha kuwekeza kwenye shughuli mbalimbali za kitaalam kwa mfano kufanya *research.* Utamaduni wa kufanya tafiti kwenye nchi yetu unakwamishwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa fedha ambazo kama tungekuwa nazo tungeweza kuwekeza mahsusi kwa kujenga vipaji vya kufanya utafiti lakini kwa sababu tuna uchumi mdogo hatuna uwezo wa kuweka kipaumbele cha kuwekeza kwenye *research* basi tunashindwa ku-*harness* vipaji ambavyo wasomi wa Kitanzania wanavyo. Hiyo ni changamoto ambayo tunayo na ni changamoto ya kimfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Mollel na Waheshimiwa Wabunge wengine kadiri uchumi wetu utakavyoendelea kukua ndivyo ambavyo Tanzania na yenyewe itaweza kuwekeza kwenye *research,* itaweza kuwekeza kwenye maabara za kisasa kubwa na kila kanda, kama ambavyo tunatamani, ili tuweze kutumia sasa uwezo wa *brains* za watoto wa Kitanzania kufanya tafiti mbalimbali kuweza kugundua vitu mbalimbali. Hata hawa anaowasifia wamegundua *DNA* hawana *brain* za ajabu sana. Wengine tumepata fursa za kwenda kusoma kwenye vyuo vyao huko nje na tumeweza ku-*shine* na kuwa wa kwanza kwenye darasa ambapo unasoma na wazungu watupu na wala siyo jambo la ajabu. Tumeshiriki nao kufanya tafiti mbalimbali na tumeona wakati mwingine tunakuwa wabunifu zaidi kwenye tafiti kushinda hata hao wazungu ambao unadhani wao wameandaliwa na mfumo wa nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunipa fursa hii ya kutoa ufafanuzi kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Wataalam wa Kemia na nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa muda wa kutosha kufanya mambo yangu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, naomba kutumia nafasi hii kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, nina mambo mawili, la kwanza nimekumbushwa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulika na mambo ya maafa ni Kamati ya Katiba na Sheria.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala kuhusu Kikao cha Wabunge Wanawake wa

Chama cha Demokrasia na Maendeleo kwamba kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Msekwa D baada ya kikao cha Bunge kuahirishwa saa 7.00 mchana huu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo mnaombwa mhudhurie bila kukosa kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, jambo la mwisho ni maelezo aliyokuwa ametoa Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha kuhusu Orodha ya Shughuli za Siku za Bunge kutokuwekwa kwatika lugha ile ambayo yeye anaweza kuisoma kwenye *braille* na pia miswada inayoletwa hapa na Serikali na taarifa mbalimbali ukiacha Wizara ya Elimu. Kwa hilo, Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha, nianze kwanza kwa kukuomba radhi kwamba ofisi haijatayarisha huo utaratibu wa kukuwekea hizi taarifa katika lugha ambayo unaweza kuisoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kwa upande wa ofisi mimi nitalifuatilia, lakini kwa upande wa Serikali nichukue nafasi hii kuwataka taarifa mnazotuletea tafadhali zimfikie Mheshimiwa Dkt. Elly Macha mapema kabla ya siku ya kikao. Wakati mwingine kuna taarifa nyingine mnaweza kumpelekea kwenye namna ambayo yeye anaweza kusoma kwenye *computer* yake, lakini tuangalie utaratibu wa kumpa taarifa mapema ili aweze kushiriki vikao hivi kikamilifu. Kwa sababu asipopewa mapema maana yake anashindwa kusoma na kujitayarisha ili aweze kutoa mchango wake. Kwa sababu hiyo, upande wa Bunge nitafuatilia lakini upande wa Serikali tujifunze kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia namna nzuri ya kumtayarishia taarifa zake Mheshimiwa Dkt. Elly Macha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 7.05 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2016 *(The Government Chemist Laboratory Authority Act, 2016)***

**na**

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa mwaka 2016 *(The Chemist Professionals Act, 2016)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala wa miswada ya sheria. Kwanza Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali yaani *The Government Chemist Laboratory Authority Act* wa 2016 na Muswada wa Sheria ya Wanataaluma wa Kemia, *The Chemist Professionals Act* 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu napenda pia kuchukua nafasi kutoa pole kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera ambao wameathirika na tetemeko la ardhi na ambalo limesababisha vifo, majeraha na kubomoka. Nataka kulithibitishia Bunge lako tukufu kwamba sekta ya afya ikiwa ni mdau mkubwa sana katika tukio hili. Katibu Mkuu wangu yupo Kagera toka jana na amekuwa akishirikiana na Serikali ya Mkoa na Ofisi ya Waziri Mkuu inayohusika na maafa katika kushughulikia majeruhi. Mpaka sasa hivi tuna majeruhi 24 ambapo wamepata majeraha makubwa sana ya mifupa, tumepeleka Madaktari Bingwa kutoka Bugando na tunategemea wengine tutawapeleka katika Taasisi ya Mifupa *(MOI)* ili kuweza kupata huduma za haraka. Kwa hiyo, niwatakie moyo wa subira wenzetu wote ambao wameathirika na janga hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kwakweli ningependa kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Peter Serukamba na Makamu Mwenyekiti Mussa Azzan Zungu kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika kukamilisha miswada hii miwili. Nikiri nimekaa katika Bunge hili takribani miaka sita lakini sijawahi kuona Kamati ambayo ipo *very committed, very professional* kama Kamati hii. Wamekaa muda wote, wamesoma kifungu kwa kifungu na walikuwa

wanatupa ushauri na walikuwa pia wanasikiliza maelezo au ufafanuzi wetu. Kwa hiyo, nataka kuthibitishia kwamba Kamati hii inayotambulika kwa jina la *Guantanamo* ni Kamati madhubuti, unaweza ukaiamini katika mambo mengine makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia Miswada hii miwili na kwa mujibu wa rekodi ambazo ninazo Wabunge 34 wamechangia ambapo Wabunge 26 wamechangia kwa kuongea na Wabunge nane wamechangia kwa maandishi. Lakini natambua kwamba kanuni haziniruhusu kuwataja, lakini katika hatua hii niseme kwa kweli tunashukuru sana kwa michango yenu na michango yenu imetunufaisha sana katika kuboresha maudhui ya miswada hii miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuonesha kwamba Serikali imekubali maoni na michango ya Wabunge, nimeleta *schedule of amendments* mbili ambazo tumezingatia ushauri na maoni ambayo yametolewa na kamati, lakini pia ushauri na maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge lakini pia na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wakati wanachangia muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako sasa niruhusu nijibu hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Hamisi Kigwangalla ambapo yeye ametoa ufafanuzi katika Muswada wa Sheria ya Wanataaluma wa Kemia. Kwa hiyo, ufafanuzi wangu utajikita katika ule Muswada wa kwanza ambapo ni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali *(The Government Chemist Laboratory Authority Act* ya 2016). Baada ya kusema hayo mwishoni nitatoa hoja ya Bunge lako likubali kukaa kama Kamati lijadili na kupitisha miswada yote miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nianze na hoja ambazo zimetolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu muswada huu ambao ninautolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ambalo limeongelewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ni kuhusu kifungu kinachohusu mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa *supreme* na *referral* kwamba inaweza kuleta muingiliano na taasisi nyingine kwa mfano, *TBS* na *TFDA* yaani Mamlaka ya Chakula na Dawa. Kama nilivyosema wakati nawasilisha miswada hii juzi kwamba Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imekuwapo katika nchi yetu tangu miaka ya 1890 na imeendelea kuwa chombo cha Serikali cha uchunguzi wa kikemia wa kimaabara kwa bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inafanya uchunguzi wa kikemia wa vyakula, dawa na vipodozi hasa pale panapotokea utata au kuhusisha masuala ya kesi za jinai.

Kwa upande wa Mamlaka ya Chakula na Dawa wao wanafanya udhibiti wa ubora na usalama wa chakula, vipodozi na dawa na maabara hii inafanya uchunguzi wa kikemia. Kwa hiyo, pale ambapo maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inapofanya uchunguzi haifanyi uchunguzi kwa ajili ya kudhibiti. Nitoe mfano wa mahindi, tulikuwa na tatizo la sumukuvu kwa hiyo, wao watasema tumefanya uchunguzi wa kimaabara na tumekuta mahindi haya yana sumu au kuna mfanyabiashara ameleta chakula nchini labda maziwa ya mtoto, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali watafanya uchunguzi watasema labda kuna sumu au kuna kemikali nyingine ambazo sio salama kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Sasa mwenye jukumu la kusema mahindi haya yasiuzwe au maziwa haya yasiuzwe ni *TFDA*. Kwa hiyo, sio maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, wao wanafanya tu ile *laboratory analysis* wa masuala hayo nimesema ya chakula, dawa na vipodozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili lakini kwa mfano kuna mtu ameleta bidhaa yake, halafu *TFDA* inamwambia hii bidhaa sio salama lakini yule mtu anasema hapana hii bidhaa yangu ni salama. Kwa hiyo, pale pale panapotokea *dispute, how do I put it,* utata kwa hiyo, watu ndio tunaposema unaweza ukakata rufaa kwenye Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuweza kuthibitisha kwamba ile *TFDA* ilisema kwamba hichi kitu sio salama ndipo sasa tunasema sasa inakuwa *supreme* na *referral.* Kwa hiyo, pale ambapo kuna utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala kwa mfano la *TBS*. *TBS* wao wanaangalia viwango kwa mujibu wa Sheria ya Viwango ya mwaka 2009 na ina jukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa viwango vya Kitaifa kwa bidhaa mbalimbali na kutoa hati kwa bidhaa zinazokidhi viwango. Kwa hiyo, tunatambua kwamba *TBS* nayo ina maabara yake kwa ajili ya kupima viwango vya bidhaa mbalimbali. Kwa hiyo, Mkemia Mkuu hapimi kwa sababu ya kudhibiti, yeye anapima kwa ajili ya masuala ambayo yana maslahi ya Taifa, lakini la pili masuala ambayo pia yana utatanishi au ushindanishi. Lakini pia inaweza ikapima kwa ajili ya kujenga uwezo wake wa kuchunguza na ukiangalia vizuri kwa kweli huwezi kukuta muingiliano wa masuala haya makubwa mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa niunganishe na hoja ambayo pia imetolewa na Mheshimiwa Kangi Lugola kwamba inakuwaje hii sasa hivi Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali iwe ni maabara ya rufaa na itasajili vipi maabara nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kwa mujibu uendeshaji wa hizi maabara za kikemia katika nchi mbalimbali kwa mfano Marekani, Hong Kong na India utaratibu upo hivyo katika nchi yoyote lazima kuwe na chombo ambacho ndicho msemaji wa mwisho linapokuja suala la uchunguzi wa kikemia, vinasaba na sayansi jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sheria hii haifuti sheria au maabara nyingine ambazo zinaanzishwa kwa mujibu wa sheria mbalimbali. Lakini tu inaweka wazi utaratibu wa usajili wa hizi maabara kwa sababu tunataka zifanye kazi kwa mujibu wa viwango vya kimataifa na viwango vinavyokubalika, lakini pia tunataka kuhakikisha tunajenga uwezo wa maabara zetu ili ziweze kukidhi viwango vya kimataifa na ithibati kwa kukaguliwa na vyombo kama vile *Southern Africa Development Corporation Accreditation Services,* lakini pia kuna *UCAS.* Kwa hiyo, hii maabara itasimamia maabara nyingine lakini na yeye itasimamiwa na taasisi nyingine za Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama nilivyosema Mheshimiwa Kangi Lugola anasema kwamba unakuwaje wewe ni rufaa *at the same time* unafanya *operations.* Ukiwa hospitali ya rufaa ni lazima pia ujenge uwezo wa kufanya shughuli za kawaida; kwa hiyo maabara hii lazima iweze kuwa na uwezo wa kufanya shughuli za kiuchunguzi lakini sio kwa lengo la ku-*regulate,* lakini ina *build capacity* na pale ambapo kama hakuna *dispute* kwa hiyo ni kwa ajili ya kujenga uwezo wake wa ndani na kwa kiasi fulani haiingiliani kabisa na sheria au maabara nyingine ambazo zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaamini Muswada huu utaweza kwa kiasi fulani kuboresha utendaji wa maabara nyingine zilizopo nchini na pale ambapo kuna tatizo kama nilivyosema ndipo basi chombo hiki kinapokuwa cha juu. Lazima Serikali iwe na msemaji wa mwisho linapokuja masuala ya uchunguzi wa kikemia, sayansi jinai na vinasaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hilo ndilo lilikuwa la jumla kubwa sana ambalo liliweza kutolewa kama maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba hakuna mgongano wowote, lakini tutaweka kanuni pia ambazo zitatuwezesha sasa kuweka mgawanyo wa majukumu vizuri kati ya taasisi mbalimbali ambazo zinafanya pia shughuli za uchunguzi wa kimaabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili la jumla ambalo limeongelewa ni suala la bajeti kwamba unaweza ukawa na maabara nzuri, lakini usiwe na bajeti ya kutosha, usiwe na vifaa vya kutosha na usiwe na watumishi wa kutosha. Nasema kwamba Serikali tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge na tunaamini kwa kupitishwa kwa sheria hii kwa sababu tunaipa sasa ile hadhi Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa mamlaka, kwa hiyo pia hata fungu lake litakuwa zuri lakini pia tutaweza kuwa na watumishi wa kutosha;

tunahitaji watumishi takribani 400 lakini sasa hivi tuna watumishi 192. Kwa hiyo, katika mwaka ujao wa fedha niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutatenga fedha ya kuajiri watumishi lakini pia tutatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuendesha Mamlaka hii ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Augustine Manyanda Masele, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Godwin Mollel, Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Salum Rehani wamesisitiza umuhimu wa maabara hii sasa kutengewa bajeti ya kutosha ili kuweza kufanya kazi zake kikamilifu na nataka kuwathibitishia ndio maana tumeweka katika sheria hii kifungu ambacho Serikali itawajibika kutenga fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za maabara hii ambayo sasa hivi tunaita mamlaka. Kwa hiyo, ukisoma kifungu cha 36 utaona kwamba kuna hela ambazo Bunge litatakiwa ku-*appropriate* kwa ajili ya kuendesha kazi za maabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijielekeza katika kujibu hoja za Kamati ya Bunge wamezungumzia pia kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mashtaka dhidi ya Serikali Sura ya Tano iliyofanyiwa mapitio kwamba tuifute au sheria hii iifute. Serikali imepokea ushauri wa Kamati, lakini suala hili kwa kweli sheria hii haiwezi ku-*repeal* au kurekebisha Sheria ya Kuendesha Mashauri dhidi ya Serikali. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo hapa nashauri kwamba tutafute jukwaa jingine kama tunadhani sheria hii ni kikwazo katika kutafuta haki katika kuharakisha mashauri mbalimbali dhidi ya Serikali na taasisi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai tu kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba hili suala tuliangalie katika muktadha mwingine, lakini katika muktadha wa miswada hii miwili ambayo nimeileta hapa Bungeni tunadhani kwamba inajitosheleza. Hivyo bado itabakia kwamba siku 90 pale ambapo mtu inabidi atoe taarifa pale ambapo mtu anataka kuishitaki Serikali na hili limeongelewa chini ya kifungu..., nikienda kwenye vifungu nitakuja kuliongelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo pia limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge ni suala la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ni suala la kuharakisha utungaji wa kanuni ili sheria ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kukuthibitishia na kuithibitishia Kamati na Waheshimiwa Wabunge kwamba mara tu Bunge hili litakapoitisha miswada hii na *Inshallah* Ummy Mwalimu nipo pale basi ndani ya muda mcheche tutahakikisha tunatengeneza kanuni zitakazowezesha sheria hii kuanza kufanya kazi haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, sheria hii kwa kweli imechelewa na kama mnakumbuka ilikuwa iwasilishwe

muswada huu katika Bunge lililopita la Kumi lakini kutokana na ratiba ya Bunge kubadilika hatukuweza kuwasilisha. Kwa hiyo, sisi wenyewe Wizara ya Afya ni dhamira yetu kwamba miswada hii iwe sheria haraka iwezekanavyo ili tuweze kutekeleza yale ambayo tumeyaweka katika miswada hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge pia imetuelekeza kwamba hii Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inahitaji kufanya uchunguzi wa shisha na kemikali zinazotumika kuua vijidudu kwenye maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani ili kubaini athari zake na kuishauri Serikali kuhusu hatua za kuchukua kukabiliana na madhara hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepokea ushauri wa kuhakikisha kwamba tunafanya uchunguzi wa matumizi ya *shisha* na kubaini kuwa tayari Mkemia Mkuu wa Serikali ameshafanya uchunguzi wa shisha na kubaini kuwa bidhaa hiyo huchanganywa na dawa za kulevya kama vile bangi, *heroine* na *cocaine* na hivyo Serikali kupelekea kupiga marufuku. Lakini sasa hivi tutajikita ndani zaidi ili kuonesha ni kiasi gani ni *contents* gani, *ingredients* ngapi ambazo zinakuwa katika shisha na kwanini Serikali iendelee kupiga marufuku matumizi ya shisha nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili pia Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali hufanya uchunguzi wa kemikali za kuua vijidudu kwenye maji ya kunywa ili kubaini ubora na usalama wake kabla ya kuruhusu kemikali hizo kuingia na kutumika nchini. Aidha, kemikali za viwandani na majumbani ambalo Mheshimiwa Salum Rehani aliliuliza jana zinasimamiwa na Wizara yangu kupitia Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali chini ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182. Kwa hiyo, kwa mujibu wa sheria hii muingizaji, mtumiaji, msambazaji na mdau yoyote anaejihusisha na kemikali hizo ni sharti asajiliwe na kupata kibali cha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge pia imetoa maoni kwa Serikali kwamba umefika sasa wakati kwa Maabara hii ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuelimisha jamii shughuli mbalimbali ambazo zinafanywa na taasisi hii, tumepokea ushauri huu. Lakini nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge tumeshakuwa tukifanya shughuli mbalimbali za kuelimisha jamii lakini ushauri tumeupokea na tumeona kwamba Waheshimiwa Wabunge wanataka tutoe elimu ya vinasaba. Lakini niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba masuala ya vinasaba hayagusi tu uhalali wa mzazi kwa mtoto maana naona Wabunge wamelishabikia sana hili, lakini kwenye masuala ya teknolojia ya vinasaba yanahusu pia utambuzi wa jinsi, kuna watu wanazaliwa wanawake, wanaume kwa hiyo tunaangalia jinsi tawala ni ipi. Kwa hiyo, unaweza ukawa na jinsi mbili lakini Mkemia Mkuu wa Serikali kupitia maabara yake ndio atasema jinsi hii ndio ina nguvu sana kuliko jinsi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna suala la kuhakikisha utambuzi wa binadamu, hasa wakati wa kutokea majanga lakini pia watu wanaosafiri kwa makundi. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe, tumeng'ang'ana sana kwenye masuala ya uhalali wa mzazi, lakini mimi mswahili wa Tanga, waswahili wa Tanga tunasema kitanda hakizai haramu. Lakini kwa hiyo tunafanya elimu hiyo ya kuhakikisha kwamba tunawaelimisha wananchi, huu msemo uliuanza Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeuchagiza tu.

Kwa hiyo, hoja ninayotaka kusema tutaendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu shughuli hizi za Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kupitia vyombo vya habari, mikutano, warsha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio tu masuala ya vinasaba, dada yangu Mheshimiwa Mushashu pia amezungumzia masuala ya watu ambao wanawapa pia ujauzito watoto wa shule na lilitoka ombi kwamba tupime wakati ujauzito bado yule mtoto hajazaliwa, lakini mpaka sasa hivi teknolojia yetu hairuhusu, hatuwezi kupima uhalali wa mzazi mpaka pale ambapo mtoto atakuwa amezaliwa.

Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo tutalisisitiza sana kwa sababu na mimi nina dhamana ya kulinda wasichana hasa kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya masuala hayo ya jumla ya Kamati, nizungumzie masuala ya jumla ambayo yamewasilishwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, na naamini kwamba ule utangulizi umefutwa kwenye *Hansard,* kwa sababu kama haujafutwa nina maelezo hapana, kwa sababu tunayo majibu ya kuwajibu, kusingekuwa na demokrasi msingekuwa mko hapa Bungeni. Kwa hiyo, umefutwa… ndiyo maana nilikuwa nataka…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, tulishayafuta, ndiyo maana asubuhi pia tumekumbushia hilo jambo.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuyafuta kwa sababu majibu tunayo.

Kwa hiyo, nitajikita kwenye suala lao moja la jumla linaposhauri kwamba Mamlaka hii ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, pamoja na kutekeleza majukumu yake ijikite katika kufanya utafiti wa uhandisi wa vinasaba *(genetic engineering)* kwenye maeneo ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kukabiliana na changamoto za magonjwa mbalimbali na mabadiliko ya tabia nchi. Wizara yangu imepokea huo ushauri na nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba mamlaka itafanya tafiti kwenye maeneo ambayo

yanahusiana na majukumu yake lakini pia tutajikita kwenye maeneo ambayo yana maslahi kwa Taifa ili kuweza kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu itashirikiana na Wizara zinazojihusisha na masuala ya utafiti wa uhandisi wa vinasaba *(genetic engineering)* kwenye maeneo ya kilimo, mifugo na uvuvi, kwa hiyo, ushauri huu tumeupokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele na Mheshimiwa Vedasto Ngombale walikuwa na maoni ya jumla kuhusu Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kwamba kupitishwa kwa muswada huu kunaweza kufuta sheria mbalimbali au kunaweza kupelekea marekebisho katika sheria mbalimbali. Nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema kwamba muswada unaopendekezwa au sheria inayopendekezwa haitafuta au kurekebisha sheria yoyote ambayo inatumika isipokuwa tunaweka sasa sheria moja ambayo inatambua majukumu na mipaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaamini kwamba sheria hii ikipita itatatua changamoto zilizopo ambazo maabara imekuwa ikikumbana nazo kutokana na majukumu yake kutobainishwa katika sheria yake peke yake. Nilitoa mfano, kwa mfano kuna Sheria ya Masuala ya Ushahidi inasema kwamba Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ndio atakuwa anatoa ushauri wa kitaalam *(expert opinion)* kwenye masuala ya jinai lakini maabara yenyewe haina sheria ambayo inasema hiyo kazi au majukumu hayo inaweza kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa niende kwenye mapendekezo ya marekebisho ya vifungu ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge na ningependa tena kuanza na Kamati ya Bunge, wao walipendekeza kwamba katika kifungu kile cha 8 kinachohusu majukumu na mamlaka ya bodi basi tuseme kwamba Mwenyekiti wa Bodi anatakiwa kuwa na sifa *at least a masters degree* ambayo inatoka katika chuo kinachotambulika kisheria nchini. Suala hili tumelifanyia kazi na kwenye jedwali langu la marekebisho ambalo nimeliweka hapa utaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, niende kwanza Kamati ya Bunge imeonesha kifungu cha 8 kuhusu majukumu na mamlaka ya bodi, kwa hiyo, tumebadilisha pale nime-*renumber* kwenye sehemu ambapo yalikuwa yanaonekana ni majukumu ya Mkemia Mkuu wa Serikali tumeyafanya ni majukumu ya Bodi majukumu ya Bodi tumeyafanya ni majukumu ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kwa hiyo hilo ni jambo ambalo nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge tumelizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini na Mheshimiwa Kakunda naye na Mheshimiwa Japhet Hasunga wote walikuwa na mapendekezo katika kifungu hiki cha 8.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya kudumu ya Bunge pia katika kifungu cha 10 imetaka tuseme kwamba yule Mkemia Mkuu wa Serikali angalau awe na *degree* inayotoka katika chuo kinachotambulika, hoja hii pia ilitolewa na Mheshimiwa Mwita Waitara, tumezingata katika Jedwali la Marekebisho tumeonyesha kwamba huyo Mkemia Mkuu wa Serikali lazima awe na *masters* inayotoka katika chuo kinachotambulika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Kamati ya Kudumu ya Bunge imetushauri kwamba tuweze kuzingatia kifungu cha 13 kinachohusu *appointment* na *functions* za *government laboratory analyst,* kama nilivyosema, tumebadilisha kwenye Bodi na tumerekebisha katika majukumu ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11 pia tumeleta Jedwali la Marekebisho ambapo tumekubaliana na mapendekezo yaliyotolewa kwanza kabla sijaenda mbali kwenye kifungu cha 7, Wabunge wengi wameongelea kuhusu uwakilishi wa jinsia katika Bodi hii ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Hili tumelizingatia na tumetumia neno kwamba wakati wa uteuzi wa wajumbe wa bodi, Waziri ata-*take into consideration gender representation,* kwa hiyo nataka kuwathibitishia dada yangu Mheshimiwa Susan Lyimo, dada yangu Mheshimiwa Lucia Mlowe na Mheshimiwa Benardetha Mushashu, wote ambao mmeliuliza suala hili kwamba tumeweza kuliwekea ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limejitokeza katika kifungu cha 16(4), kwamba mamlaka haitawajibika na mabadiliko ambayo yatatokea wakati na baada ya uchunguzi kwenye ile sampuli. Ufafanuzi ni kwamba hapa tulilenga labda kwa mfano Jeshi la Polisi limeleta sampuli labda ya mkono wa mtu ambaye ameuawa, lakini ule mkono ili uingie kwenye maabara kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi unaweza ukakatwakatwa, kwa hiyo, tulichotaka ni kuilinda mamlaka kutowajibika kwamba wewe umeleta mkono wa mtu lakini leo mnatuletea vipandevipande.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lengo letu lilikuwa sio kwa ajili ya kulinda mabadiliko ya sura au *physical characteristics,* lakini lengo letu ni kulinda zile *chemical composition.* Kwa hiyo tumeweka pia kwenye jedwali la marekebisho kwamba tumesema *if that change does not affect the original nature of chemical composition,* kwa hiyo hii tume-*clarify* vizuri. Sio kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Mama Mushashu, dada yangu kwamba tunasema ni bangi halafu sisi tunaibadilisha tunasema ni mchicha, lengo

halikuwa kulinda hivyo lakini ilikuwa ni kulinda vitu vikishaingia kwenye maabara vinaweza visitoke kama vilivyo, unaweza ukaingiza koti zuri lakini koti baadaye likatoka na madoa au limechanika chanika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge pia imetoa ushauri kuhusu kifungu cha 21 kinachohusu huduma za maabara, kifungu cha 28 kinachohusu utoaji wa taarifa ya kufunga na kubadilisha umiliki, kifungu cha 34, kifungu cha 53, vyote hivyo nataka kuithibitishia Kamati ya Bunge kwamba tumepokea mapendekezo yao na nimeyaingiza kwenye Jedwali la Marekebisho na ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi sasa katika hoja za vifungu kwenye Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, walipendekeza kwenye kifungu cha 3 tutoe tafsiri ya neno *poison* na ushauri tumeupokea na nimeweka kwenye *further schedule of amendment* kwamba tutatoa maana ya neno hilo *poison.*

Pia Kambi ya Upinzani ilipendekeza katika kifungu cha 7(2) tuongeze idadi ya Wajumbe wa bodi kutoka saba hadi tisa kwa kuongeza mwakilishi kutoka taasisi binafsi zinazojishughulisha na maabara na mwakilishi kutoka vyuo binafsi, lakini pia hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Japhet Hasunga, kwa hiyo, ushauri tumeupokea na kwenye Jedwali la Marekebisho nimeleta mapendekezo haya kwa hiyo naamini Waheshimiwa Wabunge watayapitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia imetoa hoja katika kifungu cha 10(1) na Mheshimiwa Lucy Owenya kwa maandishi na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara kwamba Serikali itoe uhuru wa Mheshimiwa Rais kuteua Mkemia Mkuu wa Serikali kutoka ama ndani ya utumishi wa umma ama sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri lakini nataka kusema, kutokana na unyeti wa majukumu ya Ofisi hii ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali bado kwetu sisi tunapendekeza kwamba Mkemia Mkuu wa Serikali ateuliwe ndani ya utumishi wa umma, asiwe ni mtu ambaye ametoka nje ya utumishi wa umma. Na hii pia lengo letu ni kutaka pia kuhakikisha tunajengea uwezo watu ambao wamo ndani ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja pia kuhusu kifungu cha 16(4) kwamba, nimeshazungumza maabara kutowajibika kwa mabadiliko yoyote ya muonekano, nimeitolea ufafanuzi. Lakini pia Kambi ya Upinzani ilikuwa inahoji kwa nini wajumbe wa bodi, kamati na watumishi wa mamlaka hupewa kinga ya kisheria. Kifungu hiki ni utaratibu wa kawaida katika utungaji wa sheria na hutumika katika sheria nyingi. Aidha, muswada wa sheria hii kupitia kifungu cha

53 umeweka utaratibu wa kumwajibisha mtumishi wa mamlaka iwapo atapatikana na hatia kuharibu nyaraka au ripoti ya uchunguzi wa kimaabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwamba Wabunge sasa baada ya kujibu hoja za Kamati na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Waheshimiwa Wabunge mbalimbali pia wamechangia katika vifungu tofauti kwa mfano kuna kifungu cha 7(2) kwamba Serikali itoe uhuru wa Mheshimiwa Rais kuteua kutoka ndani ya utumishi wa umma, hilo tumelikataa lakini tumekubali pendekezo la Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Abdallah Chikota na Mheshimiwa Anna Lupembe kwamba tunataka Mwenyekiti wa Bodi badala tu ya kwamba anatoka katika utumishi wa Umma lakini pia awe amebobea katika masuala ya kisayansi. Kwa sababu jambo hili kwa kweli ni la kitaalam kwa hiyo pendekezo hilo pia nimelizingatia katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia suala la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe *gender representation,* Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa mama Mushashu na kaka yangu pia Mheshimiwa Boniphace wamelizungumzia hilo suala, hili tayari nimeshalijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na pendekezo kwenye kifungu cha 7.5 kwamba bodi iongezewe muda kutoka miaka mitatu hadi miaka mitano ili kuwa na muda wa kutosha kupanga na kufanya kazi. Tumeona kwamba bado tubakie katika kipindi cha miaka mitatu lakini tumetoa *option* ya wajumbe wa bodi kuteuliwa kwa kipindi cha pili, kwa hiyo, tunadhani miaka sita inawatosheleza na inaweza kuwasaidia kufanya kazi zao za kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja pia ambazo zimetolewa kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali asiingilie kesi au shauri, kwamba hicho kifungu tukifute, kifungu cha 4(4) na (5) na (6). Tunatengeneza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambayo ni taasisi ya umma, lakini katika kifungu cha 36 pia tumesema kwamba *source* ya *funds* za hii mamlaka ya maabara zitakuwa *appropriated* na *parliament,* kwa hiyo hizi ni fedha za Umma, utamtoaje Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika mashauri yanayohusu mamlaka hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado kwetu ni jambo la busara kuhakikisha kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali anahusika katika utekelezaji wa sheria hii lakini hasa atahusika pale ambapo kunatokea mashauri dhidi ya bodi au dhidi ya utendaji wa Mamlaka hii ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna swali ambalo limeulizwa sana na Mheshimiwa Kangi Lugola kwamba labda sheria hii itafuta au itaweza, na kaka

yangu pia Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab walionesha wasiwasi kuhusu uhusiano wa mamlaka hii na maabara ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tunatambua kuwepo kwa maabara mbalimbali ikiwemo hii maabara ya Jeshi la Polisi ambapo inahusika na masuala ya vinasaba vya binadamu, na sheria hii ambayo naipendekeza muipitishe haitazuia Jeshi la Polisi kuwa na kanzidata yake au kuendelea na utaratibu wake wa kufanya uchunguzi ikiwemo uchunguzi wa vinasaba vya binadamu lakini ni lazima iwe *accredited.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo lazima ipewe ithibati na Mamlaka hii ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na lengo kwa kweli ni kutaka kuhakikisha kwamba maabara zetu zinazingatia weledi, utaalam, vigezo na sifa za uchunguzi wa kikemia, sayansi jinai na vinasaba. Kwa hiyo, niwatoe hofu tu wote ambao wameuliza suala hili kwamba bado maabara ya Jeshi la Polisi litaendelea kufanya kazi zake lakini tunaamini sasa kupitia taarifa hii, kupitia Muswada huu Jeshi la Polisi litaweza kufanya shughuli zake kwa ukamilifu lakini pia nataka kuwathibitishia kaka yangu Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, tutajenga uwezo wa Maabara ya *Forensic* ya Jeshi la Polisi lakini na maabara nyingine zote nchini na ndiyo lengo kwa kweli la muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limetolewa la muda wa miezi mitatu ni mfupi kwa mamlaka kuweza kuwasilisha taarifa za fedha *(audit),* kwamba tutoke kwenye miezi mitatu na sasa hivi twende katika miezi sita, tumepokea ushauri huu na katika *schedule of amendment* ambayo nimei-*table* hapa suala hili tumelizingatia. Na kulikuwa na ufafanuzi wa kifungu cha 13 pia kutoka kwa kaka yangu Mheshimiwa Kangi Lugola kwamba utaratibu wa uteuzi wa wachunguzi wa Serikali chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ukoje. Kama nilivyosema kuna sheria ambayo inasimamia uteuzi wa wachunguzi wa Serikali na chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali sisi tunatambua jinsi sheria ile mabayo inaitwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 ambapo kifungu cha 203 kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya afya kufanya uteuzi huo.

Kwa hiyo, sio kwamba kupitia sheria hii tunajipa mamlaka ya kuteua *government analyst,* lakini kuna sheria ambayo nimeitaja ya *Criminal Procedure Act* yenyewe ndiyo inasema kwamba Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Waziri ndiyo ataweza kuteua wachunguzi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa michango yao na niwathibitishie kwamba kwenye *schedule of amendments* ambayo nimeweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye *further schedule of amendments* ambayo nimeweka tumezingatia kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri wa Wabunge, ushauri wa Wajumbe wa Kamati na kwa kweli baada ya kusema hayo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako lipitishe sasa hii miswada yote miwili, Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Muswada wa Sheria ya Wanataaluma wa Kemia *(The Chemist Professionals' Act)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, nitawahoji baadaye Waheshimiwa Wabunge. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Bunge Zima.

Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya mwaka 2016 *(The Government Chemistry Laboratory Authority Bill 2016)***

Kichwa cha Muswada

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza. Ninazo sababu za msingi kwa nini nimeona *title* ya muswada huu irekebishwe na isomeke kwamba *The National Laboratory Regulatory Authority* badala ya kubeba *title* ambayo imeletwa kwenye muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefikia misingi hiyo kwanza kutokana na maudhui yenyewe ya muswada. Maudhui yenyewe ya Muswada kwenye ukurasa wa 34 ile sentensi ya pili inasema, *The bill intends to complement to the Government efforts in improving the well being of its people and the*

*environment.* Msingi mkubwa ni huku kwa ku-*improve the well being of its people* na *environment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini msingi mwingine ni kwenye ukurasa wa nane katika zile *functions* zinazotokea ukurasa wa saba. Kwenye ukurasa wa nane *function number (b)* inasema *"to regulate chemical"* na kuendelea. Ukienda (f), *"to regulate and conduct"* na kuendelea. Ukienda (g), *"to develop and provide guidance and instructions."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu haina Maabara za Serikali tu, ina Maabara za watu binafsi ambazo zimekuwa zikitumika kuharibu *well being* ya Watanzania pamoja na kuharibu mazingira, nikawa najiuliza kama huu siyo wakati muafaka wa kutunga chombo ambacho ndiyo hiki Mamlaka ambayo inakuwa ni ya Kitaifa ikiwa *independent* kwa ajili ya kuangalia Maabara zote za Serikali pamoja na za watu binafsi kwenye kilimo na mifugo wako watu binafsi wanatengeneza dawa, kwenye saruji kuna *chemicals*, kwenye migodi kuna *chemicals*, kwenye viwanda vya nguo. Kwa hiyo nikaona ni wakati muafaka wa kuja na sheria ya Mamlaka ambayo haijikiti tu kwenye *Government Laboratories,* inajikita kwenye maabara zote ambazo zipo hapa nchini na ndiyo maana kutokuwa na chombo kinachosimamia hizi Maabara katika kuzisajili, katika kuzisimamia au kuzifuta, maisha ya wananchi yataendelea kuwa na matatizo kutokana na *chemicals* mbalimbali kwa hiyo nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri alifikirie hili na kwa kweli Waheshimiwa Wabunge...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Kangi Lugola kwa kuleta mapendekezo haya, lakini bado ningemuomba nimsihi kwamba tuendelee ku-*maintain* jina *The Government Chemistry Laboratory Authority Act*. Kwanza kwa sababu ya historia ya Maabara hii kama nilivyosema ilianza miaka ya 1890 na tumekuja Bungeni siyo kwa ajili ya ku-*debate whether national or government.* Tumekuja Bungeni kwa ajili, kwanza ya kuhakikisha tunakuwa na sheria moja ambayo itaweza kusimamia utendaji kazi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Sasa kwa nini tukaamua kuja na neno *authority* ni kwa sababu sasa tunataka hii Maabara pia tuwe na *supreme* na *referral laboratory* nchini ambayo itakuwa inatoa maamuzi ya mwisho katika masuala ya uchunguzi wa kikemia, sayansi jinai na vinasaba, lakini nataka kumsihi kaka yangu Kangi Lugola ninayo sheria chini ya Wizara ya afya ambayo ina-*regulate laboratory* hizi nchini, kwa hiyo hapa tunazungumzia masuala matatu; kemia, sayansi jinai na vinasaba kwa hiyo nakuomba sana kaka yangu Kangi Lugola ukubali

mapendekezo ambayo nimeyaweka hapa, na ninayo bodi ya *private laboratories* ambayo inafanyakazi kwa ajili ya pia ya kuangalia hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa hapa siyo kulumbana na dada yangu Mheshimiwa Ummy ambae tulisoma nae darasa moja darasa la sheria tukiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe. Lakini ninachojaribu kusema hapa ni msingi wenyewe ambao uko kwenye muswada kwamba tunashughulikia maisha ya watu pamoja na mazingira, lakini ananiambia tu kwamba kwenye Wizara ya Afya kuna chombo kingine, hicho chombo hakisemi na ninataka nimhakikishie, tunataka tujue kwamba sasa hivi ni wakati siyo wa kuwa na hicho chombo unachokisema kwenye Wizara pengine ni kaidara au ni kakitengo. Ni wakati sasa wa kuwa na mamlaka kama hii ambayo ameileta kwa nia njema ili iweze kusimamia mambo yote haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri, sheria hii ni wakati muafaka wa kuwa na mamlaka ya namna hii na unaposema kwamba uwe na *referral* ukatolea mfano hospitali ya Muhimbili. Hospitali ya Muhimbili ni *referral,* lakini hospitali ya Muhimbili haisajili hospitali zingine hapa nchini na wala hospitali ya Muhimbili haifuti hospitali zingine hapa nchini.

Kwa hiyo, jambo hili lina umuhimu wake, namuomba Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge, kama Mheshimiwa Waziri safari hii hatanipa majibu ya uhakika suala hili tulijadili, Bunge hili tutahukumiwa kwa kutotunga sheria ambazo zinaenda kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii tutaiua kwa masumu haya migodini, viwanda vya nguo, kwenye kilimo kule watu wanaungua mikono. Lazima tuwe na chombo ambacho kina mamlaka kama tunachokitunga leo.

Nitaomba Waheshimiwa Wabunge msimame tuweze kuhakikisha kwamba tunatunga sheria nzuri na siyo ili mradi sheria. Mheshimiwa Ummy unipe majibu ya uhakika vinginevyo nitaomba Wabunge wasimame ili tuzuie muswada huu usisonge mbele kwa sababu hautasaidia maisha ya wananchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nukushukuru na namshukuru Mheshimiwa Kangi Alphaxard Ndege Lugola kwa mapendekezo yake, lakini kiukweli amekwisha kujibiwa na Mheshimiwa Waziri kwa kuwa bado anang'anga'ania

tu na hii hoja yake, naomba nitoe mchango wangu kwamba kuwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kwanza jina lile lenyewe linalenga kutunza ile historia ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambayo ni maabara ya rufaa ya Serikali ambayo imekuwepo hata kabla ya uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kusema kwamba huwezi kulinganisha rufaa za hospitali na rufaa za kwenye maabara nakubaliana na yeye ila ni lazima aelewe kwamba tunapozungumzia Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa Maabara ya Rufaa tunamaanisha kwamba sasa tunapata neema ya kuwa na chombo cha juu kabisa ambacho kitakuwa kinatazama na ku-*regulate* utendaji wa maabara nyingine ambacho hakikuwepo huko tunakotokea na hili ni jambo la muhimu sana. Lakini pia kuwa na hii maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuna maana nyingine tofauti. Kwamba masuala yoyote yale ya kimaabara yatakapofika kwenye vyombo vya sheria hususani mahakamani na ikaonekana kuna utata basi Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali itakuwa *consulted* kama maabara ya mwisho na ya juu kabisa yenye maamuzi ambayo ni *conclusive* ambayo hayatopingwa na chombo kingine chochote kile ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo uwepo wa Maabara hii na *supremacy* yake na *referral nature* ya maabara hii unalenga kuweka mahala ambapo patakuwa kimbilio siyo tu la Serikali pia hata la wananchi lakini pia taasisi nyingine mbalimbali kwa sababu itakuwa ni *third party laboratory* ambayo iko pale na inakwenda kutoa ushahidi wake kwenye mashauri yoyote yale mahakamani ama mahala pengine popote pale. Ninaomba Mheshimiwa Kangi Lugola ukubaliane na jinsi tulivyoleta mapendekezo yetu

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola naona bado umesimama.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nimesimama kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri majibu anayoyatoa amekwenda kwenye *section 4* inayozungumzia mambo ya *supremacy*, mambo ya *referral* ambako na kwenyewe tutakwenda lakini…

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Kangi Lugola kwa sababu umeshaongea mara mbili wacha tusikilize mtu mmoja atakaye kuunga mkono wewe.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti Wabunge wengi…

**MWENYEKITI:** Sawa ngoja tusikilize basi mtu mwingine Mheshimiwa Kangi Lugola kwa sababu ukiongea wewe mara tatu, aongee mtu mwingine ijibiwe hoja muda utaenda sana kwenye hii hoja moja tu.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA**: Nimesimama tu kuwakaribisha siyo kuongea, kuwakaribisha hao wengine. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia katika haya marekebisho ambayo yamehusishwa na Mheshimiwa Kangi Lugola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachokijadili ni kuanziasha sheria ambayo itasimamia Mkemia Mkuu wa Serikali na majukumu makubwa ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni moja; kusimamia masuala ya vinasaba, masuala ya kikemia lakini kubwa lingine ni masuala ya sumu.

Mheshimiwa Mwenyekti, mimi kama Mbunge, taaluma yangu ni pamoja na daktari ni masuala ya maabara na maabara ni pana sana. Haiwezekani kwa mujibu wa taratibu hizi kwa sababu maabara kama nilivyosema kuna maabara ya *micro-biology*, kuna maabara ya *histo-pastology*, kuna mabaara ziko chungu mbovu sana, sasa haiwezekani kulingana na *scopia* ya Mkemia Mkuu Serikali akawa *regulatory authority* ya hizi maabara nyingine. Ndani ya Wizara kuna maabara ambayo inasimamia ubora wa maabara nchini *(National Quality Assurance Laboratory),* lakini kuna chombo ambacho kinaitwa *Private Health Laboratory Board* ambayo inasimamia ubora wa Maabara nyingie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama ni mdau, mimi nafikiri jina ambalo limependekezwa na muswada huu liendelee kuwepo kama ilivyokuwa imependekezwa na Serikali. Naskukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ndugulile. Lakini pia Waheshimiwa Wabunge maana ya haya maneno hii inayopendekezwa na Mheshimiwa Kangi Lugola ya *National Laboratory Regulatory Authority* ni kana kwamba huyu Mkemia Mkuu wa Serikali sasa ataanza kushugulika na zile maabara, yaani kwamba yeye ndiyo msimamizi wa zile maabara kwa hiyo itapoteza ile maana ya muswada mzima kwa hiyo nadhani tukubaliane na hoja ya Serikali baada ya maelezo ya mtaalam Dkt. Ndugulile pale, Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna mambo mawili tusichanganye.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa basi nilitaka kujua umekubaliana au hapa ngoja tulihoji Bunge ili turahisishe.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mimi kama mtoa hoja nilikuwa na-*summarise* na wale walioniunga mkono baada ya ku-*summarise* ya walioniunga mkono ndiyo tunaenda kupiga kura, ndiyo utaratibu.

**MWENYEKITI:** Sawa ngoja nitoe maelezo kidogo samahani naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, tuangalie hapa tunayo Miswada miwili kama kila mtu hoja yake itatuchukua dakika 15 sidhani kama ni lengo hasa ambalo tunataka kulifikia na kwa jambo kama likifikia hapa lilipofika inabidi lihojiwe kwa sababu mtoa hoja alishatoa kwa kirefu na maelezo yameshatolewa kwa kirefu. Sasa ikirudi tena hoja ya kuendelea tena halafu ndiyo tupige kura nadhani tunaweza tukachukua muda mrefu sana. Mheshimiwa Kangi Lugola dakika moja.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposema kwamba tuwe na *the National Laboratory Regulatory Authority* nilikuwa namaanisha kwamba hata Mkemia Mkuu wa Serikali na yeye atakuwa ana maabara yake na anakuwepo na yeye anasimamiwa na hii mamlaka ambayo iko *independent*. Simaanishi kwamba tukiwa na hiyo mamlaka basi Mkemia Mkuu wa Serikali hatakuwepo, atakuwepo na atabeba jukumu lake hilo hilo la *referral* wala sina  shida yeye akiwa *referral* lakini yeye huyu awe sawa na maabara zingine zote akiwa anasimamiwa. Hawezi yeye huyo huyo anasajili, huyo huyo anafuta, huyo huyo sijui anafanya nini haitawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge nimalizie kwa kusema, Bunge la Makaburu wakati ule lilipotunga sheria ta kuwauwa watu weusi, Bunge lile lilifurahia sana, lakini baadae wakaja kugundua kuuwa watu weusi ilikuwa ni dhambi.

Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tukipitisha sheria ya namna hii tutawauwa Watanzania, tutawachinja Watanzania. Tunakwenda kwenye kura, lakini ninaamini kwamba Waheshimiwa Wabunge wamenielewa na ninaamini kwamba kwenye kura mambo mazuri yataweza kujitokeza, Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kangi Lugola. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kangi Lugola kwa mapendekezo aliyosema hapa mwishoni ni kana kwamba anapendekeza sheria mpya kabisa ambayo siyo hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Lugola alikuwa anapendekeza mabadiliko kwenye jina, lakini kilichomo humu ndani kitabaki kuwepo pamoja na marekebisho mengine, lakini sasa kwa maelezo aliyotoa mwisho ni kana kwamba sheria nyingine mpya lakini wacha niwahoji Waheshimiwa Wabunge kwenye mapendekezo ya

Mheshimiwa Kangi Lugola kwenye jina la huu muswada ambao uko mbele yetu. Nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Katibu.

Ibara ya 1

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ile *title* imeshindikana kuirekebisha na hii niliyokuwa ninaendea sasa hii ya *clause 1* ilikuwa inapendekeza kubadilisha ile *the Governmet Chemistry Laboratory* basi nikubali tu kwamba hiki ni kisu kingine tena kwamba ambacho kinaenda kuwauwa Watanzania, naomba nikiondoe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola unatumia maneno mazito sana kana kwamba tumepitisha hapa kitu cha sumu hivi, lakini tuendelee. Katibu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Kifungu cha tatu kina mabadiliko ya Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Godwin Mollel na Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa sita baada ya *definition* ya *laboratory analytical report* napendekeza tu-*insert definition* ya *Minister* kwa maneno *Minister means the Minister responsible for health.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *further schedule of amendments* nimekubali, ninakubali kwa mapendekezo ya Mheshimiwa Kakunda kwamba *Minister means Minister responsible for health.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hiki kifungu cha 3 tulikuwa na marekebisho mawili. Moja ilikuwa ni suala la *poison* ambayo tulihitaji ilikuwa ni tata na tulihitaji kwamba muswada huu utoe *definition* ya neno *poison* kwa sababu ukiita tu *poison* inatumika sehemu mbalimbali *clause 3 by inserting the word interpretation of the word poison just after interpretation of the word Ministry which read as a substance that is capable of causing the illness or death or of a living organism when introduce or absorbed.* Tumendekeza *definition* hiyo lakini vilevile tulikuwa na (b) ambayo *clause 3, interpretation of the word Government laboratory analystis by deleting the word appointed by the Minister to perform which appear between the word person and duty also by substituting the word who performs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tulichomaanisha hapa, ukiona *Government Laboratoty Analyst* imeonekana kama ni mtu anayekuwa *appointed* na *Minister,* lakini tulifikiri hii ni *profession* yuko *by virtual of his prefession* kwa hiyo tukafikiri iondoke hilo neno *Minister.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tumekubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba tuweke *definition* ya neno *poison,* lakini hatukukubaliana na *definition* kama ambavyo ameipendekeza yeye. Na sisi kwenye *schedule of amendment* ya Mheshimiwa Waziri tunapendekeza *definition* nyingine ambayo itakuwa iko *broader* kuliko hii ya kwake kwa sababu ya kwake inaji-*narrow* kwenye vitu vichache ambavyo amevitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tunapendelea sisi *definition* ya *poison* ambayo iingie kwenye Muswada huu isomeke kama ifuatavyo; kwamba; *poison means substances that cause harm or death to organisms.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nasikia Mbunge mmoja anasema hamna hizi *amendments* za Serikali, lakini zimegawiwa *amendments* kadhaa watusaidie wale wahudumu nadhani kwa sababu bado zinaendelea kwenye hii karatasi iliyogawiwa. Kwa hiyo, waendelee kugawa lakini inasomeka hivyo alivyosema *means substances that cause harm or death to organisms.*

Sasa Mheshimiwa Dkt. Mollel ulipendekeza kwamba iingizwe hilo neno *poison* na maana yake. Sasa Serikali imekubaliana na wazo la kuingiza haya maneno, lakini inaweka maneno tofauti na yale uliyoyaweka wewe, sasa sijui hii ya Serikali kama unayo ama huna. Ngoja …

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Sina ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Hii ya Serikali ngoja wakusogezee hapo uione.

Mheshimiwa Mollel kwa sababu hii sio ndefu unaweza ukaisikiliza tu, inasema hivi; *poison means substances that cause harm or death to organisms* ambayo hii ya kwako ni kwamba tu ni ndefu kidogo lakini ina mantiki ile ile. Ya kwako inasomeka; *a substance that is capable of causing the illness or death of a living organism when introduced or absorbed.* Kwa hiyo, karibu Mheshimiwa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana. Tuendelee.

**MWENYEKITI:** Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naona tayari kimsingi ilikuwa inafanana kabisa na ya Mheshimiwa Kakunda na tayari Mhesimiwa Waziri tayari ameshasema ameiweka. Ilikuwa ni *definition* ya neno *minister* kwa sababu natambua kwamba lazima kuwe na hiyo *definition* ili tujue nani *responsible* kwenye huu muswada. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tumemaliza Wabunge waliokuwa na marekebisho katika kifungu namba 3.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kifungu namba 3 kuna hoja yangu ya pili hapa haijajibiwa.

**MWENYEKITI:** Ipi Mheshimiwa Mollel?

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Kwenye…

**MWENYEKITI:** Hii ya kuondoa maneno *appointed by the Minister to perform…*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** *Yes, yes yes!*

**MWENYEKITI:** Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa wakati najumuisha kwamba hiyo *definition ya Government Analyst* isomewe kwenye *section 13* ambapo *section 13* wakati juzi natoa maelezo yangu kwamba tatizo la kazi za Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali zimekuwa zikitamkwa katika sheria nyingine. Kwa hiyo, ukisoma Sheria ya Mwenendo ya Makosa ya Jinai ndiyo inasema kwamba hawa *Government Analysts* watateuliwa na Waziri ambaye anahusika na masuala ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa sana sana ukisema tunabadilisha hapa maana yake tukabadilishe pia *Criminal Procedure Act* ambapo ni jambo ambalo haliwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado ningemuomba Mheshimiwa Mbunge kwamba *definition* ibaki hivi hivi *Government Analysts* inakuwa kama ilivyosemwa kwamba ni *analyst means a person appointed by the Minister to perform duties of laboratory analysis as provided for under this act or any other written law*. Kwa hiyo *any other written law* ndiyo utazikutwa hizo sheria mbalimbali ambazo zinampa Waziri mwenye Waziri mwenye mamlaka ya kuteua hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kumthibitishia ni wataalam wanakuwa tu kwamba wanateuliwa kwamba sasa wewe ndo utakuwa ni mchunguzi wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, pia nadhani kifungu cha 13 kilichotajwa kinatoa huo mwanga wa hilo eneo. Una maelezo ama umekubaliana na Waziri?

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inamaanisha kwamba kuteuliwa sio ndiyo kinachompa hiyo *proffesion* inamaanisha ni ile cheo tu cha kufanya kutekeleza *policy,* nakubaliana na Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kifungu cha 13 ndiyo kinatoa hayo maelezo Mheshimiwa Mollel. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge Kifungu cha 3 nitawahoji.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KAMATI MEZANI:** Ibara ya 4 kina marekebisho ya Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Adadi Rajab na Mheshimiwa Lugola.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nina mapendekezo ya marekebisho kifungu (4)(4) kinachosema bila kujali masharti yaliyotangulia katika kifungu hiki Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa na haki ya kuingilia katika kesi au shauri lolote lililofunguliwa hidi ya mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimependekeza kwamba afanya hivyo kwenye, nimesema afanye hivyo bila kuathiri haki ya upande mwingine *unless* kama kuna tafsiri nyingine, lakini kama anaingilia kwa maana ya kuvunja au kuharibu haki ya upande mmoja ndiyo nilikuwa nasema isiwekwe hivyo pale. Nikasema kwamba; *"except that if the suit or matter is against the government, the Attorney General shall refrain from the proceedings of such suit or matter."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama atakuwa anaingia kwa maana ya kutaka kuharibu ushahidi au kwa maana ya kuingia kwa vunja haki za upande mwingine. Maana hapa kutakuwa na kesi au malalamiko kati ya Serikali na mtu mwingine yeyote, anaweza akawa Waitara *or someone else* lakini nikasema ni muhimu hiyo haki ya upande mmoja iweze kulindwa ndiyo mapendekezo yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwansheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Moja ni kwamba Serikali nayo ina haki yake ya kujitetea, ina *legal personality* na ndiyo kuna sheria inaitwa *The Government Proceedings Act* (Sheria ya Mwenendo wa Mashauri dhidi ya Serikali) na inapojitetea sio kwamba maamuzi yake ndiyo ya mwisho, inajitetea wapi? Inajitetea mahakamani na hapa Waheshimiwa Wabunge tunazungumza juu ya shauri ambalo limeshafunguliwa dhidi ya hii *authority* mahakamani. Kwa hiyo, ndipo wanapomuona Mwanasheria Mkuu anaingia pale. Na anaingia tu pale moja; kuisadia hii *authority* sasa kama mtu wa kuwateteta mahakamani, lakini yeye mwenyewe haamui kesi. Hiyo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia *authority* yenyewe inaweza kuwa inataka kushtaki, kwa hiyo *authority, Attorney General* anaingia mle aende aiwakilishe hiyo *authority* kule mahakamani ndiyo hivyo tu. Kwa hiyo, haiwezekani akaingia kwa namna ambayo inamnyima huyu mwingine anayeishitaki Serikali haki yake kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali sio anaeamua, anaeamua ni mahakama.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba kushauri Mheshimiwa Mwita Waitara akubali kwamba kifungu hiki jnsi kilivyo hakina madhara yoyote kwa mtu yeyote yule anayetaka kuishtaki hii *authority* na ndiyo maana kifungu kinachofuatia pale

yenyewe ile *authority* ina mamlaka ya kushtaki yenyewe au na kujitetea yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mazingira ambapo sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaingia pale. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kushauri Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waitara baada ufafanuzi huu nadhani unaona sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali hata akiingia hana namna ya ku-*influence* mahakama iamue kwa namna anavyotaka. Ni kuitetea tu ile taasisi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mwanasheria amejitahidi kutoa maelezo vizuri leo, naunga mkono hoja, tuendelee. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilikuwa na wasiwasi na *clause* hii ya nne na wasiwasi wangu kwa kweli bado ninao, kwanza naiona kama inaji *contradict* na *clause* ya pili kwa sababu *clause* ya pili inasema sheria hii itatumika *Tanzania Mainland* tu, lakini *clause* hii ya 4(2) inasema kwamba hii itakuwa *supreme and referreral to the United Republic of Tanzania,* sasa labda tupate ufafanuzi inakuwaje tena hii itatumika *Tanzania Mainland* baadaye hii *clause 2* ina *include* tena *United Republic of Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni haya maneno *supreme* na *referreral,* sasa yananipa tabu kidogo kwa sababu tutakapoipa uwezo ni muhimu sana kuwa na uwezo na maabara moja ambayo ita-*control* maabara zote hapa nchini. Lakini sasa tabu ni kwamba hapa maabara nyingine ambazo zitatoa *analysis* baadaye hizo a*nalysis* watakata rufaa, sasa hapa tuta-*encourage report* ziwe zinapingwa sana kila ambaye ripoti ambayo itatolewa na maabara basi inapingwa na hii ni ripoti tu ya kitaalam.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba labda kifungu hiki kwa sababu ya muda kiondolewe kabisa, ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Adadi Rajab anazungumzia kuhusu matumizi ya sheria hii kwamba inasemekana ni ya Tanzania Bara, lakini hapa kuna neno limewekwa *United Republic of Tanzania,* mbele ya macho ya

sheria itategemea tafsiri itakayotumika kwa wakati huo kwamba *United Republic of Tanzania* inatumikaje, kwa sababu *United Republic of Tanzania,* wakati mwingine inatumika kumaanisha Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Bunge ni Bunge la Jamhuriya Muungano wa Tanzania, lakini pia linashughulikia mambo yanayohusu Tanzania Bara tu bila kushughulikia mambo kwa wakati wote mambo yanayohusu Muungano. Kwa maana hiyo kama tafsiri kwa wakati huo itakuwa ni hiyo basi kutakuwa hakuna shida kwenye kutumia neno *United Republic of Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hoja yake ya pili kuhusu *supremacy* ya hii maabara ni kweli tunaweka ukuu wa hii maabara kwa sababu za kitaalam. Kwamba ni lazima tuwe tuna ngazi, tuna ngazi za chini, ngazi za kati mpaka ngazi ya juu na katika nchi ni lazima tuwe tuna chombo cha namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwisha kulieleza kwa mapana pale mwanzoni na umuhimu wa kuwa na chombo cha namna hii ni kwamba maabara hii sasa itakuwa ndiyo inatoa sauti ya mwisho kuhusiana na jambo lolote lile la uchunguzi wa kimaabara lakini hususan *within the scope* ya sheria yenyewe, sio kwenye kila kitu, kwenye *scope* ya sheria yenyewe, kwamba kwa mfano tunazungumzia vinasaba, sayansi jinai, *within that scope,* sheria hii itakuwa ndiyo inatoa sauti ya mwisho. Maabara hii ya Mkemia Mkuu wa Serikali itakuwa inatoa sauti ya mwisho kwenye mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna *supreme bodies* za maabara zinazohusika na mambo mengine, nazo zitatoa sauti ya mwisho kwenye mambo haya. Sasa sidhani kwa nini Mheshimiwa Rajab anaendelea kuwa na mashaka na ukuu wa maabara hii lakini naona ni utaraytibu wa kawaida. Maabara hii kama mtu hataridhika na matokeo yake maana yake mahakama inaweza ikaagiza rejea kupitia *panel* ya wataalam kwenye maabara hii hii, hakuna maabara nyingine kwa sababu bila kuwa na hii maana yake tutapeleka kwa nani sasa? Hatuna mahali pa kupeleka zaidi ya maabara hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Naibu Waziri lakini ni lazima kuangalia kwenye hili suala la utoaji wa ripoti, *especialy* hizi ambazo wanataka kukata rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hivyo nazingatia maoni ya Sheria ya Ushahidi hasa kifungu cha 48 ambapo maabara hii inatakwa itoe *expert opinion,* kwa hiyo, *expert opinion* hii inaweza kutolewa hata na upande wa *defence.* Sasa tunapokaribisha mambo haya ya rufaa tutaleta mkanganyiko mkubwa sana kwenye taarifa ambazo zitapelekwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka muangalie mtalifanyaje au kwenye kanuni zenu ambazo mtakuja kuzitengeneza suala hili mlipe umuhimu wa kipekee. Ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ameshakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, alikuwa anatoa tu maelezo ya zaida kabla hajakaa. Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba marekebisho yangu yalilenga kwenye maeneo mawili *clause 4(1), 4(2)* lakini niseme nimefanya kazi kwenye Jeshi la Polisi miaka mingi. Kati ya eneo ambalo linasababisha msongamano wa mahabusu magerezani ni upelelezi usioisha na upelelezi usioisha unatokana na sampuli nyingi ambazo zimepelekwa kwenye Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wakati ule Mkemia Mkuu wa Serikali hakuwa na Sheria hii ya kuwa rufaa, sasa leo tunampa meno ya rufaa nina amini sasa tutajenga magereza mengi sana katika nchi yetu, mahabusu watasongamana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi tulisema lina programu ya *modernization,* tunataka Jeshi la kisasa na walikuwa wameanzisha miundombinu. Walishakuwa na *DNA* mtambo pale pamoja na *forensic* sasa kama tutasema kwamba Jeshi la Polisi mtu aki-*dispute,* halafu aende kwa rufaa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, tutarudi kule kule. Tutakuwa tumetunga sheria ambayo haitusaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba pamoja na yote hayo, lazima Mheshimiwa Waziri hapa akubali kwamba ili ku-*avoid* suala la *conclusive* na *final report* na ili ku-*avoid* rufaa ambazo zitakaa muda mrefu pale, vyombo kama Jeshi la Polisi viwe vinachunguza na taarifa zake zinakwenda mahakamani moja kwa moja kwa sababu nachoni chombo cha Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola nilipokugongea kengele nilijua unamalizia sentensi, naona unaendelea, muda wako umekwisha.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Naomba majibu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kweli kutoa ufafanuzi kati ya uhusiano wa Mkemia Mkuu wa Serikali na Jeshi la Polisi na nataka kwanza kusema tuna uhusiano mzuri sana kati ya Jeshi la Polisi na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Lakini ni kweli kwamba kumekuwa na ucheleweshwaji wa matokeo na hiyo haisababishwi na muuundo wa kisheria. Ni kuna masuala ya vitendea kazi, watumishi, lakini pia kuna masuala wakati wa ku-*collect* sampuli na vielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwanza ninchotaka kumthibitishia Mheshimiwa Kangi kwamba sheria hii wala haizuii maabara kwa mfano ya vinasaba ya Jeshi la Polisi ya *Forensic* kufanya kazi zake, lakini kama alivyosema Naibu Waziri wakati tunajadili suala la *supremacy* na *referral status* ya hii maabara. Katika nchi mwisho wa siku lazima uwe na msemaji wa mwisho ambaye atakwambia kwa mujibu wa *laboratory analysis* ambazo nimezifanya *especially* katika haya maeneo matatu ya kemia, sayansi jinai na vinasaba huyu ndiyo mtu ambaye utamuamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mwisho wa siku kama livyosema Naibu Waziri, kama mahakama itasema labda ushahidi huu umecheleweshwa au kuna matatizo inaweza ikaamua kufanya *re-examination.* Nataka kumpa mfano kaka yangu Kangi nawe ni mwanasheria hata kwenye masuala ya *Judiciary* kuna mtu kule *supremacy, Court of Appeal* yeye ndio akisema hii ndiyo *final, final,* utaenda kukata rufaa mbinguni. Kwa hiyo, ndicho tunachotaka hapa kwamba tuwe na *supreme board* ambayo lakini kubwa tunalolisisitiza ni utaalam na viwango na misingi ile ya kufanya uchunguzi wa kikemia katika maeneo haya niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kaka yangu Kangi nataka kukuthibitishia wala hatuna shida na maabara ya Mkemia Mkuu ndiyo kwanza inajenga uwezo wa Jeshi la Polisi katika kufanya uchunguzi na tumeshawajengea mpaka jengo. Kwa hiyo, naomba ukubali tu kwamba hii *section 4* haina tatizo na kazi za Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola utakumbuka haya maelezo yaliyoko kwenye mapendekezo yako hayana tofauti sana na yale mapendekezo uliyokuwa umeyatoa kwenye jina. Sasa kama jina tulishalipigia kura na limepita vile, haliwezi kubadilishwa tena huku mbele Waheshimiwa Wabunge. Kwa sababu sheria unapoisoma unaisoma kuanzia mwanzo mpaka mwisho, sasa kama mwanzo tuliyakataa yale itakuwa ngumu kuyaingiza hapa. Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *clause 4* hiyo kuna suala hili la *supremacy* pamoja na *referral* na ndipo hapo nilipo. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini katika maelezo yangu

nimezungumzia pia msuguano utakaokuwepo kati ya Sheria hii na Sheria ya Ushahidi ya mwaka 1967. Kwa sababu huu ni ushahidi utakaopelekwa mahakamani, huwezi wewe ukatunga sheria kwamba utakuwa ni *conclusive* na *final* na ndiyo maana kule mahakamani ni *persuasive* kwa sababu kuna ushahidi mwingine. Kwa hiyo leo tuzingumzia suala la *finality* hapa, *finality is good but justice is better.* Kwa hiyo, lazima maneno hayo yanayogongana Mheshimiwa Waziri ayatolee maelezo na hakuyatolea maelezo, dada yangu Ummy naomba yatolee maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola, mapendekezo yako yanaongelea *regulator,* huku yanaongelea *supremacy* na hiyo *referral* uliyoisema. Sasa nataka kuelewa vizuri kwa sababu huyu *regulator* ndiyo yale maelezo ulipewa mwanzo kwa sababu huyu *Government Chemist* haji ku-*regulate other laboratories,* zile zipo isipokuwa kule wakishafanya ya kwao yeye wakimpelekea sampuli na yeye anafanya. Sasa hii tukiendelea kuijadili tunapata yale yale ya mwanzo ambayo walishajibu. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nafikiri hapa Mheshimiwa pengine tunachanganya kwanza Mkemia Mkuu wa Serikali haya maoni yake ni ya utaalamu haihusiani na kutoa haki*, it is not about just delivery,* ni haki tu ni *technical* na hii mahakamani kama alivyosema Mheshimiwa Lugola ni *persuasive it is just an expert opinion, it does not bind the court*. Kwa hiyo, Mheshimiwa akishaelewa vile na ulivyoelekeza pale hatutakuwa na ugomvi kwenye hili kwa sababu wanachozungumza ni kwamba kwenye mambo ya *technical know how,* kwenye utaalamu wa maabara hili Mkemia Mkuu wa Serikali yeye ndio anakuwa na ....ya mwisho, ni wa Serikali, *that is all.* Taasisi zenyewe hata zenye maabara zenyewe zinaweza zika-*volunteer* kupeleka kule hiyo namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili mahakama kama kuna *issue* pale kwa mfano polisi wao wanapeleleza, wanakamata, sasa ya kwao nayo iwe ni *final* itakuja kuwa shida. Kwa hiyo, kule mahakamani kukiwa na *context* mahakama inaweza ikasema hebu ngoja tumsikie tena Mkemia Mkuu wa Serikali anasema nini *and that is it*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri maelezo haya ambayo Waheshimiwa Waziri wameyatoa na hicho walichokiona hapo wakisema kinatosha nimuombe Mheshimiwa Lugola kwamba aridhike na hayo maelezo ya Serikali, tunatunga sheria hizi, sheria *is a living document,* leo ita-*save purpose* ipo-*save purpose* Wabunge wana haki hata ya kufanya *amendment* wao wenyewe *on their own* au watatushauri tutaleta muswada hapa tutarekebisha kama kutakuwa na shida ya utekelezaji wa sheria hii, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola malizia hoja.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Nashukuru tuendelee Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kifungu namba 4 mapendekezo yaliyokuwa yametolewa na Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Adadi Rajab na Mheshimiwa Lugola yote hayajakubalika wote wameondoa mapendekezo yao kwa hivyo nawahoji. Kifungu namba 4 kinakubaliwa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Kifungu namba 5 kinamarekebisho ya Serikali, Mheshimiwa Dkt. Mollel, Mheshimiwa Adadi Rajab, Mheshimiwa Mbogo na Mheshimiwa Lugola.

**MWENYEKITI:** Sasa sina uhakika kama wote tumeshapata marekebisho ya Serikali ili anaposimama mtu kutoa hoja yake ajue kama Serikali imeshayachukua ama hapana. Tumeshapata wote marekebisho ya Serikali?

**WABUNGE FULANI:** Hapana

**MWENYEKITI:** Hapana sawa. Basi tuendelee Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN A. MOLLEL:** Kwenye kifungu namba 5 ninapendekeza kwenye *clause 5 by adding the new word* kwenye *sub clause* 2 *which will read; "Notwithstanding the provision of sub section 1, a person aggrieved by the results of the authority shall have the right to challenge the result to the High Court."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nikimaanisha kwamba ukisoma vizuri kwenye hili eneo wanasema *the authority shall be the referral laboratory and it is analytical result shall be final and conclusive on matter releted to laboratory analysis.*

Sasa ukisema hivyo ni *final* maana yake ni kwamba kuna wakati sawa ni *final* hatukatai kwamba ni lazima tuwe na sehemu ambayo itakuwa ni mwamuzi wa mwisho lakini inawezekana mtu huyo hakuamini hicho kilichofanyika basi apewe nafasi ya matokeo kurudiwa na hata akienda mahakamani kusema

kwamba haamini kilichotolewa, basi ipatikane nafasi mpya ya *test* kufanyika kwa mara ya pili ili kujiridhisha zaidi na kutengeneza utaratibu ambao mhusika atashiriki na kuamini hicho kinachofanyika kwamba ndio ukweli, nawasilisha.

**MWENYEKITI:** Serikali, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wakati kila mtu ana haki ya kwenda mahakamani, mahakama huwa inaangalia haki kwa mujibu wa sheria kwamba kama jambo limefanyika kinyume na utaratibu wa sheria, kwa hiyo mahakama wakati mwingine sio sehemu ya kutoa majibu ya kitaaluma sasa hizi rufaa za kimaabara ni kwa ajili ya kujiridhisha kisayansi lakini si kujiridhisha kwa haki ya kisheria kwa hiyo, itakuwa ngumu kidogo  Majaji wakageuzwa kuwa ndio Wakemia  katika hili kwa maana hiyo tunasema kwamba hakuna sababu ya kufanyia marekebisho suala hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN A. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala hiki anachokisema Mheshimiwa Possi naona kwamba ana-*support* ninachokisema na sisi tunachotaka ni mtu kuwa na *room* pale itakapofanyika *conclusive result* ku-*challenge* kile ambacho kimefanyika kwamba sio kweli kirudiwe na maabara hiyo hiyo, kwa mfano naambiwa Dkt. Mollel umebaka, lakini najua *exactly* sijabaka, *assume* ikapelekwa kitu kinachoonesha kwamba ni mimi na ni *sample* ambayo inaonekana ni ya kwangu, lakini naamini sivyo, maabara ikatoa ni mimi inawezekana kikatokea kitu chochote nipate nafasi ya kwenda mahakamani itoke kitu kitakachochukua *sample* na kuhakikisha kile wanachokifanya nikione kabisa kwamba ndicho kilichoingia kwenye mashine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokisema hatukatai kwamba ni saini tunataka mahakama itoe nafasi ya *scientific analytical process* nyingine ifanyike ndicho tunachokisema, hatusemi ifanyike kimahakama lakini irudiwe kwa agizo la mahakama, sayansi tena irudiwe tena kwa mara ya pili na namna ya uwazi zaidi mtakaouamini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mheshimiwa Dkt. Mollel ni kutoa fursa kwa maelekezo ya mahakama ama kwa kutokuridhika kwa mteja wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kupata *re-examination* ya *sample* zake, kwamba labda matokeo yaliyopelekwa mwanzoni hajaridhika nayo, kwa hiyo anataka sasa ifanyike *re-examination* sijui Kiswahili rahisi ni nini kwamba

marudio ya kipimo kile ambacho kilifanyika pale awali. Kwa kawaida kwenye mambo haya ya kisayansi, hicho kitu kinatolewa *automatically* tu, wala huhitaji kuweka *clause* kwenye sheria kwa sababu mahakama ina nguvu ya kuweza kuiagiza maabara ifanye *re-examination* kwa utaratibu ambao mahakama itaona ni utaratibu unaofaa, wala hakuna haja ya kuweka hapa na fursa hiyo kwa kawaida ikitolewa kule ndani ya maabara yenyewe wataweka *panel* na watafanya *procedure* za kimaabara za kuwa-*blind* baadhi ya wale wanayoifanya ile kazi wasijue wanachokifanya ni nini ili kuhakikisha matokeo yatakayotoka pale yatakuwa ni ya uhakika na ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hakuna shaka ya makosa kwenye upimaji wa *sample* kutokea na kuna fursa hiyo niliyoisema ya mahakama kuagiza maabara kwenda kufanya *re-examination,* ni *procedural* wala haihitaji kukaa kwenye sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel malizia hoja.

**MHE. DKT. GODWIN A. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Waziri bado amekubali lakini ameweka siasa kidogo kama alivyo mzuri kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba huwezi ukawa una wasiwasi na maabara humo humo ndani ya maabara hiyo wanakupa fursa ya kukupa kitu ambacho kiko huru cha kuweza kukusaidia kupata ukweli, haiwezekani. Lakini haiwezi ikabaki hivi hivi bila sheria kutamka halafu kikatoa hiyo fursa kutoka hewani. Nafikiri kwa sababu tunatengeneza sheria ni vizuri ikaingizwa itamkwe kabisa kwa sababu hili eneo ni *sensitive,* unaposema huyu mtu ndio muamuzi wa mwisho na haojiwi popote ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nasema ni vizuri kukawepo na namna ambayo inaonesha tunakubaliana wote kwamba wawe *conclusive,* lakini vilevile inapotokea maana yake itakuwa ni *rare cases,* inapotokea kitu kama hicho basi ionyeshe kuwepo na kitu kimeingizwa kitaalamu ya kisheria cha kuonyesha kwamba huyu mtu anaweza. Kwa sababu inaweza ikatokea sio kwa makusudi nimechanganya *sample* mtu amechukua kwenye *referral* huko Moshi anapita hivyo akachanganya kwa bahati mbaya na imeshatokea mara nyingi kwa hiyo tunasisitiza. Niwaombe wenzangu mniunge mkono kwa sababu hili ni muhimu sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nitawahoji wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Mollel waseme ndio, wasiokubaliana waseme sio.

Waheshimiwa Wabunge kama mmenichanganya kidogo narudia kuhoji wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mollel ya kuongeza hayo maneno kwenye hiki kifungu waseme ndio wasiokubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Mollel kwenye kifungu hiki waseme sio. Waliosema sio wameshinda.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Mheshimiwa Adadi Rajab.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa inasambaa pamoja na Dkt. Mollel kwamba haya maneno *final and conclusive* katika *sub clause* yataleta mkanganyiko mkubwa sana mahakamani kwa sababu kisheria sasa hivi kwenye sheria za ushahidi taarifa zinazojulikana kwamba *at least* haziwezi kuwa *challenged* ni taarifa wa *finger prints* labda na wa *DNA*. Lakini pamoja na taarifa hizo pia hizo zinakuwa *challenged* sasa wasiwasi wangu ni hayo maneno ya *final and conclusive,* labda Waziri angetoa ufafanuzi zaidi au Waheshimiwa Wabunge wameona kwamba wameridhika basi niendelee na kifungu kingine cha tatu. Lakini ni hisia tu kwamba taarifa kama hizi wataalam watakapozipeleka mahakamani zitaleta matatizo sana ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Balozi Adadi Rajab tukisoma *section 5* tunasema *analytical result on matters related to laboratory analysis,* kwa hiyo, hilo ndio maneno. Kwa sababu sisi tumeshasema ni *supreme board when it comes to analytical laboratory analysis* kwenye masuala ya kemia kwenye masuala ya sayansi jina na vinasaba lazima katika nchi uwe na mtu mmoja akasema hizi ndio *result* zangu na hazihusiani au hazimzuii mtu mwingine kufanya shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeeleza kama mtu hujaridhika Naibu Waziri amesema hapa unaweza ukaomba sasa *re-examination* na mimi natoa mfano wa *court of appeal* ikishafanya *decision* labda kuna mgogoro wa ardhi ikishakuwa ni decision *final you cannot appeal* sana sana utakachoomba ni *AG* kutizama *re-examination,* lakini ni *final.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika masuala ya *lab analysis* pia tulikuwa kuwa na *supreme board* ambapo matokeo yake yatakuwa ni ya mwisho na hayawezi kuhojiwa na chombo kingine yaani katika masuala ya *analysis.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado ningemshawishi kaka yangu Adadi Rajabu akubaliane na kifungu hichi kama kilivyo.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee sijaelewa umesimama kwenye kufanyaje, ameshakubali Mheshimiwa Adadi. Haya Mheshimiwa Richard Mbogo. *(Kicheko)*

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho yangu ni kifungu cha 5(2)(a) katika kutaja vitu vinavyofanyiwa utafiti ilisahaulika kemikali zinazotumika majumbani ikatajwa tu za viwandani. Kwa hiyo marekebisho yangu ni kwenye kuongeza hiyo *industrial and consumer chemicals* kwa hiyo kama Serikali inaridhia tuendelee.

**MWENYEKITI:** Serikali anayesimama ni nani hapo, sioni aliye tayari au hamna haya marekebisho.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kutafuta *further schedule of amendment* tumekubali mapendekezo, tume-*insert industrial and consumer*. Mheshimiwa Mbogo nadhani umeridhika ahsante tunashukuru kwa mapendekezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo mapendekezo yako yamechukuliwa na kuwekwa kwenye marekebisho ya Serikali. Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hii *clause 5* in mahusiano na mambo ambayo huku juu nimeyaacha lakini niende kwenye moja hili la *supremacy* na *referral* na kama alivyosema Mheshimiwa Adadi na Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna zile *sample* ambazo zinaweza zikatokea ambazo haziwezi zikashughulikiwa na maabara zingine, sasa *sample* kama hizi zitapelekwa wapi wakati sisi maabara tunayozungumzia hapa ni maabara ya rufaa yaani inapokea vitu ambavyo tayari vimekwishafanyiwa uchunguzi na *laboratory* nyingine. Sasa ndio maana nikaona kwamba mambo ya *supremacy* au itakuwa ni *final* na nini yanaweza yakaleta shida na matokeo yake tukaendelea kuona maabara hii ambayo tunaiita ni ya rufaa ikawa pia inapokea *sample* zingine ambazo sio za rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimemsikia pia Mheshimiwa Waziri mwanzoni anasema kwamba hata kama hospitali ni ya rufaa lakini inakuwa na shughuli zingine mle sasa ndio wasiwasi wangu Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo shughuli zingine wakati hii ni ya rufaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba tunaposema kwamba matokeo ya maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali yatakuwa ni ya mwisho tunamaanisha tu yale matokeo yaliyotokana na uchunguzi wa sampuli mbalimbali ambazo zimefika kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ama kupitia maabara nyingine ambazo zimeshindwa kuchunguza ama hazina uwezo wa kuchunguza ama kupitia amri ya mahakama kwamba *sample* hizo zichunguzwe na Mkemia Mkuu wa Serikali ili mwisho wa siku Mkemia Mkuu wa Serikali apeleke ushahidi wake wa kitaalamu kuhusiana na *sample* ambazo amechunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na labda niweke sawa jambo moja hapa kwenye ushahidi wa kitaalam mara zote ni maoni ya yule mtaalamu husika na hayahusiani na ule mwenendo wa ile kesi. Yeye anapeleka maoni yake kuhusiana na kitu ambacho ameambiwa akichunguze hivyo hivyo inatokea kwa mashahidi wa kitaalam ambao ni madaktari na wanapopeleka pale maoni yao yanakuwa ni ya mwisho kwamba alichokisema ndicho hicho kama wewe hujaridhika ukaieleza mahakama kwamba pale hujaridhika na maoni ya mtaalam huyo ambayo yametolewa pale mahakamani, mahakama itapima hujaridhika kwa vigezo vipi na mahakama itaamua, aidha, ikutume kwa mtaalamu mwingine akafanye uchunguzi ama ikutume kwa mtaalamu yule yule akafanye uchunguzi wa marudio *(re-examination)*. Hakuna namna nyingine yeyote ushahidi wa kitaalamu ni wa kitaalamu na utabaki kuwa ushahidi wa kitaalamu na kwa maana hiyo kwa kuwa hauhusiki na uamuzi utakaofanywa na mahakama utabaki kuwa ushahidi wa kitaalamu kama ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi tunasema huu utakuwa ndio ushahidi wa mwisho kwa sababu ndio utakuwa wa mwisho kwa sababu hatuna Mkemia Mkuu wa Serikali na hatujampa mamlaka ya kuwa ndio ushahidi wa mwisho kwenye mambo yanayohusu vinasaba, *forensic* na vitu vya namna hiyo maana yake hatuna tu mtu anayeweza kufanya hivyo sasa tutafanyaje kwa mfano tusipompa ukuu Mkemia Mkuu wa Serikali tumpe nani sasa hatuna namna nyingine naomba mapendekezo kama tulivyoyaleta kwenye Muswada huu yabaki kama yalivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola kwa sababu haya mapendekezo yangeambatana na hicho kifungu cha 4 na hicho kilishapitishwa nadhani inabidi ukubaliane tu kwamba hayo maneno *referral* bado yapo na hayo maneno *supreme* bado yapo kwa hiyo hayawezi kuondolewa tena kwa sababu kile cha nne kimeshapita. Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuendelee. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 6 kina marekebisho ya Serikali na Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *Clause* 6…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda! Mheshimiwa Adadi Rajab nakuona umesimama.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, nilikuwa nangojea, kwenye *schedule of ammendment* yangu nili-*propose new provision* kwenye *clause 5(3)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi, bahati nzuri ama mbaya tukishahoji kifungu kimeshapita, uliposimamishwa kuongelea kifungu hiki ulipaswa na hayo pia uyaseme kwa sababu sasa tumeshawahoji Wabunge hatuwezi tena kurudi nyuma kwenye kifungu hichohicho. Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 6, Mamlaka itakapokuwa inaanzisha Idara, Vitengo na Kanda pamoja na kuajiri watumishi kilielekeza pale kwamba washauriane tu na Waziri wa Utumishi na Waziri wa Fedha.

Sasa napendekeza yaongezwe maneno, *the Minister,* baada ya neno *with;* kwa maana kwamba kumhusisha Waziri wa Afya vilevile kabla hawajafanya hayo maamuzi.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Kakunda. Tumeiweka kwenye *my further schedule of ammendment* kwa hiyo, tunakubali mapendekezo yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda mapendekezo yako yamechukuliwa na Serikali. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji. Kifungu cha 6 chenye mabadiliko ama marekebisho ya Serikali na Mheshimiwa Kakunda kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 7

**NDG. LAWRENCE MAKIGI- KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 7 kina marekebisho ya Serikali, Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Dkt. Mollel, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Lyimo, Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab na Mheshimiwa Mbogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika orodha ya Wajumbe wa Bodi, kama ilivyo kwenye kifungu cha 7(2)(a) mpaka (f) nimependekeza kwamba kifungu (a) kiondolewe badala ya mwakilishi kutoka Jeshi la Polisi, awekwe mwakilishi kutoka Wizara ya Maji kwa sababu Wizara ya Maji ndio inaongoza kuwa na maabara takribani 17 hapa nchini na kwa sababu, kazi hii ni ya kitaalamu, wanaweza wakawa wanamchango mzuri zaidi kwenye bodi badala ya Jeshi la Polisi ambalo wakati wowote ukitaka huduma za Jeshi la Polisi, kwa mujibu wa *Police Force and Auxiliary Services Act,* wako tayari kutoa huduma ikiwa ni pamoja na ku-*inspect premises* za mamlaka yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa isije ikawa kwamba, tunamuingiza Polisi humu ndani ili kuwapunguza nguvu Jeshi la Polisi katika kutenda kazi zake; naomba tuache Jeshi la Polisi libaki huru katika kutekeleza kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha (e) nilikuwa napendekeza badala ya mwakilishi kutoka Wizara ya Utumishi, awekwe mwakilishi kutoka *TBS.* Kwa maana kwamba *TBS* ndio inashughulika na viwango vyote, *standard* zote nchini hapa. Kipengele (f) badala ya mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha inazo kazi zake za msingi nyingi tu, kama tunataka hela tutapata tu kutoka Wizara ya Fedha, kwa hiyo, hamna haja ya kumuweka mtu kwenye bodi kutoka Wizara ya Fedha, badala yake awekwe kutoka Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa sababu nchi yetu hii ina mambo mengi ya kufanya kwenye viwango vya samaki tunaowasafirisha nje na minofu ambayo tunaitumia hapa hapa nchini na kusafirisha nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu yalikuwa ni hayo tu. Ahsante sana.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Kakunda, lakini kwenye *amendment* ya kwanza ambaye anataka tumuondoe, *a representative from the Police Force.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunadhani ni muhimu sana kwa sababu kama hoja ambayo Mheshimiwa Kangi Lugola na kaka yangu Mheshimiwa Adadi Rajab, ambayo walikuwa wanaisimamia walikuwa na wasiwasi kuhusu uhusiano kati ya Jeshi la Polisi na Mkemia Mkuu wa Serikali na *especially* wakati tutakapoanzisha hii kuwa ni mamlaka. Kwa hiyo, bado mwakilishi wa Jeshi la Polisi anatakiwa kuwemo kwenye Bodi ya Mamlaka ya Maabara ili pia kuweza kushauriana kwa karibu, lakini pia kwa ajili ya kuongoza utendaji wa maabara hii kwa hiyo, tunakataa mapendekezo ya kuondoa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kaka yangu pia, Mheshimiwa Kakunda anasema tuondoe mwakilishi wa Waziri ambaye anahusika na masuala ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatengeneza *authority.* Tukitengeneza *authority* maana yake hii ni mamlaka, kwa hiyo, mwakilishi wa Wizara ya Fedha na hapa tunamlenga sana sana Msajili wa Hazina. Kwa hiyo, ndio utaratibu kwamba ikishakuwa ni Mamlaka ya Serikali kunatakiwa na mwakilishi wa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la pili labda ni kusema kwamba tuongeze huyo mwakilishi kutoka Wizara ya Maji, Mifugo na Kilimo, *especially* na mtu wa *TBS.* Bado sisi tulidhani kwamba kwa sababu nime-*move schedule of amendments* hapa tunadhani kwamba, tusiongeze hao watu kwa sababu *focus* ya kazi hii ya maabara ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kama tulivyosema itakuwa kwenye masuala ya kemia, sayansi, jinai, na masuala ya vinasaba. Kwa hiyo, hatuingilii, hatutaenda sana kwenye..., tutafanya, lakini tunaona tusiingize mambo ya *TBS* na mambo ya maji moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba tu kumshawishi kaka yangu Mheshimiwa Kakunda, bodi ibaki na watu haohao wachache.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatoa ushauri tu kwa nia njema. Nimezungumza wakati nawasilisha pale mwanzo kwamba uhuru wa Jeshi la Polisi ni muhimu sana ukalindwa. Watakapokaa kwenye bodi wakafanya maamuzi ambayo maamuzi yenyewe lazima yawe *question* na yenyewe, Jeshi la Polisi litapungukiwa nguvu ya kutekeleza kazi zake kwa sababu watakuwa ni wahusika kwenye maamuzi yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri kwamba hata kama hao wengine hawataingizwa, basi huyu wa Jeshi la Polisi aondolewe ili kusudi Jeshi la Polisi libaki na msingi wake wa kufanya kazi kwa uhuru kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi. Asante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na niungane na hoja ya Mheshimiwa Waziri, kwanza kabisa nitofautiane na Mheshimiwa Kakunda kwa sababu kwanza lazima turudi kwenye majukumu ya bodi hii inafanya kazi gani. Shughuli za kwenda kwenye mambo ya *analysis* sio kazi ya bodi, kwa hiyo, bado polisi ikiwemo kwenye bodi hiyo haiwezi ikawa imeingilia masuala mazima ya utendaji. Kwa hiyo, kibaki kama mapendekezo ya Serikali yanavyopendekeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda malizia hoja.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kwenye sehemu hiyo, kuna mapendekezo yafuatayo; kwenye *clause 7(2)(a), delete the word person appearing between the word amongst and with and substitute with the word citizen.* Tulichofikiri ukisema *person* anaweza akawa hata Mkenya ni *person,* mzungu ni *person,* lakini ukitumia *citizen* basi, itakuwa imeelezea kabisa kwamba ni mtu yeyote lakini Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini (b) naona kama mawazo yetu yameshachukuliwa na Serikali kwa hiyo, nipite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye (e) tulisema *in clause 7(2)(c), by re-writing the following, two representatives from public and private higher learning institution or research institution whose specialist is in either,* lakini vilevile (f) *by adding the new sub-clause (g) which will read as, a representative from private sector.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri inaeleweka eeh! Kwamba, tunajaribu kutengeneza kwamba, kwa sababu, tumesema itakuwa inahusika na watu wengi, basi iwe na watu kutoka *private sector,* lakini vilevile kuwepo na watu kutoka *learning institution* za *private* na za *government.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasilishe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *clause 7(2),* ambapo ni *composition of the board;* nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mollel kwanza kwenye *my further schedule of amendment* nimeongeza *two representatives from higher learning or research institutions in order to take into consideration* hoja yako ya kuwa na watu kutoka kwenye hizo *private institutions,* kwa hiyo, ipo pale. Na ya pili ulikuwa unataka *Tanzanians, I think it is well known* kwamba, tukishasema *shall be appointed* sheria inasema kwamba *the board shall consist of a chairperson appointed by the President;* Rais hawezi kuteuwa Mkenya, Rais *obvious* atateuwa Mtanzania, wala hatuna haja ya kuiweka kwenye sheria na ndio *standard format* ya sheria zetu, hatusemi, tunadhani inajitosheleza kama ilivyo, lakini ya pili tumeikubali kwamba, ya ku-*take into consideration representative from private institutions.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel mapendekezo yako Serikali inasema imeyachukua. Naam, karibu!

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Waziri, ila nina wasiwasi kidogo kwenye hili la *person.* Labda hebu tuangalie kwenye Katiba imekuwa *defined* ni *icitizen* au *person,* ili tujiridhishe twende mbele, lakini kwa nadharia ulichokisema nakubaliana na wewe, lakini hebu tuangalie kwenye Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa iwe ni *citizen* kwa sababu, ukisema *person* imetoa *room,* siku moja tunaweza tukapata mtu anayependa watu kutoka, akaamua kutumia hii *loop* kuchagua mtu yeyote. Kwa hiyo, ni vizuri tuseme *citizen* ioneshe kabisa asije akatokea mzungu yuko *research* ametokea Havard akapewa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tafsiri ya sheria, wakati mwingine, *of course* huwezi uka-*explain* kila kitu la sivyo tungekuwa tuna mavitabu makubwa yameandika mambo mengi mno. Ni utaratibu wa kawaida kabisa katika sheria mbalimbali ambapo mamlaka, kama ni Waziri au Rais, anateuwa; kuna hizo *clauses* kwamba *he shall appoint from among persons and so on.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo hayo mambo kwa mfano kwenye sheria kwa mfano zinazounda Baraza la Watu Wenye Ulemavu, sheria zinazounda kwa mfano *SUMATRA,* sheria zinazounda *TCRA* na kote huko hakujawahi kutokea ubishi eti kwamba *definition* ya hiyo, ya *person,* maana yake inatoa *allowance*

kwa mamlaka husika ku-*appoint* mtu ambaye si raia! *Afterall* taratibu za kawaida za utumishi zita-*take precedence*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, malizia hoja.

**MHE. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nisimsumbue Mwanasheria Mkuu asisimame, nakubali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye hii Ibara ya, umesema kama mmeishapiga kura imepitishwa ile habari ya polisi tusirudie, lakini mimi nilikuwa na shida na Ibara ya 7(2)(a), lakini vilevile pamoja na kwamba Waziri ameleta marekebisho hapa, nilikuwa nadhani kwamba hizi sheria tunapotunga pia, tuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kuangalia Wakenya wanayo *Pharmacy and Poison Board* na wana watu karibu kumi. Watu wote ni *professional* ambao wameteuliwa kwenye hii bodi yao, wote ni *professional,* lakini ukiangalia hapa nilipendekeza kwamba tuwe na mtu ambaye ni mwakilishi kwa mfano wa *organization umbrella of laboratory technicians* kwa sababu hawa na wenyewe kwenye hii bodi watakuwa wanahusika, ndio nimependekeza kwenye (g) pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilipendekeza pia, kama alivyosema Mheshimiwa Mollel hapa awe *a qualified Tanzanian* katika ku-*appoint*. Sasa mimi sioni kuna shida gani ya ukakasi wa lugha kwamba kwa mfano kama sheria nyingine hazijataja, Mheshimiwa Possi anavyosema, kwani kikiwa kitu kipya kuna dhambi gani kama watu wana wasiwasi na hayo maneno? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado napendekeza hilo neno libadilishwe tusiseme *person,* tuseme tu *qualified Tanzanian* au *citizen* ieleweke kwamba ni Mtanzania. Na sioni kama kuna shida, maana ni *wording* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nina mapendekezo na nilipendekeza kwamba, hawa watu wapewe miaka, *at least* huyu awe na uzoefu wa miaka 5 tofauti na miaka kumi iliyotajwa kwa sababu, ninaamini kwamba, kama huyu amefanya kazi na akawa na uzoefu wa miaka mitano, inatosha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini (h) pale nilipendekeza pia kwamba tuwe na mwakilishi wa *private universities* ambaye ana utaalam wa mambo hayo na bado nilikuwa nimesisitiza kwamba, kuna haja ya *TBS* pamoja na mambo ya Wizara ya Kilimo. Hayo ndio mapendekezo yangu kwenye hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sehemu ya mwisho kwenye *paragraph* pale kwenye nyongeza (c) walitaja kwamba hawa watu watafanya kazi miaka mitatu, napendekeza iwe miaka mitano, ili wapate muda wa kutosha na tujenge *institution,* yaani kuwa na mwendelezo. Akipewa kazi miaka mitatu mwaka mmoja anapata uzoefu, miwili anaanza kufanya kazi, muda umeisha anaweza, anaweza sio lazima ateuliwe, lakini *at least* miaka mitano anaweza akatumia uzoefu wake aka-*plan* na akawa amejenga taasisi. Ni hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwebnyekiti, kwanza nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Mwita, juzi Ijumaa alitupa maoendekezo mazuri sana na tulifurahi kwamba yeye ni mmojawapo wa wakemia kwamba badala ya kuwa na *one representative from higher learning or research institution* kwamba tuweke wawili kusudi angalau upate mtu ambaye ana masuala ya *chemical* na masuala ya *biology*. Kwa hiyo, tume-*take into consideration* kwenye *my further schedule of amendments.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba nilikubali. Nakubaliana na yeye kwamba, tuna haja pia ya kuwa na mwakilishi kutoka *umbrella organization* ya *professionals.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani, *it is an oversight* kwa sababu sheria ndio hii ambapo hatujapitisha kwa hiyo, kwa sababu tutapitisha hii sheria ambapo kutakuwa pia na *umbrella organization* ya *professionals* kwa hiyo, tunakubali pia, hayo mapendekezo ya kuwa na mwakilishi katika Bodi hii ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mapendekezo yake mengine mawili ya kuwa na..., *actually* ni moja, la kuwa na mwakilishi wa *TBS* tumeshalitolea maelezo. Na kwenye *private university* tayari tumeshasema *from higher learning or research institution,* hatujasema *whether is a private or is a public* kwa hiyo, *private* tayari wako *covered.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kaka yangu Mheshimiwa Mwita, akubali kuridhia muswada huu pamoja na ile *my further Scheduile of Ammendments* ambayo nimeiweka Mezani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, sina uhakika kama umeshapata hayo marekebisho ya Serikali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyapata.

**MWENYEKITI:** Lakini baadhi ya haya yamechukuliwa. Karibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyapata na nimeyasoma na hayo unayozungumza hayakuweko *actually.* Kwa mfano, ile wanavyosema *private,* haijasemwa. Hiyo kama kuna *private university* watawakilishwa haijasemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hapa kwa mfano, katika huko kote nyuma wana-*insist* kwamba awe ni *public serving, which means* atakuwa ni sekta ya Serikali. Tukasema watu binafsi wawakilishwe hasa *university* zile ambazo zina-*deal* na mambo ya kisayansi na utafiti na *research* kwa hiyo, tungependa isemwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni hili la hapa *language.* Nilikuwa tu nimependekeza, amesema, *the Board shall consist of chairperson appointed amongst qualified Tanzanians.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mheshimiwa Naibu Waziri alikataa kwamba Mheshimiwa Dokta Possi kwamba, ibaki *citizen* tuna-*insist* kwamba, hili neno litajwe. Wala haliongezi, wala halipunguzi, lakini kwa uelewa nadhani ikawa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nahitaji maelezo kama Mheshimiwa Waziri hajakubaliana, basi ningeomba Bunge lijadili, kwa sababu ni jambo muhimu sana na *of course* ni kitu kipya, tunahitaji mawazo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema wenzetu Wakenya *member's* hapa bodi ni watu kumi na wote ni *professional,* ili kuwa na uhuru wa kuweza kufanya. Kwa sababu mwisho wa siku hii bodi ikifanya kazi *results* zake zote zinaenda Serikalini; yaani kama ni Polisi wataipokea, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataipokea, Waziri ataipokea kwa hiyo, wala haina shida. Sisi tunapendekeza kwa maana ya kuboresha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri ambaye ana dhamana ya sera ya sheria hii. Amezingatia sana hoja za Mheshimiwa Waitara na amekubali na kama tulivyoona amewasilisha mapendekezo yale, lakini na sisi Serikalini, Mheshimiwa Waziri katika mapendekezo zaidi amesema kwamba ile *amendment* amesema hivi; *two representatives from higher learning or research institutions whose speciality is,* wameyataja pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ni *two representatives from a higher learning institutions* na Mheshimiwa Mwita Waitara anataka watoke, yeye alikuwa anafikiri kwamba wote hawa watatoka kwenye *public institutions* tu.

Kwa hiyo, katika ku-*appoint* Mheshimiwa Waziri ni lazima achukue aidha, mmoja kutoka kwenye *public service* mwingine kutoka kwenye *private,* yaani *public institution* mwingine kutoka kwenye *private institutions.* Kwa hiyo, hapo watakuwa wamezingatiwa Mheshimiwa Waitara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo kifungu cha 7(4) cha hii sheria kinasema hivi, *the Board may, where it considers as necessary, co-opt any person to attend its meeting provided that such person shall not have a right to vote.*

Kwa hiyo, watu ambao bodi ikiona kwamba kwenye hili tunaloenda kuliamulia, Waheshimiwa Wabunge, ni vyema tuwasikilize hawa watu wanaweza bado wakamuita huyo mtu ili wafanye maamuzi wakiwa *well informed.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba kushauri kwamba kwa hiyo, maelezo haya ya Waziri aliyoyatoa kuhusu uteuzi huu kwenye hii bodi tuyazingatie kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri ameleta hayo mapendekezo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara naomba umalizie hoja yako.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba niseme mawili, moja hiyo *language*, maana hapa anasema:-

*7(2) the Board shall consist of a Chairman appointed by the President from the amongst persons with ten years of managerial experience in public service…*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *of course* hii ipo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho mimi niseme kwamba Waheshimiwa viongozi na hasa wanaosaidia Waziri kujibu maswali, niseme kwa mfano nimesema *pharmacy and poison board* ya Kenya wamemu-*appoint chairperson in the light of medical service, registrar* wamempa *chief pharmacist, director of veterinary services* halafu wakawakilisha *pharmaceutical society, civil society, community;* yaani watu 10 wote ni *professional.*

Kwa hiyo, ningeomba kwa zinazofuata tunapokuwa tunaleta mapendekezo si kwamba tunataka kupambana na Serikali, tunataka

kuboresha; kwa hiyo wanapokuwa wanatujibu wajibu pia katika *professional ways.* Nataka niseme hivyo, vinginevyo naomba tuendelee kwa sababu kuna mapendekezo mengine huko mbele tutachukua muda zaidi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nina mapendekezo kwenye hoja hiyo hiyo. Msingi wa hoja yangu ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na *balanced representation* ya *private* na *public*. Pamoja na maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri sijajua ni kwa nini kwa sababu haya mapendekezo yake aliyoleta anasema *two representative from higher learning or research institution.* Swali langu ni kwamba tutahakikishaje kwamba mmoja kati ya hawa anakuwa *private* na mmoja anakuwa *public?* Nasema hivyo kwa sababu ukiangalia hata ule Muswada mwingine na nimemsikia sana Mheshimiwa *AG* akisema; ameeleza *precisely* anasema kwamba kutakuwa na *a chemist of level of senior or above representing a public universities and a chemist of level of senior above representing private universities.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni kwa nini kwenye hii tusione kabisa kwamba kuna utenganisho kati ya *private* na *public?* Kwa sababu lengo hapa ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na hiyo *well balanced*. Ukisema kuwa ataamua, kwa nini isiwe hapa ili ikaonekana wazi kwamba *private universities or institution* nazo zimekuwa *represented?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya kutuambia tu two *representative* mimi nadhani si sawasawa, iwekwe wazi wazi ili tujue kabisa kwamba kuna *representation* ya *private universities or institution* na pia kuna *representation* ya *public;* hasa ukizingatia kwamba hii ni maabara kuu ambayo inachukua pia *private laboratories*. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu sana hicho kipengele kiwepo. Mheshimiwa Waziri sioni kama kuna tatizo lolote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mapendekezo ya Serikali yanatoa fursa kwa vyombo vya aina mbili tofauti kwa hii nyongeza ambayo tumeileta kwenye *further schedule of amendments* na sisi tunapendekeza wawepo wajumbe wawili ambao watawakilisha taasisi za elimu ya juu yaani *higher learning institutions* ama *research institutions.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuweka hivi wawili hawa maana yake ni kwamba mamlaka ya uteuzi wakati inateua itaangalia *balance*, *either* atoke kwenye taasisi ya elimu ya juu ama atoke kwenye taasisi za utafiti; ama atoke

katika zile taasisi za elimu ya juu kwenye taasisi za Serikali ama kwenye taasisi ambazo zinamilikiwa na watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha msingi hapa ambacho tusikichanganye, hatutengenezi chombo ambacho kina uwakilishi wa watu, tunatengeneza chombo ambacho kitaenda kufanya maamuzi kwa kutumia hekima na busara. Kwa maana hiyo watakaoingia mle watakuwa wajumbe wa chombo hicho, si wawakilishi wa taasisi ambazo wanatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo tutakachokiangalia sana atakayekuwa anateua atapaswa kuangalia *quality* ya watu ambao anawaweka kwenye chombo chenyewe kuliko kuangalia uwakilishi wao, kwamba lazima tu awe mwakilishi wa *private sector* ama lazima awe tu mwakilishi wa *research institution* ama tu lazima awe mwakilishi wa *higher learning institution*, ataangalia *quality* ya mtu ambaye anamteua kwenda kwenye kile chombo kutokana na mahitaji ya wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ni vyema mapendekezo ya Serikali kama yalivyoletwa na Mheshimiwa yakabaki kama yalivyo kwa sababu hatutoi uwakilishi wa *private sector* kwenye chombo hiki ama *public sector* kwenye chombo hiki, hapana tunataka wateuliwe watu ambao ni wataalam wabobezi kwenye *either* elimu ya juu ama kwenye utafiti. Inaweza ikawa ni chombo cha utafiti cha *private* ama *NGO* kikatoa mwakilishi akaja kwenye chombo hiki cha kufanya maamuzi. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba wataangalia *quality,* lakini watambue nchi hii sasa hivi ina vyuo vikuu vingi sana vya *private* na hata hizo *institute* na sisi hatusemi kwamba, atateua mtu kwa sababu ya kule alipotokea, hapana. Tunazungumzia dhana pana ya hiki chombo, kwamba, inawezekana kabisa hata wenye *qualities* wakatoka zaidi kwenye vyuo binafsi kuliko hata vya Serikali. Hoja hapa ni kwa nini Serikali inaona kigugumizi cha kuweka kwamba mmoja atatoka *private* na mmoja atatoka kwenye *public,* hasa tukitambua kwamba hawa watu mpaka wamefikia kwenye hiyo *level* ni watu wenye *qualifications* zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi bado nasisitiza ni muhimu sana kwa sababu tunaona kabisa wengine wote tayari wamekuwa ni wa *public* kwa nini huyu mmoja tu kusemwa hadharani kwamba anatoka *private* inakuwa tatizo? Kwa hiyo, nasimamia hoja yangu na naomba hoja hii ijadiliwe ili tuweze kuhakikisha kwamba *private sector* nayo inathaminiwa kwa sababu tuna msemo wa kusema *PPP,* kwa hiyo nadhani *PPP* ionekane vilevile kwenye hii Bodi ambayo ni muhimu sana katika uhai wa Watanzania. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu Suzan Lyimo, akitazama kwenye Muswada ilikuwa inasema *a representative from public higher learning institution or research institution*. Nime-*accommodate* maoni yake na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, nimefuta neno *public*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mamlaka ya uteuzi itapima inapotaka kuteua wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Maabara, anaweza akiamua; maana nikisema mmoja atoke *private* mwingine atoke *public* Waziri anaweza akasema nawachukua wote *from private,* Waziri habanwi. Kwa hiyo, bado nimesha-*take into consideration* maoni ya Mheshimiwa Suzan Lyimo na Mheshimiwa Mwita tumesema *two representatives*, tumeondoa neno *public*. Hivyo, bado unamwachia Waziri afanye maamuzi. Anaweza akaona ninaye mtu wa kutoka Serikalini, Polisi, Mambo ya Ndani, Wizara ya Fedha; hawa wawili nawatoa kwenye *private sector.* Naomba dada yangu Suzan akubaliane na mawasilisho yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba yapite kama yalivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Suzan Lyimo ameomba hoja yake ijadiliwe, lakini ngoja niwakumbushe tu kidogo kwamba tuna Miswada miwili na tutatakiwa kutengua kanuni hapo baadaye tu kidogo, na wote tunauona muda. Nataka tu tusifike mahali ambapo huko nyuma maamuzi yalishawahi kubaki humu ndani na Wabunge wachache, tusifike huko. Kwa sababu hiyo, naomba pengine tukubaliane kwamba mtoa hoja ataruhusiwa kuongea zile mara zake zote ambazo kanuni zinamruhusu, lakini pale ambapo Mbunge mwingine angependa kuchangia nadhani hilo kwa leo itakuwa ngumu kidogo kwa sababu ya muda tulionao. Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba tupo nyuma ya muda, lakini niseme tu kwamba hoja ya wengine kuchangia ilikuwa ya msingi sana, lakini bado nasisitiza kwamba Mheshimiwa Waziri anasema inawezekana akawachagua wote *private, well and good* anaweza akawachagua wote *public*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi ni kwa nini Serikali inakataa kuainisha kwamba wataweka mtu mmoja wa *private* na mmoja wa *public* hasa ukizingatia kwamba hawa wengine wote ni wa *public*? Yaani hiyo ndiyo hoja yangu ya msingi, ni kwa nini? Wakati tumeona hata huu Muswada mwingine tunaoenda kuufuata uko hivyo hivyo ume-*specify,* mmoja atatoka kwenye *private*, mmoja atatoka kwenye *public*. Hili tatizo linatoka wapi? Wakati hawa watu wote kama ni suala la *qualifications* mpaka mtu anafika *higher*

*learning institution* ni watu ambao wamebobea kwenye masuala haya, ni watu wamebobea kwenye *research.* Sasa sijajua tatizo ni kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado kwa kweli hoja yangu naona ni *valid* kwamba ni lazima tuzingatie suala zima la *private public partnership* ambao ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yetu. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Suzan Lyimo.

*(Hoja ilitolewa ili iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nimeleta *amendments* katika kifungu cha 7(3) ambapo nimeomba kwamba kiingizwe kifungu maalum ambacho kitawajumlisha wanawake na watu wenye ulemavu, kwa sababu tukiangalia kwa ujumla, pamoja maoni mazuri yametolewa na wajumbe, lakini pia Mheshimiwa Waziri akazungumzia kidogo bado kuna umuhimu wa kuweka hiki kipengele iwe ni sheria kamili ambayo basi itajumlisha na kuona kwamba makundi haya yanazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tunapozungumzia masuala ya watu wenye ulemavu wapo walemavu wenye matatizo ya akili lakini pia wapo walemavu mbalimbali ambao wamekuwa wakipewa mimba na baadhi ya watu na matokeo yake kwamba wanapoambiwa kuhusu suala zima la mimba, wengi wao wamekuwa wakikana na kusema kwamba hawahusiki na hizo mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiwaweka watu wenye ulemavu katika kifungu hiki tukaingiza kwanza wana uzoefu na masuala hayo kwa hiyo wataweza kuwasaidia hata na wenzao kuwashauri kuhakikisha kwamba haki inapatikana kwa kundi hili. Pia katika masuala ya wanawake kwa ujumla, ukiangalia hata ile sheria ya *SOSPA* ambayo ilipitishwa hapa ni wanawake waliweza kuchangia kusaidia kwa kiasi kikubwa na hatimaye ikapitishwa kuwa sheria. Kwa hiyo, tukiingiza hapa masuala ya watu wenye ulemavu na wanawake pia wakajumuishwa ikawa ni sheria Waziri utakuwa ni wajibu wake kuhakikisha kwamba watu hawa wanakuwa *included* tofauti na sasa hivi kwamba hawapo kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kifungu hiki ambacho nimekileta hapa kitakapoingia moja kwa moja kitazingatia na Waziri atakifanyia kazi kuhakikisha kwamba wanawake pamoja na watu wenye ulemavu wanaingizwa katika

sheria hii. Katika sheria hii kifungu hiki namba 7(3) nimeomba iingizwe ibara ndogo ya (4) na baada ya hapo katika ibara hii ndogo ya (4) ndipo tutaweza kuorodhesha zile namba nyingine na nimeomba kifungu hiki kisomeke…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia. Kisomeke *the composition of the Board shall have adequate representation of women and persons with disability.*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Amina Mollel kwa ushauri wake na maoni yake. Kwanza niseme Serikali inatambua na kuthamini ushiriki wa watu wenye ulemavu na kwa kweli eneo ambalo tunalipa kipaumbele. Lakini hapa tunatengeneza chombo cha kitaalam cha wabobezi kwenye masuala ya uchunguzi wa kimaabara katika kemia, katika vinasaba na katika sayansi ya jamii; hatutengenezi *Professional Board.* Ukija ule Muswada wa pili, *Chemist Professionals Act,* pale unaweza ukasema tunatengeneza *Professional Board,* kwa hiyo utataka *representation* ya kila kundi, ya kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba dada yangu Mheshimiwa Amina Mollel, nakubali sehemu ya pili ya mapendekezo yake ya kuhakikisha kunakuwa na uwakilishi wa wanawake katika Bodi hii. Lengo kwakweli ni kutaka kuwa-*encourage* wanawake ambao ni wabobezi katika masuala ya kemia, katika masuala ya sayansi kushiriki katika Bodi. Kwahiyo, kwenye *schedule of amendments* nimesema kwamba *when appointing members of the Board and Technical Comitees under this Act the minister shall take into account gender representation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Amina Mollel naomba akubali hii ya kwanza, hii ya *representation* ya *people with disability* ningeomba tusiiweke kw asababu tuta-*open a Pandora box,* utataka sasa tuwakilishe tena *indigenous people*, utataka tuwakilishe watu. Kwa hiyo, nadhani inatosha na lakini natambua sana mchango na umuhimu wa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ni-*clarify* tu, *clause* 7(4) Bodi inaweza ika-*co-opt*. Kwa hiyo, kama kuna jambo mahususi linahusu watu wenye ulemavu, basi hii itakuwa ni fursa kwa Bodi kumwalika mtu ambaye atakuwa anatoa huo mchango wa kitaalam na ambaye ni mkemia ana ubobezi katika masuala ya sayansi lakini pia ni mtu mwenye ulemavu. Nadhani hii inatosha, dada yangu Amina naomba akubali hii sehemu ya pili ya mapendekezo yake ambayo tumeyakubali.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa dada yangu Ummy, naamini kabisa wapo watu wenye ulemavu wenye *professional* hizo. Kwa hiyo, ni muhimu pia kuhakikisha kwamba tunazingatia haya; katika vyuo vyetu wapo. Nimwambie dada yangu Ummy tu kwamba, kwa kuingizwa mtu ambaye ana taaluma hiyo; na lengo langu ni kuangalia hapa si kama tumuingize kwa upendeleo tu kuhakikisha kwamba wanaingia wale wenye sifa, wapo watu wenye ulemavu ambao wamesoma. Kwa hiyo, kwa kuangalia hivyo bado kutakuwa na uzito na umuhimu wa kuhakikisha kwamba wanakuwa ni wawakilishi wazuri na kuweza pia kuwasaidia hata hawa wengine ambao ni kutoka Serikalini, kuwapa ushauri na kuona ni kwa jinsi gani masuala haya yanaweza kuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba, pamoja na majibu yake mazuri bado naona umuhimu wa kuingiza kipengele hiki kwa kuzingatia taaluma, sijasema kwamba kwa kupewa upendeleo bali kwa kuzingatia taaluma. Wapo watu wenye ulemavu wenye sifa hizo.

**MWENYEKITI:** Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza tena na napenda nimshawishi Mheshimiwa Amina Mollel. Wakati wa mjadala nakumbuka *it wasn't even easy* kuingiza *gender consideration* kwa sababu ilikuwa inaonekana kama tuta-*open a Pandora box*. Lakini kubwa tunaposema *gender consideration,* naamini hapo tu tayari inatosha Mheshimiwa Amina Mollel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wengine naamini kama kuna mtaalam mzuri wa masuala haya na ni mtu mwenye ulemavu, basi naamini kabisa Waziri ambaye atateua ata-*take into consideration representation* ya hawa watu, wala siyo jambo la kuliweka kwenye sheria. Ni jambo ambalo kwa kweli litawezekana hata tukiliacha kama lilivyo. Muhimu tunataka *atleast* kwa sababu tuna wanawake 51 *percent* na wanaume 49 *percent so at least* tuwe na *representation* ya haya makundi makubwa mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ningemwomba Mheshimiwa Amina Mollel akubali mapendekezo yetu kama yalivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel malizia hoja

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwa ajili…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel naomba ukae kidogo, Mheshimiwa Dkt. Elly Macha naona umesimama.

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kuunga mkono hoja ya Amina na namwomba sana Waziri asione suala la *disability* kama *adhoc*. Tumeshaeleza na kama alivyokubali *gender* nafikiri pia asilimia 10 mpaka 15 ya nchi hii ni watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri suala la watu wenye ulemavu si suala dogo, si suala la *adhoc* ni suala kamili kama alivyokubali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel naomba umalizie hoja.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge liamue.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya naona ulisimama tena.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kusema mimi ni muumini katika kusimamia ushiriki wa makundi yote na ni jambo ambalo nimekuwa nikilipa kipaumbele. Sasa nataka kukubali naona dada yangu Amina na Dkt. Elly wote wamesimama na wamesimamia hii hoja, kwahiyo nita-*amend* kwamba the *Minister shall take into account gender representation and persons with disability, so shall take into consideration*. Nakubaliana na wao, nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Adadi Rajab.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ninayoyaomba ni kidogo, kwenye *clause* ya 7(2)(a). Sasa hivi Jeshi la Polisi lina wataalam mbalimbali. Hapa ilipoandikwa kwamba patakuwepo na mwakilishi kutoka Jeshi la Polisi ina maana kwamba kuna wataalam wa kemikali, kuna wataalam wa *DNA,* kemikali ile *toxicology* na kila kitu na kuna vyombo maalum kabisa vya kisasa kwenye hiyo *Police Forensic Unit.* Sasa hapa waliposema kwamba huyu *representative* awe kutokea kwenye cheo cha Inspekta *or above* nataka *para* hii iwe *deleted* na tuwape uhuru hawa Jeshi la Polisi waweze kuangalia ni mtaalam gani ambaye wanaweza kumpeleka kwenye Bodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hao wote siyo askari pia kuna askari ambao ni wataalam na raia ambao ni wataalam ambao wanasaidia hiyo *forensic unit* iliyopo pale Polisi. Kwa hiyo marekebisho ambayo niliyaomba ni kama ambavyo ina-*appear* kwenye 7(2) kwenye *schedule* yangu (a), kwamba isomeke *a representative from Tanzania Police Force,* nafikiri Mheshimiwa Waziri atakubaliana na pendekezo hilo ambalo ni dogo tu. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tunashukuru kwa mapendekezo haya ya Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, lakini lengo la Serikali kupendekeza awe ni afisa wa Jeshi la Polisi wa cheo cha Inspekta ama juu tuliangalia zaidi *seniority,* sasa kama mtaalam wa mambo ya polisi anapendekeza hivi, sisi hatuoni kama inatuumiza chochote, kwa hiyo tunakubaliana na mapendekezo yake. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki cha 7(2)(b), kwa sababu hii Bodi ina-*comprise discipline* mbalimbali na masuala haya ni ya kiutaalam, maoni yangu ni kwamba, mwakilishi anayetoka kwenye Wizara ya Afya awe na elimu ya mambo ya kemia na uzoefu usiopungua miaka mitatu, hayo ndiyo marekebisho yangu. Kwa sababu tayari tuna watu wa *professional* na huyu wa Wizarani naye awe mtu wa *professional,* kwa hiyo hayo ndiyo maneno yangu, inakuwa ni vema, ni jambo jepesi tu kwa Serikali kulichukua.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana sana na kaka yangu, Mheshimiwa Richard Mbogo lakini kuibadilisha au kuiweka hapa kwenye sheria hatudhani kwamba ni jambo zuri kwa sababu huyu ni mwakilishi wa Waziri wa Afya, Waziri ana sera zake anatazama maslahi yake kutokana na mazingira na muda na *context* iliyokuwepo. Kwa hiyo tukisema lazima huyu mwakilishi wa Waziri wa Afya awe ni mbobezi katika masuala ya kemia inaweza kukatokea masuala mengine yasiwe ni ya kemia, labda iwe na *associated field* lakini *otherwise* sisi bado tungependekeza ibaki kuwa ni mwakilishi wa Waziri wa Afya. Kuna mambo mengine tu ya kisera, huhitaji kuwa mtaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikapeleka pale mtaalam wa *procurement,* labda kwa sababu *procurement* nyingi zinafanyika, au naweza kupeleka mtaalam wa fedha kwa sababu ya fedha ambazo azi-*appropriate* hapa kwenye *parliament.* Kwa hiyo, bado ningemshauri mtani wangu, Mheshimiwa Mbogo akubali kibaki kama kilivyo. Nikienda kutengeneza kanuni basi nitazingatia hiyo hoja au ushauri ambao ameutoa kwamba lazima tuwe *specific,* kwamba huyo mwakilishi wa Waziri awe na sifa gani, lakini kwa mujibu wa sheria ningemwomba kaka Mheshimiwa Mbogo akubali libaki kama lilivyo.

**NAIBU SPIKA:** Labda Mheshimiwa Mbogo pia ungeweza kujifunza kwa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab kwamba *Police Force* walikuwa wametajiwa hapa, ni mtu wa aina gani, kwa hiyo labda ni katika tu kuona kwamba wao wenyewe waamue mtu wa kumleta. Ili kifungu hiki kisiwe na upande mmoja tumekubali kwamba *Police Force* walete yote halafu Wizara tunataka kuweka maelezo marefu sijui wewe uonavyo lakini, ni ushauri.

Mheshimiwa Richard Mbogo!

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri ila nimkumbushe tu kwamba hii Bodi ime-*comprise* mtu wa kutoka fedha kwa hiyo atachangia masuala ya kiutaalam, kuna mtu wa kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali atachangia masuala ya kisheria, kuna mtu wa kutoka utumishi atachangia hayo masuala. Sasa kuna watu wa kutoka kwenye taasisi hizi za vyuo vikuu ambapo umekubali kwamba watakuwa wawili waliosomea haya mambo na imeoneshwa hapo kama mambo manne, sasa kama unaji-*commit* kwamba kwenye kanuni utakuwa *specific, I agree* kwamba uwe *specific* kwamba ni mtaalam wa hayo mambo na huo uzoefu. Hilo nalikubali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbogo. Waheshimiwa Wabunge, kuna mapendekezo kwenye kifungu hiki kabla sijawahoji, kuna mapendekezo ya Serikali na mengine ya Waheshimiwa Wabunge ambao ni wengi sana hapa ambayo yamekubaliwa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho kulikuwa kuna mapendekezo yangu mengine, bado…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo, nimeshahoji, na ni hivi jamani Waheshimiwa Wabunge nimetoka kukumbusha, kifungu tukishakifikia unaposimama kusema ni lazima useme yote kwa sababu usipofanya hivyo ndiyo kama hivi, tunajikuta kwamba tukidhani tumemaliza tukishakutaja wewe ndiyo maana tunaenda kwa mtu mwingine, kwa kujua kwamba wewe unakuwa umeshamaliza ya kwako. Kwa hiyo ni hilo tu la kukumbusha lakini kifungu kimeshahojiwa Mheshimiwa Susan Lyimo.

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko )*

Ibara ya 10

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihitaji kwenye hiki kifungu 10(1), *by deleting the word public servant and substituting with qualified Tanzanian which appears between the words amongst and who.* Nilichokuwa nafikiri kwenye hilo ni kuondoa ile ya kumfanya yeyote anayefanya uteuzi kulazimisha kwamba awe ni mtu kutoka kwenye *public servants* lakini impe wigo mpana akiona mtu nje ya *public system* anaweza akamchagua kama ana uwezo mzuri wa kufanya kazi husika.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Bado tunaendelea kusimamia mapendekezo yetu kwamba kifungu hiki kibaki kama tulivyopendekeza kwa sababu taasisi ya Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni mamlaka nyeti ya Kiserikali na tuliona kwamba ni vema ikabaki na unyeti wake kwa kuhakikisha watumishi wa umma ambao wana uzoefu wa kutosha kwenye utamaduni wa kuendesha mambo mbalimbali nyeti ya Serikali wakaendelea kushika hatamu za uongozi wa taasisi hii.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimsaidie Naibu Waziri awe anatumia maneno mazuri kidogo kama anavyotumia Waziri wake, kwa sababu suala la kusema bado tunasimamia sidhani kama ni sahihi. Nafikiri kwamba suala ni kwamba hata nje ya Serikali kuna watu wazuri na wanaoaminika, yaani naamini nchi hii hata leo Rais Mheshimiwa Magufuli anao watu nje ya *system* anaowaamini hata kuliko wale tulionao ndani ya Serikali, kwenye *public service,* kwa sababu naamini *system* ya nchi hii hai-*operate* tu peke yake kwenye *system* ambazo ziko ndani ya *public,* tunao watu vilevile nje ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukisema kwa umuhimu wa hii ni lazima wawepo watu, labda useme unataka kuwapa *advantage* waliopo Serikalini, lakini kwa Rais, kwa Waziri wa Afya watu wote walioko *public* na walioko *private* ni watu muhimu kwa Waziri wa Afya. Ndiyo maana haya kama unazungumzia suala la afya katika nchi hii asilimia kubwa inachangiwa na mashirika ambayo sio ya Kiserikali. Kwa hiyo, tusiweke neno hilo na nimwombe Waziri mara nyingi hebu aangalie anatumia maneno gani ili twende vizuri, aongee kama anavyoongea Waziri wake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie maneno aliyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, bado tunasimamia kwenye hoja yetu kama ilivyo. Tunataka Mkemia Mkuu wa Serikali atoke kwenye utumishi wa Umma. Haifuti ukweli kuwa *implementation* ya *Health Policy* (Sera ya Afya) kuna *PPP* tunakubali lakini katika *context* hii

hapa ya Mkemia Mkuu wa Serikali na unyeti wa majukumu yake tunasimamia kwenye msimamo wetu atoke ndani ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natafakari kutafuta huo umuhimu maana najaribu kuupata unanitoka. Hebu Mheshimiwa Waziri anifafanulie ana maana gani anaposema umuhimu ili tuweze kuelewana kwa sababu hapa hatubishani, tunajaribu kutafuta namna gani tunaweza tukatengeneza kitu ambacho *really* kitakuwa cha Watanzania na kikaaminika na Watanzania wote, anaposema umuhimu hebu anifafanulie. Kwa sababu, naendelea kutafakari hebu anifafanulie ile maana yake ya umuhimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, tulikubaliana kwa ajili ya muda inabidi mwenye hoja tu amalize halafu tuhoji Bunge, kwa sababu sasa ni saa 1.30 na tuko na Muswada wa kwanza.

Waheshimiwa, mimi hata saa 10.00 nafika lakini naangalia watu wengine hapa. Kwa hiyo na kwa sababu tulishakubaliana hivyo naomba tusivunje kwa sababu kuna wengine ambao niliwakatalia kwa sababu hiyo, wale niliowakalisha ili wasijisikie wao wameonewa inabidi ule msimamo tuliokubaliana mwanzo uendelee. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye hiki kifungu cha 10(1)(a) neno langu ni dogo tu, hapo anaposema:

10.-(1)(a) *at least a masters degree in chemistry or any other associated discipline; and*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hoja yangu hapa ni kwamba hili neno lenyewe tu, kwamba huyu anatakiwa awe ni mkemia, *be a Chief Government Chemist, who is a chemist?* Hiyo yenyewe ukipata maana yake, maana yake huyu mtu anatakiwa awe anajua *chemistry.* Kwa hiyo, nikapendekeza hapa hili neno la *chemistry and any other associated discipline* liwepo kwamba huyu mtu awe tayari amesoma *chemistry.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukiruhusu kama ilivyo maana yake anaweza akawa amesoma *chemistry* au masomo mengine ambayo yanafanana na hayo. Lakini kama unazungumzia *Government Chief Chemist* lazima awe ni mtu ambaye amesoma *chemistry,* ndiyo pendekezo dogo tu kwamba hilo neno liongezwe *and,* basi mengine yote yabaki kama yalivyo,

ndiyo pendekezo langu, kwa maana ya *qualify* hilo jina la *chemist* kama ni Mkemia Mkuu wa Serikali, kama itamaanisha kwamba ni mtu mwingine basi inaweza ikawa tofauti, ndiyo pendekezo langu.

**MWENYEKITI:** Serikali nadhani imempata, badala ya neno *or* linalo-*appear* hapo kwenye (a) anataka liwe *and.* Nani anasimama, sioni. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yetu kama ambavyo yanasomeka kwenye Muswada kwa sasa, tunaomba yabaki kama yalivyo, kwa sababu tunaona kwamba ni lazima awe mtaalam wa kemia ama *discipline* mbalimbali ambazo ziko *associated* na kemia na kazi zinazofanywa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, si lazima awe na vyote. Kwa hiyo, hatuwezi kutumia neno *and,* tunatumia neno *or* ili kutoa fursa kwa wataalam wengine ambao wamebobea pengine kwenye vinasaba ama wamebobea kwenye sayansi jinai waweze kupata fursa ya kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kitendo chako cha kuamua kwamba ajadili mtu peke yake maana yake umeamua, hawa watu wameanza, hata majibu ya Serikali yameanza kubadilika sasa hivi baada ya wewe ku-*rule out* na kwa kweli hukutuhoji kama tukubali au tusikubali, hii sio sawasawa. Kwa sababu maana yake hili ni Bunge, ukisema ni muda, hii ni sheria ambayo tunatunga kwa miaka mingi ijayo na Wabunge hawajasema kwamba wanataka uwahishe ili waende wapi, hii ni kazi ambayo imetuleta hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba, kwa sababu majibu ya Serikali yalivyo, kwa mfano katika lugha ya kawaida tu kule nyuma mmependekeza kwamba anaweza akateua watu wawili ambaye ama ni mtu ambaye ni *biologist* au kitu kingine chochote kile, lakini hapo unazungumza Mkemia wa Serikali, sasa Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri mtaalam anitafsirie, unaposema *chemist,* hiyo ni lugha ya Kiingereza ya kawaida ya sayansi, maana yake ni nini? Kwa sababu ukisema kwamba *or* maana yake ni kwamba huyu anaweza akaitwa ni Mkemia wa Serikali lakini hakusoma *chemistry,* anasoma masomo mengine yoyote yale na nimesema wakati nachangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwanza hukututendea haki, kitendo cha ku-*command* kwamba mmoja achangie, mimi nina mawazo haya, tungependa tusikie watu wengine hapa, basi nipeni mimi nipitishe peke yangu vipengele. Nini maana ya Bunge? Yaani kupiga makofi humu ndani! Wakati wa maoni hapa kuna wataalam wengine wanataka kuchangia hoja, ili sasa isiwe maamuzi ya Waziri, kwa sababu najua ana *majority* watu wanapiga makofi watamuunga mkono, lakini ningetaka Wabunge wengine ambao wana

mawazo tofauti tuchangie *then* Serikali ichukue maoni. Kwa hiyo, bado nasisitiza kwamba hili neno liondolewe vinginevyo wabadilishe jina, isiwe Mkemia Mkuu wa Serikali, hii ni sayansi ya kawaida kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waitara, rafiki yangu, anaongea kwa hisia kweli, lakini labda nimrudishe kwanza nyuma kidogo kwenye kazi zinazofanywa na taasisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ni kazi zipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye kile kifungu kinachoelezea kazi za Mkemia Mkuu wa Serikali utajua kwa nini tunasema anaweza akawa mtu mwenye taaluma ya kemia ama *associated disciplines.* Sasa *by associated disciplines* tunamaanisha *disciplines* zipi? Tunamaanisha anaweza akawemo mtaalam wa baiolojia ambayo ndani yake kuna ubobezi kwenye taaluma ya *DNA,* anaweza akawa mtaalam wa *molecular biology, pathology, toxicology;* zote hizi ni taaluma ambazo zinatumika kwenye ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Kuna uwezekano mkubwa, kwa mfano kwa sasa hivi pale kwenye ofisi ya mkemia mtaalam anayehusika na vinasaba si mtu aliyebobea kwenye kemia peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesomea kemia labda *degree* ya kwanza, *degree* ya pili amesomea mambo yanayohusika na *DNA* ambayo ni *molecular biology.* Sasa huyu ambaye amekaa pale katika kurugenzi inayohusika na mambo ya *DNA* (mambo ya vinasaba) huwezi kusema siku moja hawezi ku-*grow* akawa Mkemia Mkuu wa Serikali wakati amekaa maisha yake yote kwenye ofisi hiyohiyo moja.

Mheshimiwa Mwenyeiti, lakini vilevile mtu anaweza akawa amesoma kemia kwenye *degree* ya kwanza lakini *degree* ya pili akasoma *sub profession* nyingine ambayo inahusika na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo amesoma kemia kwenye *degree* ya kwanza, lakini *degree* ya pili na *degree* ya tatu amebobea kwenye *molecular biology for instance*. Sasa mtu huyu huwezi kusema sasa ni lazima tu awe amesomea kemia tu, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kamati pia mjadala mkubwa uliibuka kwenye suala hili lakini mwisho tulikubaliana baada ya kuamini kwamba kusema hii ni Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali *actually* unaweza ukasema it's a *misnomer* kwa sababu inafanya vitu zaidi ya kemia, inafanya vitu vingine vya *molecular biology, DNA, toxicology,* mambo ya *poison studies* na vitu kama hivyo, yote haya yako chini ya Mkemia Mkuu wa Serikali na wanaweza wakawepo wataalam mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waitara kwa sababu na yeye ni mtaalam wa kemia, nadhani nimefafanua kwa kina, bila shaka

amenielewa, naomba mapendekezo yetu yabaki kama yalivyo kwa sababu yanatoa fursa kwa wataalam wengine waliopo chini ya Mkemia Mkuu wa Serikali hiyo hiyo waweze na wenyewe ku-*grow* kuja kuwa siku moja Mkemia Mkuu wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa muda wetu uliobaki tunalazimika kusitisha kidogo shughuli za Kamati ya Bunge Zima ili Bunge liweze kurejea.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa mujibu wa kanuni ya 153 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kutoa hoja ya kutengua kanuni ya 28(4) ya Kanuni za Bunge inayoelekeza kikao cha Bunge kumalizika saa 1.45 usiku ili shughuli za Bunge ziendelee baada ya muda huu hadi hapo tutakapomaliza shughuli iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono sasa nitawahoji. Kwa hivyo tutaendelea na kazi yetu. Katibu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:** Kamati ya Bunge Zima, majadiliano yanaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Bunge zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Tukae. Mheshimiwa Waitara naomba umalizie hoja yako.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho mimi nitakubaliana na Naibu Waziri ni kipengele kidogo tu kwamba kama ingekuwa inaeleza kwamba huyu amesoma maana yake inasema *atleast a masters degree in chemistry*. Kama alikuwa amesoma *first degree* halafu anaongezea ingekuwa sawa sawa, lakini vile vile mimi hapa nimesoma sayansi siwezi kuwa

Mhasibu. Ukisema Mkaguzi Mkuu wa Serikali lazima atakuwa na elimu hiyo, ndiyo ilikuwa hoja yangu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani niombe Bunge tu liamue ili *record* iandikwe hapo kwa namna ambavyo Mheshimiwa Mwenyekiti unataka na Serikali inataka kwa sasa tangu ulipoamua kwamba tujadili sisi peke yetu, lakini hoja ingeweza kuungwa mkono watu wangeweza kuongeza mawazo mengine na maamuzi yangekuwa na afya zaidi kwa upana wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara unaweza kuungwa mkono saa ya kupiga kura. Waheshimiwa Wabunge nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwenye hiki kifungu cha 10 kutokana na sifa za mwanzo kifungu cha (a) na (b) nikaona niongeze kifungu kidogo cha (c), kwamba, kwa sababu tunapitisha sheria hii ya wataalam wa haya mambo basi na huyu anayeteuliwa na Mheshimiwa Rais awe ni mtu ambaye amesajiliwa katika hilo Baraza la Wataalam. Kwa hiyo, kwa maono yangu hiyo (c) kwamba huyu mtu awe *registered* kwenye hiyo *chemistry profession council.* Kwa hiyo, nafikiri Serikali itaona umuhimu kwa sababu tunahimiza *professionalism.* Hili naomba walichukue.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nishukuru maoni ya Mheshimiwa Mbogo. Ni pendekezo ambalo kwa kweli ningependa kulikubali, lakini tatizo ninaloliona hapa *Chemistry professionals Bill* haijapita, ndiyo changamoto, kwa hiyo *you cannot predict,* labda likija kukataliwa hili la Muswada wa Wanataaluma wa Kemia, ndiyo shida, kwa sababu hii ndiyo itataka kila Mtaalam wa Kemia awe *registered.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hiyo ndiyo changamoto yangu tu. Kwa hiyo Mheshimiwa, tunaipenda yaani nashindwa, Mwanasheria Mkuu labda atatu-*guide,* huu Muswada haujapita, je usipopita na hakutakuwa na *council* ambayo itakuwa ina-*register chemistry professionals* tunafanyaje? Ndiyo hiyo tu, lakini tupo tayari kuikubali hatuna shida.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja aliyokuwa ametoa Mheshimiwa Waitara na maelezo aliyokuwa ametoa hayatokuwa tofauti sana na ya Mheshimiwa Richard Mbogo. Kwa sababu ukikubaliana na hoja ya kwamba hii 10(1) hapa juu iseme lazima huyu mtu awe *a registered chemist* maana yake haya maneno kwenye 10(1)(a) uliposisitiza, *actually* Mheshimiwa Waziri, kwamba iwe *at least a masters degree in chemistry or any other*

*associated discipline* tutarudi pale kwenye ile hoja. Kwa sababu kama unataka haya maneno *any other associated discipline* wakati huku mwanzo umesema lazima awe *registred chemist* utakuwa tayari wewe mwenyewe unaji-*contradict unless* mimi ndiyo sijaelewa. Hebu upande wa Serikali toeni hayo maelezo ili tujue tunasimama wapi.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenye hoja ya Mheshimiwa Mwita Waitara, *clarity* ni kwamba *at least a masters degree*. *What we have in mind* kwamba huyu mtu atakuwa na *first degree in chemistry,* kwa hiyo hilo ndilo la kwanza. Hata hivyo, tunataka sasa ili uweze kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali lazima uwe na *Masters degree* kwenye *chemistry or associated field* na tumesema kwa mfano kuna dada yangu pale ndiyo Mtaalam wa vinasaba, unamnyima yule mama haki ya kuja kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali na amefanya *first degree* kwenye *chemistry* kwa hiyo hilo ndiyo nataka kulisisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, baada ya kueleza kwa hiyo naomba nikatae mapendekezo ya Mheshimiwa Mbogo, ibaki kama ilivyo ili ku-*accommodate* maelezo yetu ya 10(1); kwamba tunazitaka *associated field* ziwepo siyo lazima mtu awe na mambo ya *chemistry* anaweza akawa na masuala ya *Pathology* lakini anaweza akawa kwenye masuala ya vinasaba na vingine.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti wakati Naibu Waziri anaelezea kwamba wanaosajiliwa siyo wote tu ambao wamesomea *chemistry,* wapo ambao wamesomea pia masomo mengine, nilifikiri linaenda sambamba na kwamba wataokwenda kusajiliwa kama wataalam wa kemia, siyo wote ambao *hundred percent* wamesomea Kemia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu sisi ndiyo watunga sheria *anyway next year* tutaileta baada ya kupitisha hiyo sheria nyingine ya *professionals*, tuendelee.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Richard Mbogo. Waheshimiwa Wabunge haya ndiyo tuliyokuwa nayo kwenye kifungu cha 10.
Ibara ya 10

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Mbogo naomba tuwe tunaitikia kwa sababu Taarifa Rasmi za Bunge ni lazima zijue watu walikubali ama walikataa. Sasa kama hatuitiki tena wakati tumekubaliana kukesha hapa inakuwa siyo sawasawa. Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti kifungu cha 13(1) nimependekeza kwenye kushauriwa Waziri iondolewe na kushauriwa na Mkemia Mkuu iwekwe kushauriwa na Bodi ili iweze kufanana na kifungu kinachofuata cha 14 kwa sababu tutakuwa tunairuka Bodi ambayo inapaswa ijue kila kitu ambacho kinafanyika. Kwa hiyo, nafikiri Serikali itakuwa ime-*adopt* hii, naomba kuwasilisha.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyoona kwenye *further schedule of amendment* ya Serikali. Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Mbogo. Kwa hiyo sasa Waziri atakuwa anashauriwa na Bodi badala ya kushauriwa na Mkemia Mkuu wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo mapendekezo yako yameafikiwa, nadhani na wewe umeyasikia wakiyasema.

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika kifungu hicho cha 15(3)(c) kati ya maneno *members* na *to* nataka maneno *fails to* yaondolewe. Ni pendekezo langu kwa Mheshimiwa Waziri ambaye ameleta *draft* nzuri. Pendekezo hili linalenga kwamba tumeshasema *fails to or refuses,* sasa kama mtu ameshindwa maana yake hapa Mwanasheria pia anaweza

kutusaidia kutuongoza, kwa sababu kuna kushindwa kutoa kitu kwa sababu huna uwezo wa kukitoa lakini kuna kukataa. Kwa hiyo, nikafikiria kwamba sheria ikazanie mtu anayekataa; anakataa ku-*cooperate* na sheria, lakini sasa mtu ameshindwa labda kitu hakipo, ndiyo maana yangu, ni suala la msingi la kisheria kwa hiyo la sivyo naomba niunge mkono juhudi zozote zinazoendelea hapa, naomba kuwasilisha.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno yana maana mbili tofauti. Ile ya kwanza ni ile mtu anashindwa tu kutekeleza wajibu wake lakini ile ya pili anakataa kwa makusudi kabisa. Kwa hiyo, haya yana maana mbili tofauti, kwa hiyo napendekeza haya jinsi yalivyo kwenye Muswada yabaki.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kama hivyo ndivyo ilivyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali nadhani ataona kwamba kama mtu ame-*fails to* basi iwe *qualified* kama anavyo-*qualify* katika sheria hii hii na maeneo mengine. Kwamba mtu amefanya jitihada lakini ameshindwa sasa hivi ni *blanked failure* bila kujali umeshindwa kwa sababu gani lakini katika aya zinazofuata hapa hili neno linakuwa *complied with.* Kwa hiyo, nafikiri kwamba huo ndio uelewa wangu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Serikali. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi huo ndiyo unabaki hivyo na kwenye makosa haya hawezi kumhukumu bila kujieleza. Kwenye *criminal justice* kuna kitu kinaitwa *Actus Reus* kitendo chenyewe, halafu kuna dhamira, ile *Mens rea,* kwa hiyo kwa namna hii kama huyu mtu amefikishwa mahakamani atajitetea, watajua kwamba huyu alichukua hatua lakini nia yake haikuwa kukataa. Kwa hiyo watamfikiria na hata Polisi wenyewe wanaopeleleza wakifanyakazi yao vizuri akitoa maelezo ya kutosha wanaweza siyo lazima wampeleke kule. Kwa hiyo naomba kushauri kwamba maneno hayo jinsi yalivyo na alichokwishakitolea ufafanuzi ni tofauti na yanaweza kutusaidia katika sheria hii jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni namna tu ya kutoacha *weakness* na unavyoandika sheria hii huiandiki kwa namna ambayo unaacha *loopholes* ndiyo maana sheria inavyoandikwa ina *punctuation mark* nyingi za *conjuctives or, or, or, or* ili kutotoa fursa kwa mtu mwingine kutumia kile kingine ambacho hakipo pale kupata upenyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti ndiyo hivyo, kwa,hiyo, naomba kumshauri Mheshimiwa Profesa Tibaijuka akubaliane na mapendekezo haya ya Serikali jinsi ilivyo kwa sababu hii siyo *strict liability offence.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa profesa Anna Tibaijuka malizia hoja yako.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na elimu aliyotoa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti kifungu cha 15(2)(f); kwenye wakaguzi kuziteketeza zile sampuli baada ya kuwa uchunguzi umefanyika, kinatoa nafasi ya kwamba yeye au kwa kushirikiana na taasisi nyingine ambazo zilikuwa zimeteuliwa ndiyo wanaoweza wakafanya hilo zoezi. Sasa hapa nilichofanya ni kuondoa ule uhuru wa kwamba anaweza akashirikiana, sasa ashirikiane na taasisi nyingine kwenye kuteketeza hizo sampuli baada ya uchunguzi kwa hiyo *the word 'or'* liwe *removed* na *ku-inse*t *'and'*. Kwa hiyo *in person in collaboration with other authorities to be appointed,* kwa hiyo nafikiri ni kitu rahisi tu kama Serikali. Hii ni kwa ajili ya ku-*establish internal control* katika utendaji wa taasisi. Ni kitu rahisi tu kwa Serikali ku-*accommodate*. Nawasilisha.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Hatuoni haja ya kuondoa neno *or* na kuweka neno *and* na hii inapata msingi kutokana na maelezo aliyoyatoa hapa mapema Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwamba tukiweka *'and'* kwa mfano maana yake tunalazimisha lazima awepo yeye mwenyewe huyo *in person* na lazima huyu mwingine, mamlaka nyingine ambayo anapaswa kusaidiana nayo iwepo, hivyo wawepo wote, kwa hiyo, tunaweka *bureaucracy* ambayo haina ulazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunachopendekeza hapa kwenye Muswada kama kilivyo ni kwamba tunasema *either* huyu mtu *in person* na kama kuna haja ya kushirikiana na Mamlaka nyingine yoyote ile, basi atashirikiana nayo, kwa hiyo, neno zuri zaidi hapa linakuwa ni *or* kuliko kusema *'and'* kwa sababu *and* litaleta urasimu kwamba ni lazima awepo yeye mwenyewe huyo mtu ambaye ametajwa *in person* na iwepo hiyo Mamlaka nyingine ambayo anapaswa kushirikiana nayo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo Waziri ananipa wakati mgumu, kwa sababu tumeshuhudia kupitia vyombo vya habari kwamba hilo tendo linafanyika. Kwa mfano; kuna wakati waliwahi kukamata madawa yakaenda kuteketezwa kule Tanga kwenye kiwanda cha *cement* kwenye kile kinu. *In presence* kulikuwa na taasisi mbalimbali ambazo zilikuwa zinashuhudia katika kuangamiza yale madawa. Sasa na hizi kemikali ambazo ndizo sampo za *evidence* kwa nini tumuachie mtu mmoja aweze kuteketeza; kama kuna *coalition* ambayo imeshafanyika yakatoka majibu ambayo siyo

halafu kwenye kuteketeza ni yeye mwenyewe na anafanya yeye mwenyewe bila kuhusisha taasisi nyingine?

Hapa tunachofanya kwa upande wa Serikali tuna-*strengthen internal control* kwenye utendaji. Kwa hiyo, sioni haja ya kuikatalia hii kwa sababu *practically* inafanyika na nyie ni mashahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Sasa nimemwelewa vizuri Mheshimiwa Mbogo na nakubaliana naye, lakini sisi tunapendekeza maneno yote sasa *inperson or* yaondoke ibaki tu ile *in collaboration with any other authority* kama ambavyo pia ipo imeandikwa kwenye *further schedule of amendments* ambayo tumewasilisha mapema.

**MWENYEKITI:** Sasa upande wa Serikali mtusaidie hapa Bunge. Mkiondoa maneno *in person* maana yake hawa *inspectors* ukisoma kuanzia huku mwanzoni mmewaondolea kabisa yaani hawana haja ya kwenda kule wanaweza tu kufanya *in collaboration*. Kwa sababu nilidhani maana ya hii *or* hapa ni kwamba, aidha, mazingira yakiwa yale ambayo wao wameshindwa *then* wanaweza kufanya na hicho chombo kingine kwa kushirikiana nacho lakini sasa mkisema kwamba mnataka kuondoa maneno *in person* halafu muache tu *in collaboration* maana yake mmewaondolea kabisa hawa *inspectors,* ukiisoma kuanzia huku mwanzo kwenye mbili, hebu mtusaidie uelewa ili tujue tunaitungaje hii.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokipendekeza hapa ndicho ambacho pia tumekiwasilisha kwenye *further schedule of amendments;* kama ukiisoma utaiona pale itaeleweka vizuri zaidi. Kimsingi ndicho anachokipendekeza Mheshimiwa Mbogo. Yeye anataka tu tuseme kwamba *in person and,* wawepo wote wote wawili kwa lazima. Sasa sisi tunasema hakuna haja ya yale maneno *in person or,* yale yaondoke ibakie tu *inspector* anaweza akashirikiana na hiyo mamlaka nyingine. Maana ni ile ile lakini tumeweka tu *wording* vizuri kwenye mapendekezo yetu ambayo yapo kwenye *further schedule of amendments;* maana ni ile ile kwamba lazima *collaboration* iwepo asiwe peke yake.

**MWENYEKITI:** Sawa! Waheshimiwa Wabunge ibara hii ina marekebisho ya Mheshimiwa Tibaijuka – aliyaondoa na Mheshimiwa Mbogo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Ibara ya 16

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hicho Kifungu cha 16(4) napendekeza *to delete the word not* kwa maana ya kwamba ukisoma hiki Kifungu kinasema: "*The authority shall not be liable for any change of form or alteration to a sample that may occur during and after analysis.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikia Waziri wakati anajaribu kufanya *briefing* alisema tunarekebisha na alitoa maana yake ambayo ilikuwa ni nzuri, lakini ukisoma kwa haya maneno ya Kiingereza yaliyoko hapa naona kama hai-*correlate* na ile maana aliyomaanisha Waziri, ingekuwa maneno haya yameonesha ile maana aliyomaanisha Waziri wala nisingekuwa na shida, lakini maneno yaliyoko hapa hayaoneshi maana aliyokuwa nayo Waziri na kwa sababu inaweza ikatokea mtu anabeba *sample* alitakwa aweke kwenye *temperature* fulani au kwenye kitu fulani kikaharibika kwa sababu hiyo kwa makosa yake ambayo ni *technical* halafu asiwe *liable* lakini kuna mambo mengi ambayo yanaweza yakatokea. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa mollel. Kwa hiyo nilichofanya tumeleta *amendments* kwenye 16(4) kwamba:-

*16.-(4) The authority shall not be liable for any change of form or alteration to a sample that may occur during or end after analysis.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nikaongeza maneno:-

*if that change does not affect the original nature of chemical composition.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hiyo ndiyo nimependekeza kwa sababu nimesema inaweza ikawa ni mfupa wa mtu mwenye ulemavu wa ngozi lakini itabidi ukatekate. Kwa hiyo, hatuwezi kuurudisha kama ulivyo lakini kwenye *chemical composition* itabaki ni ile ile lakini kwenye ile *substance* inaweza ikabadilika. Kwa hiyo naomba tu, tumei-*take into consideration his concerns.*

Aangalie kwenye *clause H,* nimeweka pale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel anaweza kuwa hana hiyo, lakini msomee ili aipate vizuri ili ajue ya kwake imechukuliwa au hapana, ama umeshapata nakala?

**MHE. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Waziri alivyokuwa anaelezea pale, imekaa vizuri. Tuendelee.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni hiyo hiyo ni 16(4), hilo neno, *not,* lakini kwa maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa amenichanganya kidogo mwishoni anaposema, kama nimemwelewa vizuri anasema *if that change does not affect the original composition.* Sasa nadhani hapa tunapozungumza kwamba hii *sample, form or alteration of any sample that may occur during and after analysis* hivi tunamaanisha *composition* au *result expected.* Maana kuna habari kwamba kama hayo mabadiliko hayataathiri matokeo; maana *the issue* hapa ni *product* ya kila *analysis* ambayo inafanyika, si *physical appearance* ya hiyo *sample,* na mimi ndiyo ilikuwa *target* yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wataweka vizuri maneno haya na hoja yetu ni kwamba, kama maneno hayajawekwa vizuri *in a way* ya kwamba huyu anaweza akawa na sample hii, *wherever specimen,* lakini mabadiliko yoyote yakitokea yasiathiri matokeo, sina shida na hilo. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukaweka sawa, kwa maana ya hiyo *language* tu ili ieleweke vizuri, *otherwise* nitaunga mkono kwamba haitaathiri matokeo ya *analysis.*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELE YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waitara kwa wasiwasi wake, lakini kiukweli wasiwasi wake na hata wasiwasi wa Mheshimiwa Mollel umekuwa *taken care of* na mapendekezo ambayo tumeyaleta kwenye *further schedule of amendment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa maelezo yetu ni kwamba, *sample* kwa mfano ya mfupa imechukuliwa imepelekwa kwenye maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, baada ya kufika pale imebidi zichukuliwe *sections* za ule mfupa ili ziweze kufanyiwa *analysis.* Kwa hiyo, vile vipande ambavyo vitachukuliwa pale ni wazi kwamba vita-*alter physical composition* na *physical structure* ya ule mfupa ambao umefikishwa maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lengo la kifungu hiki ni kuilinda Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali dhidi ya mabadiliko haya ya muundo wa *sample* ambayo imepelekwa kwa ajili ya kufanyiwa *analysis.* Sasa mwanzoni

ilivyokuwa imekaa haikuwa *clear* sana lakini kwa haya mapendekezo tuliyoyaleta sasa tumesema ili mradi tu tusibadilishe *composition* ya ule mfupa, kwamba kama ulikuwa ni mfupa wa mwanadamu sasa usiende ukabadilika baadae ukawa ni unga unga kumbe ni unga unga unaotokana na mti au ni unga unga unaotokana na plastiki ndicho tunachokiongelea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo mtu akitaka ku-*confirm* kwamba hii *original sample* ambayo imepelekwa pale imebadilika kiasi gani aweze kurudi kusema bado ni mfupa na ni mfupa wa binadamu lakini umekatwakatwa na haujabadilika kutoka kuwa unga wa mfupa ama mfupa mwenyewe, umekwenda kuwa kipande cha plastiki ama vipande vidogo vidogo vya plastiki, ndiyo malengo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ni kwamba wakati *sample* ile imepelekwa maabara inafanyiwa uchunguzi na baada ya uchunguzi matokeo yatatoka kwamba ni *sample* ya kitu gani. Sasa kinachobaki kule kinatunzwa, baadaye mtu akiwa ana *dispute* anataka kuthibitisha kama kweli yale matokeo anayoyaona pale yanatokana na *sample* ambayo ilipelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali aweze kurudi ataoneshwa *sample* iliyochukuliwa ni hii hapa, lakini itakuwa imebadilika *form* yake. Sasa pamoja na kubadilika *form* yake anaweza aka-*confirm* kwamba kweli ni ile ile na ndiyo imetoa matokeo haya. Ndilo lengo la hiki kifungu, kuilinda mamlaka dhidi ya watu kudai kwamba tulileta mfupa, kwa nini leo mnatupa pande pande ya vitu ambavyo hatuvielewi, tunataka mfupa wetu. Hayo ndiyo malengo ya kipengele hiki.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tutaelewana tu na Naibu Waziri na wenzake. Ninachozungumzia hapa; sina shida kama unazungumzia *physical change,* kama unazungumzia utakuwa ni mfupa – *fine! Suppose* sasa si mfupa, mabadiliko yapo pale na yanabadili matokeo, *of course chemical change* inaathiri matokeo, *product* ambayo kimsingi ndiyo maana ya maabara hapa, ndiyo maana ya *analysis,* tunapo-*analyse* ili kujua kwamba ni mfupa, inaweza isiwe nanihii sana, *issue* ni kwamba, mfano wa mfupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *suppose* unazungumzia *chemical,* yaani hao watu wamechukua *chemical* hii wamekaa nayo, na unajua *scientifically* kwamba hizi kemikali zinabadilika kutokana na muda mwingi ambayo itachukua pale. Sasa ikibadilika maana yake *product* yake haitakuwa ile ambayo tunategemea sisi na hiyo ndiyo itakayoleta madhara katika *either* upande wa Serikali au mtu ambaye anatuhumiwa, ndiyo hoja yangu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo *language* iwekwe vizuri hapo kwamba, haitaathiri matokeo. Hiyo habari ya mfupa au *whatever* mimi sijui, lakini *issue* ni *product analysis* yake. Nilitegemea nipate *caffeine* kutoka

kwenye *chemical* ile, sasa kama watakaa nayo kwa muda kama alivyosema Mollel, kwamba *temperature* imekuwa ni *low* itabidi nifanyie kwenye *temperature* ambayo ni ya kiwango fulani, ikapunguzwa; sasa kwa uzembe wao halafu wasiwe *liable* sio kweli, maana yake watakuwa wameshaharibu ushahidi sababu tutasema *either* huyu mtu anakula hela au amekula rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano rahisi tu hata kama hu-*analyze*, ile mirungi akienda kuvuna ukamkata nayo ni madawa ya kulevya. Sasa tunataka iende mahali ikafanyiwe *analysis,* madhara ni makubwa kiasi gani. Akikaa nayo hapa akasema sina usafiri, wao wenyewe kule, oh! gari haina mafuta, imeharibika, baadaye hayatakuwa madawa ya kulevya tena, kwa hiyo ina maana itabidi umlipe, umemsumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hoja yangu umeielewa, ni hiyo tu. *Scientifically* matokeo haya yatabadilika au hayatabadilika? Kama hayawezi, kubadilika na yakibadilika kwa uzembe wao watawajibika mimi sina shida. *Whatever language*, hata mkiandika Kikurya mradi sina shida na hiyo, hata kama utaandika Kikurya ilimradi ieleweke hiyo.

**MWENYEKITI:** Hapa mwishoni Mheshimiwa Waitara hata sijajua umeongea lugha gani…*(Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hata kama ataandika Kikurya ilimradi ionekane kwamba haitakuwa na madhara ya kubadilisha *product* yake, sina shida. Lugha yoyote, hata Kikurya kinakubalika lakini ioneshe hivyo.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza sana Mheshimiwa Mwita. *Section 16* inazungumzia *management of samples* hatuzungumzii *analytical reports of findings,* kwa hiyo bado, nadhani tulivyoleta haya mapendekezo ya kusema kwamba hiyo *sample as long as* haitabadilisha *chemical composition* ya hiki kisampuli au kielelezo kilichochukuliwa; mwanzoni kwa kweli ilivyokuwa imependekezwa ni kama Mkemia hawajibiki kwa chochote; lakini tumesikiliza maoni ya Kamati na wadau ndiyo maana tukaja na mapendekezo haya. Kwa hiyo, kaka yangu Mwita nikutoe shaka, hapa hatuzungumzii *result or findings* ya *analysis,* tunazungumzia *management of samples.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposoma kifungu tukisome *in totality,* tusichukue tu *specific,* kamstari kamoja. Bado tungetaka kukibakisha sambamba na marekebisho ambayo tumependekeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara naomba umalizie hoja yako.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tena amenisaidia, yaani hiki kipengele wala sikusoma *specific* nilisoma kwa ukamilifu wake, anasema hapa;

16.-(4) *The authority shall not be liable for any change of the form or alteration to a sample that may occur during and after analysis.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana tumesema hizi ni *chemicals,* kama wanatunza…

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Waitara, hiyo unayosoma ni ile yenye marekebisho au isiyo na marekebisho?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Marekebisho sina, mimi nasoma iliyoko kwenye Sheria.

**MWENYEKITI:** Ahaa! Sasa ipo ambayo imerekebishwa, ngoja Mheshimiwa Waziri aisome ili uweze kuhitimisha hoja yako vizuri. Mheshimiwa Waziri tusaidie kusoma yale mapendekezo.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichosema kwamba ukishasoma *clause 16(4)* tumeongeza mapendekezo kwamba:-

*"if that change does not affect the original nature of chemical composition."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mwita mbona imekaa vizuri tu kaka yangu? Ndicho hiki. Ninyi hamna? Kuna *two schedule of amendments* ambazo tumeweka ya kwanza ile na *further schedule of amendments,* basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara naomba umalizie sasa hoja yako baada ya kusikia marekebisho ama maneno yaliyoongezwa kwenye hicho kifungu. Hizo *amendments* ziko wapi sasa si walikuwa wana….

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *amendment* ambayo ninayo hapa hii *clause* 16 amesema tu kwamba *by deleting the word not, appearing in subclause (4)* hakuna maelezo anayozungumza hapo, hayo maandishi mengine hayapo kwenye hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita haya uliyoyasikia kwa Mheshimiwa Waziri unakubaliana nayo ili tuanzie hapo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Naomba ayasome kwanza niyasikie, naomba ayasome.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, yasome tena ili Mheshimiwa Waitara ahitimishe hoja yake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ibara (h) ya marekebisho ya Serikali, yale ya kwanza si yale ya pili inasema hivi:-

*in clause 16(4) by adding immediately after the word "analysis" appearing at the end of that subclause the phrase, "if that change does not affect the original nature of chemical composition."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya kama yalivyoletwa na Serikali yanajenga hoja ya kumsaidia anachokisema yeye Mheshimiwa Waitara. Mara ya kwanza ilikuwa imefungwa kwamba Mkemia hatakuwa na uwajibikaji wa aina yoyote ile, kama akipelekewa hizi *samples* zikiharibikia huko vyovyote vile hataguswa. Sasa kwa mabadiliko haya ya Serikali, baada ya kushauriana na Kamati imeleta mapendekezo kwamba ah' ah' hataguswa tu kama yale mabadiliko hayataleta *change* lakini sasa kama yakishaleta *change* anawajibika sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hayo mapendekezo ambayo tumeyaleta sasa hapa yanamsaidia Mheshimiwa Waitara alichokuwa anakipigania kwamba kama amepelekewa *specimen* halafu imeharibika kabisa kule sijui na nini, yaani Mkemia Mkuu abaki tu hivi hivi hata kama amekaa nayo muda mrefu? Sasa Serikali imeyafirikia haya, imekubali, kwa hiyo hiki ambacho kimeletwa na Serikali kwenye mapendekezo haya ndicho ambacho Mheshimiwa Mwita Waitara anakipendekeza kuliko kuifunga kabisa maana mara ya kwanza ile ilikuwa imefungwa kabisa. Wakiharibu zile *specimen,* wakifanyia ufisadi vyovyote vile hawawezi kuwajibika, lakini sasa hii inawapelekea wawajibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshauri Mheshimiwa Mwita, baada ya mapendekezo haya ya Serikali akubaliane na Serikali kwa sababu hicho anachokisema ndicho ambacho Serikali imekizingatia kwenye mabadiliko haya. Naomba kushauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara malizia hoja.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Kama maelezo hayo yataandikwa kama anavyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ambavyo amesema Naibu Waziri na Waziri, naunga mkono, kama wataleta kama ilivyo kwamba haitaathiri, naunga mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara nikutoe wasiwasi hata kama haisomeki hivyo, hicho alichosoma ndicho kitakachotokea kwenye hiyo Sheria yenyewe kwa sababu ndiyo makubaliano ambayo Bunge litakuwa limeyakubali sasa hivi saa ya kutengeneza hiki kifungu.

Mheshimiwa Tibaijuka!

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wasiwasi wangu ulikuwa ni kama wa Mheshimiwa hapo mtani wangu Waitara, kwamba hapa palikuwepo na uhuru mwingi, lakini sasa baada ya kuona; maana yake wasiwasi wangu wala si *sample* ingeweza kubadilika lakini pia; wanasema aisifuye mvua imemnyea; inaweza pia ikatokea *sabotage* kitu kikapelekwa kule wale watendaji wakafanya mambo yao ukaenda kubambikiziwa vitu ambavyo wala hukukusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lakini sasa hivi baada ya kuona *amendment* ya Serikali na maelezo ya Mwanasheria Mkuu nimeridhika, maneno yangu mimi si ya kisheria yalikuwa yanataka kuangalia tatizo kusudi sheria iandikwe vizuri. Sasa hivi Mwanasheria Mkuu kwenye hii *revision* waliyoleta hapa Mheshimiwa Waziri na mimi ameniondoa wasiwasi, kwa sababu kama mtu aki-*temper* na ile *sample* basi utakuwa hicho kitu kimekuwa *null and void!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naondoa mapendekezo yangu baada ya kuona *amendment* ya Serikali inajitosheleza.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 17

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimesikia kuna mapendekezo ya Serikali, lakini nina vipande vipande sana, lakini niende kwenye hoja yangu. Hoja yangu ni kwamba, hiki kifungu cha 17(3)(a) kinaonesha kwamba adhabu ambayo inapendekezwa ni kwa mtu wa kawaida. Sasa nimependekeza kwamba ataje na *an officer of the authority* ili ionekane kwamba na yeye hata akifanya makosa hiyo *fine* inamhusu. Hiyo ni (a).

Mheshimiwa Mwenyekiti, (b) anaonesha kwamba huyu mtu anapigwa *fine* lakini baada ya hapo kama ni *company* inakuwaje? Kuna mambo ya leseni yake ya kufanyia biashara, kuna usajili; sasa ukisema tu kwamba atapigwa *fine* ya shilingi 120 anaweza akapiga tu *deal* akagundua kwamba nikicheza *deal* ya *chemical* fulani ni *very expensive* nikapata bilioni moja, nikienda nikapigwa *fine* ya milioni 20 anapiga mahesabu ya cha kwake pembeni, maana yake haitakuwa na maana sana. Kwa hiyo, nikaona kwamba kuna haja ya kuonesha kwamba anaweza akapigwa *fine* lakini pia usajili wake utakuwa shakani na leseni yake ya kufanya kazi hiyo. Hayo ndiyo mapendekezo yangu. Kwa hiyo, nina mapendekezo hapa (a) na (b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, (a) hata mtumishi wa Serikali au mamlaka hiyo husika awajibike. Hii ninayopendekeza kwamba *an offender is an a natural person* iseme *an officer of the authority* naye vile vile ahusike ili iwabane wote wawili kwamba mtu akifanya makosa atawajibika, hata mtumishi wa mamlaka pia akifanya makosa na ikithibitika kwamba amefanya makosa naye pia aweze kuwajibishwa. Isiache upande mmoja kana kwamba iwe *loose*. Naomba niwasilishe.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *An offender is a natural person,* nadhani hili lisimpe shaka sana Mheshimiwa Waitara. *Natural person* ni mtu yeyote yule haimaanishi kwamba ni raia ambaye si mfanyakazi wa taasisi hii. Kama kosa likifanywa pia na mfanyakazi wa taasisi hii ya Mkemia Mkuu wa Serikali naye pia ni *natural person,* naye ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria hii, wala hakuna tofauti yoyote ile. Kwa hivyo haijabagua kama ambavyo anafikiri.

**MWENYEKITI:** (b)?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili Mheshimiwa Waitara anataka kupendekeza adhabu mbili kwa kosa lile lile moja ambalo mtu atakuwa amekutwa nalo na hatia. Kimsingi kwenye kanuni za *natural justice* mtu hawezi kupewa adhabu mbili kwa kufanya kosa lile lile moja. Kwa hivyo, adhabu iliyowekwa hapa ni kwa kosa moja ambalo atakuwa amekutwa nalo na kwa maana hiyo ataadhibiwa kwa kupewa adhabu hii moja. Hatuwezi kuweka adhabu zote mbili kwa wakati mmoja kwa mkupuo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kabla Mheshimiwa Waitara hajasimama nadhani ametumia maneno *or* kunamaanisha kuwa inaweza kuwa ya milioni 20 ama hiki anachokipendekeza yeye. Kwa hiyo hajasema yote mawili. Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza hiyo (b), nianze na hapo, nilimaanisha hivyo, ametaja adhabu moja tu kwamba hii ni kampuni ina shughuli zake na leseni na nini na akaonesha kama anaweza akapewa *fine* na aka-*afford* kwa hiyo nadhani hilo ni muhimu wakalijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, (a) kama anamaanisha kwamba kama maelezo yake yataandikwa ni mtu yeyote anaweza akawajibishwa hamna shida, nilidhani kwamba hao walilenga mtu mwingine wa kawaida tu, kwa hiyo ndio maana nikataka itamke kwamba hata mtumishi anawajibika katika eneo hilo. Kama itaonesha namna hiyo, basi nitakuwa sina shida.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara tofauti ya (a) na (b), (a) inasema *natural person* maana yake ni tofauti na huyu hapa (b) anayesema *board corporate* kwa hiyo ni hicho tu, kwa hiyo *natural person* ni mtu yeyote ila (b) ni kampuni sio mtu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema (a) nilitaka ionekane kwamba mtu yeyote akifanya kosa awe mtumishi au mtu yeyote wa kawaida atawajibishwa. (b) ametoa mapendekezo ya adhabu ya milioni 20 kwa kampuni ambayo itakuwa imethibitika na makosa, kwa hiyo nikasema hili ambalo limeongezeka inawezekana akapewa adhabu nyingine au hiyo *fine*. Nikasema huyu mtu mfanyabiashara na leseni amesajili na vitu vya namna hiyo kama ni *corporate* ndiyo ilikuwa hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, nimekuelewa nilikuwa nakusaidia tu maana ya hayo maneno kwamba *natural person against corporate board*. *Natural person* ni mtu yeyote, *corporate board* hawezi kuwa yeyote ndio lazima iwe kampuni, lakini yale maelezo yako ya mwanzo Mheshimiwa Naibu Waziri atoe maelezo ya ziada.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye (b) tunaona tukubaliane na mapendekezo ya Mheshimiwa Waitara, tuweke hii *or* ili aweze kupata hii adhabu moja ama hii nyingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa lakini mtusaidie upande wa Serikali ili sheria isomeke vizuri, Mheshimiwa Waitara amependekeza *or cancellation of licence and or registration.* Kwa hiyo mtusaidie kama hii sheria inatoa *licence* ama ina-*register,* ili mtu awe ni *registered* kitu kama hicho ili haya maneno yawe yamekaa vizuri kisheria kuliko kuyaweka tu hivi kwamba mmekubali *registration* ama *licence* lazima ni kimojawapo ambacho hii sheria inakitambua. Kwa hiyo, mtatusaidia hiyo kuiweka vizuri lakini maelezo ya Mheshimiwa Waitara mmeshayakubali ahsanteni. Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si natakiwa ni-*windup* hoja au?

**MWENYEKITI:** yakikubaliwa huna haja ya ku-*windup* kwa sababu hatutahoji tena.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** *Okay.*

**MBUNGE FULANI:** Hujatuhoji.

**MWENYEKITI:** Sijahoji kifungu chote kwa sababu Mheshimiwa Tibaijuka hajamaliza wapendwa katika Bunge. Mheshimiwa Tibaijuka ana maneno hapa hapa, kwa hiyo siwezi kuhoji. Mheshimiwa Tibaijuka. *(Makofi)*

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa nina tatizo la msingi hapa au labda kupata maelezo kwa sababu hapa baada ya kupeleka kupata *analysis* ya *Government Chemist* huna ruhusa, kuna katazo hapa kwamba:-

17.-(3) A *person who uses a certificate of analysis issued under this Act for the purposes of advertisment without a written consent from the Chief Government Chemist, commit an offence…"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza utamaduni tulionao sasa hivi tuna-*promote* kujua kwamba hiki kitu kimepitia viwango, ndiyo maana utaona watu wengi wanaandika *TBS.* Sasa huyu mtu Mkemia wa Serikali anaangalia *product* yoyote, *concoction* yoyote, labda kuna Profesa Majimarefu, waganga wa kienyeji wapo wana vitu vyao wanataka sasa viwe *certified,* kwa hiyo mtu anapeleka ile *sample Chemist* anaipitia sasa anatuletea hapa *composition* ndizo hizi. Sasa huyu mtu nilivyofikiria, labda kama kuna kitu naki-miss, hapa anakuja kusema jamani Mkemia Mkuu wa Serikali anasema hapa niko hivi, hivi au sivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *this person is committing an offence? I am lost.* Kwa hiyo naomba aidha nipate ufafanuzi. Hoja yangu Waheshimiwa Wabunge ndio hiyo kwamba hapa kuna tatizo la msingi. Labda kama tukipata maelekezo yakaridhisha kutakuwa hakuna shida lakini nafikiri ndio ukakasi wangu, kwa sababu utamaduni wetu tuna-*encourage certification* ya vitu, sasa kama Mkemia Mkuu wa Serikali hata-*certify* kitu mpaka sasa kuna *bureaucracy* ameshakupimia sasa urudi kutafuta tena *permission* hapo ndio pia na ufisadi unaweza ukaingia. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Mheshimiwa Profesa Mama Tibaijuka anacho-*propose,* najaribu kumpata, kwenye 17(3) *a person who is also required by any other written law uses certificate,* ndivyo anavyotaka Mheshimiwa Mama Tibaijuka. Kama hivyo hatuna shida, kwamba kuna *any other written law and then this person is allowed to use analysis* kwa ajili ya *advertisement without a written consent from the Chief Government Chemist* ndicho anachoshauri. Kama ni hicho hatuna shida nacho, naomba tu labda aki-*clarify* vizuri.

**MWENYEKITI:** Hicho ndicho anachokitaka kiingizwe hapa. Kama unakubaliana na mapendekezo yake na hapa mko na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama yanakaa vizuri semeni mnakubali mapendekezo ya Mheshimiwa, ndiyo anayomaanisha hayo uliyotoa Mheshimiwa Waziri, lakini sasa muwe mmekisoma vizuri hiki kifungu na maneno yanayomalizia huku mwisho muone ni yapi ya kuyafuta.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa Profesa hapa anasema kwamba lisiwe kosa la jinai kwa mtu kutumia *certificate of analysis* bila ruhusa ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Sasa hoja inaweza ikawa nzuri, lakini labda tufikirie namna ya kuiweka vizuri kwa sababu anaweza akawa mtu amepata hiyo *certificate of analysis* kwa madhumuni ya kitu fulani tu, sasa tukiweka iwe *open* huyu mtu anaweza akaanza kuitumia ile *certificate of analysis generally for other purposes.* Kwa hiyo, nadhani kuwa ni hii *written consent* ni muhimu kwa ajili ya kufanya hiyo *control.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge ushauri.

**MHE. ANDREW J.CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijafika kwa upande wa mapendekezo ya Mheshimiwa Profesa Tibaijuka na…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, humu ndani tuko watu wa aina mbalimbali, sasa ni kwamba hatutaki Mheshimiwa Chenge atoe ushauri ama? Hajadili hoja anatoa ushauri ili sheria yetu hii ikae vizuri, ndicho anachokifanya sasa hivi. Mheshimiwa Chenge naomba ukae tuendelee.

Waheshimiwa Wabunge tunasahau tena sisi wenyewe hoja ambazo huwa tunazitoa, lakini ni vizuri kama hivi tulipofikia. Mheshimiwa Tibaijuka Serikali… unataka kutoa maelezo mengine tena Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba nimejaribu kumwelewa mama Tibaijuka lakini nataka kusema *certificate of analysis ya Chief Government Chemist* haitumiki kama ishara ya ku-*regulate* na nilitoa mfano wa *TFDA.* Kwa mfano mtu ame-*import* maziwa labda amekuja na amepeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, Mkemia Mkuu yeye atasema maziwa haya labda yana *substance* fulani ambazo zina sumu, lakini ni jukumu la *TFDA* sasa kwenda kuyapiga marufuku au kuyakataza yasiuzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bado tungeomba mama Tibaijuka tuache kifungu kiwe kama kilivyo kwa sababu Mkemia Mkuu tu anafanya *lab analysis* ya hivyo vitu halafu anapeleka kama ushauri kwenye mamlaka ambazo zinatakiwa ku-*regulate* na si kuanza kutumia cheti, nimeruhusiwa! Hapana wewe utakipeleka kule ambapo unatakiwa kukipeleka ili uweze kujitangaza kama ulivyosema.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hiyo *proposal* yangu pamoja na *trick waters* za sheria; ndiyo maana nasema kama hakuna sheria nyingine maana yake hii kuiacha hivi hivi kidogo naona; *if is not so required by any other written law;* kwa mfano Waziri hapa ameelezea vizuri labda kuna vyombo vingine ambavyo lazima vikupe kibali kama *TBS, TFDA*, lakini cheti hiki cha Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa na *value,* hakiwezi kwenda kikafichwa uvunguni, ikibidi kitumike maana yake *what is the value of it?* Kwa hiyo, nafikiria kwamba hapa hili ni suala la msingi kwa sababu kwanza *proposal* yangu iko *very careful* maana yake nilijua kwamba panaweza pakawepo *other conciliations'* kama anavyosema Waziri Possi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nafikiria kwamba kuchukua hiki cheti na kukiweka uvunguni *then what are we doing here?* Hii ndiyo mantiki yangu na nimekuwa *careful,* kama kuna vitu vingine vya kufanya lazima pia uvifanye kwa sababu sheria zile zitakuwa zinakutaka kwamba uweke *TBS, TFDA et cetera.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumefikia mahali pa kuhoji, lakini nitoe tu maelezo kidogo. Mheshimiwa Tibaijuka mapendekezo yako yangepaswa kufuta maneno ya mbele huku, kwa sababu ukisoma yale ya *is not so required by any other written law* halafu huku mwisho unasema *commits an offence* sasa kama hatakiwi na sheria yeyote sasa ana-*commit* vipi hiyo *offence*?

Waheshimiwa Wabunge, maana yake ni kwamba, huku juu ukishasema yaani hajatakiwa na sheria yoyote maana yake hafanyi kosa. Sasa ukimwekea kosa huku wakati hakuna sheria inayomtaka, unakuwa unamwonea tena. Lakini Waheshimiwa Wabunge mapendekezo ya Mheshimiwa Tibaijuka nadhani wote

tunayo, kwa hiyo, tumefika sehemu ya kuhoji. Ndiyo tunataka kuamua sasa hivi. Mapendekezo ya Mheshimiwa Tibaijuka kwenye kifungu namba 17(3).

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima zote, tunatunga sheria ya nchi kwa upande wa mapendekezo mazuri ya Mheshimiwa Waitara nauliza *cancellation* ya leseni ipi *are we talking about business licence?* Kama ni *business licence* sheria lazima iseme *and or registration.* Kama ni kampuni huwezi ukaifuta kampuni kwa sheria hii, ndiyo maana napata matatizo sana na mapendekezo ya kutunga sheria kwa utaratibu huu, lazima tujielekeze *specifically* katika kile tunachotaka. Kama tunataka *business licence* ya huyu *body corporate* tuseme ni *business licence,* lakini mjue pia sheria ya *business licence* ina utaratibu wa jinsi unavyoweza ukamfutia. Ndiyo maana mapendekezo ya Serikali yalikuwa yanalenga kutoa adhabu *monetary,* haikutaka kufika kwenye maeneo mengine. Sasa kwa nia njema ya mapendekezo ya Mheshimiwa Waitara tunataka sasa tuguse na sheria nyingine na ndiyo inayonisumbua sana mimi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Halima Mdee uzuri wake wewe ni Mwanasheria na unajua namna itakavyokuwa ngumu kutekeleza sheria ambayo tutakuwa tunaiandika isivyo sawasawa. Mheshimiwa Waziri naomba ukae.

Mtakumbuka mimi mwenyewe niliikumbusha hapa Serikali kwamba mapendekezo ya Mheshimiwa Waitara mnapokubaliana nayo lazima mwangalie sheria hii inaongelea *licence* ama inaongelea *registration* ya kitu gani unachotaka wewe kufanya *cancellation.* Sasa ukisema utafika mahali una-*cancel* tu hauwezi ku-*cancel,* ni lazima u-*cancel* kitu ambacho kinaanzishwa na hii sheria ndipo utaweza, lakini huwezi kuwa una-*cancel* kitu kingine. Ndiyo maana niliikumbusha hapa Serikali, mnapokubaliana na mapendekezo haya mwangalie sheria hii inaongelea *licence* au inaongelea *registration* ambayo sheria hii itaweza kufanya hivyo?

Sasa mapendekezo ya Mheshimiwa Waitara ya kifungu cha 17(3) (b) ya kuongeza maneno ama kuongeza adhabu nyingine kwamba iwe ni milioni 20 sawa, lakini yaongezeke na haya mengine. Sasa mtusaidie Serikali tufanye maamuzi hapa. Sijahoji bado nilikuwa nataja, Waheshimiwa Wabunge tuko wote humu ndani na tunashindwa kuelewana, sijahoji, nimetaja kifungu nikaanza kumtaja Mheshimiwa Waitara sikufikia mahali pa kuuliza wanaosema ndiyo au hapana na hiyo ndiyo namna yetu ya kikanuni ya kuhoji mbona wenyewe tena tunapigana vichwa? Hatuna sababu ya kufanya hivyo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpe nafasi Mheshimiwa Halima Mdee naye achangie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa vile tu hurudi kwetu kwa hiyo hatukufunga hiyo hoja ya Mheshimiwa Waitara. Kimsingi sisi tulikuwa tunakubaliana na mapendekezo kwa maana ya kwamba *cancellation* iwe ni ya *permit* ambayo inatolewa kwa mujibu wa sheria hii. Si *cancellation* ya certificate ama leseni nyingine yoyote ambayo inatolewa na sheria nyingine. Ni kwa mujibu wa sheria hii ambayo inakuwa *regulated* na sheria hii kwa sababu Mkemia Mkuu wa Serikali atakapokuwa ana-*regulate* hizi maabara nyingine zinazo-*deal* na *chemicals* maana yake atakuwa anazipa kibali chake kwamba zinaweza zika-*handle chemicals,* kwa namna ambavyo kitakuwa kinatolewa, kama ambavyo tutaweka kwenye kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama amekosa chini ya sheria hii na akahukumiwa chini ya kifungu maana yake anaweza akanyanganywa kile kibali ama akapewa *fine* hiyo ya milioni 20 ama vyote viwili, ndiyo mapendekezo ambayo sisi tunayakubali.

**MWENYEKITI:** Tusaidie ni *cancellation* hapa or *cancellation of?*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *cancellation of a permit or licence which is issued under this law or a fine of not less than 20 milion shillings or both.* Sasa baadaye watakapokuwa wanarekebisha sheria nafikiri wanaweza wakaiweka vizuri zaidi, lakini muktadha ndiyo huo.

**MWENYEKITI:** Nadhani tutakuwa tumeelewana mpaka hapo. Kwa hiyo, ni *permit or licence*. Lakini sasa haya maneno yawepo humu kwenye hii sheria, kwamba huyu *Chief Government Chemist* anatoa *licence* na pia atatoa *permit* kwa sababu kama hayamo halafu tukawa tumetaja *permit* hapa ama *licence then we have problem* kwenye; anatoa nini. Mheshimiwa Waziri kwa hiyo ni *registration,* kwa hiyo *cancellation of registration*, sawa. Kwa hiyo nadhani Mheshimiwa Waitara tutafuta hayo maneno *cancellation of licence and* tutaishia hapo kwenye *cancellation of registration.*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nawahoji.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kifungu hiki hakina marekebisho makubwa, zaidi ni kuweka maneno ili kieleweke vizuri. Nimeleta mabadiliko ya kufanya marekebisho ya *subclause* (2) *by deleting the whole subclause and replace it with the following* nimefanya mapendekezo haya kwa sababu ukisoma hii *Subclause (2)* inasema hivi:-

*27.-(2) The Minister may, within thirty days or allow any appeal alter, or vary the decision of the board and make any order as he deems fit.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukisoma hiki kifungu jinsi kilivyo kinajikanganya. Kwa hiyo, nimependekeza kuboresha, kuwe kuna vifungu vidogo viwili ambavyo vinafanya maboresho na kile cha (3) kitabaki kama kilivyo, isomeke kama ifuatavyo:-

*27.-(2) On receipt of the appeal, the Minister shall within thirty days consider and determine the appeal.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nimependekeza vilevile kiongezwe ki-*Subclause* cha (3) ambacho kinasema:-

*27.-(3) In determining the appeal, the Minister may uphold, quash or vary the decision of the board.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kile kifungu ambacho kilikuwa cha (3) kiwe cha (4). Kwa hiyo, tufanye *just renumbering* kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo dhana ni ileile, sema nimeshusha kwenye mpangilio ambao ilivyo hivi ilikuwa imejichanganyachanganya, hujui kipi ni kipi. Sijabadilisha *concept* nzima, ni hayo tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna *typographical error* hapa pale, *within thirty days or allow* nafikiri hii ndiyo ika-*cause all confusion.* Kwa hiyo, tutasema *the Minister may within 30 days allow any appeal alter or vary any decision of the Board and make any other order.* kwa hiyo, anaweza akakubali, anaweza akabadilisha, anaweza akatoa uamuzi mwingine wowote ambao unaweza ukawa ni kutengua kabisa, labda kuwaambia Bodi ianze upya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukitoa hii *or* mapendekezo ya Mheshimiwa Mdee yanakuwa *taken into consideration* vizuri tu, yapo kwenye *Schedule of Ammendment.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee. Sina uhakika kama umeshapata ile *schedule* ya Serikali, lakini wanasema maneno *or* kwenye hii sheria tuliyonayo yameondolewa. Kama yakiondolewa, je, yanaondoa huo utata?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Abdallah Possi, amesema wakiondoa haya maneno na kwa mujibu wa *amendment* yao ambayo sijaiona, kunakuwa kuna maana ya sawa na kile ambacho nilikuwa nimekimaanisha. Sasa kama hicho ndio kitu sahihi kwa sababu, sijaona *amendment, then* nakubaliana na Serikali sina shida, kama hiyo maana ambayo niliitaka ndivyo itakavyokuwa kwenye *amendment* yao. Sasa kwa kuwa sina, wangenisomea *that amendment* ili tuweze kujua kama tunaenda kwenye kitu kimoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukitoa *or* hapa inasomeka hivi, *the Minister may within thirty days allow any appeal, alter or vary the decision of the board and make any order as he deems fit.*

**MWENYEKITI:** Tusaidie Mheshimiwa Dkt. Possi, baada ya neno *days* kuna koma pale au hakuna?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU – WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hapa ni suala la uandishi. *The Minister may within thirty days allow,* nafikiri kuna hiyo koma hapa *then allow any appeal,* koma, *alter or vary the decision! Yes,* kwa hiyo, *after thirty days there should be a coma.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, kwa sababu, hapa isipokuwepo koma, halafu ukawa umeondoa hayo maneno *or,* inaweza ikaleta tabu, lakini nadhani umesomewa kwa hiyo, maana yake, *within thirty days, allow any… then* inaendelea. Umekubaliana nayo Mheshimiwa Halima?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unavyosema Waziri ndani ya siku 30 ataruhusu rufaa, *what does!* Yaani kuna kitu hakijakaa sawa hapa kwa sababu, najaribu kupata maana ya neno wanalolitumia wao naona kama halileti maana ya moja kwa moja.

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Halima.

Waheshimiwa upande wa Serikali kwa sababu, ukiweka *the Minister may, within 30 days, allow any* Maana yake unaweza haya maneno ya kwenye *within 30 days* ukayaacha kidogo ukapitiliza kule mbele. Sasa itasomeka hivi, *the Minister may allow any appeal, alter or vary the decision of the Board and make any other order as he deems fit!*

Sasa ni kwamba, tunataka hizo siku thelathini zitumike kwenye kuruhusu hiyo *appeal*, kubadilisha na ku-vary hiyo *decision of the Board.*

Kama ni hivyo, Mheshimiwa Halima ukiweka hii koma baada ya *days, then* hiki kifungu kitakuwa kinasomeka vizuri, kitakuwa kina-*flow* vizuri, ukiweka koma, bila koma kutakuwa na tabu, lakini ukiweka koma kitakuwa kinasomeka vizuri.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *senior citizen* amenyoosha! Si ulimruhusu saa ile, mruhusu na sasa hivi!

**MWENYEKITI:** Nashukuru Mheshimiwa Halima Mdee kwa kutambua *senior citizenship* ya Mheshimiwa Mtemi Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi narejesha *compliments* kwake, kama Mwanasheria. Mheshimiwa Halima Mdee yeye

alikuwa anataka Kifungu Kidogo cha (2) akiandike upya, akifute na akiandike upya. *Attempt* yake ilikuwa ni nzuri, lakini haifikii ya Serikali kwa sababu, ya Serikali ina *concept* ya siyo rufaa tu, anaweza akaruhusu uamuzi wa Bodi, anaweza aka-*alter,* anaweza aka-*vary* yote hayo. Sasa lazima tuyabebe na ndiyo maana pendekezo la kufuta neno *or* na kuweka koma ina *flow* vizuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba msomi mwenzangu, Mwanasheria Msomi, Mheshimiwa Mdee, akubali pendekezo la Serikali twende mbele.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nilikuwa nafanya *conclusion* kwamba, kama Serikali imekubali kuweka *comma, then* kungekuwa kuna ile *flow* nzuri. Nimtoe wasiwasi tu Mheshimiwa Chenge, Kifungu cha (1) na cha (2) kilikuwa kime-*cover* hayo maeneo mawili uliyokuwa ukiyazungumza. Nisisitize kwamba, kama Serikali imekubali kuweka *comma,* sababu mwanzoni walikuwa hawajaiweka, *then* kutakuwa kuna hiyo maana ambayo ilikuwa imejificha. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 28
Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo huu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki nimependekeza mabadiliko kwenye *subclause (3) by deleting words not less than five years, appearing between the word term and years and substituting them with the words not less than one year but not exceeding five years.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivi kwa sababu, lengo hapa sio kujaza watu kwenye magereza na kuwapa *harsh penalty,* ila ni kuweza

kuwabadilisha, lakini vilevile kuwatoza *fine* kwa kadri ambavyo tunadhani ukubwa wa kosa utaruhusu. Kwa hiyo, ndiyo maana sijaleta mabadiliko ya *fine,* kwa sababu najua *fine* itapimwa kutokana na kiwango cha ukubwa wa kosa, lakini nikaona tukisema makosa kama haya yasiwe pungufu ya miaka mitano, tunaweza tukajikuta kwamba, watu wanaumizwa bila sababu. Ndiyo maana nikapendekeza kifungo basi, kiwe kwa kipindi ambacho hakipungui mwaka mmoja, lakini hakizidi miaka mitano ili kutoa fursa kwa Mahakama kucheza hapa katikati kutokana na uzito wa kosa, lakini vilevile kumuadhibu mtu *in terms of monetary* kutokana na ukubwa wa kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimesema hivi kwa sababu, vilevile kwenye sheria nyingine ambazo tumepitisha hapa Bungeni tumesema kwamba, hatutaki kuwajaza watu mahabusu kwa miaka saba, nane au tisa kwa vitu ambavyo wanaweza wakawekwa ndani kwa muda *reasonable,* lakini wakati huohuo wakalipia hasara ambayo wameisababishia Serikali *in terms* of fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali ikubaliane na mimi kwamba, kifungo kisiwe pungufu ya mwaka mmoja, lakini kisizidi miaka mitano; lakini , masuala ya fedha yanaweza yakafanywa kutokana na uzito wa *cases* kwa kadri zitakavyotofautiana. *Given the fact* wametwambia magereza yamejaa, wametwambia tokea uhuru magereza yaliyojengwa sijui ni 20, sasa inakuwa ni shida kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Actually part seven* ya mapendekezo ya hii sheria inasema inahusika na *National Human DNA Data Base*. Kwenda moja kwa moja kwenye Kifungu cha 33(3) tunapendelea mapendekezo yetu kama tulivyoyaleta yabaki kama yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa kuendelea kubaki na mtazamo huo ni kwamba, makosa yatakayohusisha mtu kuiba siri zilizomo kwenye kanzidata ya Serikali ni makosa makubwa sana, si makosa madogo. Kwa maana hiyo, tunalenga kuweka *deterrence* mtu asithubutu hata kuvujisha *(leak)* taarifa ambazo zipo kwenye *database* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, hapa unaongelea *database* hii ikiwa ina kumbukumbu zote za uasili wa watu wote wa nchi yetu. Kwa hivyo, kutakuwa kuna kumbukumbu za watu wahalifu kabisa, wauaji, wahaini, watu wanaohusika na madawa ya kulevya kumbukumbu zao zitakuwemo kwenye *database* hii. Sasa mtu ambaye anaenda kutoa kumbukumbu za mtu pengine ni *terrorist* ni gaidi, anavujisha *(leak)* ama anazipoteza kwenye Kumbukumbu za

Serikali hatuwezi kusema tunaweka *leniency* ya namna yoyote ile. Huu ndiyo msingi wa kuweka adhabu kali kabisa kwenye kifungu hiki.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni hivi; unapokuwa na kiwango cha chini cha adhabu ya kifungo ambayo ni kubwa sana unatengeneza mazingira ambayo hiki kitu kinaweza kikawa *abused,* kwa sababu, hapa kuna adhabu za aina mbili. Kuna adhabu za *fine* ambayo haina kikomo, lakini vilevile kuna adhabu ya kifungo ambayo haina kikomo. Kitu ambacho nimekigusa hapa ni kifungo kisichokuwa na kikomo, lakini adhabu *in terms of monetary* isiwe na kikomo kutokana na uzito wa kosa kwa kadri Mahakama itakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema hivi, kwa sababu hatutaki kutengeneza mazingira ambayo huu uwazi unaweza ukaja kuwa *abused,* tutengeneze kifungo, *yes* kiwepo, lakini kifungo hicho kiwe *based* kwenye namba ambazo ni *reasonable.* Huwezi kuniambia kwamba, unatoa *sentence harsh* hivi, lakini katika sheria hiyohiyo unazungumzia kufifilisha makosa, kwa sababu huku kwenye sheria hii hii kuna kufifilisha makosa. Mtu anaweza akakubaliana akatakiwa alipe kiasi gani cha fedha na asipelekwe Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ndiyo tuko *on that strict,* basi kile kifungu kinachohusiana na kufifilisha makosa kingetolewa kabisa ili tujue kwamba, hii sheria mtu hata kama akifungwa miaka 10, 15, 20, *it is ok!* Ndiyo maana nasema lazima tuwe *reasonable,* tusitunge sheria ambazo zina lengo la kuumiza, kwenye *penalty* tunaweza tukamuumiza kwa kadri ambavyo tunaona inafaa kutokana na uzito. Kwenye kifungo, kwa kuangalia Mahakama zetu na magereza yetu yalivyo, hatuhitaji ku-*encourage* kujaza watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli ukimfunga mtu miaka mitano utakuwa hujampa adhabu ya kutosha? Ukimfunga mtu miaka mitatu utakuwa hujampa adhabu ya kutosha, huku ukimwambia kwamba, unatakiwa ulipe milioni 100, 200 hata bilioni moja kutokana na uzito wa kosa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, dhana ni hiyo na tumefanya hivyo kwenye sheria nyingi tu tena nyeti kuliko hizi ambazo tumezipitisha, tuone hiyo dhamira. Ndiyo maana sikusema kuwe na *limit* ya fedha kwa kutambua kwamba, kuna mazingira mengine yanaweza yakawa ni makubwa sana tuipe Mahakama *room* ya kuweza kumuadabisha huyu mtu hata kama atauza mali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja yangu ni hiyo. Dhamira tu ni njema, tusitunge sheria ambazo kesho na kesho kutwa zitakuja kutudaka na sisi, tusije tukafikiria tunatungia wengine. Tujaribu kuwa *reasonable* kwa kujua kesho

na kesho kutwa unaweza ukaguswa wewe, mtoto wako, mjukuu ama kitukuu, ili kuweza kufanya hivi vitu viweze kutekelezeka na kuweza kubadilisha watu. Ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, pengine kabla hujajibu kuna vifungu vingine ambavyo tumepitisha huku ambavyo hizo fedha ukiziangalia, kiasi cha adhabu na muda wa kifungo vinatofautiana, lakini hiki ndicho kimepewa uzito zaidi. Kwa mfano, 17 inaongelea kwamba mtu ambaye amefanya kosa atapewa adhabu, si pungufu ya milioni tano ama kufungwa kwa si pungufu ya mwaka mmoja ama vyote viwili. Kwa hiyo, hapa tuna milioni tano na tuna mwaka mmoja.

Nimechagua tu vichache, ukienda 28 kinatoa pia adhabu, kinatoa adhabu ya si pungufu ya milioni 10 halafu ama kifungo cha kipindi ambacho hakipungui miaka mitatu ama vyote viwili.

Sasa ukija kwenye hii 33, kwamba, zitakuwa ni milioni 10 halafu kifungo kisichopungua miaka mitano, labda hicho kimevuka sana ukilinganisha na hizi nyingine, kwa sababu katika uandishi wa sheria lazima uangalie mtiririko wa vifungu vingine. Kwa hiyo, tusaidie wakati unajibu ujibu na hii halafu tutarudi kwa Mheshimiwa Mdee, amalizie hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenisaidia kuonesha huku kwingine kidogo adhabu ilikuwa ndogo, huku kubwa. Hapa tunazungumzia kanzidata ya Taifa ya vinasaba vya binadamu, *National Human DNA Database,* kwa hiyo, hili ni jambo kubwa, ndiyo usalama na uhai sijui naweza nikasema wa Watanzania, *information* zetu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, baadaye tunakotaka kwenda hata mtoto akizaliwa leo tunataka taarifa zake ziingie kwenye hii *database*. Kwa hiyo, Taifa linaweza likapukutishwa tu kwa sababu mtu, hivi mpaka unaenda ku-*access database* ya *human DNA* unatafuta kitu gani bila *authorization?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, kuna neno, *without authorization by the Chief Government Chemist.* Kwa hiyo, hapa hakuna nia njema, huyu mtu hana nia njema na Watanzania, hana nia njema na Taifa letu. Kwa hiyo, tumeweka adhabu kubwa kutokana na *sensitivity,* kutokana na unyeti wa hili suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Kamati ilikuja juu ikataka tuongeze, lakini sisi tukasema, tukaangalia kuna Sheria ya Udhibiti wa Vinasaba vya Binadamu, Sura ya 73, imezungumzia kudhibiti. Kwa hiyo, tukasema hatuwezi

kuondoka kwenye sheria ile tukawa na sheria nyingine ambayo kidogo inatoa adhabu kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maoni ya Kamati ilikuwa tuongeze hii adhabu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Halima Mdee bado tuiache Mahakama ipime. Mahakama itapima kutokana na uzito wa hili jambo, huyu anastahili miaka mitano jela au anastahili miaka 10 au 15. Sasa hivi tunawapeleka wabakaji wa watoto *30 years minimum!* Sembuse huyu anayetaka kuingilia kanzidata ya vinasaba vya Taifa! *No! No! this is a very serious offence*. Kwa hiyo, nataka tu kumshawishi Mwanasheria mwenzangu akubali tu ibaki kama ilivyo; maana sanasana tunaweza tukalishawishi Bunge, tukaliomba liongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nadhani kama hoja ni kuweka adhabu kali, lakini ukawa umeacha kiwango kilekile cha fedha ambacho huko nyuma umekiwekea adhabu ndogo, maana yake mtu anashindwa kuiona sasa hiyo tofauti! Kwa sababu, hapa imesema milioni 10 au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote viwili. Sasa ukiongeza tu kwenye ya kufungwa wakati Mahakama itaamua yoyote, hapa kuna milioni…

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *not less than!*

**MWENYEKITI**: Si ndio! Maana yake ni kwamba, anaweza akaweka hiyo 10, lakini miaka wewe umempa mingapi, mitano, ana uwezo huo!

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *not less than!*

**MWENYEKITI:** Ni sawa. Ninachomaanisha hata huku nyuma tumetumia maneno hayo hayo. Kwa hiyo, kama tunaona ni nzito fedha mbona tumeiacha pale? Sawa, Mheshimiwa Halima Mdee malizia hoja yako. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru umenielewa lakini Waziri hataki kunielewa, sitaki kupoteza *energy* bure kwa kitu ambacho hakitaki kueleweka, kwa hiyo, acha Bunge liamue, lakini nashukuru wewe umenielewa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mahali ambapo inabidi kuhoji, Kifungu cha 33 Mheshimiwa Halima Mdee ameleta mapendekezo ya kupunguza adhabu badala ya kusema *not less than five years iseme not less than one year and not exceeding five years.*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mbona wengine hamsemi?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *clause 36(2) by deleting the whole sub clause and rewriting the new one as "(2) The full amount monies from time to time appropriated by Parliament under paraghraph (a) shall be paid by the Treasury out of Consolidated Fund into Authority Fund, into which all other monies received by, or acquiring to the office shall be paid; and the fund shall be independent of control of any person or authority other than the Government Chemistry Laboratory Authority or other person or body acting on that behalf.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la hapa ndipo pale tunapozungumzia kwamba tunataka kutengeneza tanuri la fikra, tunataka hii Bodi kwa sababu huku nyuma tumekuwa muda mwingi tunashindwa kuweka hela za kutosha kwenye *research* na watu wanapoteza muda mwingi kufikiri kuhusu matatizo ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukafikiri kwamba hili eneo kwenye suala la pesa basi lianze kupata hela ambazo kwanza zinatoka huku kwenye *Consolidated Fund* lakini inapata hela kama ambavyo hii Mihimili mingine inapata ili iweze kuwa na nguvu na uhuru wa kutosha wa kufanya kazi zake, hata wakati mwingine kuwa na uwezo wa fedha hata kama wanafikiri kuna *genius somewhere* ambaye anaweza akaletwa kwa hizo pesa na kuweza kusaidia kuweka *input* ambazo zitaleta *solutions* za matatizo makubwa ya kisayansi

tuweze kupata. Ndiyo maana nikafikiri tuweke kwa namna hii. Naombeni mniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mamlaka kama ambavyo mamlaka nyingine zilivyopewa fursa na yenyewe inapewa fursa kwa mujibu wa mapendekezo ya kifungu hiki kwamba inaweza ikakusanya pesa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ikiwemo pesa ambazo itapewa na Bunge, pesa kutoka kwenye zawadi ama ufadhili kutoka kwa wafadhili na marafiki mbalimbali na vyanzo vingine ambavyo vimewekwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuoni haja ya kuviondoa vyanzo vyote hivi vya fedha kwa ajili ya kuweka hiki kimoja ambacho anakipendekeza Mheshimiwa Dkt. Mollel kwa sababu mapendekezo yake yanaongelea fedha zitoke Serikalini tu, kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, wakati kwenye kifungu hiki ambacho kipo kama tunavyokipendekeza kwenye Muswada tumeweka pia mapendekezo yake kwenye Kifungu cha 36(1)(a), pia kwenye Kifungu cha 36(2) ambapo pia mamlaka hii itapata fedha kutoka Serikali Kuu kwa maana ya Mfuko Mkuu wa Hazina kupitia Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya mamlaka hii kupata pesa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, pia kupata pesa kwenye vyanzo vingine ni kwanza iweze kujiendesha yenyewe kwa sehemu fulani, pia iweze kuendesha shughuli mbalimbali ambazo ni za Kiserikali *for that matter* hususan zile shughuli za kupeleka wataalam kutoa ushahidi kwenye Mahakama, ambapo moja kwa moja siyo shughuli ambazo ni *income generating* kwa mamlaka yenyewe, hizi shughuli nyingine ambazo mamlaka itakuwa inapata pesa basi zitafanywa kwa pesa ambazo zimetokana na mamlaka yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, mapendekezo yake yanaenda kubadilisha maana hasa ya kuanzisha mamlaka hii, kwa sababu tunapoanzisha mamlaka hii tunasema hii ni *corporate body* ambayo inaweza ikakusanya pesa. Sasa kuifunga tu kwamba ni lazima ipokee pesa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina siyo sahihi sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, aah! kuna Mollel wawili humu ndani ili rekodi ikae vizuri Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu kubwa kwa kweli siyo kuondoa wasipate hela kutoka kwenye sehemu zingine; ni

kwamba hizo sehemu zingine kuchangiwa kufanya nini kama ambavyo imetajwa sikatai, nakubaliana nayo kabisa, ni jambo jema, lakini kilichopo kichwani kwangu kikubwa ni kwamba tunatamani iwe *funded* kwa *procedure* kama Bunge linavyokuwa *funded* yaani hiyo tu. Maana yake sasa inawezekana kisheria kwa sababu siyo Mwanasheria haya maneno yananipita, lakini maana yangu nitumie mfano iwe inakuwa *funded* kwa maana ya *freedom* hela ambazo haziingiliwi na hii *organ* iwe huru, kama ambavyo Bunge linakuwa huru, ndiyo maana yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itakuwa ina uwezo wa kupata *sources* nyingine sawa, ninachojaribu kukizuia ni hii kuwa *funded* kama tunavyo-*fund* labda Wizara, yaani kuna sehemu inafanya ile *organ* sasa isiwe huru na isiwe *independent,* inaweza ikaingiliwa na mtu mwingine. Tukifanya wakawa huru kwa maana ya kupata hela zao wenyewe *direct* kama Bunge linavyopata wanaweza wakawa na uhuru lakini wasiweze kuingiliwa wakati wa kufanya vitu vyao, ndicho ninachomaanisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo nyingine ya kwamba isiharibu hizo zingine ambazo amesema hapo, nakubali iendelee kubaki kwa namna hiyo, lakini tuipe basi uhuru wa kutosha kama ambavyo nitoe tu mfano wa Bunge, inawezekana maneno ya kisheria, mimi ni Daktari, sasa sielewi wewe Daktari umesomea wapi sheria? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel Wanasheria wapo wengi sana humu ndani na Mwanasheria Mkuu wa Serikali amekaa naye pale karibu. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Dkt. Mollel. Mawazo ya Dkt. Mollel yanalingana na ya mawazo ya Serikali. Tulipokuwa tunaleta mapendekezo haya mbele ya Bunge lako Tukufu tuliona umuhimu wa Mkemia Mkuu wa Serikali, Kifungu hiki cha 36(2) tumechukua maneno ambayo yanatoa fursa hata kwa Bunge na Mahakama. Tulitaka hii Taasisi iwe na fedha ambazo zitaweza kutosheleza kutekeleza majukumu yake. Nikisome Kifungu kinasema hivi: "*subject to the provision of subsection* (1) ambayo ndiyo sasa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema vyanzo vingine vya mapato ya hii taasisi, *The Government shall, mind this* jina *shall within each financial year*, katika kila mwaka wa fedha *allocate and disburse to the Authority monies appropriated by the Parliament to cover expenditures for the activities of the Authority.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mawazo ya Serikali na ya Mheshimiwa Dkt. Mollel yote tunakubaliana, tunatofautiana tu namna ya uandishi. Sasa kwa namna ya uandishi bora wa sheria ningependa kuwashauri Waheshimiwa

Wabunge tuchukue hii ya Serikali, tuiache hii aliyoipendekeza. Naibu Waziri ameifafanua vizuri hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiyachukua maneno ya Dkt. Mollel kama alivyoyaweka tunaua tena fursa nyingine kwa hii taasisi kupata vyanzo vingine vya fedha, lakini hapa Serikali imeji-*commit* kwamba kila mwaka wa fedha Serikali itatenga na kuzitoa zile fedha kwa hiyo taasisi *(authority)* kwa ajili ya kutimiza kukidhi shughuli, *to cover the activities za hii authority.* Kwa hiyo, Serikali imezingatia hili na kama inavyoonekana kwenye hiki kifungu. Naomba kuwashauri Waheshimiwa Wabunge na Dkt. Mollel kwamba wasiwasi tumeuondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mollel ambaye siyo Daktari wa Sheria, karibu.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na alichokisema Naibu Waziri na namsikiliza vizuri sana Mwanasheria Mkuu, ila nataka nisaidiwe maana yake kuna *issue by the Treasury or out of Consolidated Fund into the Authority Fund. Consolidated* sijui! Najaribu kutofautisha hivi vyanzo hebu nisaidiwe, *please* nataka kuelewa uhuru hasa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo gani anazungumza? Fedha zote za Serikali zinatoka Mfuko Mkuu wa Hazina tu ambayo ndiyo *Consolidated Fund.* Fedha zinakusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato halafu vinawekwa Mfuko Mkuu wa Hazina, kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ndiyo inagawanywa, uzuri ni kwamba sasa hivi, pamoja inaweza ikatokea kukawepo labda ufinyu au *whatever,* lakini sheria inaitaka Serikali "*shall*" hawa wapewe fedha za kukidhi utekelezaji wa majukumu yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel malizia hoja.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itakuwa inamaanisha hizo hela siyo kwamba tunakuja tunambana Waziri wa Afya ndiyo anaingiza kwenye Fungu lake la Wizara ndiyo wanapelekewa. Kama haimaanishi hivyo inamaanisha itakuwa inatoka *direct* kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zinakuja sijui, nakubaliana na hoja. *Essence* ni hiyo ya kuwepo na hela za uhakika, lakini pamoja na hizo zingine kama Naibu Waziri anavyosema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, ahsante kwa kukubaliana, lakini fedha atakazopewa hata kama zinapita kwa Waziri ama zinapita popote lazima ziwe

zilikuja hapa na zimepitishwa kwenye bajeti. Kwa hiyo, hatoweza kupewa hela kutoka kule bila Bunge kuwa lilipitisha hizo fedha na nadhani ndiyo maana ya hapa mwanzo kwamba zitatoka kule lakini lazima Bunge liwe linajua anapewa shilingi ngapi na lazima lipitishe kwenye bajeti. Baada ya kuelewa hilo, Waheshimiwa Wabunge nitawahoji.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara 37

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nimepitia *further schedule of amendment* ya Serikali naona Serikali imekubaliana na mapendekezo yangu. Kwa hiyo, naafiki mapendekezo ya Serikali. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeyachukua mapendekezo yangu, kwa hiyo naafiki. *(Makofi)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijapata hayo marekebisho ya Serikali, lakini msingi wa mapendekezo yangu ilikuwa kwamba katika Kifungu cha 39(1), kwanza kilikuwa kimetaja kwamba mwisho wa mwaka watatengeneza hizo ripoti za mwaka, lakini hawakuweka muda ambapo sasa katika sheria zingine inaonekana kwamba vitabu vile lazima viwe vimekamilika ndani ya miezi mitatu, kwa hiyo, niliongeza iwe *within three months.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu (b), kwa sababu tunazungumzia sasa hesabu zilizokaguliwa niliona kwamba ule muda ambao ulikuwa umewekwa ulikuwa hautoshi, kwa hiyo nikapendekeza kwamba iwe ndani ya miezi sita badala ya ile miezi mitatu ambayo inakuwa siyo *practical,* nafikiri Serikali hiyo wanakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 39(3) nimependekeza iongezwe (f) ambayo isomeke *Directors report.* Napendekeza hivi kwa sababu katika hiki

Kifungu namba 39(3) wameweka *financial statements* ambazo zitatakiwa kutayarishwa, katika hizi *financial statements* ambazo zimetajwa hapa msingi wake mkubwa zote zinalenga masuala ya fedha tu, lakini taasisi ili uweze kuipima vizuri kunahitajika kuwe na masuala ya fedha lakini pia kuwe na taarifa zingine ambazo unaweza ukazitumia katika kui-*assess* taasisi.

*Directors report* inakuwa na mambo yote hayo, inakuwa na mambo ya rasilimali watu, inakuwa na malengo ya taasisi na mambo mengine yote ambavyo jinsi taasisi ilivyoweza kutengeneza. Hiyo nayo ni sehemu ya *financial statement.* Kwa hiyo, nimependekeza iongezeke hiyo ili kusudi iweze kusomeka vizuri badala ya kutaja tu masuala ya fedha. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga kwenye ile 39(1) Serikali hatujayakubali, lakini mapendekezo katika Kifungu 39(2) na ile (f) yote tutayakubali kwa sababu ile 39(2) ni sawa na anachokipendekeza Mheshimiwa Chenge ambayo tayari imekuwa *taken care of* kwenye *further schedule of amendment* ya Serikali. Ile anayoipendekeza ya *Directors Report* pia tunaikubali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, mapendekezo yako mawili Serikali imeyachukua, hilo moja la 39(1) ndiyo ambalo unaweza ukalitolea maelezo ya ziada.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hiyo (a) ambayo Serikali inakataa bado haina matatizo sana kwa sababu kwenye sheria zingine bado inataka kwamba ripoti hizo zikamilike ndani ya miezi mitatu, hata kama hatutolisema bado halina madhara yoyote katika hii sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga ahsante. Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji. Ili nijue nahoji sawa sawa Serikali mapendekezo ya Mheshimiwa Chenge na Mheshimiwa Hasunga yapo tayari kwenye mapendekezo ya Serikali?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mheshimiwa Japhet Hasunga tumekubali ile ya *Directors report* lakini nataka ku-*clarify,* ana-*propose* tuweke *under* 39(3) ambayo inazungumzia *financial statements shall include.* Kwa hiyo, kama anataka hizi *Directors report* tungeiweka juu kule kwenye 39(1), kwa hiyo haina shida Waandishi wataliangalia. Halafu hapa tujikite tu kwenye *financial report; it's okay.*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakimshauri jambo Mheshimiwa Waziri)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** *No!* mnanichanganya, isiwe kwenye (3) kwa sababu hapo kwenye (3) tunazungumzia *specifically financial statement shall include, statement of financial performance, financial position, cash flows, changes of equity and financial statement.* Wataalam wanasema *Directors report it is part of the financial statement, then* tunakubali.

**MWENYEKITI:** sawa, baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nawahoji.

*(Ibara ilitajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 40

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukiri kwamba Serikali imeyachukua mapendekezo yangu. Kwa hiyo, sina tatizo na hiyo. *(Makofi)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, japo sijayaona vizuri hayo marekebisho, nafikiri kwamba imezingatia kwa sababu kinaendana na mapendekezo yale ambayo Mheshimiwa Chenge ameyapendekeza. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 45

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki Kifungu kinaonesha kwamba hawa wanaotajwa wote, Bodi, *Chemist* na *Members* wengine wa *Committee* wanaweza wakafanya mambo wanasema kwa nia njema. Sasa tunasema

ionekane nimependekeza hapa kuna maneno mengi lakini hili neno *Act shall, if done, recklessly,* hiki kipengele kiwahusu na hii kinga iondoke kama watakuwa wamefanya kiuzembe, ni neno moja tu nataka tubadilishe tuseme kama watafanya kiuzembe wawajibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake hapa inaonekana kwamba inasema kwa nia njema, nia njema haina tafsiri lakini pia wamewekewa kinga, kwa hiyo inaweza ikawa kichaka watu wakajificha hapa. Kwa hiyo, nataka maneno yote yabaki kama yalivyo, kinga iondoke lakini kama atafanya *recklessly then* hawa watu wawajibishwe, ndiyo mapendekezo yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo tu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utumishi wa Umma, hawa watu wanafanya kazi wanaweza wakafanya makosa lakini wanalindwa tu hapa kwa yale ambayo wameyafanya *in good faith*, *the test is objective* siyo *subjective*. *Test* ya hii kitu siyo *subjective,* kwamba mimi najitetea kwamba nilifanya kwa nia njema, wataangalia *in totality of the sorrounding circumstances* halafu wanakuja wanasema huyu hakuwa na nia mbaya, *in good faith.* Kwa hiyo, naomba kushauri Waheshimiwa Wabunge tukiridhie hiki kifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi sana kwenye sheria nyingi vifungu kama hivi tunaviandika kwa namna ya *in good faith.* Sasa anachosema kama ni uzembe au ufisadi, hatakuwa-*covered,* kwa sababu *that is not in good faith.* Kwa hiyo, Mheshimiwa Waitara Ndugu yangu nakuomba tu, hili jinsi lilivyo halina matatizo, vinginevyo hata watu wenyewe hawa badala ya kuisaidia Serikali kutekeleza wajibu wao wakijiamini, watakuwa waoga sana hatutafika sehemu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndivyo walivyo tu Watumishi wa Umma, *they are so much protected,* lakini hii haina maana kwamba hawashtakiwi! Unamshtaki yeye mwenyewe au unaweza ukamshtaki *vicariously* yule mwajiri wake ambaye sasa ni Serikali, ndiyo maana unaona mara nyingi sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali anashtakiwa Mahakamani kwa mambo ambayo yamefanywa na Watumishi wa Taasisi fulani za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri tu kwamba Mheshimiwa Waitara asiwe na wasiwasi sana kwa sababu siyo kwamba hawa wanajipimia tu wanasema aah! kwamba mpaka kinawekwa hapa kifungu, unaona kabisa nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba moja, Watumishi wanafanya wajibu wao kwa kuzingatia sheria na uadilifu. Kwa hiyo inafungua fursa ya kuwashtaki lakini kuwashtaki tu kwa mambo ambayo hawakuyafanya *in good faith,* vinginevyo kama aliyafanya *in good faith,* basi Mwajiri wake, Serikali atawajibika. Naomba

kushauri tu Waheshimiwa Wabunge walikubali pendekezo hili la Serikali kama lilivyo kwenye hii Ibara ya 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yangu bado inabaki palepale tu kwamba, kwa nini haya maelezo ya kwamba ni nia njema, asiachiwe aje aeleze yeye, kwa nini tumwekee kwenye sheria na nini maana ya nia njema. Kwa sababu mambo mengi yanafanyika, hili neno likiwepo litaweza kutumika vibaya ndiyo wasiwasi wetu. Kwamba yeye angebanwa na sheria za kawaida, kwamba anapaswa kuwa mtiifu, afuate sheria, afuate taratibu za kawaida kikazi na awe mnyoofu katika mambo yake. Kama itatokea kwamba anashtakiwa hayo maelezo ndiyo yaseme lakini tusimwekee hapa kinga. Hiki ni kichaka cha kuficha mambo yao, ndiyo hofu yetu hapa tangu siku ya kwanza nilisema kwamba hili neno hapa siyo zuri, imesemwa kabisa hii ni kinga ya Wajumbe wa Bodi na Maafisa wa Mamlaka, kwa hiyo wameshakingwa wao. Kinga unawawekea watumishi hawa, lakini wananchi wengine ambao wanahitaji huduma yao hawajawekewa kinga, kwa hiyo itakuwa *double standard.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo *double standard,* ukienda mbele kwa mfano kwenye Ibara ya 53, unaona hata hawa watumishi wa *Authority* wanawajibika kisheria kwa mambo ambayo wameyafanya. Kwa mfano, "*Any employee of the Authority who knowingly or intensionally destroys, varies or alters a document or laboratory analysis report generated in the process of carrying out activities under this Act commits an offence and shall, on conviction, be liable to a fine of not less than five million shillings or to imprisonment for a period of not less than six month or to both*".

Kwa hiyo, hata hawa unaona kuna sehemu wanawajibika moja kwa moja. lakini tukiwaacha tu hivi hivi mnasema tunananihii hapa, Kwa hiyo hata unaona imefungua pia, hapa hakuna *double standard.*

Waheshimiwa Wabunge, naomba kushauri tu Waheshimiwa Wabunge tukubali mapendekezo ya Serikali. Mheshimiwa Mwita, kesi yako imeshafanywa, *you have made a case,* lakini pia unaona kabisa mapendekezo ya Serikali yanawawajibisha pia hawa jamaa wanaofanya mambo kinyume na maadili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.*(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili wanasema wasiwasi ndiyo akili. Bado wasiwasi wangu umebaki pale pale, naomba Bunge liamue rekodi iwepo tu kwamba mimi siungi mkono hii hoja.

**MWENYEKITI:** Sawa, Mheshimiwa Waitara. Waheshimiwa Wabunge maneno haya ya kwa nia njema huwa ni ya kawaida katika uandishi wa sheria. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waitara.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 48

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49
Ibara ya 50

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 51

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kifungu hiki *sub-clause* (5), napendekeza yafutwe maneno *not less than five appearing between the words term and years and substituting them with the words not less than one year but not exceeding five.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa hoja Mosi; kama niliyojenga katika Kifungu cha 33. Pili, kwa hoja ambayo uliiona baada ya hoja yangu ya uwiano wa adhabu. Nisisitize kwamba kwa mfano haiingii akilini Kifungu kilichopita cha 33 wamesema *fine* isiyopungua milioni 10 na kifungo kisichopungua miaka mitano, wakakipitisha kwa sababu ambazo wanadhani zinafaa. Kifungu cha 51 wanasema *fine* isiyopungua milioni tano na kifungo kisichopungua miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 51 kinahusiana na usiri na utoaji wa taarifa, ambacho hakitofautiani na Kifungu cha 33, pia hakitofautiani na vifungu vingine vilivyopita. Hoja yangu hapa ni kwamba Serikali inatakiwa itoe adhabu ambayo ina dhamira ya kumrekebisha mtu, lakini siyo adhabu ya kukomoana, ndiyo maana sijapendekeza mabadiliko ya fedha, nimependekeza mabadiliko ya vifungo kwa kuzingatia mtiririko wa vifungo mbalimbali ambavyo vimetolewa huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali inasema hivi vitu ni vizito sana, basi kwenye fedha iwe sawasawa na kwenye vifungo katika vifungu vyote, kwa sababu huwezi kusema kwenye kanzidata kutoa siri ni *issue* wakati hiki kifungu kinazungumzia siri *generally, penalty* umeweka chini kidogo. Kwa hiyo, ni muhimu wakati tunatunga sheria tusitunge sheria kwa dhamira ya kukomoa, tutunge sheria ambayo inawiana lakini yenye nia ya kurekebisha mtu, siyo kuacha wigo mpana ambao unaweza kuja kuwa *abused.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana niliiuliza Serikali, wakati wananijibu haya kabla hatujafika Kifungu cha 55, naomba wanipe tafsiri ya hiki Kifungu cha 55 cha mamlaka ya kufifisha kosa ambapo mamlaka hii imepewa jukumu. Naomba nisome, natanguliza shughuli lakini nafanya rejea kwa sababu vina uhusiano, kinasema mamlaka inaweza, ikiwa imejiridhisha kuwa mtu huyo ametenda kosa chini ya sheria hii, itafifisha kosa kwa kumkubalia mtu huyo kulipa kiasi cha fedha kisichozidi milioni tano. Pili inasema, mamlaka iliyotolewa chini ya Kifungu hiki yatatumika pale ambapo mtu atakiri kwamba ametenda kosa chini ya sheria hii. Tatu, kiasi chochote cha fedha kitakachopokelewa chini ya kifungu hiki kitachukuliwa kama vile ni kiasi cha fedha kilichotozwa na Mahakama kwa kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu Serikali inieleweshe hiki Kifungu cha 55 ambacho kinaonesha kuna *some kind of leniency,* kina-*apply* katika mazingira tofauti lakini siyo katika mazingira ya sheria hii, kama ana-*apply* katika mazingira ya sheria hii basi kuna haja ya kuangalia hizi *penalties* tunazozitoa ziwe: Mosi; zinatekelezeka, pili; ziwe na uwiano na tatu; ziwe na nia ya kumrekebisha mtu siyo kumkomoa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zangu ni hizo tu, nakushukuru.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumekuwa *referred* hapa kwenye *Section 55* lakini nianze na hii, *is it 51 (5), right?*

**MWENYEKITI:** *Yes.*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU – WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niweke wazi tofauti kati ya Kifungu kile kilichokuwa kinahusiana na mtu kupata taarifa za *database* ambayo ilikuwa ina taarifa kuhusu vinasaba na nini na hii hapa ni *any person who, or has been engaged in the,* mtu ambaye anahusika na utekelezaji wa sheria hii kwa ujumla. Kwa hiyo, kuna tofauti ya uzito wa makosa hapa. Lile la *database* tulishasema ni kosa kubwa sana kutokana na *nature* ya *information* iliyokuwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *nature* ya *information* ambayo ingeweza kutolewa kule kwenye *database* ingeweza kusababisha kwa mfano mtu kutengana na mzazi wake *for the rest of his life,* hapa ni makosa ya kawaida ile *information* unazozipata katika hali ya kawaida ya utendaji wa sheria hii, kwa sababu sheria ili-*aim specifically* kuweka adhabu kubwa kule, hii haiwezi ikaingiliana na kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliposema kwamba iungane mamlaka ya kufifilisha kosa, hapa kwanza *Section 55(1)* imesema *the Authority may,* kwa hiyo siyo wakati wote kwamba *the Authority* itakuwa ina-*compound offence,* halafu pia imeweka masharti ya ku-*compound offence* mojawapo inapatikana pale katika sub *section (2)* ambapo mtu kwa hiari yake amekubali kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake, Kifungu 55 ambacho alitupeleka Mheshimiwa Mdee hakitumika wakati wote, ni pale ambapo masharti yake yaliyotajwa humu yamekamilika wakati hiki kingine kita-*apply.* Hivyo Kifungu Na. 51(5) basi kitafsiriwe kwa mazingira yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee kabla hujamalizia hoja yako, nadhani upande wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi, hapa kama adhabu inasema isiyopungua milioni tano, au kifungo kisichopungua miaka mitano. Katika ule uandishi tu wa ile sheria ikae vizuri hii adhabu maana yake lazima umeipima kwa uzito fulani.

Hapa kwa sababu umeipa fursa Mahakama ya kuamua kutoa adhabu ya fedha ama ya kifungo, kule umetaja milioni 10 miaka mitano, hapa milioni tano miaka mitano, kwingine milioni tano miaka mitatu, kwingine milioni tano miaka miwili. Kwa hiyo, yale makosa lazima sheria moja iweze kuyaona yale ambayo yanaendana kwa sababu ukiweka adhabu ya miaka mitano maana yake inalingana na milioni tano.

Mheshimiwa Halima Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru unanielewa kweli, halafu nashangaa kwa nini Serikali hainielewi, ndiyo hicho ninachoshangaa, sasa sijui ni ushabiki ama la au tumechoka labda tuahirishe

shughuli? Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri wakati anajibu amesema kuna tofauti ya vifungu, kama nimemnukuu vizuri, amesema uzito wa makosa unatofautiana na amesema haya ni makosa ya kawaida. Sasa kama haya ni makosa ya kawaida kwa nini useme *imprisonment for a term not less than five years,* sawa na yale makosa mazito ya Kifungu cha 33, hiyo ndiyo hoja, iko nyepesi tu wala haihitaji kuwa na akili nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali inakiri kwamba haya ni makosa ya kawaida *then it's high time* kwa wao kukubali haya mabadiliko yangu niliyosema *not less than one year, but not exceeding five years.* Tunaweza tuka-*range* pale kwa sababu ni makosa ya kawaida, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Serikali imekiri yenyewe kwamba kuna Kifungu cha 55 ambacho kinasema *power to compound offenses,* mamlaka ya kufifilisha makosa, kwamba hii *Authority* tuliyoiunda inaona mtu amefanya kosa, huyo mtu anakiri amefanya kosa, baada ya kukiri amefanya kosa mamlaka inamtoza kiasi cha fedha cha shilingi milioni tano kwa kosa lolote kwenye sheria hii. Sasa Mheshimiwa Possi anasema *may, what does may imply, yes* anaweza akafanya na kama umempa mamlaka ya kuweza, atafanya, huhitaji kumwambia lazima afanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama dhamira kwenye sheria hii kuna mazingira ambayo mtu akawa amefanya kosa kubwa lakini akasema kweli nimekosa, nakiri kosa, akatozwa milioni tano, kwa nini kwenye sheria hiihii kuwe kuna vipengele ambavyo vina *penalty* ambazo ziko *very harsh* tusiwe *reasonable,* hiyo ndiyo hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekiri kile Kifungu cha 33 kilikuwa ni kizito, hiki kifungu cha 51 ni kidogo, ikubaliane na mapendekezo yangu ili tuweze kutoka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ametoa maelezo mazuri kuhusu hili suala. Moja, ile ya kwanza ya 33 ilihusu *disclosure* ya *database* ya *DNA* na Waziri alivyofafanua ni kwamba ile ilikuwa ni *reconciliation,* ilikuwa ni *reference* ya sheria nyingine ya *DNA* kwa hiyo hizo sheria lazima zisomeke zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo unaiona iko *so much specific* kwenye *disclosure ya DNA database,* hii sasa ni *general,* kwa hiyo kama unashtaki utachagua kwamba yule ambaye ame-*disclose* ile ya *database* unam-*page* kwenye 33, hivi vitu vingine ndiyo unamleta kwenye Kifungu cha 55, hivyo

makosa yenyewe hayo yanaweza yasiwe *so much serious* kulinganisha na ile ya kwenye Kifungu cha 33, ndiyo msingi wa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu *compounding,* huu ni utaratibu wa kawaida kwenye *principles* za *sentencing,* kwanza zinapunguza ule urasimu. Kama tulivyofafanua, Waheshimiwa naomba muangalie kwenye *first schedule of amendments* ambayo imekuwa *moved* na Serikali, hiki Kifungu kimefutwa na kuandikwa upya ili kuleta *clarity.* Kwa kawaida makosa ambayo kwenye *principle za practice* za makosa ambayo yanaweza mtu *Authority* ika-*compound* ni yale makosa ambayo siyo makosa makubwa na pia ni lazima huyo mtu akubali, kama hakubali haiwezekani tu lazima mwende Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho utaona kwenye marekebisho yetu, makosa yapi sasa yanaweza kuwa-*compounded,* tunapendekeza kwamba Waziri ataeleza hayo kwenye Kanuni, ndiyo anasema makosa haya na haya kwa *nature* ni madogo, haya yanaweza kuwa *compounded otherwise* lazima yaende Mahakamani. Vifungu hivi jinsi vilivyo vinatoa funzo, kwa sababu makosa mengine, kwa mfano *disclosure* ya *confidentiality* huwezi ukaya-*belittle* ukasema kwamba sasa tupunguze adhabu, inategemea pia ni *nature* ipi sasa ya hiyo *kind of confidential matters* ambayo anai-*disclose,* ndiyo maana tumeona kibaki hivi hiki kifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata kwenye uandishi wa sheria tu adhabu zinatofautiana kutokana na *nature* ya kosa lenyewe. Huwezi ukatengeneza sheria ambayo tangu mwanzo wa adhabu kama ilikuwa faini ya shilingi mbili basi yote faini ni ya shilingi mbili tu, ni lazima zi-*vary*. Sasa uzuri wa hili ni kwamba, tunaipa mamlaka Mahakama na kwenye *jurisprudence* sasa ya *sentence* hii *whatever* na uhuru wa Mahakama wanasema Mahakama isifungwe sana, tunapendekeza hapa *minimum* lakini Mahakama inaweza ikasema *minimum* hiyo mimi na-*enhance* kama ni zile *fine* i-*enhance* halafu *minimum* kwenye *sentence* ikamfunga na *minimum* hiyo ama ika-*enhance* zile kutegemea na *nature* ya *information* ambayo itakuwa imekuwa *disclosed* humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mapendekezo ya Serikali na baada ya Serikali kuleta marekebisho haya kwenye jedwali hili la kwanza la Kifungu cha 55 ambacho ninaki-*refer* tu kwa sababu Mheshimiwa Halima Mdee amezungumza hii, nilikuwa naomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane na mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee malizia hoja yako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hii biashara ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusema kwamba kuna mabadiliko ya Serikali wakati anayo yeye mwenyewe, sidhani kama ni sahihi. Kwa hiyo kama unayo ulete huku ili watu wayaone, siyo unafanya rejea rejea zako hapo kivyako vyako halafu unatuingiza kwenye chaka. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naliomba hili Bunge liamue kwa sababu Mheshimiwa Possi amekiri na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuongezea maneno ya Mheshimiwa Possi amekiri na Mwenyekiti mwenyewe umekiri kwamba Kifungu cha 51(5) ama 51 kiujumla wake kinahusiana na makosa ya kawaida, siyo makosa mazito kama kifungu cha 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo inashauri na nimwambie Mwanasheria Mkuu wa Serikali; huwezi kusema Mahakama itaamua wakati kifungo cha chini ulichokiweka wewe ni kikali kiasi kwamba hata hiyo Mahakama ikiamua itakuwa imemuumiza huyo mtu. Kwa kuwa, Serikali mnakiri kwamba hiki ni Kifungu ambacho ni chepesi siyo kama Kifungu cha 33 kwa maneno yenu, napendekeza hili pendekezo langu la kati ya mwaka mmoja mpaka miaka mitano likubaliwe na Serikali. Hiyo itakuwa imejibu hoja ya Mheshimiwa Possi na itakuwa imejibu hoja ya *AG*, pia itakuwa imetengeneza mtiririko wa kisheria ambapo faini na vifungo vinaendana. Ukiiambia Mahakama sasa hivi kifungo cha chini kiwe miaka mitano kwa kosa la kawaida, hivi tunasahau kwamba kesho na keshokutwa haya mambo yatatuhusu sisi, tusitunge sheria kama tunatungia watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize kwamba *as long as,* nashukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amekiri mwenyewe kwamba hiki Kifungu cha 55 cha kufifilisha makosa kina-*apply* katika vifungu vyote hivi hayo ndiyo maelezo yake aliyozungumza. Sasa kama kuna kifungu huku kinasema *penalty* ama faini isizidi milioni 20 ama milioni 15 lakini Mamlaka inaruhusiwa mtu akikiri kulipa milioni tano, hivi tunaona madhara gani kama tukiweza kutengeneza vifungo ama kupendekeza vifungo ama faini ambazo ni *reasonable,* sikwenda kwenye *fine* kwa sababu nilijua, mtu kama atafanya makosa ambayo yana maslahi mapana ya Taifa, ataumizwa sana kwenye *fine* kutokana na uzito wa kosa, ikija kwenye kifungo tuwe *rational*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuamue wewe umeona, Naibu Waziri ameona, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameona, tunachokifanya hapa tunabishana tu kwa vitu ambavyo viko *straight forward.* Makosa hayalingani, haiwezekani ukamlinganisha mtu ambaye anaua na mtu ambaye……

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, kengele iligonga muda kidogo, kwa hiyo hoja yako nadhani imesikika na imeeleweka

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Naomba Bunge liamue kwa nia njema tu kutokana na Serikali ilivyokiri. Mheshimiwa Ummy Mwalimu Waziri wa Afya alikuwa anatikisa kichwa anataka kukubali Mwanasheria Mkuu akamdanganya danganya pale kabadilika, fanya mambo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee umeshaeleweka. Sasa tumefika mahali ambapo natakiwa kulihoji Bunge. Serikali bado inaona milioni tano na miaka mitano kwenye kifungu hiki kibaki hivyo, siyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 53

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 54

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa marekebisho yangu naona Waziri ameweka hapa vizuri.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 55

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu hiki nilipendekeza kuongeza *sub-clause (4)* ambayo itasoma hivi; "*The Minister shall make regulations prescribing offences to be compounded and procedures for compounding*". Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema na wao wameleta mabadiliko, *assumption* mabadiliko yanayofanana hivyo kwa sababu kifungu hiki kama nilivyosema mwanzo wakati nakifanyia rejea, kikiachwa kama kilivyo inawezekana kuna makosa mengine mazito Mamlaka itatumia mamlaka yake kumsamehe mtu kwa sababu amekiri na kwa kumtoza fedha ndogo, nikasema Waziri akipewa Mamlaka kwa kuweka huo utaratibu ama Kanuni, ambazo zitaelezea aina ya makosa yanayoweza kuwa *compounded* ita-*limit* haya mamlaka mapana ya Mamlaka, unajua tatizo *Authority* na yenyewe ni Mamlaka. Mamlaka mapana ya hii Mamlaka tunayoianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, dhamira ndiyo hiyo kwamba hiki kifungu kisiwe na wigo mpana, ila kuwe kuna mazingira ambayo Waziri amepewa Mamlaka ya kuweka ni makosa gani yanaweza yakafifilishwa, ni makosa gani hayawezi kufifilishwa ili *spirit* nzima ya sheria iwe na tija. Tukiacha hivi ni kama vile tunatwanga maji kwenye kinu tu na kupoteza muda hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu, naamini wamenielewa *at last.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumshukuru Mheshimiwa Halima Mdee, anachokisema Serikali imekizingatia kwenye *first schedule of amendments* ya Serikali na kimeandikwa hivyo na anasema hajapata haya marekebisho ni kwa sababu kama mkiangalia Waheshimiwa Wabunge yameletwa mengi tunayachanganya hata sisi humu ndani, kwa vyovyote vile atakuwa nayo pale, lakini watu wazima hatuwezi kusimama hapa kama watu *genuine* tukaweza kulidanganya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mdee ukubali tu kwamba, kwanza kile Kifungu kimefutwa na kuandikwa upya na *sub-clause (5)* sasa kinasema "*The Minister shall make regulations prescribing offences to be compounded and procedures for compounding offences under this Act.*" Kwa hiyo, *the cases has been taken care of.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambacho naomba kushauri hapa ni kwamba, utaratibu wa kutunga hizi Kanuni ni shirikishi. Waziri huwa anashirikisha wadau, *if will anything* watu wote wale ambao wanahusika *stakeholders* watashirikishwa, *but* cha muhimu sana ni kwamba hoja ya Mheshimiwa Mdee imekubaliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** *Senior citizen,* Mheshimiwa Chenge

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Niishukuru Serikali, nimshukuru Mheshimiwa Mdee katika Kifungu cha 55 Serikali imekiandika vizuri sana na kuyabeba hayo ambayo Mheshimiwa Mdee ameyapendekeza. Nasimama kwa hoja moja tu. Ukisoma marekebisho ya Serikali kwenye Kifungu cha 55, dhana nzima sasa ya *compounding* nadhani wamefanya tu siyo kosa la makusudi, ni *omission* tu kwa sababu mtu lazima akubali, akiri kosa sasa ilivyokaa, *admission* hiyo huipati mahali popote kuanzia *one* mpaka mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusaidia tu kwamba katika Kifungu 55(1) tunapoanza kusema *notwithstanding the provision of this Act relating to penalties, where a person* sasa hapo ndiyo tukubaliane kuingiza maneno ambayo yatabeba dhana ya *admission, admit* inaweza kuwa *in writing* lakini anasema; *admit to have committed any offence.* Sasa ukienda namna hiyo ndiyo utakuwa umeipata dhana nzima ya *compounding*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi uka-*compound an offence* na wala huwezi kuipeleka kwenye *regulation* ukasema utaitengeneza kwenye *regulation* kama msingi hauko kwenye Sheria Mama ndiyo maana nimeona nisimame, tusaidiane na Serikali wakiliona hilo, mahali ninapoona mimi pa kuingilia ni kwenye mstari wa pili wa marekebisho yao 55(1) *admits in writing to have committed* itakuwa imekaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwanza nimshukuru Kaka yangu Mtemi Andrew Chenge na kama alivyosema ni *omission* kwa sababu ukisoma Muswada kwa mara ya kwanza kiliwekwa hiki kifungu kwamba ni-*admit,* kwa hiyo ni *omission* tu tunakubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Chenge.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji hiki kifungu cha 55

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 56

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1
Jedwali la 2
Jedwali la 3
Jedwali la 4

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 5

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Adadi Rajab

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la hili Jedwali la (5) ni *clause* 32 na *clause* 32 ni mambo ya *DNA*. Nimepata wasiwasi wa hili jedwali kuingizwa *data* ambazo naona labda Mkemia Mkuu *Authority* atapata tabu kuzipata. *Data* ambazo zinahusiana na *offences* za *criminality,* kwa mfano kama hiyo *crimes* au *convicted* Wafungwa ambao wamefungwa au mahabusu na *sexual offenders.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiria kwamba labda kulikuwa na *omission* na jedwali hili lilikuwa lina-*meant* kupata *database* ya *forensic cases* ambazo zimewasilishwa pale kwa *Authority.* Hivyo nilileta mapendekezo ya kuangalia hayo marekebisho na ku-*delete opening statement* ya mwanzo ambayo ilikuwa inasema "*the information in the database contain but not limited to,* sasa kitu ambacho nimeongeza ni *The information in the data base shall contain the cases reported but not limitedto* ili uongeze zote hizo, kwa mantiki kwamba *database* hii ilikuwa inataka ku-*cover cases* zote ambazo zimekwenda *for forensic analysis for DNA* katika *authority* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba marekebisho hayo madogo yafanywe ili iweze kuleta *meaning,* kwa sababu utakapoisoma *on the first of it* mtu utafikiri kwamba ni ngumu kwamba utapata wapi *data* za wafungwa Mkemia Mkuu utazipata wapi? *data* za mahabusu utazipata wapi?, *data* za *sexual offences* ambazo huwezi kuzipata zote, *sexual offences* nyingi zinakuwa huko Polisi au *CID,* lakini huwezi kuzipata kule zote. Kwa hiyo, *I thought* kwamba, alikuwa na maana ya kupata *database* ya *cases* ambazo zimefanyiwa *forensic analysis* kwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, naomba marekebisho hayo yakubaliwe na Mheshimiwa Waziri kama ambavyo nimependekeza kwenye *schedule of amendments.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Nadhani wasiwasi wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab tumeuelewa vizuri, lakini tunapenda ibaki kama ilivyo kwa sababu ndipo sasa tutamwezesha Mkemia Mkuu wa Serikali aweze kufanya *effort* za kupata hizi taarifa akifanya jitihada za kupata hizi taarifa maana yake atafanya kazi yake vizuri zaidi, kwa sababu sasa atakuwa anao uwezo wa kufanya hata *investigation* kwenye makosa kwa mfano haya ya ubakaji ambayo Waheshimiwa Wabunge wameongea hapa kwa hisia sana toka tulipoanza kuujadili Muswada huu. Kwa maana hiyo ataweza kutoa ushahidi wa uhakika Mahakamani ambapo atatakiwa kutoa ushahidi wake wa kitaalam. Kwa msingi huo ni bora ikabaki kama ilivyo ili kumlazimisha sasa kwa mujibu wa sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali kutengeneza utaratibu wa namna ya kupata hizo *data* ambazo atazitumia katika utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wake Mheshimiwa Adadi ni kwamba tu unajibiwa na hii *sentence* ambayo imewekwa hapa mwanzoni kwamba *The information in the data base shall contain but not limited to.* Kwa hiyo, anachokisema kinakuwa *covered* na hii *but not limited to.* Kwa maana hiyo tunaomba ibaki kama ilivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Adadi Rajab.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma hiyo *sentence is not clear*, mtu akiisoma mwanzoni tu anajua kwamba hapa zinatakiwa *databases* za makosa yote haya ambayo yameorodheshwa kuanzia namba moja mpaka namba 11, hata kama Mkemia utataka kupata taarifa au utataka kupata taarifa hizi, utapata vizingiti, huwezi ukapewa taarifa za *let say* kwenye mambo ya *Defence Forces, Police Forces,* zinahusiana nini hapa? Huwezi ukapewa taarifa za *case* zote za *crime scene*. *Crime scene* ina-*involve a lot of scene* kwenye *crime,* siyo *cases* tu zile ambazo zinaletwa kwenye Mkemia Mkuu wa Maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukapata *data* za *sexual offences all of them* au *violent offences* huwezi kupata ni *a lot of cases,* sasa wewe Mkemia Mkuu unazitaka hizo za nini? Wewe pata *data* zako ambazo umefanya *forensic analysis* zinazokuhusu. Huwezi ukapata zote hizi! Kwa hiyo, *concentration* hapa iwe ya *database* au *statistics* zinahusiana na *forensic analysis* ambazo zimepita kwa Mkemia Mkuu kwa ajili ya *DNA* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri samahani kidogo ili utakapokuwa unatueleza wote tuwe na uelewa sawa. Alichokuwa anaeleza Mheshimiwa Balozi Adadi mwanzo mimi nilimuelewa vizuri, kidogo Mheshimiwa Waziri

aliposema ni kana kwamba sasa Mkemia Mkuu wa Serikali baada ya kuanzisha hizi *index* hapa, atatakiwa kwenda kuzitafuta taarifa ili aweke.

Uelewa inaposomeka hapa ni kwamba huyu Mkemia Mkuu wa Serikali anapaswa kuwa na hizi *index,* yaani atakapoletewa *violent offender* aweke, atakapoletewa sijui za mtoto aweke, atakapoletewa nyingine aweke, zile alizopima yeye, lakini kwamba ataenda kuzitafuta hapo ndiyo kidogo Mheshimiwa Waziri nadhani utuweke sawa. Huyu Mkemia Mkuu wa Serikali anatunza zile alizopima yeye au anaenda kuzichukua kule ili aweke.

Mheshimiwa Waziri tueleweshe vizuri hapo ili tujue maamuzi tunayofanya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru umeliweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama alivyosema Mheshimiwa Kaka yangu Balozi Adadi Rajabu, *schedule* ya tano unaisoma pamoja na *section 32,* kwa hiyo *section 32(5) 'The Board may review or vary the list of information to be contained in the database'*. Hiki kitu *any time Board* inaweza ika-*review* na mimi *actually understanding* ni kama ulivyosema. Mtakapofanya *analysis* ya masuala labda kwenye masuala ya *criminals* ina maana Mkemia itabidi afungue *registry* ndiyo maana yake, lakini kwenye ile ya watoto ataanza mwenyewe moja kwa moja, kwa hiyo ndiyo uelewa.

Mheshimiwa Kaka yangu Mheshimiwa Adadi Rajab hili jedwali lisikutie wasiwasi ni kwa sababu pia *any time can be reviewed by the Board* na tunachotaka lazima awe na *registry* jinsi *cases* zimekuwa *referred* kwake. Ndiyo maana yake.

**MWENYEKITI:** Kwa maana hiyo Mheshimiwa Waziri, samahani Mheshimiwa Adadi Rajab, hapa namna inavyosomeka kama uelewa ni huo, pengine basi hakuna haja ya kuongeza maneno, kwa sababu huyu Mkemia Mkuu anajitengenezea yeye haya yaliyoandikwa na ataongezewa mengine kadri itakavyoonekana inafaa. Kwa maana hiyo hakuna haja ya kusema yale anayopelekewa, lakini sasa kwa maelezo ya Naibu Waziri ndiyo yalileta hiyo tabu ya kusisitiza.

Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, ukiisoma hii 32 huku mwanzo ukaisoma hii utapata picha kwamba anayoyatunza ni yale aliyoletewa yeye. Ndiyo atatakiwa kutengeneza hizi *compartments,* hawezi kupelekewa huyu *violent offender* akasema, aah! Mimi unajua huwa situnzi za hao' kwa hiyo ni kitu kama hicho. Kama ni hivyo, Mheshimiwa Balozi nadhani hapo ilipo itakuwa ipo sawa ikisomwa na ile 32.

Mheshimiwa Balozi karibu umalizie hoja yako.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa kabisa *observation* zako ambazo umeziweka, sasa kwenye hiyo *schedule* haipo *clear* na ndiyo maana nikaongeza *the only cases reported* kwa Mkemia Mkuu, lakini ukiiweka kama hivi ilivyo ina maana kwamba anatakiwa atunze *data* zote ambazo ziko hapa hata na hizi *criminal offences* ambazo hawezi kuzipata. Hata ukisema unaenda kuzitafuta Polisi au *Prisons* hawawezi kukupa hizi, watakwambia unazitaka za nini, zinakuhusu nini wewe Mkemia Mkuu? Kwa hiyo, ni hayo marekebisho madogo tu ambayo nafikiri Mheshimiwa Waziri ajaribu kuyaelewa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi, ukienda 32(1) nadhani inatoa hiyo picha kamili kabisa. Nadhani katika usomaji wa kawaida utakuwa umekaa vizuri. Yale mapendekezo yako ukisoma 32(1) kwa sababu hii *fifth schedule* ni lazima usome na ile 32. Ukizisoma hivyo unapata picha kwamba ni taarifa zile alizopelekewa yeye. Kwa hiyo na zingine ambazo atakuwa ameweka vizuri.

Mheshimiwa Adadi umekubali nataraji!

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri nimekubali kwa maelezo ya jopo lote hilo, kwa hiyo nimekubali tuendelee.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Balozi Adadi. Sasa nitawahoji.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imekamilisha kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (*The Government Chemist Laboratory Authority Act, 2016)* Kifungu kwa Kifungu pamoja na marekebisho yake na kuukubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu pamoja na marekebisho yake sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka *(The Government Chemist Laboratory Authority Bill, 2016)***

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hongera. Sasa natangaza kwamba Muswada huu ambao tulikuwa tunaupitia katika Kamati ya Bunge Zima umekwisha kupita, sasa utasubiri Mheshimiwa Rais aweke saini kwa mujibu wa Katiba. Kwa hiyo, hongera sana Mheshimiwa Waziri, sasa tunaendelea na hatua inayofuata. Katibu!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI- KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI- KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi Wanataaluma wa Kemia, 2016**
***(The Chemist Professionals Bill, 2016)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pendekezo langu ni katika *sub clause* ya (7), napendekeza kwamba maneno: *of whom at least three shall be women* kwa wale wanaoteuliwa kuingia kwenye hii *Council* yawekwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu sasa hivi kuna *tendency* ya uteuzi maana hii ni *professional body* na nadhani mapema leo hii nilimsikia Waziri Ummy akisema kwamba hii ni *category* ya *professional body,* wanawake kulinda hapa kuonesha kwamba *gender balance* inapatikana, wakati mwingine sheria zisaidie mamlaka ya uteuzi, ziwawezeshe wanawake wasisahaulike, katika *profession* hii *Chemist* wako wengi lakini unaweza kukuta kwamba wanakuwa *put by the way side.* Kwa hiyo pendekezo langu ni kwamba angalau Wajumbe watatu wawe wanawake wenye sifa *of course,* lazima sheria isaidie wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya!

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mama Tibaijuka na nataka kumthibitishia Miswada hii imeletwa na Waziri Mwanamke Mwanaharakati. Kwa hiyo, kwenye *schedule of amendments* ambayo tume-*move* tumeweka *sub clause (9) in appointing members of the Council and Committes the Minister or Council shall consider gender representation and senior members.*" Nadhani ina-*take into consideration* hoja yako Profesa Mama Tibaijuka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba *amendment* ya Serikali imekuja inatusaidia, lakini *amendment* yangu nimehakikisha kwamba angalau wajumbe watatu wanakuwa wanawake. Naomba suala hili ni la msingi kama ilivyo hata kwa Bunge hili na mahali pengine pengi ni *affirmative action, affirmative action* ni lazima sasa kama Bunge tuelekeze kabisa *categorically,* haiwezi kuachiwa tena kwenye *discretion* ya Waziri wakati unajaribu kuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jamani nadhani jambo hili kwa sababu *it is a bit late* lisitucheleweshe, ni utamaduni ambao tunao. Bunge hili lenyewe lina *affirmative action* ambayo imetuwezesha kuwa humu, kwa hiyo naomba hao watu watatu wapatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa sana Profesa Mama Tibaijuka, lakini ningependa kwenda na marekebisho ambayo Serikali imeyaleta kwa sababu hiyo ungesema angalau, mimi ningependa Waziri akiamua tu kwamba anaweza akawa na wanawake watano wanaume wawili, kwa hiyo tuiache tu Waziri mwenyewe afanye maamuzi lakini anabanwa kwamba lazima a-*take into consideration gender representation.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Tibaijuka malizia hoja yako.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kuchelewesha hoja Mheshimiwa Waziri Ummy anajua ninachokisema. Leo tunamwombea na tunajua kwamba atakuwa pale kwa muda mrefu sana, lakini hiki kitu ni muhimu sana hawezi tu kuachia tu *discretion* ya Waziri, hapa Bunge limwongoze Waziri na *amendment* yangu haisemi watatu, inasema *at least,* kwa hiyo wanaweza wakawa sita, wanaweza wakawa watano, lakini angalau watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, au nitoe hoja Bunge hili lijadili, nafikia kwamba, basi natoa hoja kwamba tujadili kama Waziri hajaridhika.

**MWENYEKITI:** Kwa hapo tulipofikia Mheshimiwa Tibaijuka hakuna mjadala isipokuwa ni kulihoji Bunge. Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali mapendekezo ya Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kwa sababu hii ni *professional body,* kwa hiyo ni kweli angalau wajumbe watatu wasipungue wanawake. Kwa hiyo wanaweza wakawa wanne, watano, sita, angalau. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekti, nakushukuru. *Amendment* yangu iko kwenye *clause* 4(4) ambayo inasema *by adding*

*immediately after the word council appearing at the end of the clause;* napendekeza kuongeza haya maneno: *except that if the matter is against the Government then the Attorney General shall refrain from the matter.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kabisa kwamba Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 59(3) kuna Mamlaka aliyopewa pale na ni mdau mkubwa sana katika Serikali na kuishauri Serikali, pia tutambue kwamba hili Baraza la Wanataaluma wa Kemia, Naibu Waziri alitamka bayana kwamba inachukua ambao ni Watumishi wa Umma lakini pia inachukua na kwenye Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia hili Baraza pale ambapo kutakuwa labda kuna shauri au kesi dhidi ya Serikali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa *side* ipi? Ikitokea Baraza likawa na shauri dhidi ya Serikali. Kwa hiyo, napendekeza kama mtaona inafaa tuongeze hili neno, hii sentensi kwamba, *except that if the matter is against the Government then The Attorney General should refrain from that matter.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mashauri mengine yote kama kuna Baraza dhidi ya watu wengine na vitu kama hivyo tunaweza tukamhusisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunavyosema kila mtu yuko sawa mbele ya sheria, maana yake hata pale Serikali inavyoshtakiwa Mahakamani na yenyewe pia ina haki ya *representation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo Wakili wa Serikali, Serikali haina Wakili mwingine, sasa kwa mujibu wa *The Government Proceedings Act,* suala lolote ambalo linahusu *Institution* yoyote ya Kiserikali *automatically* Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaingia, kama sikosei kuna *amendment* ilikuja ku-*clarify* hapo katika miaka ya karibuni. Kwa hiyo, ikawa imeongeza nguvu ya ile *Government Proceedings Act.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kinachosemwa hapa, *well,* labda watu wanaamini kwamba *AG* akiingia tu tayari *right* yao imekuwa *hindered,* sidhani kama ni *presumption* sahihi na italeta *something which is very alien to the normal practice with laws in the Country.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nipate ufahamu zaidi. Hili Baraza la Wanataaluma wa Kemia ni Taasisi ya Kiserikali au *it is an entity* kama inavyokwenda kuwa *TLS, if that's the case,* kama mmeruhusu na watu binafsi, wanataaluma wa kemia kutoka sekta binafsi wanaingia kwenye Baraza, bado mtaita hii ni Taasisi ya Serikali? Bado Mwanasheria Mkuu anatakiwa a-*intervene*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza zaidi, ikitokea kuna shauri, Baraza lina malalamiko dhidi ya Serikali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali utakuwa *side* ipi? Uta-*stand* na Baraza au uta-*stand* na *Government* ambayo ndiyo *role* yako kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uwepo wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye Mabaraza haya wala siyo suala la mjadala ama la kubishaniwa, kwa sababu ni kama vile ni kitu *generic* tu. Mabaraza yote ya taaluma yaliyopo chini ya Wizara ya Afya yana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama Mjumbe. Msingi wa kumweka pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kile anachokiuliza Mheshimiwa Matiko kwamba je, Baraza hili bado tu lina Serikali kwa sababu tu limeleta wajumbe kutoka kwenye *private sector.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza hili bado ni chombo ambacho kinafanya kazi chini ya Waziri, Waziri atakayekuwa na dhamana ya mambo ya Afya anasimamia Sera ya Afya, kwa msingi huo Mabaraza haya yanaanzishwa kutokana na Sera ya Afya na kwa msingi kwamba yanaanzishwa kutokana na Sera ya Afya, maana yake yako chini ya Waziri wa Afya. Kwa maana hiyo sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama Afisa ambaye ana majukumu ya kuishauri na kuisaidia Serikali kwenye mambo yote yale ya kiufundi yanayohusu sheria ni lazima awepo mle ili aangalie maslahi ya Serikali ndani ya Baraza hilo. Kwa hivyo, hatuwezi kwa namna yoyote ile kumtenganisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mabaraza ambayo ni taasisi zilizo chini ya Waziri anayesimamia sera ya Afya kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni muhimu sana kwenye Baraza hili, hata kama tumeamua kusema kwamba basi kwenye Baraza hili tukubali Wajumbe kutoka Sekta Binafsi nao waingie mle ndani. Wale wanaingia tu kama Wajumbe wala haimaanishi kwamba wanakwenda kuwakilisha *private sector,* hapana, wanaingia mle kama Wajumbe wengine ambavyo wanaingia, Mwanasheria Mkuu wa Serikali

anaingia mle kama Wajumbe wengine wanavyoingia lakini yeye ana dhamana ya kuangalia maslahi ya Serikali kwenye Baraza hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko malizia hoja yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hawajanielewa nilivyosema, sijamwondoa kabisa Mwanasheria Mkuu kuwa ndani ya hii au ku-*intervene* kwenye *matter,* ila nimesema itakapotokea kuna shauri dhidi ya Serikali basi kwenye shauri hilo Mwanasheria Mkuu asihusishwe, pale ambapo itatokea siyo kwenye kila *activity* zote ambazo zinaendelea, ikitokea kuna shauri dhidi ya Serikali basi Mwanasheria Mkuu awekwe pembeni *by then*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko, nadhani mwanzo uliuliza maswali mawili kwamba je, hii ni Taasisi ya Serikali au ni Taasisi kama taasisi zinazoendesha wataalam kwenye maeneo fulani, ukataja mfano wa Chama cha Wanasheria nchini *(TLS)*. Kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba chombo hiki kiko tofauti na Chama kama *TLS,* hiki ni cha Serikali, kwa hivyo huyu Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo tu, hawezi kukimbiwa *whether* wao wanashtaki ama yeye ndiyo anashtakiwa vyovyote vile, yeye lazima awepo kwa sababu ni chombo cha Serikali, kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri maana yake ni kwamba hakwepeki kwa sababu ni chombo cha Serikali, ni tofauti na hivyo vingine.

Nadhani amekubali kwamba sheria hii inahusu chombo hiki ambacho kiko chini ya Waziri, baada ya kusema hayo Mheshimiwa alishaleta hoja yake kwa hivyo nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ili nisije nikasahau vipengele vingine kama ule Muswada wa kwanza *clause* (4) nimeangalia marekebisho ya Mheshimiwa Waziri kile kipengele cha 4(7) kinasema kwamba *the council shall consist of nine members to be appointed by the Ministers as follows:* katika *amendment* za Serikali wameongeza badala ya *a representative* wameongeza ikawa tu *representatives that means* uki-*totalize* wanakuwa ni 10 *members instead of nine*, kwa hiyo nilikuwa nafanya marekebisho badala ya kuwa *nine members* sasa wawe 10 *members.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kwenye *paragraph* (f) ya *clause* hiyo hiyo inasema *a Law Officer representing the Attorney General,* mapendekezo yangu

nikizingatia kwamba hiki ni chombo kikubwa sana ni Baraza kubwa na ukiangalia kwamba kwenye sehemu nyingi wameweka ni *Senior Officer* ili wakati wanafanya maamuzi yawe ni maamuzi ambayo hayahitaji tena uende kusema kwamba lazima nimlete mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikafikiri kwamba kuna haja ya kuweka a *Senior Law Officer representing the Attorney General* ili kuwa na ile *sequence* ukiangalia pale (h) ni *a Senior Officer representing Public Service Management,* ukija pia kwenye Polisi unakuta ni *a Policy Officer of a rank of Inspector or above representing the IGP.*

Kwa hiyo, nadhani tukiweka 'a *Senior*' inakuwa rahisi, inakuwa ina-*fall* hapo, lakini vilevile kwenye suala zima la maamuzi kwa sababu wanaweza wakafanya maamuzi, kwa hiyo, kama ni mtu ambaye siyo *Senior* anaweza akasema labda mpaka nikamwite fulani. Kwa hiyo, nadhani kuna haja pia ya kuweka hivyo ili kuleta ulinganifu au kuzingatia hiyo *Seniority* katika hili Baraza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Susan Lyimo, tukienda kwenye kwanza amezungumza tu *general,* amei-*relate* na *sub clause* (7)(c) kwamba mwanzoni tuliweka *representative of an umbrella society,* lakini tumeweka *two,* kwa hiyo ni kweli *in total* watakuwa 10, kwa hiyo tunakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili anapozungumza kwamba kwenye *a Law Officer representing the Attorney General* nilikuwa nashauriana hapa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuna Sheria ya Tafsiri *(Law of Interpretation Act),* inazungumzia pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwenye hii sheria inasema *Law Officer* ni Mwanasheria Mwandamizi ambaye ni *Senior,* kwa hiyo hatuoni haja ya kusema lazima awe *Senior,* iko *covered* ukienda kwenye *Law of Interpretation Act*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kama hiyo kwenye *interpretation* ipo, basi hamna sababu. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mapendekezo ya Mheshimiwa Suzan Lyimo katika kifungu cha 4(7) marekebisho maneno tisa kuweka 10 yamekubaliwa, kwenye (f) ndiyo ambako hayajakubaliwa lakini Mheshimiwa Suzan Lyimo amekubaliana nayo kwa sababu hiyo sasa nitawahoji. Kifungu namba 4 pamoja na marekebisho ya

Serikali na Mheshimiwa Suzan ambayo yamekubaliwa na Serikali kifungu hiki kinaafikiwa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwenye kifungu namba 9(1) napendekeza kufutwa kwa hicho Kifungu kidogo na badala yake tuweke haya maneno: (1) *The Council shall ensure fair and justice competition for a position of Principle or Senior Chemist with a minimum requirement of Master Degree to be the Registrar of the Council.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba tulishaafiki hili Baraza linakuwa linachukua wataalam kutoka kwenye sekta ya umma lakini pia binafsi. Napendekeza kufutwa kwa *clause* hii kwa sababu inampa mamlaka Waziri kumteua Mkemia Mwandamizi anayetokana na Watumishi wa Umma. Tunapotunga hizi sheria tunatakiwa tujitahidi kuondoa ubaguzi na kama tumesharuhusu kwamba tutakuwa tuna *composition* ya watu kutoka kwenye sekta binafsi, kwa nini sasa tusiruhusu tu ushindanishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikitokea huyu Mkemia Mwandamizi anakuwa ni mtu kutoka sekta binafsi *well and good* au ikitokea huyu Mkemia anakuwa ni mtu kutoka ndani ya utumishi wa umma pia iwe sawa, tusiji-*limit* kwamba lazima atokane na utumishi wa umma, tuache iwe wazi, aidha awe mtaalam kutoka sekta binafsi au kutokana na utumishi wa umma*, provided* sasa atakuwa na sifa

ambazo zinakidhi, tusijifungie na kusema kwamba lazima awe mfanyakazi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mapendekezo ninayoya-*suggest*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko yanataka tufungue milango kwamba Mheshimiwa Waziri anaweza akamteua Msajili wa Baraza la Wakemia kutoka ndani ya utumishi wa umma ama hata kwenye sekta binafsi, kwa msingi kwamba Baraza hili kwanza ni chombo cha Serikali na kama ni chombo cha Serikali maana yake kinafuata taratibu za utumishi za kuwapata watendaji ndani ya Serikali ambapo ni lazima Watendaji hawa watokane na utumishi wa umma wenyewe kwa kipindi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi hii tunayoizungumzia ya Msajili wa Baraza la Wakemia ni nafasi nyeti, kwa sababu huyu ni Mtendaji Mkuu wa Baraza hili, ndiye *CEO* wa Baraza hili la Wakemia na kwa vyovyote vile tunaona kwa unyeti wa Baraza lenyewe kwa kazi za Baraza za kila siku na kwa ukweli kwamba Serikali ina utamaduni wake wa kufanya kazi tunaona ni vema Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anateua Msajili basi ateue miongoni mwa Watumishi wa Umma ambao wana sifa zilizotajwa kwenye mapendekezo ya sheria yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, tunaona kwamba mapendekezo yake tuendelee kuyakataa tubaki na mapendekezo yaliyoletwa na Serikali kama yalivyokuwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko malizia hoja yako!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi nicheke tu kwa sababu Naibu Waziri unasimama kabisa unasema kwa sababu ya unyeti inabidi huyu mtu atoke Serikalini. Sijui ni unyeti gani ambao umemaanisha *by the way,* zaidi tumesema *requirement* awe na *Master Degree do you doubt* watu wanaotoka kwenye sekta binafsi kwamba ukimwa-*assign* hiyo kazi ya usajili hawezi akafanya, hiyo kazi nyeti ambayo unaizungumzia? *That is why we say* Serikali mnakuwa *like an instruction arm* katika hili Baraza. Kwa sababu kama tumeridhia humu ndani kwamba awe anatoka sekta binafsi au mtumishi wa umma, *why do you then* unajikosoa mwenyewe kwamba ni lazima tena awe mtumishi wa umma kwa sababu kuna unyeti, *what are you hiding,* mnaficha nini *Government*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, turuhusu iwe na *fair competition that is all*. Ni kitu kidogo tu! Kama tayari mna hiyo na Waziri ndiyo ameshapewa hayo mamlaka

*definitely* mtaenda kumchagua huyo wa umma kwa sababu mmeshaiweka kwenye kichwa chenu kwamba lazima atokane na umma, lakini angalau sheria ieleze kwamba anaweza akawa wa umma au sekta binafsi, naomba sana na Wabunge tulione hili kuongeza tu kwamba atokane na umma au atokane na sekta binafsi, *provided* tu ana hizo sifa, kuna ukakasi gani, huo unyeti ni unyeti gani.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, alikuwa anahitimisha hoja yake Mheshimiwa Matiko katika Kifungu cha (9) sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Owenya.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.
Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Kifungu namba 12 kifutwe chote na kisomeke kama ifuatavyo:

*"The Members of the Council shall be paid, with annual increment such as salaries and allowances as per Government salary scales and financial regulations depending on their level of qualification and experience.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kifungu cha kwanza kabla ya marekebisho kinasema Mheshimiwa Waziri atashauriana kwanza na Hazina ili waweze kufanya malipo ya hawa *members of Council,* lakini Mheshimiwa Waziri anaweza akaamua analipa milioni moja kwenye kikao kimoja, kikao kinachofuata akalipa milioni mbili wale *members* wasipomfurahisha anaweza akaamua analipa shilingi 20,000. Kwa hiyo ni vizuri tukafuata sheria na Serikali ina *scale ya salaries* na hizo *benefit,* kwa hiyo ni vizuri tukaiweka kisheria ili Mheshimiwa Waziri asije akaitumia nafasi yake vibaya. Mheshimiwa Waziri nafikiri umenielewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12 kinapendekeza kwamba Wajumbe wa Baraza pamoja na wale wa Sekretarieti walipwe posho kwa mawasiliano ambayo yatafanywa kati ya Waziri na Msajili wa Hazina *(Treasure Register)* na wataamua hivyo kadri watakavyoona inafaa kwa nyakati tofauti tofauti. Mapendekezo ya Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya yanataka kuzungumzia kwamba Wajumbe wa Baraza walipwe mishahara kwa mujibu wa *Government Salary Scales.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza siyo waajiriwa hawapo kwenye ajira rasmi za Serikali, kwa maana hiyo mambo yote yanayohusisha *Government salary scale* hayahusiki kwa Wajumbe wa Baraza kwa sababu hawa ni wajumbe ambao wanakutana *from time to time*. Pengine kwa mwaka wanaweza wakawa wanakutana kila *quarter* mara moja na kwa maana hiyo watakapokutana pale ndiyo watapaswa kulipwa posho siyo mshahara. Kwa hiyo anachokipendekeza Mheshimiwa Lucy Owenya hakikubaliki kwa sababu hawa siyo waajiriwa na wataendelea kulipwa posho kadri ambavyo Waziri mwenye dhamana na mambo ya afya atawasiliana na Msajili wa Hazina *from time to time.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Owenya.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama siyo *salaries* basi hizo posho ziwe na viwango kwa sababu Serikali ina viwango vya posho, haiwezekani Waziri aamue tu kwa kuwasiliana na *Treasurer* aamue kwamba ni shilingi ngapi anatoa, kwa nini zisiwe kisheria hata sisi tulivyokaa hapa Bungeni kuna sheria zinazotulipa posho, kwa hiyo na hao lazima walipwe posho kutokana na *Government Scale.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kama Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya anakubaliana kwamba siyo mishahara lakini anataka iwekwe hapa ni hatari sana ku-*specify* posho za Wajumbe wa Baraza kwenye sheria ambayo inatungwa na Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu kama ambavyo inaweza ikajitokeza wanataka kubadilisha posho kama ambavyo labda taasisi zingine zimefanya mabadiliko ama wao wenyewe *income* yao imeongezeka wanataka kuhudumia posho ndani ya Baraza lao

utaratibu wa kusema iwepo kwenye sheria utakuwa mrefu sana na kwa hivyo itawafanya wapate ugumu sana wa kubadilisha malipo haya ya posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiachwa hivi ilivyo sasa, kutakuwa kuna fursa ya wao kwenda kujenga hoja kwa Waziri mwenye dhamana na mambo ya afya na yeye akawasiliana na *Treasury Registrar* kama ni posho zikaongezwa kuliko kuzi-*fix* hapa kwenye sheria. Pia kama kutakuwa kuna haja hiyo wakati Kanuni zinatungwa Mheshimiwa Waziri anaweza hizo posho akazi-*state* kule akishirikiana na wadau ndani ya Kanuni lakini siyo kwenye hii sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani hoja yake hakumaanisha uandike hapa kiasi, lakini alitaka hapa pataje kwamba watalipwa posho ya kiwango cha Serikali.

Nirudi kwa Mheshimiwa Lucy Owenya, kifungu hiki namna kinavyosomeka kwa sasa hivi ziko sheria nyingi ambazo zimemtaja huyu *Treasury Registrar* kama ndiye *custodian* wa *properties* za *Government* kwa sababu yeye ndiye anayeangalia haya masurufu wanayolipwa wote wanaofanya kazi kwenye Taasisi za Umma. Kwa sababu hiyo nadhani ndiyo maana ametajwa hivyo kwa sababu sheria nyingi sasa hivi zinataka yeye ndiye aangalie mwelekeo wa mali za Serikali na aangalie viwango mahususi vya kuweza kulipa hawa watu kwa kushirikiana nao. Kwa hiyo, nataka tu kuliweka hilo hivyo halafu umalizie hoja yako tuweze kuendelea.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunisaidia, lakini sioni tatizo kuongeza sentensi ya kusema kwamba, watawapa posho *according to* viwango vya Serikali. Hata kama wakati huo ikifika vimebadilika itakuwa Serikali nzima kwa hiyo, itabadilishwa *according to* wakati huo Serikali imesema ni kiwango gani, kuliko kuiacha tu ina-*hang* namna hii.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lucy Owenya ameshaleta hoja yake, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko, Kifungu cha 14!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kifungu cha 14(1), napendekeza kuongezeka kwa maneno yafuatayo: *by adding words at the end of the sentence, from any recognized institution,* kisomeke kwamba:

"*A Chemist shall not be registered as such unless the Council is satisfied that he has undergone internship training for a period of one year from any recognized Institution.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza tuweke hivyo pamoja na kwamba, tumesema lazima huyu Mkemia awe amefanya mafunzo kwa vitendo kwa muda wa mwaka mmoja, lakini tusiiache ielee tu. Anaweza akafanya mafunzo kwa muda wa mwaka mmoja ya vitendo, lakini kwenye chuo kipi, chuo ambacho kinatambulika au taasisi ambayo inatambulika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza mazoezi kwa vitendo hayafanyiki kwenye chuo kwa sababu, siyo mafunzo ambayo yanatahiniwa, ni mazoezi ambayo mtu anayafanya ili kupata uzoefu wa taaluma ambayo ameisomea na amepata *degree* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya anayafanya ili a-*qualify* mahitaji ya kuwa *professional* kwenye fani husika, kwa maana hiyo kwa kuwa, anapokwenda kule kwenye hiyo Taasisi, haendi yeye mwenyewe kwa kuchagua atakuwa *posted* na Msajili. Atakuwa *posted* kwa maana nyingine kwenye Taasisi ambazo zinatambulika na Ofisi ya Msajili. Kwa sababu, anapewa barua kwamba, wewe unatumwa uende kwenye Maabara ya *TFDA,* wewe unatumwa uende ukafanye mazoezi kwa mwaka mmoja kwenye Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, wewe unatumwa uende *for internship* kwa mwaka mmoja kwenye Maabara ya *Tanzania Breweries.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, anatumwa kwenye maabara fulani na Msajili wa Baraza ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Baraza na ndiye atakayekuwa anawasajili. Kwa hivyo, hakuna *chance* kwamba, atatumwa kwa barua kwenda kwenye maabara ambayo haitambuliki ama kwenda kwenye taasisi ambayo haitambuliki. Kwa hivyo, kuongeza maneno from a *recognized institution* ni kuongeza maneno ambayo yako *redundant* ambayo hayaongezi chochote wala hayapunguzi chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, tunaomba ibaki kama ilivyo kwa sababu, mapendekezo yake hayabadilishi chochote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema anatumwa na Msajili, hapa inasomeka kwamba, *a Chemist shall not be registered!* Kama bado hajasajiliwa anawezaje akatumwa na Msajili? *Shall not be registered unless* awe amefanya mafunzo ya vitendo kwa mwaka mmoja! '*shall not be registered'* sifa mojawapo ya kum-*register* awe ame-*qualify* kwamba, ameshafanya mafunzo kwa vitendo. Naibu Waziri anavyoniambia kwamba, Msajili ndiye anayemtuma akafanye mafunzo kwa vitendo, hii *clause* inasema *shall not be registered!* Huoni kwamba, *it is a contradiction?*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, akisoma ile *Sub Section (2)* ya Kifungu hicho inasema kwamba, zitatungwa Kanuni ambazo zitaelekeza, zitaweka utaratibu wa namna ambavyo hawa *Chemist Professionals* ama *Chemist Graduate* ambao wataenda kufanya mafunzo hayo ya *internship.* Maana yake ni kwamba, kiutaratibu kwanza, nafikiri haelewi hata utaratibu wenyewe ulivyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ni kwamba, ukihitimu *degree* yako ya Kemia, umeshapewa cheti pale *University of Dar-es-Salaam* au *UDOM,* una cheti chako mkononi cha kwanza utakachokifanya baada ya kuwa sheria hii imepitishwa na Msajili yupo na ofisi yake ipo, utatakiwa uchukue cheti chako uende kwenye Ofisi ya Msajili. Ukifika kwenye Ofisi ya Msajili umwambie nimemaliza kusoma *degree* yangu ya Kemia, sasa nataka kufanya mafunzo yangu ya *internship;* kwa hiyo, ndiyo pale sasa yule Msajili atakupangia kituo cha kwenda kufanya *internship.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni utaratibu wa kawaida, kama vile Baraza linalosajili Madaktari. Kwa mfano, sisi tulipomaliza masomo yetu ya udaktari, tunaenda kuripoti pale kwa Msajili wa Madaktari. Msajili ndiyo anatupangia vituo vya kwenda kufanya *internship,* wewe utaenda Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, wewe utaenda Hospitali ya Muhimbili, wewe utaenda Hospitali ya Mwananyamala. Sasa kwa kufuata utaratibu huo ndiyo maana nikasema nilichokisema Mheshimiwa Matiko kwamba, hawa wakimaliza masomo yao, ili waende *internship* watatakiwa wachukue nyaraka zao kutoka kwenye Chuo ambacho kinatambuliwa na Msajili kwenda kuripoti pale kwake, yeye ndiye atawapangia mahali pa kwenda kufanya hii *internship.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawajasajiliwa ndiyo, wataanzia wapi! Hapana, ili wakafanye hiyo *internship* yenyewe watapewa usajili wa muda, unaitwa *provisional registration,* watasajiliwa kwa muda wa mwaka mmoja ili waruhusiwe

kushika kemikali, ndiyo uratatibu ambavyo utakuwa na utawekwa kwa mujibu wa Kanuni hapo baadaye.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umetaja Vyuo vya Serikali tu hapo, ndiyo yale tunayosema! Mbona hujataja vyuo vya *private?*
Mheshimiwa Esther Matiko naomba uhitimishe hoja!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya Naibu Waziri, *I go with it.*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, Kifungu Namba 22!

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia marekebisho ya Serikali kwenye kile Kifungu 22(2), nakubaliana na marekebisho ya Serikali, lakini 22(3) kwa kuwa, maelezo niliyoyatoa wakati ule tunapitisha ule

Muswada mwingine yanafanana na hili, nimependekeza kuongeza *Directors report* katika ile *list* ambayo ilikuwa imetolewa pale, nafikiri Serikali itakubaliana na maelezo yangu, naomba niwasilishe.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayakubali mapendekezo yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kifungu cha 22 pamoja na marekebisho ya Serikali na Mheshimiwa Hasunga.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 23

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, Kifungu cha 23!

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Serikali imerekebisha kile kifungu, kwa hiyo, nakubaliana na marekebisho.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 28

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka!

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa marekebisho yangu katika *clause No. 2(c)* ya 28, napendekeza kwamba, haya maneno ya mwisho, huyu mtu ambaye amewahi kuwa *convicted of an offence under this Act,* hiyo sawa kwa sababu ya *nature* ya *profession* yenyewe. Sasa *convicted of an offence under this Act or any other written law!*

Hapa najielekeza pia kwa Mwanasheria Mkuu, labda kwa sababu ya uelewa wangu mdogo wa sheria! Nafikiri mtu ambaye aliwahi kumpiga mtu ngumi akiwa kijana akawa *convicted,* sasa anajaribu kupata hizi nafasi, hii sheria hapa inamwondoa, kama nimeelewa vizuri kama nimeelewa vibaya, nipate mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja yangu ndiyo hiyo. Kwamba, hiki kitu kiko *too broad* na nadhani *it is unnecessary.* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya!

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jedwali la Marekebisho tumezingatia hili suala, kwa hiyo, tumefuta yale maneno *or any other written law*. Kwa hiyo, Mwanataaluma wa Kemia anaweza akaadhibiwa endapo amekuwa *convicted* na makosa ambayo yamesemwa ndani ya sheria hii, siyo sheria nyingine, kwa mfano labda unaweza ukawa umemgonga mtu, *traffic offence and then* ukafutiwa, kwa hiyo, haihusiani tena, tumefuta.

**MHE. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kama hivi ndivyo ilivyo nami basi nimeridhika, tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka!

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa pendekezo langu ni kwamba, badala ya kutumia neno *fails,* tutumie *refuses without reasonable cause*. Nimetumia hii *phrase refuses without reasonable cause* kwa sababu, nimeiona katika vipengele vingine vya sheria hii. Ni *technical issue,* nafikiri kwamba, ni *much better*. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *observation* nzuri. *Sometimes* huwa tunatumia *fails without reasonable cause or refuses without reasonable cause*. Kwa uandishi mzuri nadhani *fails without reasonable cause is much better,* kwa sababu *refuses* tayari ina *negative connotation*. Kwa hiyo, tukisema *refuses without reasonable cause* kuna *somehow* namna ya kama *repetition!* Kwa hiyo, *fails without reasonable cause is acceptable*.

**MWENYEKITI:** Hebu ngoja tuelewane vizuri! Kwa hiyo, inayobaki ni *fails* ama *refuses without reasonable cause?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, *fails without reasonable cause*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka!

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee nakubali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 34

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja!

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Naomba kufanya marekebisho kile Kifungu cha 34 kiondolewe chote na kisomeke kwamba:

"*If a person is not satisfied with a decision of the Council under this Act, shall have the right to appeal to the High Court of The United Republic of Tanzania.*

Kifungu hiki kinasema kwamba, kukiwa na malalamiko yoyote mwenye malalamiko aende akalalamike kwenye Baraza na kama hataridhishwa, basi malalamiko ayapeleke kwa Waziri na Waziri ndiye mwamuzi wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri, ili kuondoa malalamiko yasiyokuwa na msingi, ili kuondoa wasiwasi na mlalamikaji aweze kuwa na haki ya kwenda Mahakamani na kupata haki hiyo. Kuna mambo mengi ambayo yanaweza yakajitokeza, Waziri akiwa ndiye maamuzi ya mwisho, Waziri anasimamia taasisi, endapo malalamiko yatafika kwa Waziri, pengine yanahusu watu ambao wako

kwenye Wizara yake, kwa hivyo, kutakuwa na *conflict of interest.* Ili kuwa wazi na kuwapa watu fursa ya kuondoa hofu na wasiwasi na kuona wametendewa haki, basi kiwepo chombo, Mamlaka kama Mahakama ambayo ndiyo itakuwa ya mwisho kutoa *decision* badala ya Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kusema taratibu tu kidogo. Kuna *notion* inataka kujengeka Bungeni kwamba, labda Bunge linaweza likatunga Sheria ambayo itakataza mtu kwenda Mahakamani. Ukweli ni kwamba, toka mwaka 1971 Mahakama zilishaamua hakuna sheria yoyote itakayotungwa na Bunge ambayo itakataza mtu kwenda Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala hapa ni anaenda vipi Mahakamani na katika mazingira yapi! Anakwenda kwa rufaa na matokeo yake yatakuwa ni nini au anakwenda kwa marejeo *(review)* matokeo yake yatakuwa ni nini? Ili kupata uelewa mzuri hapo, tujielekeze kwenye Kifungu Na. 28. Kwa mfano tu 28(2)(b) au 28(2)(d), moja ya maamuzi ambayo yanaweza yakalalamikiwa ya hiyo *Council* ni kwa kum-*declare* mtu *incompetent* kwamba, wewe hukidhi vigezo, huna viwango, suala la kitaalam kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pale ambapo *Council* inaweza ikam-*declare* mtu kwamba, yuko *unfit for practice* kwa sababu tu, ukisoma 28(2)(d)kwamba, amekutwa na hatia ya makosa ya kutokuwa mwaminifu au makosa ya wizi wa kalamu au makosa, hapa wametumia neno *moral turpitude.* Kwa maana hiyo, tunaweza tukawa tuna *situation* kwamba, Mahakama inaambiwa kwa upande wa rufaa iseme mtu anakidhi viwango au la vya kitaaluma! Suala ambalo siyo la kawaida sana au Mahakama inaambiwa iangalie rufaa inayohusiana na maamuzi ambayo mtu alikuwa *declared unfit for practice* kwa sababu, huko nyuma alishakutwa na hatia, labda ya kufanya unyanyasaji wa kijinsia ambayo tayari ina mwenendo wake wa Kimahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siku moja Mahakama Kuu itakuwa inaamua shauri la mtu ambaye alihukumiwa labda Kisutu halafu Bodi inakwambia kwa sababu, wewe ulibaka au ulifanya *sexual harassment you are not fit to practice!* Mahakama tena inataka kuyaleta hayo mambo. Kwa maana hiyo tukienda huko tutakuwa kama tunafufua, siku hizi kuna usemi unasema makaburi, lakini kuna namna nyingine kweli inawezekana Bodi ilikuwa iko *biased!* Yawezekana Bodi haikuwa *properly constituted!* Yawezekana Bodi haifanyi kile ambacho inatakiwa kufanya kwa sheria!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama hapo kazi yake haitatakiwa kusema kwamba, huyu mtu yuko *competent* au la! Mahakama itabidi iseme hii Bodi

ikae, hii Bodi impe huyu mtu haki ya kusikilizwa, hii Bodi itekeleze wajibu wake wa kisheria! Hayo ndiyo yale mambo ambayo siku zote yanakwenda kwenye utaratibu wa *Judicial review*. Kwa hiyo, haki ya kwenda Mahakamani ipo na haiwezi ikavunjwa na Bunge hili kwa mujibu wa sheria zetu tulizojiwekea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja! Kuna namna mbili, Mheshimiwa Devotha Minja, aidha wewe usiongee aongee Mheshimiwa Halima Mdee! Ama uongee wewe mwenyewe kwa sababu, yeye atakuwa hachukui nafasi yako, kwa hiyo chagua! Naona amesimama hapo nyuma yako.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu iko kwamba sasa kama suala la Mahakama lipo wazi kwa mtu wa kawaida ambaye hana hii *knowledge*, kwa nini hii sheria isiseme hivyo kama ilivyokuwa kwenye ile ya Mkemia? Kwamba endapo mtu hataridhika na maamuzi ambayo Baraza limeyafanya, tukumbuke hawa *professionals* wao Waziri anaweza akawa yeye hata siyo *professional* lakini anategemea *advise* kubwa aipate kutoka kwa hawa *professionals*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo Baraza watakachoamua wakimshauri Waziri na Waziri ndicho atakachoamua. Kwa nini sheria isiwe wazi kwa mtu yeyote ambaye hata siyo Mwanasheria aelewe kwamba endapo hatatendewa haki ana hatua nyingine zaidi ambayo itamsaidia kupata haki hiyo badala ya kuzungumza tu, lakini kitu hakipo kwenye maandishi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaweka usawa kwa watu wote mbele ya sheria. Ibara ndogo ya (6) ndiyo inayoeleza hiki ambacho Dkt. Possi alikuwa anakisema hapa. Inasema wakati haki na wajibu wa mtu yeyote inapohitajika kufanyiwa maamuzi na Mahakama au chombo kingine chochote kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu na pia haki ya kukata rufani au kupata nafuu nyingine za kisheria kutokana na maamuzi ya Mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika.

Kwa msingi huu ndiyo maana nakubaliana na ushauri wa Naibu Waziri kwamba hakuna sababu kila unapotunga sheria unataja huyu atakuwa na haki ya kukata rufaa, *that's a Constitutional right, it is there in the law*. Haiwezekani ukatunga sheria kila ukitunga sheria unasema sijui uelezee, hii ni haki yako unayo na utaratibu kwenye haya Mabaraza haya *Quasi-Judicial* ambayo yana asili ya kufanya maamuzi haya, *remedy* iliyopo ambayo huridhiki na maamuzi ya mabaraza haya unakwenda *High Court for Judicial review and this is the simplest procedure* kuliko hii anayoisema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashauri Waheshimiwa sheria tunavyozitunga siyo lazima useme kila kitu. Kwa hiyo, sasa usiposema mtu hawezi kwenda Mahakamani? Bahati nzuri hapa Waheshimiwa Wabunge hatujafunga hatujasema kwamba maamuzi ya Waziri yatakuwa *final.* Kwa mujibu wa maamuzi ya Mahakama yetu ni kwamba na hata Katiba yenyewe tu Ibara ya 107A ndiyo chombo cha mwisho cha utoaji wa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *administrative law* ni kwamba hizo *ouster* clauses yaani zinazoondoa mamlaka ya Mahakama, Mahakama huwa inazipuuza siku zote tu pale. Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana hata ninyi hata kwenye uchaguzi wenu huku ile sheria inasema kwamba maamuzi ya Tume hayatakuwa *questioned,* si ndiyo? Hata hivyo, kila siku mnapeleka Mahakamani *election petition* kwa msingi huo tu kwamba hizo *ouster clauses* haziwezi zikachukua nafasi ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri Bunge naomba mlikubalie hili kwamba hii hata kama haikusemwa hapa ni haki ya kikatiba, huyu mwanadamu atakuwa nayo ya kwenda Mahakamani kupata hiyo fursa ya unafuu anaoutaka. Siyo lazima tutunge kila kitu tunasema ataenda Mahakamani. Dkt. Possi ameeleza moja yaliyopo kwenye Ibara ya 28, hivi yale unakwenda Mahakamani ili kufanya nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali naomba umalize tafadhali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devota Minja naomba umalizie hoja yako.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza *AG;* tunaotunga hii sheria tunajua kwamba ni haki ya mtu, tunachosema kwa faida ya watu na haki itendeke. Kwa sababu kumwambia kila mtu kwamba kila sheria ni lazima ufike Mahakamani siyo hivyo! Tunasema tungeweza tukafanya hivyo ili pia iwe wazi kusaidia watu ambao nao watakuwa wanafanya hii kazi. Kwa maana hiyo ingekuwa tu ni wazi iwe *abided,* mtu ajue kwamba kuna hatua zingine ambazo zinaweza zikamsaidia mtu katika kupata haki zake. Kwa sababu Wabunge tunajua, lakini tufikirie pia na watu wengine ambao hawana huo uelewa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji ni vizuri tu tukajua katika utaratibu huu wa utungaji sheria, hiki chombo ambacho kimeundwa hapa kwa sababu kipo chini ya Waziri maana yake Waziri anatakiwa kupata fursa ya kutolea maamuzi mambo ambayo yamefanywa na chombo hicho.

Kwa hivyo, anakuwa amepewa dhamana ya kile cheo chake kushughulika pia na matatizo katika vyombo vilivyo chini yake.

Jambo la msingi kabisa la kulikumbuka ni kwamba hiki kifungu hakijasema maamuzi ya Waziri yatakuwa ya mwisho, sana kimesaidia kwa kuweka muda kwamba Waziri aamue katika muda gani. Basi yule mtu atapata fursa ya kwenda Mahakamani, bado kwa namna ambayo siyo kwa kwenda kwa kukata rufaa kwa sababu Waziri haamui jambo kama Mahakama. Kwa jambo hili huendi Mahakamani kwa kukata rufaa, unakwenda Mahakamani ili iangalie upya maamuzi ya Waziri, halafu yenyewe sasa itajua kama itayafuta yale maamuzi halafu inalirudisha jambo hilo kwa namna ambayo inategemea itakuwa imeagiza vipi.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo ni lazima tuone hizo tofauti. Unavyosemea rufaa ni lazima uamuzi uwe umetoka kwenye chombo ambacho kinaenda katika mlolongo huo. Baada ya hayo maelezo ya jumla ili tusije tukapata tabu kwenye vifungu vinavyofuata Waheshimiwa Wabunge nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa na mimi ni-*move amendment* yangu. Kwa maoni yangu naona kwamba Kifungu cha 39 kibadilishwe kama nilivyoweka kwenye *amendment* kwamba tuwe na 39(1) and (2).

39(1) iseme: "*Unless proven not guilty in the Court of Laws, any person who commits an offence under this Act shall be liable for that offence*. Pia *39(2)* iseme *without prejudice to the provisions of section 39(1) any person who is*

*convicted under this Act shall be liable to such fines and or imprisonment stipulated in this Act, or as the Court may determine.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye *marginal note* ningeomba au nitapenda lile neno *immunity* liondoke badala yake liwe *replaced* na neno *liability for offences.* Kwa nini nimeleta marekebisho hayo? Ingawa tayari najua nitajibiwa nini, lakini naomba niseme kwamba kwa nini tunatunga sheria ambazo zinawaweka baadhi ya watu juu ya sheria? Kwa nini tumekuwa na *section* 37 ambayo inaeleza makosa na adhabu lakini hapo hapo tunafika *section* 39 tunasema hawa watu wana kinga, tena kwenye Kiswahili labda Kiingereza kinaweza kuwa msamiati kidogo ambao siyo rahisi kuelewa lakini kwenye Kiswahili imesema vizuri; unajua inatamka kabisa "bila kujali suala alilotenda."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaposema tunakuwa na *professionals* ambao tunawakabidhi vitu au majukumu nyeti kama haya, halafu bado tunawapa kinga pasi na kujali kosa ambalo amefanya wala madhara aliyoisababishia jamii au huyo mhusika kwa kweli sikubaliani sana kwamba hii ni sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kama itakupendeza basi mabadiliko haya yafanyike kama ambavyo nimeomba. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hata kama kabaka?

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Vyovyote vile bila kujali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magereli anasema anajua atakavyojibiwa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama ana teknolojia ya kusoma *mind* za watu kabla hawajasema wanachotaka kukisema. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 39 kinahusu kinga, *(immunity)* na kinasomeka kama ifuatavyo kwamba

"*Nothing that is done by the Chairman, Member of the Council, Member of the Committee, employee or any other person authorized to perform, any function under this Act shall, if done in good faith in the performance or purported performance of the functions under this Act, render the member or officer personally liable for that matter or anything done*.

Mheshimiwa Lucy Simon Magereli anakusudia kupendekeza kipengele hiki cha kinga kifutwe chote na badala yake kiwekwe kipengele kingine ambacho kitahusu *liability for offences* na anapendekeza kwamba kuwe kuna adhabu za namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosemwa hapa hata wewe ulikifafanua vizuri sana pale mwanzoni kwenye ile sheria nyingine kwamba "*in good faith*" ni lugha ambayo nyie wataalam wa mambo haya ya sheria mnaitumia sana kwa nia njema. Sasa mtu amefanya kosa bahati mbaya hakuwa na nia ya kufanya kosa; imetokea bahati mbaya kwa nia njema, aidha Baraza lenyewe kwa ujumla wake ama Mwenyekiti wa Baraza ama Ofisa yeyote yule wa Baraza amefanya kosa kwa nia njema aadhibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aadhibiwe kwa nini? Tunatengeneza *precedence* ya kuwafanya watu waogope hata kuwa Maofisa kwenye chombo cha namna hii. Sasa lengo la kifungu hiki ni kuwawekea kinga ili wawe huru kufanya kazi yao kwa uhuru kama ambavyo alisema Mheshimiwa AG pale mwanzoni. Kwa hiyo, hiki kifungu anachokipendekeza kwa kweli ni kitu kipya kabisa ambacho kinalenga kuondoa kinga ya hawa maofisa ambao wametajwa kwenye kifungu hiki cha 39 cha *immunity,* yeye anataka tuweke *liability for offences.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine kwenye hii sheria kuna *offences* zimetajwa na kuna adhabu zimewekwa kwa *offences* ambazo zimetajwa kule. Kwa maana hiyo kusema kwamba tuweke tena hapa kwamba kuna *liability for offences* wakati kuna kifungu kingine ni kurudia kitu kile kile ambacho kimeshawekwa na kifungu kingine cha sheria hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mageleli.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukikubaliana ya kwamba lengo la kifungu hiki ni kuwawekea kinga, naendelea kusimamia msimamo wangu kwamba tunatunga sheria ambayo inawalinda watu au inawaweka watu kuwa juu ya sheria. Kama ni suala la *good faith who determines the good faith? It should be the Court of law.* Maana yake kama tayari kwenye 37 umeshatoa makosa na adhabu *that means* huhitaji sasa kumwekea mtu huyo kinga, kwa sababu ukisema unamwekea kinga kwa sababu ataogopa kuwa afisa wa Serikali kwenye *positions* fulani fulani tukubaliane pia kwamba unamwondolea uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akishajua tayari ana kinga anaweza ku-*commit offence* yoyote kwa sababu tena hata hamjaweka *limit* kwamba ni makosa gani akiyafanya ana kinga, ahh! Pasipo kujali ni kosa gani amefanya, *provided is in good faith, who determines the good faith?* Kwa nini tusiache liende

Mahakamani *the Court of Law will determine the good faith or the bad faith* halafu *from that point* Mahakama itaamua kwamba kosa hili alilolitenda ni kwa nia njema au ni kwa nia mbaya. *Seriously*, hii *clause* itakuwa *abused. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nadhani tufanye maamuzi sasa, hamna namna nyingine naona Serikali haina majibu imekaa, inaona imeshamaliza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Tumechoka choka, tuamue tu.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Hoja zikitoka huko ndiyo zinapokelewa.

**MWENYEKITI:** Sawa, Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho yetu ya Serikali, naomba tena tuingize marekebisho mengine pale kwenye Mamlaka ya Baraza kufifilisha makosa pale, kile kilichorekebishwa kifungu kidogo cha kwanza…

**MWENYEKITI:** Kwenye Kifungu kipi Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kifungu cha 40(1) kama kilivyorekebishwa…

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 40 sijahoji bado hapa

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Hujahoji?

**MWENYEKITI:** Bado

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kuna marekebisho tunataka kuyaingiza…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuelewane kwanza, katika kifungu cha 40 taarifa nilizonazo hapa ni kwamba Serikali ina marekebisho, pia

Mheshimiwa Matiko ana marekebisho, katika utaratibu tunaoenda nao ni kwamba hapa atakayetakiwa kuongea ni Mheshimiwa Matiko. Sasa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwamba marekebisho mliyofanya kama Serikali unataka kuyarekebisha tena?

Sawa, basi tumpe kwanza nafasi Mheshimiwa Matiko ama tumpe kwanza Mwanasheria Mkuu, usikute amechukua mawazo yako Mheshimiwa Matiko tayari, usikute yapo tayari. Mheshimiwa Matiko kaa kwa sababu inawezekana kachukua hayo ya kwako ndiyo kayaweka ili twende vizuri, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kuboresha yale marekebisho yetu Ibara 40(1) kwa ile dhana tu msingi wa kuhafifisha makosa kwamba ili wafifishe ni lazima huyo mtu awe amekubali, tulisahau hicho kitu ndiyo tunataka tuyaongeze pale. Kwa hiyo, kama Bunge lako Tukufu litakubali, baada ya neno *where a person has* tufute lile neno '*has*' halafu tuweke *admits in writing to have committed any offence,* mengine yote yaendelee kule. Kwa hiyo, hiyo ndiyo tulitaka kufanya marekebisho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba ku-*withdraw*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Wanataaluma wa Kemia, *The Chemist Professionals Act,* 2016, kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake na kuukubali. Naomba kutoa hoja sasa Bunge lako Tukufu likubali Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016*(The Chemist Professionals Bill, 2016)*.**

*(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali, Muswada umeshapita na sasa Bunge limeshapitisha hiyo sheria, kwa hivyo itafuata hatua nyingine ya kumpelekea Mheshimiwa Rais ili aweze kuweka saini na tuweze kuitumia sasa.

Nichukue fursa hii pia baada ya kuipongeza Serikali niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge ambao mmeweza kukaa mpaka dakika hii. Naomba tusikilizane kidogo, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana kwa kubaki mpaka muda huu ili tuweze kumaliza kazi vizuri, unaweza kuona namna ambavyo Wabunge ninyi mliobaki hapa katika hali ya kawaida ni ninyi wenyewe ndiyo huwa mnawahi tena asubuhi. Kwa hiyo niwapongeze sana na naamini kesho asubuhi mtawahi tu kufika kama kawaida yenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo mawili hapa, tangazo moja linatoka kwa Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho Jumatano tarehe 14 Septemba, 2016 kutakuwa na uzinduzi wa miongozo ya mfumo wa anwani za makazi na *post code* ambao

utafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa saba mchana. Mgeni rasmi katika uzinduzi huo atakuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine nimepokea barua hapa kutoka kwa Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya ambaye ameiandika kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Nyasa, hawa wananchi wametuma mchango wao kwa ajili ya wenzetu wa Bukoba waliopatwa na maafa na fedha hizi zitakabidhiwa kwa Mheshimiwa Spika ili aweze kuzikabidhi huko ambako zinapaswa kwenda. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Shilingi ngapi?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusoma matangazo hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.23 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 14 Septemba, 2016 Saa Tatu Asubuhi)*